Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 26 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. ABUU HAMOUD JUMAA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. HIGHNESS SAMSON KIWIA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Viwanda na Biashara Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali leo kwa Waziri Mkuu naona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hatumwoni. Kwa mujibu wa Kanuni zetu kama hayupo hawezi kuweko mbadala wake na kwa hiyo, nitaendelea na wale ambao walishaomba.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijamwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali, naomba tuwatakie heri Mama Anna Abdallah na Mama Makinda leo ni siku yao ya kuzaliwa, kwa hiyo *happy birthday. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa sisi wana Siasa hasa sisi tulioko humu ndani tuna uwezo mkubwa sana wa kuijenga nchi hii.

Lakini pia tuna uwezo wa pili wa kuibomoa nchi hii na hata kuiingiza katika vita. Mheshimiwa Waziri Mkuu, siku za karibuni mmeanza tabia ambayo nilikuwa sijaiona muda wote tangu nimekuwa Mbunge katika kipindi changu cha tatu hiki Wabunge kuingia kwenye Majimbo ya wenzao na kuchukua hatua ya kuwakosoa kiutendaji na kutoa maneno yasiyoridhisha mbele ya wananchi kitu ambacho kimepelekea vurugu zikatokea mwishoni mwa wiki hata kuleta madhara.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa sababu tabia hii ikiachiwa kuna siku tutaingia kwenye vita ya wenyewe kwa wenyewe? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nipongeze maana kama ni *birthday* yako nafikiri unastahili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kutoa maelezo kuhusu suala ambalo Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, amejaribu kulieleza. Mimi nataka nikubali kwamba ni kweli ziko dalili za namna hiyo. Kwa bahati mbaya hata Jimboni kwangu yalinipata. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini mimi tafsiri yangu ilikuwa ni rahisi tu kwa sababu mambo haya yanategemea ukomavu wa mwanasiasa mwenyewe ambaye anakwenda kwenye eneo hilo. Maana wale waliokomaa wenye kuelewa dhamira ya Serikali ambao wanajua nia yetu hasa ni nini anajua wajibu wake anapokuwa katika maeneo haya ni kuzungumzia Sera za Chama chake, ama kusaidia kuweka sawa baadhi ya maeneo ambayo wanafikiri yanastahili kuboreshwa zaidi. Lakini sasa ukiwa na mwanasiasa ambaye kidogo hajafikia mahali pa kupevuka ni kweli ataanza kushughulikia *individuals* badala ya ku-*deal* na *issues.* (*Makofi*)

Lakini mapema kabla hatujaja hapa Bungeni nilipata nafasi ya kuzungumza na msajili wa Vyama na nikamsihi sana kwamba asaidie vyama hivi vyote kwa kujaribu kukutana nao kimoja kimoja kujaribu kuwaelimisha juu ya ujenzi wa Demokrasia ya Vyama Vingi na maana yake hasa ni nini kwa sababu inaonekana bado wengi hatuelewi katika vuguvugu hili wajibu wetu hasa ni kitu gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wakati huo huo, Sheria ya Msajili wa Vyama ya Mwaka 1992 ambayo tulifanya Marekebisho hapa mwaka 2009 ukichukua na Kanuni zake za mwaka 2007 zinajieleza bayana kabisa,

zimetoa maelezo mazuri sana namna Vyama vinavyopaswa kuendesha shughuli zake hasa nyakati hizi ambazo si za kampeni. Zimeeleza bayana kabisa. (*Makofi*)

Lakini kizuri zaidi kwenye Sheria hizo na mimi naomba mzipitie msome kwa makini kama ni Chama ambacho kiko kwenye usajili wa muda Msajili wa Vyama anaweza akakifuta kwa matendo ambayo yanaashiria uvunjifu wa amani kwa maana ya matusi, kujaribu kudharauliana na kadhalika. Lakini hata Chama kilichoandikishwa kinaweza vile vile chini ya Sheria hiyo kufutwa endapo Msajili ataridhika na jambo hilo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nadhani nataka niwasihi viongozi wote kwa ujumla tuko hapa sisi wote ni watu wazima, tuko hapa kwa nia njema, tunataka kujenga nchi yetu vizuri, chonde chonde twende kwenye Majimbo tuzungumze masuala ya msingi ya Sera ya namna ya kutekeleza na kupeleka nchi hii mahali pazuri. Narudia tena unajua Mwanasiasa anayekaa anahangaika na *individuals,* watu hivi Pinda hiki, ujue na yeye vile vile ana tatizo kubwa sana katika upeo wake. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nadhani kwa ufupi naweza nikalisema hivyo na kuwasihi wote tujaribu kufanya kazi hiyo kwa umakini mzuri kwa lengo la kujenga taifa letu na kwa heshima ya nchi yetu. (*Makofi*)

**MHE. MWIGULU LAMECK MCHEMBA MADELU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imeweka utaratibu mzuri sana kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa

kuanzisha Mfuko wa Jimbo, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo. Lakini maendeleo hayo yanachochewa kwa kushirikiana na Madiwani. Lakini tofauti ni kwamba Madiwani wamekuwa wakichochea hayo maendeleo kwa kutumia posho zao wanazozipata.

Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kuwaangalizia utaratibu Madiwani wa kuwatengea fungu hata dogo tu linalolingana na Kata ili na wenyewe wanapoitwa kuchochea shughuli za maendeleo ambazo sote tunashuhudia wamekuwa wakisumbuliwa sana waweze kutumia mfuko huo tofauti na sasa wanavyotumia posho zao? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mwigulu Mchemba. Ni swali zuri lakini si rahisi sana kulijibu. Mimi ni Diwani vile vile wakinisikia na mimi nasema ovyo ovyo huko ni taabu vilevile.

Lakini Sheria ile inachosema hapa ni nini kwa sababu ule mfuko ni wa Kuchochea Maendeleo katika Majimbo. Kuchochea maana yake nini hapa? Sheria inasema unapokuwa katika Jimbo lako miradi inayoendelea katika maeneo hayo. Unapofika mahali fulani na ukaombwa pengine msaada kumalizia mabati 40 au 50 Mfuko huu utakusaidia kuwezesha shule au zahanati hiyo kukamilisha ule mradi. Kwa maneno mengine ni fedha ambayo inakwenda kutoa mkusumo kwa wananchi katika maeneo yanayohusika. Si fedha ambayo unakuwa nayo unatembea unagawa kwa kila mtu unayemwona hapana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, basi kikubwa ninachokiona ni vizuri Waheshimiwa Wabunge ambao ndio Wenyeviti wa Mifuko ile na katika Sheria ile tumesema Madiwani, angalau wawili wawemo, tuhakikishe wale Madiwani, wawili wanakuwemo kwa sababu wanasaidia kuainisha baadhi ya miradi ambayo iko chini ya Kata fulani fulani kwa lengo la Mbunge kuweza kujua akipita pale asaidie namna gani.

Sasa rai yake ni nzuri lakini kwa uwezo wa kibajeti tulionao leo pengine si rahisi sana. Lakini tunachoweza kuahidi tu mbele ya Bunge hili bado tutaendelea sisi kuboresha mafao/posho za Madiwani, ili kile kidogo kinapobanwa basi waweze kuchangia kwa kadri watakavyoona inafaa. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nichukue fursa hii kabla sijauliza swali kuwatakia heri Waislam wote katika huu Mfungo wa Ramadhani katika Nguzo yao Muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu swali langu, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambalo suala la Muungano ni suala la Katiba. Kila mtu anao uhuru wa kuabudu dini anayoitaka pasipokuingilia uhuru wa dini nyingine.

Tarehe 20 Julai, 2012 Waziri wa Katiba wa Serikali ya Zanzibar alilihutubia Taifa la Zanzibar kupitia Televisheni na Radio akiwaambia watu wote wanaoishi

Zanzibar na wanaoingia Zanzibar kuendana na Mfungo wa Ramadhani, akiamrisha kwamba *Hotels* zote na *Restaurant* zote zisiuze vyakula wakati wa asubuhi na mchana.

Kama vile haitoshi alisema "watu wote wanaovaa nguo fupi hasa wanawake zinazoweza kuwatamanisha wanaume vyombo vya dola vichukue hatua" alisema vile vile "kwamba yeyote anayepatikana anakula chakula wakati wa mchana mamlaka ichukue hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili ni hatari sana kwa Mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo hili linadhalilisha Dini zingine. Naomba tuvumiliane nyie mkisema tunawavumilia. Jambo hili linatikisa uhuru wetu na Muungano wetu, ninaomba msimamo wa Serikali yako. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya mimi sikusikiliza hiyo taarifa naomba kwanza niseme hilo. Lakini la pili sielewi hasa alisema nini naona ume-*quote* hivi. Kwa hiyo, sina hakika kama ndivyo ilivyokuwa au hapana.

Lakini vyovyote vile itakavyokuwa kama unazungumza Serikali mbili iko Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na iko Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kauli imetoka kwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofi*)

Ninachokifikiria hapa kwamba inawezekana kabisa kwa mazingira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani wameona hilo linaweza likasaidia kuwafanya wawe na mfungo mzuri. Kwa hiyo, mimi nadhani rai nzuri hapa ni kusema tuache waliendeleze kwa namna wanavyoona kwa mazingira yao inafaa. (*Makofi*)

Lakini moja hili la uvaaji wa nguo fupi, nguo fupi nadhani tunakubaliana tu kwamba ni jambo ambalo si zuri halina staha. Linahitaji kwa kweli kusemwa na kila mtu, wala si jambo ambalo nasema linahatarisha Muungano hata kidogo, ni jambo tu ambalo linaeleweka tu. Kwa hiyo, mimi nadhani tuwaachie wenzetu katika mazingira yao wataona nini wanafikiria kwa mazingira yao kinafaa na wakitumie kulingana na mazingira yao. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na majibu yako ambayo kiukweli hayaridhishi kabisa kwa mstakabali wa taifa hili, naomba niulize swali la nyongeza. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimesema haina Dini, Je, ni wakati muafaka kwa Serikali yako kutangaza sasa kwamba upande mmoja wa Muungano unafuata Sheria za Kidini na upande mwingine wa Muungano hauna Dini? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Ndugu yangu Mchungaji mimi naelewa kwa sababu wewe ni Mchungaji inawezekana unaliona kama jambo kubwa sana. Tuelewane tu hapa kidogo, nasema hili kwa maana ya mazingira ya Zanzibar, ninachosema ni nini ni kwamba

ukienda Zanzibar tukichukua tu takwimu za jumla jumla unaweza ukaona kabisa karibu 99% hivi ni Waislam *okay!* Ndio maana nasema kwa mazingira ya Zanzibar viko vitu ambavyo vinaweza vikafanyika na mimi nadhani kwa sehemu kubwa atakuwa alipima vile vile mazingira akaona ridhaa hiyo na pengine si mara ya kwanza mimi sijui.

Lakini usilifanye likawa jambo kubwa. Angekuwa anazungumza kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa *Tanzania of course* ingekuwa *different*. Lakini inazungumza kwa mazingira hayo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea na mwingine, wenyewe wanaridhika sasa ninyi inakuwaje tena? Naomba utulivu kidogo. Haya basi msigombane humu ndani. (*Kicheko*)

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni ukweli ulio dhahiri kwamba katika Mikoa yetu ya Tanzania tumeendelea kutofautiana, inawezekana ni historia tangu ukoloni. Lakini kuna sababu nyingi. Lakini kuna sababu nyingi, lakini pia ni dhahiri kwamba ili uwekezaji wa kibiashara uweze kufanyika lazima kuwe na vivutio ambavyo vinakuwepo.

Lakini ni dhahiri pia lazima Serikali ionyeshe *commitment* kwamba inapeleka vivutio baadhi ya maeneo. Vivutio hivyo ni kutegemea na fedha ya maendeleo ambayo inatengwa na Serikali.

Mheshimiwa Waziri ni data za miaka mitatu mfululizo kuhusiana na Mkoa wa Rukwa pamoja na Lindi ambayo inatajwa kama Mikoa ya Pembezoni.

Mkoa wa Rukwa mwaka huu katika fedha zilizotengwa za Maendeleo umekuwa wa pili kutoka mwisho. Mwaka jana ilikuwa ya 16 kutoka mwisho, kwa mwaka uliotangulia imekuwa ya 15 kutoka mwisho, hali kadhalika Lindi miaka miwili mfululizo imekuwa ya mwisho na ule mwaka uliotangulia ilikuwa ya pili kutoka mwisho. Serikali yako inatekeleza dhana ya kwamba Mikoa iliyoko pembezoni itabaki kuendelea kuwa nyuma kwa kutoitengea fedha ya kutosha?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu Ndugu yangu Kandege swali lake zuri tu na lazima na mimi nitangulie kusema na mimi natoka Rukwa kwa hiyo najua *concern* yake ni nini.

Lakini ni dhahiri vile vile kwamba kwa sababu bahati nzuri Mwenyezi Mungu amenijalia ndiye Kiongozi wa shughuli za Serikali ni Waziri Mkuu, ungetegemea katika mazingira ya kawaida tu kwamba pengine Mkoa wangu ndiyo ungeongoza kwa maana ya kubwa wa Bajeti kwa maana ningeweza nika-*determine* kwamba nipe zaidi kuliko Mikoa mingine. Hii maana yake nini?

Maana yake ni kwamba Bajeti hizi zinapotengenezwa, viko vigezo vinavyofuatwa. Kwa hiyo, kwanza kuwa kuna mgao tunaita prorata, mgao

ambao unagawiwa kwa Mikoa yote sawa sawa kama hatua ya kwanza, lakini pili tunaingia kwenye vigezo vinavyoonyesha mambo mbalimbali, kiwango cha umasikini, kiwango cha huduma kwa mfano za barabara, kiwango cha miundombinu ya msingi kwa mfano kwenye afya, elimu na kadhalika. Kwa sababu viko vitu ambavyo ndivyo vinavyoonyesha kwa nini Mikoa fulani ipate huduma zaidi, iko vile vile suala la muhimu la idadi ya watu na ndiyo maana utaona kwenye Bajeti ya mwaka huu na mimi wakati wameniletea yale maelezo Mikoani, nilijitahidi kupitia kuona hali ikoje. Utaona Mkoa ambao umepata fedha nyingi sana ni Mwanza, wao wana bilioni karibu 37, wanafuatiwa na Mkoa wa Mbeya bilioni 36, halafu Mkoa wa Dodoma bilioni 32. na ukitazama, viko vitu ambavyo vinafanya miradi katika maeneo haya iwe ndiyo inachochea sana ukuwaji huo wa Bajeti katika maeneo hayo.

Sasa ni kweli Mkoa wa Rukwa tumekuwa mara nyingi tuko mwisho na safari hii nadhani sio wa mwisho kwa sababu Mikoa ya mwisho sasa ni Njombe na Katavi kama ukitazama ile orodha ya Mikoa. Katavi ni bilioni 8, Njombe wana bilioni 13, lakini vile vile kwa sababu ni Mikoa mipya, hatujaanza kujenga uwezo, pole pole itaweza kuongezeka. Kwa hiyo, mimi nataka nikuombe tu kwamba unalolisema ni la kweli lakini lazima tuzingatie vigezo. Mimi jambo ambalo nadhani na wewe ni ile Mikoa ambayo kwa muda mrefu imebaki nyuma, si kwa sababu ya upembezoni lakini kutokana na sababu mbalimbali.

Ni wakati muafaka nafikiri sasa, badala ya ule mgao prorata wa kwanza, iwekwe vile vile *element* ya Mikoa ambayo kwa muda mrefu imekuwa nyuma kimaendeleo waongezewe kiwango fulani kabla hawajaingia katika vile vigezo vingine vya msingi.

Bahati nzuri unalisema hili kwa sababu tulishalizungumza wakati tunaanda Bajeti, nilishawaagia TAMISEMI wakae na Hazina, tuone hii Mikoa maana lazima tutafute namna ya kuisukuma na yenyewe iweze kwenda mbele kwa haraka zaidi kama Mikoa mingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani rai hiyo ndiyo tutakayoizingatia tuone namna tutakavyosaidia kidogo kuweza kuongeza viwango vya Bajeti kwenye baadhi ya Mikoa hiyo. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niulize swali dogo sana la nyongeza:-

Kwa kuwa busara imetumika ya Bunge kwamba Finance Bill ije mwishoni baada ya kwamba tumeshapitia mchakato wote mzima na hili Mheshimiwa Waziri Mkuu amekiri kwamba ni kweli kwamba kuna Mikoa ambayo inahitaji kusukumwa.

Je, Mhehsimiwa Waziri Mkuu utakuwa tayari Mheshimiwa Waziri wa Fedha akileta mapendekezo kwamba hili lianze kutekelezwa katika kipindi hiki? (*Makofi*)

**SPIKA**: *Finance Bill* tunajaribu kukubali *sources of revenue, expenditure* ndiyo haya maneno mnayosema kila siku. Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nimwombe tu Ndugu yangu Kandege haraka haraka kiasi hicho haitawezekana kwa sababu bajeti hii mmeshai- *frame up* tayari, tayari tunajua kipi kinakwenda wapi, lakini tunahitaji maandalizi vile vile kwa sababu lazima uwepo mjadala kidogo mkubwa maana hata hiyo Mikoa maana yake nini ya pembezoni ambayo iko nyuma maana yake nini, itabidi tukubaliane mambo fulani, fulani na kiwango gani.

Maana haiwezi kuwa kwa Mkoa mmoja unaitwa Rukwa hapana. Kwa hiyo, lazima tuangalie Mikoa mingi zaidi kidogo ambayo tunafikiria inahitaji kupewa msukumo zaidi.

**MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kumwuliza Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naelewa fika kwamba tuna mchakato wa Katiba na ninaelewa kwamba Serikali ya Tanzania ina Kamati zilizoundwa kutatua matatizo ya Muungano.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pale Bandarini, kutokea Tanzania Bara kwenda Zanzibar, kuna kodi inayotozwa ambayo ni usumbufu mkubwa kwa vijana, pamoja na wanawake wajasiliamali na sidhani kama pato linalokusanywa pale lina ongezeko kubwa ndani ya Tanzania kutufanya kwamba tushindwe kuondoshewa kodi ile.

Mheshimiwa Waziri Mkuu unawaambia nini vijana hususani wakati huu wa Ramadhani na vijana na wanawake itaondoka lini kodi ile?

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri Mkuu, labda unaifahamu kodi hiyo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Tauhida Nyimbo swali Lake. Nilikuwa najaribu kulielewaelewa kwamba hasa hasa kinachosemwa ni nini kwa sababu hapa kuna mambo mawili; ziko bidhaa zinazotoka nje kuingia nchini, zinaweza zikaingia kupitia Bandari ya Zanzibar, zinaweza kuingia nchini kupitia mipaka mingine mahali popote hapa Tanzania.

Kwa hili, tulikwishakubaliana kwamba kimsingi bidhaa popote zitakapoingilia zikishaingia nchini, tozo yake ya ushuru itakuwa ni sawasawa kwa wote maana tumeshakubaliana chini ya utaratibu huo.

Hili lina tatizo lake kidogo kwa upande wa Zanzibar na bado liko tatizo pale la bidhaa zinazoingia zinatozwa ushuru, lakini zikitoka pale, zikija Bara zinafanyiwa *assessment* upya. Sababu yake ilikuwa ni hiyo hiyo kwamba tulikuwa hatujakubaliana kwamba ni vizuri *points* zile za kuingilia zote zifanane.

Sasa bado hilo eneo kidogo linahitaji kuka na wenzetu wa Zanzibar bahati Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia tumeshawapa hiyo kazi waweze kuondoa hicho kikwazo mara moja kabla hatujaingia kwenye kikao kitakachofuata. Lakini kama ni bidhaa za

kawaida, maana yake mtu ana mchele, sijui anataka kuleta visamaki kidogo, sina hakika kama katika eneo hilo kuna bugudha maana ulikuwa unazungumza vijana, akina mama ndiyo maana nikapata picha kwamba inawezekana ni bidhaa za humu humu ndani.

Kwa kweli kwa hili sidhani kama tunapaswa kuwa na tatizo hata kidogo, lakini kama lipo, basi nitaomba pengine Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais ajaribu kulifuatilia tuone majibu yake yanaweza kuwa ni nini kwa sababu ni bidhaa zetu za ndani tu, hazina uhusiano na zile zinazotoka nje. (*Makofi*)

**MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako mazuri. Lakini Mheshimiwa Waziri, ndani ya Bandari unatokea Tanzania Bara, kodi zinazotozwa, mwanamke mjasiliamali anatoka Zanzibar anakuja kuchukua mzigo hau-cost laki mbili au laki moja na nusu, akifika Bandarini, anapata usumbufu ingalikuwa ndani ya boti hata ushuru wa aina yeyote hatozwi au halipii na unakuta kijana wa Tanzania Bara anakuja Zanzibar, ananunua deki za TV moja na TV moja, akifika kwenye Bandari ya Tanzania Bara anaambiwa alipie. Ninadhani Mheshimiwa Waziri, uko wakati mzuri sasa wa kuwajibisha Maafisa ambao hawataki kutii amri hiyo. Nadhani wanafanya ukiritamba wa makusudi. (*Makofi*)

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri Mkuu sio Waziri tu, huyu ni Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nilitaka kusema ndiyo huyo huyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa nimesikia rai yako. Mimi nafikiri ngoja tuliangalie, nafikiri bado kuna tatizo kidogo hapo ambalo linahitaji kuondolewa kwa sababu mimi nikichukua bidhaa fulani Bara nikapeleka Zanzibar kuna usumbufu kwenye Bandari ya Zanzibar?

Je, anapokuwa mtu amekwenda Zanzibar kanunua bidhaa kwenye maduka ya Zanzibar pale anakuja Bara, je, kuna usumbufu upande wa Bara? Sasa hilo nadhani ndiyo tatizo linapoibuka. Huu usumbufu ni lazima tuuondoe kwa sababu hauna tija hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani kwenye kikao kitakachofuata, tutajaribu kulitafutia suluhu ambayo nadhani itakuwa ni ya kudumu moja kwa moja. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wabunge tukushukuru kwa majibu mazuri ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge na Wabunge mmejitahidi kuuliza maswali mazuri. Katibu tunaendelea na hatua inayofuata. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 265

**Utaratibu wa Mbunge Kutembelea Taasisi za Elimu Jimboni**

**MHE. PETER S. MSIGWA** aliuliza:-

Je ni utaratibu gani unaotakiwa kutumika au kufuatwa pale Mbunge anapotaka kutembelea vyuo au Taasisi za Elimu ya Juu zilizopo Jimboni mwake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Simon Msigwa, Mbunge wa Iringa Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni wadau muhimu wa shughuli za maendeleo zinazofanyika Majimboni. Pia ni wasimamizi, washauri na wahamasishaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo maendeleo ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, Mbunge anapohitaji kufanya ziara katika taaisi yeyote ile yaani shule au chuo anapaswa kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Mkoa (Katibu Tawala Mkoa) au Mkuu wa Wilaya (Katibu Tawala Wilaya). Mamlaka hizi zinategemewa kuona uwezekano pamoja na kuratibu ziara husika bila kuingiliana na ratiba ya taasisi inayotembelewa au ziara za Viongozi wengine katika taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hizi za Mkoa na Wilaya ni msaada mkubwa sana kwa Viongozi mbalimbali wa Kitaifa wakiwemo Waheshimiwa Wabunge katika kupata taarifa za msingi za eneo linalokusudiwa kutembelewa kwa ajili ya ufahamu na kupata maeneo ya msisitizo pamoja na kupata tahadhari za kiusalama kuhusina na ziara hizo.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru pamoja na majibu ambayo sio ya kuridhisha ya Waziri, baada ya kurekebisha nilitegemea swali hili liende kwenye Wizara ya Elimu, lakini swali langu:-

Waziri sijui utaniambia ni Sheria gani ambayo inanilazimisha nipitie sehemu zote ambazo umesema Katibu Tawala ili nipate kutembelea taasisi za kielimu? Lakini mfano mzuri, niliwahi kufuata taratibu hizo nikitaka kutembelea Chuo cha Mkwawa, nilizuiwa, nilivyojaribu kwenda kwa Waziri anaehusika naye alishirikiana na Mkuu wa Chuo hicho kunizuia kama Mbunge nisitembee maeneo hayo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kama ifuatavyo:-

Kwa vyuo vya elimu ya juu, taratibu ni nyepesi sana wala hazina mlolongo mrefu. Cha muhimu ni kwamba Mamlaka ya Chuo kifahamu ili Mamlaka ya Chuo iweze kumwelekeza Mbunge husika, kumsaidia ili aweze kufanikisha ziara yake baada ya kufahamu

makusudi ya ziara hiyo ambayo anaenda kule. (*Makofi*)

Katika vyuo vya elimu ya juu wana ratiba kali sana za kimasomo, wakati mwingine wanakuwa kwenye mitihani au maandalizi mbalimbali. Mheshimiwa Mbunge anapokwenda pale bila ya Uongozi kujua na kuridhika kwa lile analokwenda nalo na kumwandalia ratiba inakuwa vigumu Mbunge huyu kufanikiwa katika hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna matukio ninayokumbuka mawili UDOM ya Wabunge walienda bila taarifa za Viongozi na Uongozi wa Chuo na matokeo yake Wabunge hawa walipata msukomsuko wa wanafunzi wenyewe mpaka ikabidi waje kuokolewa na Usalama. Waheshimiwa Wabunge naomba tufuate taratibu zilizokuwa nyepesi na tutoe ushirikiano nkw Viongozi katika vyuo vyetu wanapokwenda kule. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa na swali moja la kuweza kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni vigezo gani ambavyo vinaisababisha Serikali kama wakati Fulani, inaonekana kama vile haina imani na Waheshimiwa Wabunge hadi kuanza mlolongo huu wa kwenda kupitia kwa Wakuu wa Wilaya, sijui Katibu Tawala wa Mkoa. Ni sababu gani ambazo zinaifanya Serikali isiwe na imani na Wabunge ambao kwenye Majimbo yao kwa nini wasiweze kuwasiliana na taasisi moja kwa moja? Nilikuwa naomba ufafanuzi ni kwa nini hali hiyo ipo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moses Machali kama ifuatavyo:-

Serikali wala haina woga wowote na Serikali inawachukulia Waheshimiwa Wabunge kama ni Viongozi muhimu sana ambao wanaweza wakalisaidia Taifa hili kuweza kusonga mbele. Kama nilivyosema katika jibu la awali kwamba wala hakuna mlolongo huo mrefu, unawasiliana moja kwa moja na mtu wa Chuo au na Uwongozi wa Chuo, mnapewa ratiba baada ya kuridhika na kile kinachotaka kwenda kufanywa kule.

Lakini pia Katibu Tawala wa Mkoa au Mamlaka ya Wilaya, ndiyo vyombo vya ulinzi na usalama katika eneo hilo, ambao ni muhimu nao wakafahamu ili watoe wale wasaidizi watakaoweza kumsaidia Mbunge anapokwenda katika eneo husika ama Wilaya ile, Mkoa ule mfano Afisa Elimu kama utakwenda kwenye Chuo cha Uwalimu, Vyuo Vikuu, Maafisa Elmu Wilaya hawahusiki sana. Kwa hivyo utapewa Afisa wa Mkoa kuambatana naye kwenda kule. Wao ni wasaidizi tu na lazima wafahamu ama sivyo utakapokwenda kule kama mfano nilioutoa UDOM ukapata msukosuko ule, unapata msukosuko ambao hauhitajiki kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge tukienda kwa nia nzuri ya kuwasaidia wanafunzi hawa bila shaka wanafunzi hawa hawatatupa misukosuko ambayo

imewahi kutokea. Ahsante sana. Nashukuru. *(Makofi)*

Na. 260

**Barabara ya Mkocho- Kivinje Kuwekwa Lami**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA** aliuliza:-

Mwaka 2010 Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Kilwa kuwa barabara itokayo Kwamkocho- Kivinje itatengenezwa kwa kiwango cha lami:-

Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kujenga barabara ya Kwamkocho-Kivinje, yenye urefu wa kilometa 5.0 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo mwaka huu wa fedha wa 2012/2013. Halmashuri ya Wilaya ya Kilwa katika Bajeti yake ya mwaka 2012/2013 iliomba jumla la shilingi milioni 800 kutoka fedha za maendeleo za mfuko wa barabara

kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 2.5 za barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kati ya fedha zilizoombwa, Halmashauri imeidhinishiwa shilingi milioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 1 kwa kiwango cha lami nyepesi (*Double Surface Dressing*) yenye upana wa mita 6. Awamu ya pili itawekwa katika mpango wa Bajeti ya mwaka 2013/2014.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu zuri la Mheshimiwa Waziri. Swali langu la nyongeza napenda kuuliza hivi:-

Kwa kuwa Rais Jakaya Kikwete aliahidi kilometa 5 na katika jibu lake Mheshimiwa Waziri anasema mwaka huu watajenga kilometa 1. Je, haoni ni bora kujenga kilometa 2.5 mwaka na mwaka 2013/2014 wamalizie kilomita 2.5?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu Swali la Nyongeza, la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tungetamani kufanya hivyo, kama fedha tuliyonayo ingetosheleza. Nataka nimthibitishie kwamba, huu mpango tunaokwenda nao ni mpango wa miaka 5 kwa hiyo, katika kipindi hiki tunategemea kwamba, tutakuwa tumemaliza kazi hiyo. Hata nikisema, sasa hapa nijibu kwamba, ndiyo, tutafanya kwa kilometa mbili na nusu Bajeti ya kwetu

ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imeshapitishwa tayari sasa; sasa nitakwenda kuzipata wapi tena?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba aamini tu kwamba, hii *commitment* ambayo imetolewa na Mheshimiwa Rais, sisi tunaisimamia, ndio maana tunasema kwamba, hapa tunazo milioni 350 ambazo zimetengwa kwa ajili, ya kazi hiyo. Sisi tutasimamia kuhakikisha kwamba, tunakamilisha kazi hiyo.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa, ahadi za Rais, hutolewa mbele ya Umma wa wananchi. Kwa kuwa, ahadi hizi zinapotolewa huwepo Waratibu, ambao wanaandika ahadi hizo. Je, kutotekelezwa kwa ahadi za Rais, hatuoni kuwa ni kuvunja heshima na haiba ya Rais, mbele ya Umma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hapa tunamzungumzia Kiongozi wa Kitaifa na anatoa ahadi. Yeye, akishamaliza kuahidi pale, na tunayo orodha hapa, Mheshimiwa Lukuvi, huwa anakuja hapa, anakuja na orodha ya ahadi zote ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais; wala haituingii kwenye akili kwamba, tunaweza tukafikiri kwamba, tutakwenda kinyume na maelekezo ya Rais, au ahadi aliyotoa Rais, haiko, wala hatudhanii, hata kufikiria tu.

Mheshimiwa Spika, tunachojua ni kwamba, akitoa ahadi sisi tunachacharika, kila Wizara inayohusika, inaanza kuchacharika kuhakikisha kwamba, inatekeleza na inafanya hivyo na jitihada zinazofanyika zinafanyika katika kipindi cha miaka 5. Bahati mbaya sasa, hakutaja ni eneo lipi ambalo kuna mahali kilifanyika, ningeweza nikajibu, lakini tu nataka nimwambie kwamba, sisi hapa kazi tuliyonayo ni kuhakikisha kwamba, tunatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nilitaka kujua, kwa nini sasa katika kutekeleza ahadi ile ya barabara ya kutoka Kwamkocho hadi Kivinje, zisifanyike jitihada za pamoja baina ya *TAMISEMI* na *TANROADS* kwa sababu, *TANROADS* nao wamepanga vilevile katika Bajeti yao ya mwaka huu, kukanilisha ujenzi wa barabara hii.

Sasa ni kwa nini sasa Serikali, isifanye jitihada za pamoja katika kukamilisha na kutekeleza ahadi hii muhimu ambayo ni barabara inayokwenda katika Hospitali Kuu ya Wilaya ya Kilwa? Asante sana.

**SPIKA:** Sasa mnasemaje? Ni barabara hiyohiyo na wafadhili wawili? Haya, endelea Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri

Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachosema hapa ni kweli. Siku moja nakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu yuko hapa, nilimsikia akijibu swali hili linalosemwa hapa; akisema kwamba, nayo Wizara ya Ujenzi, ina mpango wa kusaidia barabara hii. Kuna mambo mawili pale, la kwanza unaweza ukasema *promote status* yake hii barabara itoke kutoka Halmashauri ihamie Ujenzi. Hiyo ni moja, ndiye mwenye dhamana ya kusema mimi naichukua hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, lakini nakumbuka pia kwamba, alisema atasaidia. Hizi hela nyingine mnazosikia tunajenga hizi, kama hizi ahadi za Rais, zinazozungumzwa hapa, hela nyingine zinatoka kwenye *Road Fund* na hela nyingine zinatoka ujenzi.

Kwa hiyo, hili analozungumza, na nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mangungu, maana kila wakati amekuwa mstari wa mbele kupigania hii barabara imekuwa mbovu. Tutakwenda kuzungumza na wenzetu, ili tuone kwamba, tunatekeleza pia hili analolisema hapa, kwa ajili ya kukamilisha barabara hii.

Na. 267

## Mgao wa Mafuta ya Magari ya Polisi

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Kwa kipindi cha miaka minne, Idara ya polisi Wilaya ya Rombo, haijapatiwa Mgao wa mafuta kwa magari ya askari Polisi:-

(a) Je, ni sababu gani zilizozuia mgao huo wa mafuta Wilayani Rombo?

(b) Je, Serikali, haioni kwamba, watu wasio wema kwa Wilaya hiyo na nchi kwa ujumla, wanaweza kuwapa Polisi hayo mafuta na hatimaye kuwatumia Polisi hao katika uhalifu wao?

(c) Je, kwa nini Serikali, isitumie sehemu ya fedha zinazotokana na faini za makosa ya usalama barabarani, ambazo ni zaidi ya Shilingi Milioni 20 kwa Mwezi, kuondoa kero hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, naomba nichukue fursa hii kumpa pole kwa ajali mbaya ambayo ilimkuta yeye na familia yake, ambayo iligharimu maisha na kuleta maumivu tofauti. Kupitia hadhara hii na Ramadhani, nawaombea wale waliofariki, Mwenyezi Mungu, awaweke eneo stahiki. Kwa wale ambao walipata majeraha, nawaombea wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge

wa Rombo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Rombo, hupata mgao wa mafuta ya magari kila mwaka. Mafuta kwa ajili ya magari yote ya Polisi yaliyoko katika Mkoa, Vikosi na Wilaya, hununuliwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa au Kikosi na kugawiwa katika Kamandi husika, baada ya Kasma ya Fedha za Matumizi ya Mwezi *(Warrant of Fund)* kutumwa kutoka Makao Makuu ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba, mara nyingi fedha zinazotolewa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta hazitoshelezi, ikilinganishwa na shughuli za Jeshi la Polisi kote nchini, hii inatokana hasa na ufinyu wa Bajeti.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali, haioni ubaya wowote kwa wananchi na wadau mbalimbali kuchangia fedha au vifaa kwa Jeshi la Polisi, kuliwezesha kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi. Hii ndio dhana halisi ya Ulinzi Shirikishi au Polisi Jamii.

Hakuna wasiwasi wa Polisi, kurubuniwa na watu wasio wema, kwani kazi ya Polisi hufanyika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa. Askari yeyote anayekubali kurubuniwa na kupindisha Sheria, huchukuliwa hatua zinazostahili.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa sasa, pesa zote zinazokusanywa, huelekezwa Hazina. Wizara

ya Mambo ya Ndani ya Nchi, haina mamlaka ya kuzitumia kabla ya kutolewa idhini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri na pia kwa salamu za pole alizonipatia pamoja na familia yangu. Lakini pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Je, Serikali, ikitegemea kupata michango kutoka kwa wananchi kwa dhana ya Polisi Jamii au Ulinzi Shirikishi, kwa Taasisi nyeti kama hii, haioni kwamba, kuna hatari hata majambazi na vibaka, wakalichangia Jeshi la Polisi na kwa sababu hiyo, wakali-*compromise* na hivyo kulifanya likashindwa kufanya kazi zake sawasawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Yapo maeneo ambayo doria ya Polisi ni kubwa kuliko maeneo mengine. Kwa mfano katika Jimbo la Rombo, kuna njia mbalimbali za kuvuka mpaka, karibu 320 na hivi kutegemea wananchi watalichangia Jeshi la Polisi kutimiza wajibu wake wa doria, ni kazi ngumu sana.

Ni kwa nini, Wizara ya Mambo ya Ndani, isifanye mazungumzo na Wizara ya Fedha, ili fedha hizi ambazo zinatokana na *fine* na tozo mbalimbali za makosa madogo madogo ya *traffic* katika baadhi ya hizo Wilaya, zikatumika kwa ajili ya kusaidia mafuta katika haya magari, ili doria iweze kufanyika ipasavyo kwa ajili ya usalama wanchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kwamba, kunaweza kukawa na hatari ndogo ya kupata michango ya majambazi. Lakini jambo ambalo ninaweza kulithibitisha ni kwamba, Kanuni na Taratibu za Jeshi la Polisi, zinaweza zikaifanya athari hii ikawa ndogo.

Mheshimiwa Spika, ni hivi juzi tu Waheshimiwa Wabunge, walipongeza sana Programu ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi. Nafikiri tuendelee kuiamini kama ni Programu ambayo, inatusaidia, sio tu kwa nguvu kazi, lakini pia kwa vifaa ambavyo vinahitajika kwa Programu hii na kuhakikisha kwamba, kila mtu anatimiza pia, mahitaji ya Katiba, ya kushiriki kwenye ulinzi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahitaji makubwa ya Wilaya ya Rombo; Wilaya ya Rombo, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Mbunge, anahisi kwamba, haipati mafuta ya kutosha, kwenye hesabu ambayo nilikuwa naiangalia, ndio Wilaya ambayo imepewa mafuta mengi katika Mkoa wa Kilimanjaro, katika miaka 4 iliyopita. Kwa hiyo, ni wazi kwamba, Serikali, pamoja na Wizara, imeona umuhimu wa vichochoro vilivyoko Rombo.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu kuzungumza na Wizara ya Fedha, nafikiri hili jambo tunalifanya kila siku. Tunafanya kupeleka Bajeti, Bajeti halisi ya mafuta kwa

Jeshi la Polisi kwa sasa, ni kama bilioni 39, lakini kwa mwaka huu mfano, tumepata bilioni 12.2. Hili ni jambo nafikiri sote tunahitaji kushiriki katika kuhakikisha kwamba, ulinzi hauwi *compromised,* na Wabunge nafikiri *you have a big role to play* kwenye suala hili, tusaidiane. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa, suala la vitendea kazi pamoja na ukosefu wa magari kwa ajili ya Polisi katika Wilaya ya Rombo, ni sawasawa kabisa na hali iliyoko kule Igunga.

Kwa kuwa, Jeshi la Polisi, limeanzisha huu mpango mzuri wa Polisi Jamii na kupeleka Wasimamizi wa Polisi Jamii, katika Tarafa, lakini wasimamizi hawa hawana usafiri, hawana Magari, hawana mafuta. Kwa hiyo, wanafanya kazi zao kwa kutembea kwa miguu wakati mwingine kwa baiskeli. Tarafa ya Igurubi kule kwetu na Tarafa ya Igunga na hata wilaya nyingine. Naomba Serikali, watuambie ni wakati gani sasa, watawawezesha hawa Wasimamizi wa Polisi Jamii, kuweza kufanya kazi yao vizuri kwa kuwapa magari na mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Dkt. Kafumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, program hii, ina mahitaji makubwa kuliko ingekuwa haipo na hilo tunalifahamu. Walinzi ambao wanashajihisha au kuhamasisha Ulinzi Shirikishi, tunatambua mahitaji yao na tayari tumeshanunua pikipiki nyingi sana kuwawezesha.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwenye pikipiki kwa sababu, tunahisi kwamba, mahitaji yake ni makubwa na kwa sababu, tayari tuna matatizo ya mafuta, pikipiki zinaweza zikawa banifu katika tatizo hili, lakini linawasogeza kwenye maeneo ambayo wanatakiwa wafanye kazi. Kwa hiyo, hivi karibuni, nafikiri hicho tulichopata, kinaweza kikagawanywa ili kazi za Polisi Jamii, zifanyike vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo jingine ni kwamba, hivi karibuni tumezindua *Police Public Fund Trust Fund,* ambayo ninafikiri inategemea michango kutoka kwenye sehemu tofauti.

Mbali na ile, pengine *contact* ya moja kwa moja kwenye maeneo ya kazi, mfuko huu unaweza ukatusaidia sana kubadilisha mazingira ya usimamizi wa Polisi kwa ujumla na pia, Polisi Jamii, ili kuhakikisha kwamba, uhalifu tunautokomeza au tunaupunguza kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Na. 268

**Kuondoa Kodi ya Madawa ya Maji**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Kodi ya Madawa ya Maji imekuwa ni kikwazo katika kutoa Huduma ya Majisafi na Salama:-

Je, ni lini Serikali, itaondoa kodi ya Madawa ya Maji, kwenye Mamlaka za Maji Nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya Mwaka 2009, inazitaka Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira, kulipia *VAT* kwenye madawa yanayotumika kusafisha maji na kutibu maji. Tozo ya *VAT* kwenye madawa hayo, husababisha gharama za uendeshaji kwenye Mamlaka za Maji kuwa juu…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukiwa humu sio mahali pa kufanya mazungumzo mengi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, gharama hiyo, kuingizwa kwenye bei ya maji na kulipwa na Wateja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dawa za kusafisha na kutibu maji hutumika kwa lengo la kusafisha na

kuuwa vijidudu kwenye maji, ambayo hutumiwa na binadamu na kuwakinga dhidi ya maradhi, Wizara yangu, imewasilisha orodha ya madawa ya kutibu na kusafisha maji Wizara ya Afya, ili yaingizwe kwenye orodha ya madawa ya binadamu, ambazo hazitozwi *VAT.*

Kuondolewa kwa *VAT* kwenye madawa ya kusafisha na kutibu maji, kutapunguza gharama za uendeshaji kwa Mamlaka za Maji, kwa wastani wa 7.3% na hivyo bei ya maji kupungua.

Mheshimiwa Spika, madawa ya kusafisha na kutibu maji yanayoombewa kufutiwa msamaha wa kodi ni yafuatayo; *Magna Floc, Soda Ash, Chlorine (Calcium huypochloride), Chloride (Polimerized Alluminium Chloride), Chlorine Gas, Poly Aluminium, Alum (Aluminium Sulphate)* na *Lime Calcium Carbonate.*

Mheshimiwa Spika, tunategemea kuwa, wakati wa kupitisha *Finance Bill,* madawa hayo yataingizwa katika orodha husika.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, ametuthibitishia hapa kwamba, baada ya *Finace Bill,* madawa haya yatafutiwa *VAT,* yataingizwa katika orodha na hivyo kusababisha bei ya matumizi ya maji kupungua.

Je, Mheshimiwa Waziri, sasa yuko tayari baada ya mambo hayo yote kufanyika, kuja ndani ya Bunge hili na kutoa Kauli ya Serikali, ya kuelekeza Vyombo na Mamlaka zote, kutangaza kwamba, sasa bili za maji katika maeneo hayo yanayotakiwa kuwa zimapungua? Kwa viwango ambavyo watakuwa wamevifikia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili. Kwa kuwa, *VAT* hii ikishaondolewa, gharama za uendeshaji zitapungua sana kwa Mamlaka hizi za Maji na kwa Wizara inayohusika na kwa Serikali, kwa ujumla wake.

Je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari sasa hizo fedha ambazo zitakuwa zimepungua, zitumike kununua madawa haya na kuyasambaza katika shule zetu zote katika nchi hii ya Tanzania na katika maeneo ya Vijiji, wanafunzi wetu waanze kupata maji salama na kuwaondolea maradhi ambayo yamekuwa yakiwasumbua sana kwa kunywa maji yasiyo salama huko mashuleni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulichofanya mpaka sasa hivi, ni kwamba, tumeandaa orodha ya madawa, kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi. Orodha hii imepelekwa Wizara ya Afya, ili waweze kuitambua na

baadaye kutoa mapendekezo. Kwa taarifa nilizonazo mpaka jana, orodha hii iko kwa Mkemia Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya orodha hii kukamilika kwa sababu na ninatambua umuhimu wa suala hili na Viongozi wote wamo humu ndani, tunategemea kwamba, hii orodha itaingizwa kwenye hii *Bill* ya *Finance Bill,* itajadiliwa tutaijadili sisi wenyewe Wabunge.

Kwa hiyo, kupita kwake kunatutegemea kwanza Viongozi wa Serikali, tuliomo humu ndani kwa maana ya Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha, ambayo lazima waridhie sasa huo mchakato ufanyike na uweze kuingizwa kwenye *Finance Bill.*

Mheshimiwa Spika, lakini awamu ya pili, kupita kwake, ikiingizwa kwenye *Finance Bill,* itategemea sisi Wabunge, humu ndani, tutakavyojadili na kuona umuhimu ipite.

Kwa hiyo, niombe tu kwamba, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha, wapitishe hii orodha ambayo, ni muhimu sana kupunguza gharama za uendeshaji kwenye Mamlaka za Maji Nchini, ikiwemo *DAWASCO* hasa kwa Dar-es-Salaam, na ikipita itapunguza gharama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ina sehemu ya pili kwamba kile kiwango kitakachokuwa kimepungua kitakuwa kimekuwa *saved* basi kitumike kwenye shule za sekondari na mahali pengine haitawezekana kwa sababu mpaka sasa hivi mamlaka zote zinazotoa

huduma za maji zinakumbana na matatizo makubwa hasa ikiwemo hii ya kulipia gharama za uendeshaji.

Kwa maana umeme na nyingi ambazo kwenye group la B unakuta mzigo wake unalipwa na Serikali mamlaka kama za Kahama Shinyanga, Serikali inachangia fedha zake pale miradi ya Maswa Serikali inachangia fedha zake pale. Kwa hiyo, zenyewe bado zimeshindwa kujiendesha.

Kwa hiyo hii ikipungua itasaidia tu zile mamlaka ziweze kujiendesha ili zile bei ziwe bei ambazo ni bei za chini kwa watumiaji. Kwa hiyo, kwa sasa hivi haitawezekana kwamba fedha zile zikipungua ziende kwenye mambo ya shule za sekondari kwa lengo hilo la maji.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa madawa haya pamoja na kuwa na kodi kubwa yamekuwa pia hayafiki na imekuwa ni kazi sana kuyapata hata binafsi unapotaka kununua hizi dawa unakuwa huzipati na wananchi wengi wamekuwa wakiambiwa kwamba ili wanywe ni lazima wachemshe na nishati inayotumika kuchemshia maji ni ya mkaa au kuni ambayo pia inapelekea katika uharibifu mkubwa wa mazingira.

Je, Serikali inasema nini kuhusu wananchi hasa wa vijijini ambao wanategemea maji ya visima au madibwi. Je, nayo iko tayari kuwapelekea wananchi hao madawa kwa ajili ya kusafisha maji hayo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Wanasafishia kwenye ndoo au inakuwaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, swali ni zuri, dhamira ya Serikali ni kuwapatia wananchi wetu maji safi na salama, na ili maji yawe safi na salama lazima yapewe matibabu ya madawa yanayohusika. Lakini vilevile tufafanue kwamba hii inaendana na uwezo wa hizo Mamlaka.

Kwa sasa hivi tuna Mamlaka za maji za Mkoa tuna Mamlaka za Miji midogo, Miji midogo ambayo inatoa maji kwenye wilaya bado hazina uwezo wa kuweza kupata fedha kwa ajili ya kununua madawa kwa ajili ya kutibu haya maji.

Kwa hiyo wito wangu ni kwamba wale watumiaji wote wa maji kwenye ngazi zote za wilaya za mkoa walipe vizuri wachangie vizuri zile fedha ili mamlaka zijiendeshe ziweze kununua yale madawa na waweze kutibu yale magonjwa ambayo yanawasibu wananchi wanapokunywa yale maji.

Na. 269

**Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

**MHE. VICKY P. KAMATA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitekeleza mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kupitia vijiji 10 katika kila

Halmashauri nchini, ikiwa ni pamoja na Halmashauri zitakazokuwa katika mkoa wa Geita:-

(a) Je, ni mafanikio na changamoto zipi zimetokana na utekelezaji wa mpango huo mkoni Geita?

(b) Je, wananchi hasa wa mkoa wa Geita watarajie nini kuhusu upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira ifikapo Juni, 2012?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkoa wa Geita una jumuisha Halmashauri za wilaya ya Bukombe, Chato na Geita. Mradi wa Maji wa vijiji 10 katika Halmashauri hizo uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe visima 16 vilichimbwa katika vijiji 12 ambapo vijiji 11 vilipata maji na kijiji kimoja kilikosa.

Wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji wamepatikana na kazi zimeanza katika vijiji vya Bulugala, Masumbwe, Bukombe na Shanda. Katika halmashauri ya wilaya Chato, visima saba vilichimbwa katika vijiji saba, na vinne vilipata maji ya kutosha vitatu vikakosa. Mkadanaris wa ujenzi wa miundombinu ya maji amepatikana na taratibu za kumpata mtaalam

mshauri wa kusimamia ujenzi ziko katika hatua za mwisho.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita visima 17 vilichimbwa katika vijiji na visima 13 vilipata maji. Taarifa za tathmini ya zabuni ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi imewasilishwa Wizarani ili kupata kibali cha kuanza ujenzi kwa ajili ya miradi ya vijiji vya Ruhuka, Nyamtukuza, Nyakazomba, Kayenze, Kalumwa, Chikobe na Kabugozo. Matarajio ilikuwa ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji vilivyotajwa utakamilika katika mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa *program* ni pamoja na muda mrefu uliotumika kuwapata wataalam washauri na wakandarasi kutokana na taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia ambazo hazikufahamika kwa watendaji wa ngazi mbalimbali hapo awali. Changamoto nyingine ni visima vilivyochimbwa kukosa maji katika baadhi ya vijiji. *(Makofi)*

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, nina maswali mawili ya nyongeza. Serikali kwa kushirikiana na *GGM* walianzisha mradi wa kutoa maji ziwa Victoria mradi ambao ulikadiriwa kuwa bilioni 15.3, hadi sasa GGM imeshatoa bilioni 6.99. Je, ni lini Serikali itatoa pesa hizo kusudi mradi huu wa maji ukamilike na watu wa Geita tupate maji? *(Makofi)*

Swali la pili, kule Bukombe na sasa ni wilaya nyingine tena inatiwa Mbogwe kuna kituo cha watoto yatima kinaitwa *FTI* Masumbwe, watoto hao wamekaa katika wakati mgumu hawana maji kwa muda mrefu sana na kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo tulifuatilia tukaomba Serikali itusaidie kichimba kimechimbwa tangu mwaka jana mwezi wanne, na mpaka hivi sasa maji hayajaanza kutoka ina maana kwamba *pump* haijapelekwa.

Nitumie nafasi hii basi kuiomba Serikali kupitia Wizara ya Maji ifungwe *pump* ili wale watoto waweze kupata maji kwa sababu maji yako mengi sana na lita 5000 kwa saa ni maji yanatosha kabisa kuwasaidia watoto yatima na wanakijiji wa eneo hilo ahsante sana.

**SPIKA:** Wasiwasi tu na maswali ya kisima usichokijua hebu jaribu kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mbunge Vicky Kamata na Wabunge wote wa Geita kwa namna wanavyofuatilia katika majimbo yao wilaya nzima ya Geita bila kumsahau Mheshimiwa John Magufuli wa jimbo la Chato. *(Makofi)*

Sasa kuhusu suala *GGM, Geita Gold Mine Limited,* kwanza tuwashukuru sana kwa msaada wao mkubwa ambao wameutoa wa milioni nne nukta tano dola ambazo ni sawa na *six point nine billion* hela za Kitanzania. Sasa wao wanatoa maji kutoka kwenye chanzo wanaweka miundombinu na wanayatoa yale

maji mpaka kwenye sehemu ambayo itajengwa tenki kwa gharama zao.

Serikali iliahidi sasa kutoka pale ambapo wanaweka tenki kupeleka miundombinu kwa watumiaji ambazo ndizo fedha bilioni tisa. Sasa Serikali imeshaongea kwa sababu kuna mradi mwingine sambamba unaoitwa *Lake Victoria* Watu ambao unafadhiliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki umepata mafanikio makubwa wilaya za Nasiyo, Geita na Sengerema na Geita peke yake ina dola milioni nne nukta mbili nadhani ni kazi ambayo iko chini ya Waziri wa Afrika Mashariki ambaye yuko hapa Mheshimiwa wa Viwango.

Kwa hiyo tumekubaliana Serikali kwamba badala ya kuwa na miradi miwili *parallel* ni vizuri fedha hizi milioni 4.2 ambazo zimepangwa kwa ajili ya Geita zitumike sasa kutoa maji wale watakapoishia wale wafadhili wa *GGM* kupeleka kwa wananchi kwenye ile miundombinu. Kwa hiyo nadhani hilo litakuwa limetatatuliwa na tushirikiane kuona linatekelezwa.

Kuhusu swali la pili kwamba kule Bukombe kuna kituo cha watoto yatima, hakina maji na kisima kimechimbwa *pump* inatakiwa inunuliwa na iweke iweze ku-*pump* nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Bukombe katika *sealing* ya fedha za vijiji kumi wanazo zaidi milioni 900 sasa hivi wakiangalia orodha ambayo tulikuwa tumeweka kwenye *pigeon hole* basi wakae na Halmashauri waweke kipaumbele katika milioni 900 kununua *pump* ambayo haitazidi

milioni 50 kwa ajili ya kituo cha watoto yatima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa muda umekwenda sana na maswali yenyewe yamekwisha na uzuri waliouliza wamejibiwa vizuri. Waheshimiwa tunao wageni ambao tutawatambulisha lakini pia naomba Waheshimiwa tuzingatie kanuni ya kukaribisha wageni. Maana kuna Mbunge mmoja juzi alitoa maelezo kukaribisha wageni inatamka kabisa ni watu wagani ambao tuna nafasi ya kuwakaribisha.

Nilikubaliana na yeye aliyeulizwa kwamba tunatumia muda mwingi sana kutambulisha wageni nitaisema baadaye ile kanuni kwa kweli haizungumzii watu mmoja mmoja binafsi makundi ndiyo inakubalika kanuni ya 139 ambayo inasema hivi, kwa sababu wale vijana wanaokaribisha wale wanapata tabu sana wanagombana na nyie Waheshimiwa Wabunge.

Ile kanuni 139 inasema, Spika anaweza kuwatambulisha wageni wote wa Kitaifa na Kimataifa waliomo katika ukumbi wa Bunge, 139(1) ya 2 inasema Spika vilevile anaweza kuwatambulisha wageni wengine waliomo katika ukumbi wa Bunge ambao wanahusika moja kwa moja na shughuli za majimbo, wanatembelea Bunge kwa ajili ya ziara ya mafunzo na pia wametoa mchango wa kitafia unaohitajika kuenziwa, kwa mfano hawa wachezaji timu za mpira wale basi ndiyo vitu kama hivyo.

Sasa inakuwa tatizo sana unakuja kutambulisha wengine watoto wamebebwa mikononi hivi na mama zao unasema na mtoto fulani sasa kazi kweli. Kwa hiyo, naomba mlielewe hili lisilete ugumu usiokuwa na sababu.

Kwa hiyo, wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ni Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, ni Naibu Katibu Mkuu Dkt. Shaban Mwinjaka, kuna wenyeviti wa Bodi za taasisi zilizochini ya Wizara hiyo wasimame wote, hawakutajwa kwa majina ahsanteni sana. Kuna Wakurugenzi wa idara na Wakurugenzi Wasaidizi naomba na wenyewe wasimame ahsante sana.

Kuna wakuu wa vitengo mbalimbali Wizarani na wenyewe walipo wasimame, halafu kuna Mwenyekiti wa TUGHE Taifa Diwan A. Mrutu, Katibu Mkuu TUGHE Taifa Bwana Ali Kiwenge naomba asimame Bwana Ali Kiwenge kama yupo, kuna Katibu wa TUGHE Mkao wa Dodoma bwana John Mchenya ndiyo mwenyeji wa hawa kina TUGHE ahsante sana.

Kuna wageni wa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi ambaye ni Ndugu Lawrence Kego Masha, huyu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani wa zamani Mheshimiwa Masha yuko wapi, alikuwa Mbunge mwenzetu katika kipindi kichopita tunakukaribisha sana.

Ndiyo hivyo Mawaziri wanashirikiana sana waliotoka na wao kule wanashirikiana jambo jema.

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge sasa hapa kuna wageni wa Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi Bungeni Mheshimiwa Tundu Lissu kutoka shule ya Ali Mohamed Sheni Singida ambao ni wanafunzi 42 na walimu watano hawa wanafunzi waliko ahsante sana hawa ndiyo wanaokuja kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Kuna mgeni Said Mohamed Manoro ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Maendeleo Kusini, lakini waliniandikia pia ka-*note* wenyewe kwa mkono na hii iliandikwa pia na Mheshimiwa Seleman Bungara, naona jina hilo narudia nasikia huyu Said Manoro ni mdhamini wa umoja wa maendeleo ya mikoa ya Kusini halafu yuko na Ndugu Abdulratif Hassan mjumbe wa mkutano mkuu wa Taifa *CUF* kutoka Singida na yeye yuko wapi.

Kwa hiyo, nina wageni wengine wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ambao ni madiwani 24 kutoka Iramba Magharibi wakiongozwa na Mheshimiwa Ruta Mkoma, ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Sylivester Mabumba ambao ni Ndugu Charles Mashima Mkonge ambaye ni mjumbe ni baraza la wazee Halmashauri ya mji wa Kahama, yuko wapi Mheshimiwa Charles ahsante uliopo.

Wageni ya Mheshimiwa Rita Mlaki wengine ni familia yake ambaye ni Lawrence Mlaki, Agusta Mfuru na Rita Pallagyo, Richard Pallagyo ni mjukuu wa hayati Mzee Kawawa. *(Makofi)*

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na wanafunzi na wale tuliowataja lakini wanafunzi 66 pamoja na walimu wao kutoka shule ya sekondari Maria Dematias Dodoma, hawa wasimame walipo na walimu, ahsante sana msome kwa bidii wanafunzi wote. Tuna wanafunzi wengine 50 pamoja na walimu wao kutoka shule ya msingi kiwanja cha ndege Dodoma Kiwanja cha Ndege Dodoma ahsante sana karibu sana wanafunzi wote.

Matangazo ya kazi, Waheshimiwa Wabunge Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Magareth Sitta, anaomba niwatangazie wajumbe wake kwamba leo watakuwa na kikao katika ukumbi namba 227 saa saba mchana nafikiri saa saba na robo, kwa saa saba tunakuwa hapa.

Halafu Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa David Silinde, anaomba niwatangazie Wabunge, Wabunge wa CHADEMA, kwamba leo saa saba na robo kutakuwa na kikao kwenye ofisi ya kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni saa saba na robo.

Waheshimiwa Wabunge nimepewa hapa taarifa na Mheshimiwa Mizengo Pinda kwamba yeye ameondoka baada ya kipindi cha maswali kwenda

Mkoa wa Mara kushiriki mazishi ya Marehemu Mwalimu James Irenge, Mwalimu James Irenge ndiye aliyekuwa mwalimu wa Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo amefariki kutakuwa na mazishi mchana huu, kwa hiyo Waziri Mkuu amekwenda kule na anatarajiwa kurudi kesho.

Kwa hiyo, kwa wakati huo Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Afrika Mashariki atachukua nafasi ya kuongoza shughuli za Serikali hapa Bungeni mpaka atakaporudi Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakutakia kazi njema. *(Makofi)*

Mimi Waheshimiwa Wabunge ahsante kwa kunitakia sikukuu ya kuzaliwa kwangu lakini pia nakwenda kushiriki mazishi ya mfanyakazi wetu wa kituo cha Dar es Salaam amefiwa na Baba yake maiti nafikiri imefika sasa hivi na watazika Mailimbili, kwa hiyo nitaenda kushiriki kule.

Kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, aje aendelee na shughuli za hapa. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama)*
*Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Jafo.

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kwa idhini kwa kutumia kanuni namba 47 ambayo inasema baada ya muda wa

maswali kwisha Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kwa shughuli za Bunge kuwa shughuli za Bunge kwamba zilizoorodheshwa kwenye orodha ya shughuli ziairishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura la muhimu kwa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kanuni hii, ni kwa sababu toka jana tulivyokuwa tunafuatilia vyombo vya habari, kumekuwa na tatizo la kutofahamika katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo mbalimbali. Wafanyakazi hao wako katika utata, mara baada ya sheria iliyopitisha Sheria ya Mabadiliko ya Mifuko ya Jamii ambayo imetoa kipengele kwamba mtu anapofanya kazi na anapokoma kazi kabla ya miaka 55 kwamba mtu huyo asipate mafao yake mpaka afikishe miaka 55.

Sasa jambo hili limekuwa tete kweli kwa Taifa letu na kwa kweli nimeona ni vyema tuwatetee Watanzania ambao wametutuma katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na siyo Watanzania, hata Wabunge halisi ambao wamo humu ndani ambao michango yao wanachangia kila siku katika Shirika la *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa idhini yako na kwa kutumia kanuni hiyo namba (1), (2) na (3) naomba kutoa hoja ili jambo hili lijadiliwe kama ni jambo la dharura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo nakushukuru sana na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Jafo, kwani ametumia kauli sahihi kabisa na kanuni hiyo baada ya kuitumia ninaona kabisa hapa imeungwa mkono vizuri na Wabunge wote. Sasa nataka kusema kwamba, kwa kweli jambo hili ni jambo ambalo lina umuhimu wake sana. Sasa kabla sijatoa mwongozo wa kukubali tulijadili, nilikuwa naomba kwa sababu limekosa kitu kimoja tu ambacho ningependa sana Wabunge tunapojadili hapa ndani angalau tungekuwa nacho ili itusaidie kuwasaidia na kuwatetea wafanyakazi.

Kitu cha kwanza ambacho naomba kumshauri Mheshimiwa Jafo ni kwamba tunaweza kwa mamlaka ya Kiti na mamlaka nilizonazo, nikakurudisha tena ukafanya hicho unachotaka kukifanya, lakini unisaidie kulifanya jambo hilo lijadiliwe vizuri, ulilete likiwa na taarifa za maeneo muafaka ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na nini, hasa ambacho tunatakiwa tuwasaidie wafanyakazi kwenye maeneo gani.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tukifanya hivyo, tutawasaidia sana wafanyakazi kujua hasa tuwasaidie kuwatetea katika eneo lipi, ingawa ninakubali kabisa hali hii imekuwa tete kwa wafanyakazi na watu wengi kwa ujumla wao wamekuwa wakilisemea hiili ndani ya siku mbili au tatu zilizopita.

Sasa naomba sana Mheshimiwa Jafo ututafutie kabisa maeneo ambayo ni tata ambayo yanatakiwa wafanyakazi tuwasemee na mimi kwa kutumia mamlaka ya Kiti nitaona ni utaratibu gani tuufanye ili

jambo hili liweze kupata nafasi nzuri ya kujadiliwa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu.

**TAARIFA**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba turejee kwenye kanuni ya taarifa. Aliyekuwa anaongea ni kiongozi anayesimamia shughuli za Bunge, yaani *Preceding Officer* na kwa mujibu wa kanuni ninaposimama mimi sipewi taarifa.

Mheshimiwa Zitto, nimekuona na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo Mheshimiwa Jafo amelizungumza ni zito na limekuwa na malalamiko makubwa sana na pia hatujapata kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushauri kwamba uitishe Kamati ya Uongozi sasa hivi ili pia Waziri wa Kazi aweze kuwepo na tuweze kulijadili kwenye Kamati ya Uongozi ili baadaye tuweze kujua ni utaratibu wa namna gani ambao unatakiwa uweze kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ushauri huu uweze kuuchukua.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nafikiri ni wazi kwamba jambo kubwa linaloleta huu mtafaruku ni suala la mabadiliko ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwazuia wafanyakazi kupata mafao yao mpaka watakapofikisha miaka 55 au 60. Nafikiri badala ya Mheshimiwa Jafo kwenda kuandika na kurudi, hili ndilo suala kubwa linalotatiza wafanyakazi wetu na Waheshimiwa Wabunge, na ninamuunga mkono Mheshimiwa Zitto kwamba ni vizuri Kamati ya Uongozi ikae na hicho ndicho kiini cha kelele zote hizi, na ninamuunga mkono Mheshimiwa Zitto kwamba Kamati ya Uongozi ikae ili iweke utaratibu wa namna ya kulijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sijui kama mmenielewa vizuri. Nilikuwa nafikiri kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu cha kufanya ungekubaliana na mtoa hoja ambaye ni Mheshimiwa Jafo ambaye amelileta jambo hili, halafu uungane na aliyetoa hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye moja kwa moja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza, nimekubali kwamba jambo hili ni zito na jambo hili lina maslahi ya wafanyakazi wetu, lakini ukiiangalia ile hoja, lazima hilo jambo liwe na maelezo mahsusi.

Sasa nilichokisema, ninampa muda wa angalau kumfanya Mheshimiwa Jafo afanye *consultation* na wafanyakazi wetu ili tujue ni eneo gani na lipi hasa ambalo linahitaji tulisimamie kwa umoja wetu. Kwa ushauri alioutoa Mheshimiwa Zitto, ni ushauri wa msingi na ushauri muafaka. Sasa labda kwa kukubaliana na hiyo yote, nimwagize Mheshimiwa Jafo angalau kwa muda wa wa masaa mawili au matatu yaliyobakia kabla ya saa 7.00 atengeneze hiyo hoja yake vizuri na maeneo hayo nyeti yanayotakiwa.

Mheshimiwa Jafo nikuagize, na Kamati ya Uongozi, sasa nimwombe Mheshimiwa Spika, tuone uwezekano wa kukutana saa 7.00 kwenye Kamati ya Uongozi, wakati huo Mheshimiwa Jafo mpaka hiyo saa 7.15 utakuwa umepata hasa yale yanayohitajika ili tuweze kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge. Lakini tukisema tuanze kujadili, nadhani hatutawatendea haki Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, mwongozo wangu ni huo. Mheshimiwa Jafo tafadhali kafanye kazi hiyo, wasiliana na wafanyakazi ili ujue tatizo lao ni lipi na Mheshimiwa Waziri wa Kazi tungeomba na wewe ujiandae ili uweze kushiriki kwenye Mkutano huo.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu.

Mheshimiwa Kangi, bado kwenye hilihili tena?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako chini ya kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. Katika maelezo ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Jafo ambaye ametoka kusema muda mfupi uliopita, kwamba wafanyakazi wanalalamika juu ya mafao yao kwamba sasa kulipwa ni mpaka wafikishe miaka 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni suala la kisheria na ni sheria ambayo ilitungwa na Bunge hili, na kusema kwamba wanalalamikia sasa mifuko ya jamii au yule *Regulator*, mimi nashindwa kuelewa kwa sababu hizo ni dalili kwamba Bunge hili hatupo makini katika kutunga sheria ambazo zinawahusu wananchi wa nchi yetu. Tuliwa wapi wakati sheria hiyo tunaitunga hapa? Halafu leo tunakuja kusema wananchi wanalalamika. Wananchi hao wanalalamikia Bunge hili kutokuwa makini na kutotunga sheria ambazo zinawahusu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kama ni halali Bunge hili kuleta hoja hii kwamba ni ya dharura, tujadili wakati Bunge hili hili ndilo lililotunga sheria hiyo kwa kutokuwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kama kweli inaruhusiwa.

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane! Mheshimiwa Kangi umeniomba mwongozo

na ninaomba nitoe mwongozo wangu kama ifuatavyo:-

Katika jambo lolote ambalo linatokea kwenye nchi yetu na lina maslahi kwa Watanzania, sisi kama Wawakilishi hatuna budi kulitazama kwa mapana yake. Haijalishi limepitishwa humu ndani ama halijakupitishwa. Lakini kazi ya Bunge hili, sheria zilizopitishwa na Bunge hili siyo msahafu, kwani zinaweza wakati wowote kutazamwa na kuona kama zinaweza kurekebishwa au namna gani, na Bunge litaishauri Serikali na kufanya maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, mmekuwa mkishuhudia hapa tunaletewa mabadiliko ya sheria nyingi tu, sasa kama ingekuwa hivyo ndivyo, basi tusingekuwa hatufanyi mabadiliko ya sheria yoyote katika Bunge hili. Kwa hiyo, naomba nibakie kwenye mwongozo nilioutoa na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tusiendelee kupoteza muda na suala hili liingie kwenye Kamati ya Uongozi na Kamati ya Uongozi italishauri Bunge kitu cha kufanya ili tuweze kusaidiana katika hilo.

Tunaendelea!

## Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa Fedha 2013/2013 - Wizara ya Viwanda na Biashara

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha hotuba yangu ya bajeti ya Madirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka

wa fedha 2012/2013, kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Viwanda na Biashara, ningependa kuungana na Watanzania wote kutoa pole nyingi kwa wenzetu waliofikwa na msiba huu mkubwa wa kufiwa na ndugu, jamaa na marafiki katika ajali ya Meli ya MV. Skagit. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu majeruhi wa ajali hiyo, wapone haraka na kuungana na Watanzania wengine katika kulijenga Taifa. Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 5 – 7 Juni, 2012, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake aliyonayo kwangu kunipa dhamana ya kuongoza na kusimamia majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Mheshimiwa Gregory George Teu - Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitayatekeleza majukumu hayo kwa moyo, uwezo na ujuzi wangu wote kwa kushirikiana na Baraza la

Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami - Mbunge wa Moshi Vijijini ambaye alikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu - Mbunge wa Singida Kaskazini na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa misingi imara waliyoiweka ya kutekeleza majukumu ya Wizara hii ambayo inanibidi niiendeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wabunge wapya: Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo - Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Janet Mbene - Naibu Waziri wa Fedha. Aidha, nawapongeza, Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi; Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu - Mbunge wa Jimbo la Igunga; Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari - Mbunge wa Arumeru Mashariki; Mheshimiwa James Mbatia - Mbunge wa Kuteuliwa; na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum - Mbunge wa Kuteuliwa. Nawatakia mafanikio katika majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa - Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini (CCM) na Makamu wake Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo - Mbunge wa Mbinga Mashariki (CCM), na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuendelea bila kuchoka kutoa ushauri na

maelekezo yao makini wakati wa kujadili muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii. Ushauri na maelekezo yao yametumika ipasavyo kuboresha hotuba hii ninayoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wenu mnaotupa katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya Wizara yangu, ikiwemo Miswada ya Sheria na mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwahakikishia kwamba Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kutekeleza malengo ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao. Namshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Mbunge wa Jimbo la Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake fasaha na inayobainisha mafanikio na mwelekeo wa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Steven Wassira - Mbunge wa Jimbo la Bunda (CCM) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uratibu na Mahusiano kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa uchumi. Nampongeza pia, Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga (CCM), kwa hotuba

yake makini inayobainisha malengo ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Handeni kwa dhamana kubwa waliyonipa kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Pia, kwa namna ya kipekee naishukuru familia yangu hususan mke wangu, watoto na ndugu zangu wote kwa ushirikiano na upendo ambao wamenipa na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuzishukuru Wizara na Taasisi za Serikali na wadau wote, hususan Asasi za Sekta Binafsi zikiwemo Chama cha Wadau wa Ngozi na Mazao yake; Baraza la Kilimo Tanzania; Baraza la Taifa la Biashara; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania; Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania; Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania; Chama cha Wafanyabiashara Wanawake na Vikundi vya Biashara Ndogo kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ambazo Wizara yangu inazisimamia.

Aidha, nawashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wao kwa njia ya kutoa maoni na mapendekezo yao kupitia vyombo vya habari na wengine kutoa malalamiko yao moja kwa moja kuhusiana na utendaji wa Wizara. Maoni yao yamesaidia kuboresha utendaji wa Wizara. Ni mategemeo yangu kuwa katika mwaka unaofuata, wataendeleza ushirikiano waliouonesha ili kuchangia

maendeleo ya sekta na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Viwanda na Biashara nikianzia na Naibu Waziri - Mheshimiwa Gregory George Teu; Katibu Mkuu - Bi. Joyce K. G. Mapunjo; Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Shaaban R. Mwinjaka; na Wakuu wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, kwa ushirikiano wanaonipa kutekeleza majukumu ya Wizara hii. Aidha, nawashukuru wataalam na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kujituma katika kutekeleza majukumu yao. Vilevile, napenda kuwashukuru wale wote ambao kwa njia moja au nyingine tulishirikiana nao katika maandalizi ya hotuba hii ninayoiwasilisha leo. Sina budi kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara yangu kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliotangulia kutoa hotuba zao na kutoa msisitizo na kuwahamasisha Watanzania washiriki kikamilifu katika zoezi la sensa tarehe 26 Agosti, 2012. Kwa namna ya kipekee, napenda kuwahimiza wadau wote wa Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, kushiriki kikamilifu katika siku hiyo ili kuweza kuhesabiwa. Taarifa za sensa ni muhimu kwa kila mfanyabiashara, mjasiriamali, wenye viwanda na wafanyakazi na kwa maendeleo ya sekta. Kwa hiyo, Wizara ya Viwanda na Biashara inatarajia kutumia

taarifa za wadau katika kupanga na kuboresha mipango ya sekta na inawatakia kila la kheri Watanzania wote siku hiyo ya kuhesabiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara ni mojawapo ya sekta za kipaumbele katika utekelezaji wa MKUKUTA II, Kilimo Kwanza, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016), Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi wa Mwaka 2011 - 2025 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, ili kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati unaoongozwa na maendeleo ya viwanda ifikapo mwaka 2025. Ili kufanikisha azma hiyo, suala la kuongeza thamani ya mazao na bidhaa zake limepewa kipaumbele hususan katika Mkakati Unganishi wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda *(Intergrated Industrial Development Strategy)* ulioandaliwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, ukuaji wa Sekta ya Viwanda ulikua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.9 mwaka 2010/2011. Pamoja na ukuaji wa sekta kuwa chini ya matarajio ya sera, mikakati na maazimio mbalimbali ya kitaifa, mchango wake katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 9.6 mwaka 2010/2011 na kufikia asilimia 9.7 mwaka 2011/2012. Ongezeko dogo la mchango wa sekta ni pamoja na matokeo ya mdororo wa uchumi duniani na mgao wa umeme nchini uliosababisha ukuaji wa sekta kupungua. Hata hivyo, kutokana na jitihada zinazoendelea za Serikali za kuimarisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa

Miaka Mitano uliobainisha maeneo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na Sekta ya Viwanda inategemea kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011, uzalishaji katika baadhi ya viwanda kama vile vya konyagi, sigara, pombe ya kibuku, bia na chuma uliongezeka. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizo katika soko la ndani. Uzalishaji wa konyagi uliongezeka kwa asilimia 38.0 kutoka lita 11,186,000 mwaka 2010 hadi lita 15,432,000 mwaka 2011. Aidha, uzalishaji wa pombe ya kibuku uliongezeka kwa asilimia 11.6 kutoka lita 21,037,000 mwaka 2010 hadi lita 23,474,000 mwaka 2011. Uzalishaji wa mabati uliongezeka kwa asilimia 7.9 kutoka tani 71,276 mwaka 2010 hadi tani 76,912 mwaka 2011. Uzalishaji wa bia uliongezeka kutoka lita 242,689,000 mwaka 2010 hadi lita 323,393,000 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 33.3. Uzalishaji wa sigara uliongezeka kutoka sigara milioni 6,181 mwaka 2010 hadi kufikia sigara milioni 6,630 sawa na ngezeko la asilimia 7.3. Uzalishaji wa chuma uliongezeka kwa asilimia 19.7 kutoka tani 33,384 mwaka 2010 hadi tani 39,955 mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeshirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Duniani *(UNIDO)* katika nyanja mbalimbali zinazolenga kuongeza ufanisi wa Sekta ya Viwanda. Kufuatia ushiriki wa Wizara katika Mikutano ya Nchi Maskini Duniani *(LDC)* na Mkutano Mkuu wa *UNIDO (UNIDO General Conference)* iliyoandaliwa na *UNIDO* ili kujadili maendeleo na changamoto za Sekta ya

Viwanda, Wizara iliweza kujadiliana na viongozi wa *UNIDO* na kukubaliana juu ya miradi ya kutekelezwa kwa ushirikiano.

Miradi hiyo ambayo tayari imeanza, ni Mradi wa Kujenga Uwezo wa Wizara na Wadau wake kwa kufanya uchambuzi wa Sera za Viwanda na zinazoendana na sera hiyo; Mradi wa *Industrial Upgrading and Modernisation* unaolenga kusaidia kuboresha ufanisi wa viwanda hasa vidogo na vya kati ambavyo vinahitaji msaada kidogo ili kuweza kuuza bidhaa zake katika masoko ya nje. Miradi mingine ni wa Kujenga uwezo wa wanaviwanda katika uzalishaji wa bidhaa bora na kuwaunganisha na masoko makubwa ya nje *(Subcontracting and Partnership Exchange - SPX)* unaotekelezwa chini ya *TCCIA*.

Vilevile Mradi wa *Africa Agro-processing and Agri-business Development Initiative (3ADI)* ambao kwa Tanzania unalenga uongezaji thamani mazao ya korosho, nyama na ngozi ili kuchochea utekelezaji wa Kilimo Kwanza. Pia Mradi wa Kutathmini Maendeleo ya Viwanda nchini unaotekelezwa kwa kushirikiana na *National Bureau of Statistics (NBS)* na Shirikisho la Wanaviwanda Tanzania *(CTI)* kwa lengo la kuwezesha kupata takwimu sahihi za Sekta ya Viwanda kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa mwongozo katika kupanga mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kushirikiana na Sekta Binafsi kwa kuandaa vikao vya kisekta kujadili maendeleo na changamoto za sekta husika. Vikao hivyo vilitoa mapendekezo Serikalini ya

kisera na mfumo wa kodi. Sekta hizo ni pamoja na nguo na mavazi; ngozi na bidhaa za ngozi; chuma na uhandisi; kemikali; chakula na vinywaji; karatasi na vifungashio; mafuta ya kula na sabuni. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mikutano ya *EAC, SADC* na *UNIDO/CAMI* ya kuandaa sera na mikakati ya kuendeleza Sekta ya Viwanda katika Jumuiya hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imeendelea kutoa mchango mkubwa katika ajira na hadi kufikia Aprili, 2012 imechangia asilimia 23.4 na imetoa ajira zipatazo 5,000,000. Aidha, mchango wa sekta katika Pato la Taifa kwa sasa umefikia asilimia 27.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011, mchango wa Sekta ya Biashara kwa ujumla ulikua kwa asilimia 8.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.2 mwaka 2010. Aidha, mchango wa sekta katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 12.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 12.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji huo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa fursa za masoko kwa bidhaa na uboreshaji wa mazingira ya biashara. Fursa hizo ni pamoja na zile zitokanazo na masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Ulaya, Asia, Marekani na Mashariki ya Kati. Thamani ya mauzo ya bidhaa zetu kupitia fursa hizo kwa ujumla yaliongezeka. Kwa mfano, mauzo ya bidhaa katika Soko la Ulaya yaliongezeka kutoka Dola ya Marekani milioni 1,151.1 mwaka 2010, na kufikia Dola ya Marekani milioni

1,382.0 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 20.1. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenye Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika iliongezeka kutoka Dola ya Marekani milioni 625.1 mwaka 2010 na kufikia Dola ya Marekani milioni 1,158.9 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 85.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya Tanzania kwenda nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yalikuwa Dola ya Marekani milioni 352.4 mwaka 2011 ikilinganishwa na Dola ya Marekani milioni 450.0 mwaka 2010 sawa na pungufu ya asilimia 21.7. Kushuka kwa mauzo yetu kwenye Soko la *EAC* kulichangiwa na baadhi ya changamoto ikiwemo tatizo la ukosefu wa umeme kwa kipindi husika ambapo viwanda vingi vilizalisha chini ya uwezo na vilevile, kuzuiwa uuzaji nafaka nje ya nchi, kwani nafaka ni mojawapo ya bidhaa inayouzwa kwa wingi soko la Jumuiya na hasa nchi ya Kenya.

Mauzo katika Bara la Amerika nayo yaliongezeka na kufikia Dola ya Marekani milioni 59.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na Dola ya Marekani milioni 51.0 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 17.8. Kwa upande wa Bara la Asia, mauzo yalifikia kiasi cha Dola ya Marekani milioni 1,414.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na Dola ya Marekani milioni 1,200.2 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 17.9. Bidhaa husika ni pamoja na kahawa, korosho, nguo na mavazi, pamba, vinyago, madini, samaki, na bidhaa zake, pareto na tumbaku. Bidhaa hizo huuzwa kwa masharti nafuu ya soko, yaani bila kulipa ushuru na bila ukomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje ziliongezeka kutoka Dola ya Marekani milioni 7,165.5 mwaka 2010 hadi kufikia Dola ya Marekani milioni 9,827.5 mwaka 2011, ikiwa ni ongezeko la asilimia 37.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta na ununuzi wa mitambo ya kufua umeme ili kukabiliana na tatizo la umeme lililojitokeza mwaka 2011. Mchanganuo unaonyesha kuwa kulikuwa na ongezeko katika uagizaji wa bidhaa za uwekezaji na usafiri, bidhaa za kati na bidhaa za kawaida ikiwa ni pamoja na nafaka. Vilevile, kwa wastani, bei za bidhaa katika soko la dunia nazo zilipanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa za kukuza mitaji zilizoagizwa kutoka nje kwa mwaka 2011 zilikuwa na thamani ya Dola ya Marekani milioni 3,560.5 ikilinganishwa na Dola ya Marekani milioni 2,715.2 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 31.1. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa mitambo kwa ajili ya shughuli za uwekezaji katika Sekta ya Gesi Asilia na Mafuta ya Petroli. Uagizaji wa mitambo uliongezeka kwa asilimia 49.1 hadi Dola ya Marekani milioni 1,794.3 mwaka 2011 ikilinganishwa na Dola ya Marekani milioni 1,203.4 mwaka 2010. Thamani ya uagizaji wa vifaa vya usafirishaji iliongezeka kwa asilimia 11.9 kufikia Dola ya Marekani milioni 1,008.5 mwaka 2011 kutoka Dola ya Marekani milioni 901.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uagizaji wa vifaa vya ujenzi, kulikuwa na ongezeko la asilimia 24.1 kufikia Dola ya Marekani milioni 757.7 mwaka 2011

ikilinganishwa na Dola ya Marekani milioni 610.6 mwaka 2010. Hii inaashiria mwelekeo mzuri katika kuwezesha uchumi kuimarika na kukua. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati za viwandani nao uliongezeka kwa asilimia 21.9 kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na Dola ya Marekani milioni 609 kwa mwaka 2010. Ni dhahiri kuwa bidhaa zinazotumika kuzalisha bidhaa zaidi viwandani na pembejeo za kilimo navyo vina mwelekeo mzuri wa kukua hivyo kuliwezesha Taifa kuuza bidhaa zilizoongezewa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, kwa jumla kumekuwa na ongezeko la bei kwa mazao makuu ya chakula ya mahindi, mchele, maharage, ngano, sukari, ulezi na mtama. Wastani wa bei ya jumla kwa gunia la mahindi la kilo 100 ilipanda kutoka Sh. 34,247/= mwaka 2010/2011 na kufikia Sh. 43,309/= mwaka 2011/2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 26.

Aidha, bei ya gunia la maharage la kilo 100 ilipanda kutoka Sh. 109,537/= hadi Sh. 123,606/= sawa na ongezeko la asilimia 13. Kupanda kwa bei ya mazao makuu ya chakula kulichangiwa na kuongezeka kwa bei ya mafuta ya petroli kulikosababisha ongezeko la gharama za uzalishaji na usafirishaji, na ongezeko la mahitaji ya mazao hayo ikilinganishwa na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, bei ya mkulima kwa mazao ya biashara ya chai, kahawa, mkonge, pamba, korosho ghafi na miwa iliongezeka. Bei iliyolipwa kwa mkulima kwa zao

la chai katika mwaka 2011/2012 ilikuwa wastani wa Sh. 196/= kwa kilo ikilinganishwa na wastani wa Sh. 126/= kwa mwaka 2010/2011. Aidha, kwa mwaka 2011/2012, bei ya mkulima kwa zao la kahawa ya *Mild Arabica*, ilipanda kutoka wastani wa Sh. 3,350/= hadi Sh. 3,903/= ikiwa ni ongezeko la asilimia 17. Bei ya kahawa aina ya Robusta iliongezeka kutoka Sh. 900/= hadi Sh. 941/= ikiwa ni ongezeko la asilimia tano.

Vilevile, bei ya mkonge kwa wakulima ilipanda kutoka wastani wa Sh. 921.40 mwaka 2010/2011 hadi Sh. 1,114/= kwa kilo mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 21. Bei ya Pamba mbegu ilipanda kutoka wastani wa Sh. 650/= mwaka 2010/2011 mpaka Sh. 1,000/= kwa kilo mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 53.8, wakati bei ya korosho ghafi daraja la kwanza ilipanda kutoka wastani wa Sh. 800/= mwaka 2010/2011 mpaka Sh. 1,200/= mwaka 2011/2012 kwa kilo, sawa na ongezeko la asilimia 50.

Aidha, bei ya miwa kutoka kwa wakulima wadogo imepanda kutoka Sh. 54,103/= hadi Sh. 56,240/= kwa tani sawa na ongezeko la 4%, kwa Kiwanda cha Kilombero, na kwa Kiwanda cha Mtibwa bei iliongezeka kutoka Sh. 38,000/= hadi Sh. 38,337/= kwa tani sawa na ongezeko la 1% ambapo kwa Kiwanda cha Kagera bei iliongezeka kutoka Sh. 33,600/= hadi Sh. 35,000/= kwa tani sawa na ongezeko la 4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa bei za rejareja kwa bidhaa nyingi za viwandani umeonesha kupanda. Bei ya rejareja ya sukari ilipanda kutoka wastani wa Sh. 1,700/= hapo mwaka 2010/2011 hadi

kufikia Sh. 2,200/= mwaka 2011/2012 kwa kilo. Bei hiyo ilipanda zaidi katika robo ya kwanza ya mwaka 2012 hadi kufikia Sh. 2,500/= katika maeneo mengi nchini. Kufuatia jitihada za Serikali za kuruhusu uingizaji wa sukari kutoka nje, ilisaidia bei ya sukari kushuka hadi kufikia wastani wa Sh. 2,200/= kwa kilo. Serikali ina mkakati wa makusudi wa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya na kuongeza uzalishaji wa sukari. Bei ya rejareja ya saruji ya mfuko wa kilo 50 katika masoko nchini ilikuwa wastani wa Sh. 16,940/= mwezi Desemba, 2011 na kushuka hadi Sh. 16,265/= mwezi Machi, 2012. Vilevile, bei ya bati la geji 30 ilipanda kutoka wastani wa Sh. 16,000/= mwaka 2010/2011 hadi kufikia wastani wa Sh. 19,000/= mwezi Machi, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, kumekuwa na ongezeko la bei ya mifugo kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Wastani wa bei ya jumla ya ng'ombe daraja la pili iliongezeka kutoka Sh. 393,853/= mwaka 2010/2011 hadi Sh. 427,438/= mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la 9%. Aidha, bei ya ng'ombe daraja la tatu ilipanda kutoka Sh. 285,359/= mwaka 2010/2011 hadi Sh. 328,151/= mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 15. Bei ya mbuzi ilipanda kutoka Sh. 38,805/= mwaka 2010/2011 hadi Sh. 42,323/= mwaka 2011/2012 sawa na ongezeko la 9%, wakati bei ya kondoo ilipanda kutoka Sh. 32,677/= hadi Sh. 37,078/= katika kipindi hicho sawa na ongezeko la asilimia 13. Kupanda kwa bei hizo kumechangiwa na ongezeko la ubora wa mifugo, gharama za usafirishaji na ongezeko la mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake, imeendelea kutekeleza malengo endelevu ya Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2015. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Wizara *(Strategic Plan 2011/2012 – 2016/2017)* ambao kwa sehemu kubwa umezingatia utekelezaji wa maelekezo ya Ilani. Pamoja na changamoto zilizojitokeza, mafanikio yaliyopatikana hadi sasa kwa kutumia fursa zilizopo katika kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi *(PPP)* Katika Uwekezaji na Biashara Katika Soko la Ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje *(EPZA)* imeandaa utaratibu wa kuanzisha Kituo Kimoja cha Huduma za Uwekezaji *(One Stop Services Centre)* katika eneo Maalum la Uwekezaji la Benjamin William Mkapa, kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma zote muhimu zinazohusika na uwekezaji wa viwanda.

Aidha, baada ya utaratibu huo kukamilika, Mamlaka sasa inawasiliana na Wizara husika kupata Maafisa wa kutoa huduma katika Kituo hicho. Pia, Wizara inaendelea kushirikiana na Taasisi zinazohusika na utoaji wa mikopo hususan Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* ili kurahisisha upatikanaji wa mitaji ya kuwekeza katika Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko

na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Vilevile, Wizara kupitia *SIDO* na *TanTrade* imeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali mbalimbali kuhusu uzalishaji wa bidhaa zenye ubora ili kuweza kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa 20 imekwishatenga maeneo maalum ya uwekezaji ili yawekewe miundombinu ya msingi itakayovutia Sekta Binafsi kujenga viwanda na kufanya biashara katika maeneo hayo. Hatua hiyo itapunguza changamoto ya upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wanaotaka kuanzisha viwanda nchini. Aidha, kupitia Sheria za Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje *(EPZ)* na Maeneo Maalumu ya Uchumi *(SEZ),* Serikali imebainisha vivutio mbalimbali ikiwa ni pamoja na nafuu za kodi ili kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uwekezaji. Mikoa ambayo bado haijatenga maeneo hayo ni ile mipya ambayo ni Katavi, Simiyu, Geita na Njombe. Mamlaka ya *EPZ* inawasiliana na Mikoa hiyo ili nayo iweze kutenga maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga na kuimarisha ujuzi katika biashara na kuweka msukumo zaidi katika kutumia fursa za masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Programu ya *Kaizen* itakayotoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi, usimamizi wa shughuli za viwanda na kuongeza ubora wa bidhaa. Hii ni baada ya kukamilika kwenye hatua ya majaribio kwa Sekta Ndogo ya Nguo ambapo wajasiriamali 113 waliopata mafunzo wameweza kuboresha uzalishaji wa bidhaa

na kumudu ushindani. Maandalizi yanaendelea kwa ajili ya Programu hiyo kutekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Japan kwenye Sekta ya Viwanda vya Usindikaji Mazao ya Kilimo kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma kuanzia mwezi Septemba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Viwanda vya Ngozi, Chuo cha *DIT* Kampasi ya Mwanza kimeanza kutoa mafunzo ya muda mfupi na kinaendelea kukamilisha maandalizi ya kutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya *leather technologists.*

Aidha, Wizara kupitia *SIDO* imeanzisha Kituo cha Mafunzo na Uzalishaji wa bidhaa za ngozi Dodoma. Wizara imeendelea kuwezesha na kuimarisha vituo kama hivyo ambavyo viko chini ya Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania *(LAT)* vilivyoko Mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji *(SEZ)* ya mwaka 2006 ilipitishwa na Bunge na kwa sasa Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imekamilisha uandaaji wa rasimu ya Kanuni za Sheria hiyo. Kukamilika kwa Kanuni hizo kutaufanya mfumo wa *SEZ* uanze kutumika rasmi hivyo kupanua wigo wa uwekezaji katika maeneo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuimarisha kifedha Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* ili kiwe chombo madhubuti cha kuchochea mapinduzi ya viwanda nchini kwa kutoa mikopo ya muda mrefu na riba nafuu kwa wawekezaji wakubwa, wa kati na wadogo nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelenga kuiongezea *TIB* mtaji wa Shilingi bilioni 500 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010 ili kuimarisha uwezo wa utoaji mikopo ya muda mrefu kwa wawekezaji hususan kwenye kilimo na viwanda. Hadi sasa, Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 60 kwenda *TIB*. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 10 zimetolewa katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuwekeza katika Mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma, Chuma cha Liganga na Viwanda vya Kemikali na Mbolea katika Kanda za Maendeleo Kikiwemo Kiwanda cha Mbolea aina ya *urea* Mkoani Mtwara na kuwezesha Kiwanda cha Minjingu kuzalisha mbolea bora ya *NPK* na *MPR* ili kufikia lengo lililowekwa.

MheshimiwaMwenyekiti, kama Bunge lako Tukufu lilivyoelezwa katika hotuba ya mwaka 2011/2012, mwezi Januari, 2011 Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* lilifanikiwa kumpata mwekezaji katika Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na wa Chuma cha Liganga. Kampuni ya *Sichuan Hongda Group (SHG)* ya China. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 21 Septemba, 2011 *NDC* na Kampuni ya *Sichuan Hongda Group* walisaini Mkataba wa Ubia

ambapo Kampuni ya Ubia iitwayo *Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL)* imeanzishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi husika kwa mfumo unganishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 20 ya hisa za kampuni ya ubia zinamilikiwa na Serikali kupitia *NDC* na asilimia 80 inamilikiwa na Kampuni ya *SHG*. Miliki ya hisa za Serikali inatokana na mashapo ya madini ya mawe na chuma *(free carried interest).* Hivyo, Serikali haiwajibiki kuwekeza ili kumiliki hisa hizo wala kulipa fedha taslimu. Mkataba unatoa fursa kwa Serikali kuongeza hisa zake hadi kufikia asilimia 49 baada ya Kampuni ya *SHG* kulipa deni litakalokuwa limekopwa.

Aidha, kulingana na mkataba huo, *SHG* itawekeza Dola ya Marekani bilioni 3.0 kwenye miradi hiyo. Kampuni ya ubia itaanza utekelezaji wa miradi hiyo kwa kufanya uhakiki wa mashapo ya makaa ya mawe na upembuzi yakinifu wa mashapo ya chuma cha Liganga. Zoezi la uhakiki wa makaa ya mawe limeanza mwezi Julai, 2012 na linatarajiwa kumalizika mwezi Machi, 2013. Kwa upande wa chuma cha Liganga, uchorongaji wa kutafiti wingi na ubora wa madini ya chuma unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 12 - 18 kuanzia Agosti, 2012. Inategemewa kuwa, uzalishaji wa umeme MW 300 kutokana na makaa ya mawe ya Mchuchuma utaanza mwaka 2015 na kufikia MW 600 mwaka 2017/2018 na uzalishaji wa chuma kutokana na madini ya chuma ya Liganga unatarajiwa kuanza mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha wananchi ili kunufaika na fursa za miradi mikubwa kama Mchuchuma na Liganga, Wizara kupitia *NDC* imeandaa utaratibu wa jinsi ya kuwahudumia wananchi watakaopisha utekelezaji wa miradi katika Wilaya ya Ludewa tangu mwaka 2009 kwa kushirikiana na Halmashauri husika ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maeneo mengine. Tayari maeneo mapya yamekwishatengwa na elimu kuhusu utaratibu wa kuthaminisha mali zilizopo ndani ya maeneo ya mradi na ulipaji fidia imeishatolewa.

Aidha, mwezi Desemba, 2011 *NDC* iliendesha warsha kwa Halmashauri ikieleza fursa zitokanazo na miradi hiyo. Tayari *NDC* imepata fedha kutoka *Regional Spatial Development Initiative Programume (RSDIP)* kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Kusini *(DBSA)* kwa ajili ya kuajiri mtaalamu atakayeshirikiana na wananchi kuandaa Mpango Shirikishi kunufaisha wananchi wa Halmashauri ya Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* imekamilisha tafiti za kisayansi kuhusu Kemia, Haidrolojia, Ekolojia na *Hydrodyanamics* za Ziwa Natron ili kuepusha athari katika mazingira wakati wa utekelezaji wa mradi wa kuzalisha magadi *(soda ash).* Mradi wa Magadi *(Soda Ash)* unatarajiwa kuzalisha tani 500,000 za Magadi kwa mwaka kwa kuanzia.

Aidha, *NDC* wamefanya uchorongaji katika eneo la Engaruka lililoko kilometa 50 kutoka Ziwa Natron ambalo lina mashapo yenye magadi mengi. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huo unategemea

uboreshaji wa miundombinu ya reli kati ya Tanga na Arusha, ujenzi wa reli mpya kati ya Arusha na Ziwa Natron na upanuzi wa Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuimarisha uzalishaji mali viwandani kwa kuvifufua na kuviendeleza kwa teknolojia ya kisasa viwanda vyote ambavyo viliuzwa huko nyuma kisha kutelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008, Wizara ilifanya uperembaji katika viwanda vilivyobinafsishwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Ripoti ya uperembaji huo ilibainisha kuwa kati ya viwanda 74 vilivyobinafsishwa, viwanda 42 utendaji wake ni mzuri na wa kuridhisha na vimewekeza zaidi ya ahadi za mikataba ya mauzo. Viwanda 15 vinalegalega na vimewekeza pungufu ya mkataba wa mauzo, na viwanda 17 vimesimamisha uzalishaji na kufungwa. Viwanda 45 viliuzwa mali moja moja *(asset stripping*) na hivyo kuondolewa katika orodha ya viwanda. Mwezi Juni, 2011, Wizara ya Viwanda Biashara kwa kushirikiana na *Consolidated Holdings Corporation (CHC)* na wadau wengine ilifanya uchambuzi wa kina wa viwanda na mashirika yaliyobainishwa kuwa yamefungwa au yanakabiliwa na matatizo makubwa.

Kwa sasa, *CHC* kwa kushirikiana na wadau husika ikiwemo Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha wameanza majadiliano na wawekezaji ambao hawakuzingatia mikataba ya mauzo ili kukubaliana hatua za kuchukua na kuhakikisha viwanda vinafufuliwa na kuanza uzalishaji ili kuchangia katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuboresha vivutio kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotumia malighafi mbalimbali zilizopo nchini vikiwemo viwanda vya nguo, ngozi, usindikaji matunda, mbogamboga na usanifu wa madini na vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya utoaji huduma katika maeneo maalum ya uwekezaji yameboreshwa. *EPZA* kwa sasa inaweza kutoa leseni kwa mwekezaji kwa muda wa siku mbili endapo vigezo vingine vyote vimezingatiwa.

Aidha, Wizara kwa kushirikisha wadau wa sekta, ilifanya uchambuzi wa changamoto zinazoikabili Sekta ya Nguo na Mavazi na kuandaa mapendekezo Serikalini kwa lengo la kupata maamuzi. Moja ya mapendekezo hayo ni kuondoa *VAT* katika bidhaa za nguo na mavazi zinazozalishwa hapa nchini, ambapo maamuzi yametolewa ya kupunguza *VAT* katika nguo kwa kutumia pamba inayozalishwa hapa nchini kuanzia Julai, 2012.

Vile vile Wizara imekamilisha maandalizi ya mkakati wa Sekta ndogo ya Nguo na Mavazi ambao utekelezaji wake utaanza mwezi Agosti, 2012 kwa Wizara kuunda kitengo *(Textile Development Unit)* cha kusimamia utekelezaji wa Mkakati wake. Vilevile, mkakati wa kuendeleza Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendelea kuhamasisha uzalishaji na uimarishaji wa maeneo maalum ya uzalishaji kwa mauzo nje *(EPZ)* na maeneo maalum ya kiuchumi *(SEZ).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa ajili ya Kuuza Bidhaa Nje *(EPZA)* imehamasisha na kutoa mafunzo ya uwekezaji kitaifa na kimataifa kuvutia wawekezaji nchini. Kutokana na uhamasishaji huo, jumla ya wawekezaji 59 wameanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa kwa soko la nje. Jumla ya mtaji wa Dola ya Marekani milioni 792.2 umewekezwa, ambapo mauzo nje ni jumla ya Dola ya Marekani milioni 440.2. Ajira za moja kwa moja zilizotokana na uwekezaji huo ni 16,105.

Aidha, katika eneo la *Kamal EPZ* lililoko Bagamoyo, viwanda viwili tayari vimeanza kazi. Viwanda hivyo ni kiwanda cha kusindika mazao ya kilimo *(Kamal Agro Ltd)* na cha kutengeneza gesi ya viwandani ya *Acetylene*. Ujenzi wa Kiwanda cha kuzalisha chuma pamoja na kiwanda cha kusafisha mafuta machafu cha *Kamal Refinery Ltd* uko kwenye hatua za mwisho. Viwanda vilivyopo chini ya *EPZA* vimebainishwa katika kitabu cha Mafanikio ya Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuendelea kutekeleza mkakati unganishi wa kufufua na kuendeleza Viwanda vya Ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Viwanda vya Ngozi. Kwa

ujumla kuna viwanda 13 vya kusindika ngozi nchini vikiwa na uwezo wa kusindika futi za mraba 73,977,000 kwa mwaka. Kati ya hivyo, viwanda vitano vya *Himo Tanneries* - Kilimanjaro, *Moshi Leather Industries* - Kilimanjaro, *Afro Leather Industries* – Dar es Salaam, *Lake Trading Co. Ltd* – Pwani na *ACE Leather Industry* – Morogoro, ndivyo vinafanya kazi.

Pia viwanda vipya vitano vimejengwa lakini havijaanza kufanya kazi kutokana na kushindwa kupata ngozi za kutosha kunakosababishwa na ushindani usio haki katika biashara ya ngozi ghafi. Viwanda hivyo ni *Open Enterprises (Footwear Manufacturing,* Dar es Salaam; Morogoro *Super Leather Ltd (Leather Product Manufacturing)*, Morogoro; *Leather Products Manufacturing* Mbagala, Dar es Salaam; *Petrocity Tannery (Leather Processing),* Mwanza na *Morogoro Leather Community (Leather Products Manufacturing)*, Morogoro.

Aidha, miradi sita mipya ya viwanda vya kusindika ngozi na bidhaa za ngozi ambavyo viko katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni pamoja na *Tanmbuzi Co. (leather Processing),* Kilimanjaro; *Arusha City Complex Co. Ltd. (Leather Processing),* Arusha; *Bhat Bangla Agritech (T) Ltd. (Leather products Manufacturing),* Dodoma; *Bhat Bangla Agritech (T) Ltd (leather Processing),* Dodoma; *JAET Tannery Co. Ltd*. (Mwanza) na *Zhung FU International Co. Ltd. (Leather Production and Plastic Footwear,* Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukosefu wa ngozi za kutosha na ushindani usio wa haki kati ya

wafanyabiashara wanaouza ngozi ghafi nje na wenye viwanda, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta iliwasilisha mapendekezo Serikalini ya kuzuia uuzaji wa ngozi ghafi nje ya nchi au kuongeza ushuru unaotozwa. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa ngozi za kutosha kwa viwanda vya kusindika ngozi nchini ili kuuza ngozi zilizosindikwa na bidhaa za ngozi badala ya ngozi ghafi. Makubaliano yamefikiwa na Wizara ya Fedha kuanzia Julai, 2012, ngozi ghafi zitakazouzwa nje ya nchi zitozwe ushuru wa asilimia 90 au Sh. 900/= kwa kilo kutegemea thamani iliyo juu ikilinganishwa na asilimia 40 au Sh. 400/= kwa kilo iliyokuwa inatozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Uanzishwaji na Uendelezaji wa Vijiji vya viwanda kupitia mipango mitatu. Mpango wa kwanza ni wa kuanzisha na kuendeleza vijiji vya viwanda kama maeneo maalum ya kuhamasisha na kuchochea uwekezaji wa viwanda vya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi nchini. Katika kutekeleza mpango huo, Wizara imeanza na Kanda ya Kati inayojumuisha Mikoa ya Morogoro, Dodoma na Singida; na Kanda ya Mashariki inayojumuisha Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambapo maeneo husika yamekwishabainishwa na kutengwa na Halmashauri husika. Hatua inayofuata ni ya kutekeleza taratibu za kuyatwaa maeneo hayo na kuanza kuweka miundombinu ya msingi kwa shughuli za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa pili ni wa kuwezesha wadau wa Sekta Binafsi kuyafikia na kuyakuza masoko ya ndani na nje ya nchi kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Katika mpango wa

kuwawezesha wajasiriamali wa sekta ya ngozi kutangaza bidhaa zao na kuyafikia masoko, Wizara iligharamia ushiriki wa wajasiriamali 40 katika Maonesho ya Kimataifa *DITF*, 25 katika NaneNane na 32 katika Maadhimisho ya Miaka Hamsini ya Uhuru. Vilevile, chini ya Mpango wa Kujengea Wajasiriamali wa Sekta ya Ngozi Uwezo wa Kitaalamu na Kiushindani katika Vijiji, Wizara kwa kushirikiana na *LAT, SIDO, TBS* na *TIRDO* wameendelea kutoa mafunzo ya usindikaji kwa njia ya asili na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa wajasiriamali 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuandaa Taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya maendeleo ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Maendeleo ya Viwanda unaolenga Sekta Ndogo za Viwanda umekuwa unaendelea kwa kuainisha sekta za kipaumbele ili kuwezesha utekelezaji. Sekta ndogo za kipaumbele ambazo uhamasishaji unafanyika ili kupata wawekezaji ni nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi, usindikaji mazao ya kilimo, mbolea na makaa ya mawe ya kuzalisha umeme. Aidha, rasimu ya Mpango Kabambe wa kutekeleza Mkakati Unganishi wa Maendeleo ya Viwanda iliandaliwa na kujadiliwa na kikao cha wadau kilichofanyika tarehe 19 Aprili, 2012 ili kupata maoni ya wadau. Mpango huo ukikamilika utakuwa dira nzuri ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya viwanda kwa muda mfupi, wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara ndogo napenda kuongelea yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuendeleza Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) kwa kutoa ushauri, mafunzo, mitaji na huduma za kiufundi kwa wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na zoezi la kuperemba na kutathmini shughuli za utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kulingana na malengo iliyojiwekea. Katika mwaka 2011/2012, tathmini imefanyika katika mradi wa Muunganisho Ujasiriamali Vijijini (MUVI) ulioanza kutekelezwa mwaka 2007 wenye lengo la kuchangia katika kupunguza umasikini vijijini kwa kuhamasisha wadau kujikita katika kuongeza thamani ya mazao na kupatikana kwa soko la uhakika kwa ajili ya mazao hayo. Walengwa wa mradi ni wakulima na wananchi walio vijijini ambao hupata mafunzo ya kilimo cha kisasa, masoko, teknolojia rahisi na umuhimu wa kuongeza thamani na kuwaunganisha na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mradi unatekelezwa kwa kuzingatia uboreshaji wa mawasiliano kwa ajili ya kubadilishana taarifa za masoko na kujenga uwezo wa Taasisi zinazohusika katika baadhi ya Mikoa nchini. Mikoa hiyo ni Ruvuma (Namtumbo, Mbinga na Songea Vijijini), Mwanza (Sengerema, Ukerewe na Kwimba), Tanga (Muheza na Handeni), Iringa (Kilolo na Iringa

Vijijini), Manyara (Simanjiro, Hanang na Babati), Pwani (Rufiji, Mkurunga na Bagamoyo) na Njombe. Mradi umewezesha kuundwa jumla ya vikundi 319 vyenye wanachama 15,482. Mfumo wa usambazaji mbegu bora umeimarishwa kupitia Kampuni 20 zilizopatikana kiushindani na wakulima 117 wa mazao mchanganyiko wamepata mafunzo kupitia mashamba darasa ya matumizi ya mbegu bora. Utaratibu huo umeweza kutoa mkulima bora kutoka Wilaya ya Handeni na kuzawadiwa trekta la *power tiller.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuongeza mchango wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo *(SMEs)* katika Pato la Taifa kutoka asilimia 33 hivi sasa kufikia asilimia 40 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi, Wizara haikuwa na takwimu za uhakika za ukubwa na mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika pato la Taifa na ajira. Kufuatia kukamilika kwa utafiti *(baseline Survey)* wa Sekta hiyo, imebainika kuwa mchango halisi wa sekta katika Pato la Taifa kwa sasa ni asilimia 27.9 na inachangia asilimia 23.4 katika ajira ya Taifa. Taarifa hizo zinabaini kuwepo zaidi ya jasiriamali milioni tatu ambazo zinaajiri zaidi ya Watanzania milioni tano. Takwimu hizo zitaiwezesha Wizara kupanga mipango makini ya kuendeleza sekta.

Aidha, miradi na Programu mbalimbali zinatekelezwa vijijini ikiwepo Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) na Wilaya Moja Bidhaa Moja *(ODOP)* ili kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja, pato la Taifa na uchumi kwa ujumla. Wizara pia, iko katika

hatua za awali za kuanzisha kongano za viwanda vidogo *(Industrial Clusters)* katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida, Manyara na Kilimanjaro ili kuinua kipato cha wananchi kwa kukuza shughuli za wajasiriamali wadogo na kuwezesha wengi kuanzisha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuendeleza, kuzalisha na kusambaza teknolojia za kuongeza thamani mazao kupitia Vituo vya Maendeleo ya Teknolojia vya *SIDO* vilivyopo Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Iringa na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika mwaka 2011/2012, jumla ya teknolojia mpya 174 zimetafutwa kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya miradi ya uzalishaji. Aidha, *SIDO* kupitia Vituo vyake vya Uendelezaji wa Teknolojia vilivyopo Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Lindi, na Kigoma iliwezesha utengenezaji wa mashine mpya za aina mbalimbali 604 na vipuri 2,472 zikiwemo za kubangua korosho na karanga, kupukuchua na kukoboa mahindi na mpunga, na kusindika alizeti. Teknolojia hizo zimewezesha wajasiriamali kuongeza tija katika uongezaji thamani ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kutoa elimu na kuwajengea uwezo wakulima wa kusindika mazao kabla ya kuyauza kama vile usindikaji wa asali, utengenezaji wa mvinyo, utengenezaji wa juisi pamoja na ufungashaji wa bidhaa kwa kutumia teknolojia ya Kituo cha *TBS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, *SIDO* imetoa mafunzo kwa Wajasiriamali ili kuwaimarisha katika kuendesha na kuendeleza shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji. Mafunzo yaliyotolewa ni usindikaji wa nafaka na matunda kwa wajasiriamali 1,764, ujuzi maalum wa usindikaji wa mafuta ya alizeti, utengenezaji sabuni, mishumaa, chaki, utengenezaji wa mizinga ya kisasa na usindikaji wa asali ulitolewa kwa wajasiriamali 2,054 kupitia kozi 143 na wajasiriamali 63 wa usindikaji wa ngozi na bidhaa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wasindikaji wa mazao 840 walipata vifungashio katika Mikoa yote. Vilevile, jumla ya wajasiriamali 8,880 kupitia kozi 368 wamepata mafunzo ya maarifa na stadi za kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali. Mafunzo hayo yamewawezesha wajasiriamali kufanya kazi kwa kujiamini na kuweza kuzalisha bidhaa bora zenye kukubalika na soko la ndani na nje na hususan katika soko la Afrika Mashariki na *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwaunganisha wajasiriamali wadogo na Makampuni makubwa yaliyo tayari kununua bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* imeweza kuwaunganisha Wajasiriamali wadogo na Makampuni makubwa na ya kati ambapo jumla ya biashara za wajasiriamali wadogo 228 ziliunganishwa na viwanda vya kuchambua na kukamua mafuta ya pamba na viwanda vya kusindika samaki. Pia, Makampuni kama Katani Limited, Handeni

*Mini Refinery,* SUMA JKT, *Nyanza Mine, Tobacco Authority, Prume Timber Ltd, Kampala University, Intermec Engineering, Katapala Engineering, Safari Co. Ltd; Mohamed Enterprises, Lavena U-Tum Supermarkets na* Kiwanda cha Bisikuti katika Mikoa ya Tanga, Arusha, Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Rukwa na Tabora ikilinganishwa na wajasiliamali 58 waliounganishwa na Makapuni hayo mwaka 2010/2011. Wajasiriamali wamehamasishwa kuzalisha bidhaa zenye ubora na kupata masoko ya uhakika kwenye Makampuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kujenga Uwezo wa *SIDO* na Kuwatafutia Vyanzo vya Fedha ili Kuwawezesha Kutoa Mafunzo ya Usindikaji kwa Wajasiriamali Wadogo. Aidha, Kuifanyia Mapitio Sheria Iliyoanzisha SIDO ili Iendane na Mahitaji ya Uchumi wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara imefanya jitihada mbalimbali katika kuijengea uwezo *SIDO*, licha ya ufinyu wa Bajeti ya Serikali. Kwa mfano, *SIDO* ilipata fedha za maendeleo Shilingi milioni 860, mwaka 2009/2010, Shilingi milioni 542 mwaka 2010/2011 na Shilingi bilioni 1.8 mwaka 2011/2012. *SIDO* pia, imekuwa ikifanya kazi kwa kushirikiana na Sekta Binafsi pamoja na Washirika wa Maendeleo kama vile *IFAD* kupitia mradi wa *MUVI, KOICA* na *EU* katika kutoa mafunzo na upatikanaji wa vitendea kazi. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imepeleka Maofisa 11 wa *SIDO* katika mafunzo na semina mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kitaalamu wa kuwahudumia

wajasiriamali wadogo kwa ufanisi zaidi. Katika mwaka 2012/2013 *SIDO* imetengewa Sh. 3,645,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti,katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Serikali kupitia *SIDO* imeendelea kutoa huduma za kuendeleza ujasiriamali nchini ambapo jumla ya wajasiriamali 10,964 walipata mafunzo mbalimbali na wajasirimali 16,138 walipata huduma za ushauri na ugani.

Aidha, wajasiriamali 1,518 waliwezeshwa kushiriki maonesho ya bidhaa za wajasiriamali na mikopo 4,387 yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.18 ilitolewa kupitia Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi *(National Enterpreneurship Development Fund (NEDF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendeleza Miundombinu ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha Manispaa na Halmashauri za Miji na Vijiji kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo. Vilevile, Wizara kupitia *SIDO* inaendelea na maandalizi ya awali ya kujenga miundombinu ya kuanzisha kongano ya wahunzi Wilayani Kwimba na utaratibu wa umiliki unakamilishwa. Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine wakiwemo Mamlaka ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi katika kutenga na kuendeleza maeneo kwa ajili ya wenye viwanda vidogo na biashara ndogo ambapo maeneo 23 tayari yametengwa. *EPZA* pia, inatenga maeneo ya wajasirimali wadogo katika maeneo ya uwekezaji yanayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhamasisha Matumizi ya Fursa za Masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa zikiwemo Fursa za Masoko ya *AGOA, EBA*, China, Japan, Canada na India ili Kukuza Biashara ya Nje kwa Kiwango Kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* Wizara imeendelea na uhamasishaji wa fursa za masoko baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Biashara wa Wilaya, Manispaa na Miji kuhusu fursa za masoko ya nje ikiwa ni pamoja na Sheria na kanuni za kuingia masoko hayo.

Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Misaada ya *Southern Africa Trade Hub-SATH* imetoa mafunzo kwa wadau 100. Jitihada nyingine ni kuwawezesha wajasiriamali kushirikisha wadau katika fursa za masoko hayo, ni pamoja na yale ya upendeleo maalum yanayotolewa chini ya mpango wa *AGOA* na *EBA*, China, Japan, Canada na India; na yale ya kikanda ya *SADC* na *EAC*.

Vilevile, Wizara imekuwa ikihusisha wadau hususan jamii ya wafanyabiashara katika majadiliano ya kikanda na kimataifa, misafara na maonesho ya kibiashara ili kujenga ufahamu wa mahitaji na changamoto za masoko ya ndani na nje. Pamoja na uhamasishaji huo, bidhaa zinazolenga masoko hayo zimeboreshwa na hivyo, kuongeza mauzo katika masoko hayo kama ilivyofafanuliwa katika aya 18 - 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kutoa Mafunzo ya Kuwajengea Uwezo Wajasiriamali Kuhusu Mbinu za Kuyafikia Masoko ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imefanikiwa kuwahamasisha na kuwapa mafunzo wajasiriamali 60 Kanda ya Mashariki kuhusu fursa za masoko yaliyopo katika mfumo baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa na pia masoko yanayopatikana katika Jumuiya ya Ulaya. Wajasiriamali 215 wamepata mafunzo kuhusu soko la *AGOA* na masharti yake. Wizara pia kwa kushirikiana na Sekretariati ya *SADC* imetoa mafunzo kwa wajasiriamali wapatao 90 huko Morogoro na Zanzibar kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na masharti kwenye Kanuni za Afya za Binadamu, Mimea na Wanyama *(SPS),* Vigezo vya Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin -RoO)* na Vikwazo Visivyokuwa vya Kiushuru *(Non Tarrif Barriers NTBs)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendelea na Majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Ulaya *(EU).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania na nchi wanachama wa *EAC* zinaendelea na majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Uchumi *(Economic Partnership Agreement -EPA)* kati yao na Jumuiya ya Ulaya *(EU),* yaliyolenga katika maeneo matatu; fursa za masoko, ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo na ushirikiano katika masuala ya uvuvi.

Kutokana na majadadiliano hayo, Jumuiya ya Ulaya imefungua soko lake kwa bidhaa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki kuuzwa bila kutozwa ushuru na bila ukomo *(Duty Free Quota Free)* isipokuwa kwa bidhaa za sukari na mchele ambazo zitaendelea kupewa mgao (*Quota)* katika kipindi hiki cha mpito. Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imekubaliwa kuwa nayo itafungua soko lake kwa awamu katika kipindi cha miaka 25 kwa kiwango cha asilimia 82.6 ili kuruhusu bidhaa kutoka Ulaya kuingia bila ushuru. Jumuiya ya Ulaya itazisaidia nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kifedha na kiufundi katika shughuli za uzalishaji, miundombinu na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo ya awali, majadiliano ya *EPA* yanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika maeneo ya ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo, fursa za masoko na kilimo. *EU* inashindwa kuonyesha nia dhahiri ya kuzisaidia nchi wanachama kifedha. Hii ni pamoja na kutaka kupewa upendeleo sawa pale nchi wanachama wa *EAC* zitakapotoa upendeleo zaidi kwa nchi nyingine duniani zinazoibukia kiuchumi kwa kuingia Mkataba na nchi hizo mara baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa *EPA*. Aidha, *EU* imeshikilia msimamo wa kuzitaka nchi za *EAC* kutotoza ushuru kwa bidhaa zinazouzwa katika soko lao na kutoondoa ruzuku kwa bidhaa za kilimo wanazozalisha ambazo *EAC* pia wanazalisha kwa ajili ya soko hilo. Majadiliano bado yanaendelea kwa pande zote mbili kwa lengo la kuondoa changamoto hizo kabla ya kuhitimishwa kwa majadiliano na kusainiwa kwa Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendelea na uanzishwaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Kuendelea Kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Tanzania ikiwa nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea kushiriki katika majadiliano ya kukamilisha baadhi ya vipengele katika Itifaki ya Soko la Pamoja ambayo ilisainiwa mwezi Novemba, 2009 na kuanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2010.

Hata hivyo, changamoto tuliyonayo ni kutokuwa na Sera inayoruhusu uwekezaji nje ili kutuwezesha kufaidika na fursa za uwekezaji wa mitaji katika Soko la Pamoja. Aidha, Tanzania imeendelea kushiriki katika hatua ya tatu ya mtangamano ya kuanzishwa kwa Umoja wa Fedha *(Monetary Union)* wenye lengo la kuwa na Sarafu ya Pamoja. Hatua hiyo ikikamilika itasaidia kupunguza gharama za kufanya biashara na kuwepo kwa uchumi endelevu kwa Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC)*, Tanzania imeendelea na utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya *SADC* kwa kuendelea kupunguza viwango vya ushuru hadi kufikia asilimia sifuri ilipofika mwezi Januari, 2012. Hii ina maana kuwa bidhaa ziingiazo nchi wanachama hazitozwi ushuru.

Vilevile, Tanzania inashiriki katika majadiliano ya kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa nchi za *SADC*. Aidha, nchi wanachama ikiwemo Tanzania ziko katika hatua ya awali ya kuanza majadiliano ya kufunguliana milango katika Biashara ya Huduma *(Trade in Services)* kwa kuanza na sekta sita za kipaumbele ambazo ni Mawasiliano, Fedha, Usafirishaji, Utalii, Nishati na Ujenzi. Hatua hizo zikikamilika zitapanua wigo wa biashara kwa kujumuisha biashara ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kufanya Utafiti wa kina juu ya Gharama za Kufanya Biashara Nchini kwa Lengo la Kupunguza Gharama hizo na Kuchochea Ukuaji wa Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha mapitio ya tafiti mbalimbali kuhusiana na vikwazo vya biashara visivyo vya kiushuru vinavyowakabili wafanyabiashara katika biashara ya ndani na pia, wanaposafirisha bidhaa zao kwenda nje ya nchi kupitia vituo vya mipakani. Hatua za awali zilizochukuliwa kukabiliana na tatizo hili ni pamoja na kuanzishwa kwa Kamati Maalum za Kitaifa na Kikanda kwa kushirikiana na nchi wanachama wa *EAC* na *SADC*.

Majukumu ya Kamati hizo ni pamoja na kuainisha, kutoa taarifa na hatimaye kutafuta njia za kuondoa vikwazo vilivyoainishwa.

Vilevile, nchi wanachama wa *EAC* na *SADC* zimeanzisha mfumo maalum wa kupeana taarifa kwa

njia ya mtandao *(online)* pale inapobainika kuwepo kwa vikwazo hivyo na hatimaye kuvitafutia ufumbuzi. Aidha, tumeanzisha Kamati Maalum za mipakani *(Joint Boarder Committees)* ambazo zinajumuisha Taasisi na Mamlaka zote zilizopo vituo vya mipakani ili kufuatilia kwa karibu na kuondoa vikwazo vyote visivyo vya kiushuru vinavyojitokeza.

Hatua nyingine ni kuanzishwa kwa Vituo vya pamoja vya Mipakani *(One Stop Boarder Posts)* ambavyo vitasaidia kupunguza urasimu unaochangia ucheleweshwaji wa kuvusha bidhaa mipakani. Juhudi zinaendelea kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinafanya kazi kila siku kwa saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuratibu na kuhamasisha Ushiriki wa Wajasiriamali wa Tanzania katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Ndani na Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *TanTrade* imeendelea kuhamasisha wafanyabiashara na Taasisi za Serikali kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam *(35$^{th}$ DTIF)* maarufu kama SabaSaba. Kwa mwaka 2011/2012, zilishiriki nchi 12, Makampuni ya ndani 900 na 141 kutoka nje ya nchi. Wajasiriamali 46 wa Sekta za Nguo, Usindikaji, Ufungashaji, Uzalishaji, Ubunifu Mitambo na Zana mbalimbali pamoja na ngozi waliwezeshwa kushiriki katika Maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyoandaliwa na Kanda ya Kati Mkoani Dodoma.

Vilevile, Makampuni yapatayo tisa yanaendelea kushiriki kwa awamu katika maonesho ya kimataifa ya *EXPO Korea* yaliyoanza mwezi Mei, 2012 na yanatarajiwa kuhitimishwa mwezi Agosti, 2012. Ushiriki katika maonesho hayo umewezesha bidhaa za Tanzania kutangazwa na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi na hivyo kuchochea uzalishaji na maendeleo ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kufanya Utafiti wa Masoko na Bei ili Kupanua Wigo wa Mahitaji ya Masoko ya Bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanya tafiti za kina zilizoainisha fursa za masoko na changamoto katika kutumia kikamilifu fursa za masoko zilizotolewa na nchi mbalimbali. Tafiti hizo zilihusu masoko ya upendeleo ya *EAC na SADC, AGOA, EBA,* na yale ya India, China, Japan, Korea na Mashariki ya Kati.

Tafiti hizo zimesaidia wadau na hasa wafanyabiashara kwa ujumla kufahamu kwa kina fursa na changamoto zilizopo ambapo zitawasaidia katika kupanga mikakati endelevu ya kuzitumia fursa hizo. Changamoto hizo ni pamoja na ubora wa bidhaa, ufungashaji, Kanuni za Afya za Binadamu, Wanyama na Mimea *(SPS),* Vigezo vya Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin -RoO)* na Vikwazo Visivyokuwa vya Kiushuru *(Non Tarrif Barriers - NTBs.)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuanzisha Programu ya kuwa na Utambulisho wa Kitaifa kwa Bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau kutoka Sekta Binafsi imewezesha kuanzishwa kwa Programu ya utambuzi wa bidhaa na inaendelea kuhamasisha na kuwaelimisha wenye viwanda na Wajasiriamali kuhusu matumizi ya Nembo za Mistari *(Bar Code).* Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa wajasiriamali na wenye viwanda vidogo juu ya umuhimu wa kutumia mfumo wa utambuzi wa bidhaa zao kwa kutumia nembo za mistari.

Mpaka kufikia mwezi Aprili, 2012, jumla ya wazalishaji 151 wamejisajili kutumia huduma hiyo na bidhaa 3,000 ambazo ziko sokoni zina mfumo huu wa utambuzi.

Baadhi ya viwanda kama vile *Kagera Tea Company Ltd*, *Tanzania Breweries Ltd, Konyagi Tanzania Ltd*, pamoja na wasanii wa muziki wameanza kutumia nembo hizo ambazo zinatolewa hapa nchini. Wizara inaendelea pia kushirikiana na Wizara ya Habari na Maendeleo ya Vijana ili kuwashawishi wasanii kutumia huduma hiyo ya utambuzi wa bidhaa. Mfumo huo umeonyesha mafanikio makubwa ambapo bidhaa nyingi na hasa za wajasiriamali zimekubalika katika maduka makubwa *(supermarkets).*

Vilevile, mfumo huo umewapunguzia gharama wazalishaji wetu ambao walikuwa wanafuata huduma hiyo nje ya nchi kwa mfano Kenya na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kukamilisha Mkakati wa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bodi za Mazao ya Pamba, Kahawa, Korosho, Chai, Tumbaku, Sukari, Katani na Pareto, *Agricultural Council of Tanzania (ACT)* na Sekta Binafsi imekamilisha maandalizi ya Mkakati wa Masoko ya Mazao ya Kilimo na Bidhaa za Kilimo. Ufuatiliaji unaendelea ili kupata idhini ya Serikali kutekeleza Mkakati huo. Utekelezaji wa mkakati huo utawawezesha wakulima, pamoja na mambo mengine, kupata taarifa za bei za mazao na masoko ya ndani na nje ya nchi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendeleza Miundombinu ya Masoko ya Mikoa na kuanzisha Masoko Katika Vituo vya Mipakani ili Kukuza Biashara ya Ndani na Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuhamasisha na kuibua miradi ya ujenzi wa miundombinu ya masoko ya mazao katika Halmashauri zote nchini. Uhamasishaji huo hufanyika kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP).*

Miradi ya kuendeleza miundombinu ya masoko huibuliwa Wilayani na kuingizwa katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural*

*Development Plans -DADPs)*. Uendelezaji wa miundombinu ya masoko hufanyika kupitia miradi mingine chini ya *ASDP* kama vile Mradi wa *District Agricultural Sector Investment Project (DASIP)* unaotekelezwa katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Kagera, Shinyanga, Mara na Kigoma. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya maghala 47 yaliyojengwa kupitia Mradi wa *DASIP* katika Mikoa ya Shinyanga (43) na Mwanza (4) ili kuyawezesha maghala hayo kutumika katika mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* ili kukuza biashara ya kikanda, maandalizi ya kujenga masoko saba ya mipakani katika Mikoa ya Kagera, Mara, Shinyanga na Kigoma kupitia mradi wa *DASIP* yanaendelea vizuri. Masoko hayo yatajengwa katika mipaka ya Mtukula, Murongo, Mkwenda, Kabanga, Manyovu, Sirari na Isaka (bandari kavu). Mradi wa *DASIP* unakamilisha mpango wa kumpata Mshauri Mwelekezi wa usanifu na usimamizi wa ujenzi wa masoko hayo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Nanyumbu na Songea zinakamilisha maandalizi ya kufanikisha ujenzi wa masoko katika mipaka ya Kilelema (mpaka Kigoma/Burundi). Mtambaswala (mpaka Mtwara/Msumbiji) na Daraja la Mkenda (Songea/Msumbiji). Tayari timu ya wataalam ya Wizara imetembelea Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri husika kufanikisha ujenzi wa masoko ya mipakani. Aidha, Wizara imekagua masoko yaliyoko kando kando mwa barabara kuu kati ya Dar es Salaam na Dodoma ili kuandaa mpango wa

kuendeleza masoko hayo kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje na Mpango Unganishi wa Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukuza mauzo nje, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika na Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Sekta Binafsi, *TRA, TBS, WMA*, Uhamiaji na Halmashauri husika, imeanzisha Kamati za Kufanya Kazi kwa Pamoja Mipakani *(Joint Border Committee - JBC).* Lengo ni kufanikisha ukaguzi na upitishaji wa mizigo na watu mipakani ili kupunguza muda wa kupitisha mizigo na watu wanapovuka mipaka kwenda nchi jirani. Kamati hizo zimeundwa katika mipaka ya Rusumo, Kabanga, Mtukula, Namanga, Kasumulu na Tunduma. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *USAID COMPETE* imeandaa Mwongozo wa kupitisha bidhaa mipakani *(Clearance Manual)* na Mkakati wa Kufanya Kazi kwa pamoja katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kutangaza bidhaa za Tanzania kupitia maonesho mbalimbali. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake imeshiriki kikamilifu katika maonesho ya Nanenane, Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam *(DITF)* na Maonesho ya Miaka 50 ya Uhuru kutangaza bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu. Tathmini ya maendeleo ya Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Baishara Ndogo kwa miaka 50 imeonesha kuimarika kwa

bidhaa zilizosindikwa na ubora wake, matumizi ya teknolojia za kisasa na kukua kwa biashara. Uzalishaji wa bidhaa za viwandani umeongezeka kukidhi mahitaji ya wananchi ikiwa ni pamoja na kupanuka kwa wigo wa bidhaa zinazozalishwa nchini. Wajasiriamali pamoja na taasisi nyingine binafsi ziliwezeshwa kushiriki katika maonesho ya Wakulima – Nane Nane katika eneo la Wizara.

Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake za Wakala wa Vipimo, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara *(TanTrade)*, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* zilishiriki maonesho ya Wajasiliamali Wanawake yaliyofanyika Mnazi Mmoja ili kutangaza bidhaa wanazozalisha, kujenga mtandao wa kibiashara kuwezesha kujua fursa za masoko, mikopo na kadhalika.

Ushiriki wa Wizara ulilenga kutoa mafunzo ya ujasiriamali, ufungashaji, udhibiti ubora, matumizi ya vipimo na kuwapatia usajili wa majina ya biashara wajasiriamali hao na hivyo kuwajengea wajasiriamali hao uwezo wa kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kimataifa. Kimataifa, Wizara kwa kushirikiana na *TanTrade,* imefanikisha maandalizi ya ushiriki wa *Expo 2012* nchini Korea ambayo yameanza mwezi Mei, 2012 na yatamalizika Agosti, 2012. Pamoja na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini, jumla ya makampuni tisa (9) yameshiriki katika maonesho hayo na kuonyesha na kuuza bidhaa mbalimbali za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kuwawezesha Wajasiriamali kutumia fursa za Soko la *AGOA* kwa kutoa elimu kwa wadau kuhusu fursa za soko hilo pamoja na masharti yake. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imetoa elimu kwa wajasiriamali 30 kutoka sekta ya bidhaa za mikono, asali na vinyago.

Aidha, mauzo ya Tanzania kupitia mpango wa *AGOA* yameongezeka kutoka Dola ya Marekani milioni 2.1 kwa mwaka 2010/2011, hadi kufikia Dola ya Marekani milioni 5.7 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 171. Wizara imeshiriki katika mkutano wa kumi na moja wa *AGOA* ili kuhakikisha mpango wa *AGOA* unakuwa endelevu na wenye masharti nafuu. Ujumbe wa Tanzania uliitaka Serikali ya Marekani kuuangalia upya mpango huo na pia, tumeiomba Serikali ya Marekani kuongeza muda wa kuruhusu nchi za Afrika ikiwemo Tanzania kuagiza majora ya vitambaa nje ya nchi zilizopo katika mpango wa *AGOA* kwa ajili ya wajasiriamali kutengeneza nguo na kuuza Marekani bila ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia, imeendeleza mikakati ya kutumia fursa za masoko kupitia Vituo vya Biashara vya Tanzania vilivyopo London na Dubai kwa kutoa taarifa za masoko kwa wadau kuhusu fursa za masoko zinazopatikana kupitia vituo hivyo. Taarifa za kuwepo kwa masoko ya uhakika kwa mazao mbalimbali eneo la Mashariki ya Kati imepatikana na mkakati unaandaliwa ili kuyatumia masoko hayo. Bidhaa zenye soko kubwa ni pamoja na viungo vya chakula *(spices).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Masoko, Wizara imeendelea kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza kwa wadau taarifa za masoko ya mazao makuu ya chakula mara tatu kwa wiki na zile za rejareja mara mbili kwa kila mwezi.

Aidha, taarifa za bei ya mifugo hukusanywa na kusambazwa mara moja kila juma. Wizara pia, imeandaa Mfumo Mpana na Unganishi wa Taarifa za Masoko kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Mfumo huo wa taarifa utawezesha kupatikana kwa taarifa zitakazounganisha biashara ya ndani na nje ya nchi. Wizara inajiandaa kufanya majaribio ya utekelezaji wa mfumo huu wa taarifa na majadiliano yanafanyika na Wahisani wa Maendeleo ili kupata fedha za kuufanyia majaribio ya utekelezaji wa mfumo huo nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendeleza Biashara ya Ndani ikiwa ni pamoja na kujenga dhana ya kutumia Bidhaa zilizozalishwa Tanzania (Nunua Bidhaa za Tanzania).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za Serikali kuhamasisha matumizi ya bidhaa za ndani kwa kupitia kauli mbiu ya ‘Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania’, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali ili kuzalisha bidhaa zenye ubora na matumizi ya vifungashio bora kwa kuzingatia matakwa ya soko. Ili kutimiza azma hiyo, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* imeendelea kutoa mafunzo ya ubora wa bidhaa na ufungashaji bora kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Hadi kufikia mwezi

Machi, 2012, jumla Wajasiriamali *(SMEs)* 248 kutoka mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya walipatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuboresha na Kupanua Wigo wa Biashara Mtandao Katika Ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *BRELA*, imekamilisha zoezi la kubadilisha taarifa za Makampuni na Majina ya Biashara kutoka katika Mfumo wa makabrasha na kuwa katika mfumo wa digitali *(digital).* Kukamilika kwa mfumo huo kutasaidia kupatikana kwa taarifa za makampuni na majina ya biashara kwa urahisi zaidi mara zinapohitajika na hivyo kupunguza muda wa kusajili majina ya biashara na makampuni hadi wastani wa siku mbili au tatu ikilinganishwa na siku zaidi ya saba hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na taratibu za utoaji wa leseni za biashara, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* wameandaa mwongozo wa kurahisisha maandalizi ya nyaraka *(MEMART)* za usajili wa kampuni inayopatikana katika mtandao. Serikali pia, imepunguza urasimu wa kupata leseni za biashara kwa kuondoa masharti ya kupitisha maombi ya leseni za biashara katika Ofisi za Mipango Miji na hivyo kuwezesha leseni hutolewa kwa siku moja endapo masharti muhimu yamekamilika; na Sheria mbalimbali za Biashara zimefanyiwa marekebisho ili zikidhi mahitaji ya sasa ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kupanua matumizi ya simu za viganjani katika kutoa taarifa za bei ya mazao na masoko kwa wakati. Aidha, kuangalia uwezekano wa kuanzisha mbao za matangazo katika ngazi ya Wilaya na Mkoa ili kutoa taarifa mbalimbali Ikiwemo bei na masoko kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ili kuweza kutumia simu za viganjani katika kukusanya na kusambaza bei ya mazao kwa wakati. Wizara imesaini Mkataba wa Maelewano na Sekta Binafsi na tayari majaribio ya kukusanya na kusambaza taarifa za bei za mazao na huduma za ugani katika Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Iringa na Dodoma yameanza. Lengo ni kupanua matumizi ya teknolojia hiyo ili iweze kutumika nchi nzima katika ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za bei za mazao na huduma za ugani kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ili kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinawafikia wananchi wengi zaidi, hasa wale waliopo vijijini, Wizara kwa kushirikisha Sekta Binafsi imeanza kusambaza taarifa za masoko kupitia redio za jamii *(community radios)* ambazo zipo katika wilaya nyingi nchini pamoja na mbao za matangazo katika ngazi ya Wilaya na Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendeleza mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* ilizinduliwa rasmi mnamo tarehe 01 Julai, 2011, na Mheshimiwa Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mwaka 2011/12, *TanTrade* imeanza kutekeleza majukumu yake mapya ya kuendeleza biashara ya nje na ya ndani. Ili kufanikisha hilo, marekebisho madogo ya Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania Na. 4 ya 2009 yamefanyika kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini. Marekebisho hayo yalipitishwa na Bunge tarehe 12 Aprili, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendeleza Utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania imetoa mafunzo kuwezesha kuanzishwa kwa mfumo wa Stakabadhi kwa zao la kahawa mkoani Kagera. Aidha, uhakiki wa maghala yanayofaa kwa kazi hiyo umefanyika na kwa kuanzia utekelezaji wa mfumo utafanyika kwa majaribio katika Wilaya ya Ngara.

Vile vile, timu ya Maafisa wa Wizara kwa kushirikiana na Maafisa wa Bodi ya Leseni za Maghala walikagua maghala yaliyojengwa kupitia Mradi wa *DASIP* katika Mikoa ya Shinyanga na Mwanza ili kubaini yale yanayofaa kwa ajili ya matumizi ya Mfumo wa stakabadhi za Maghala. Uhakiki huo ulilenga kuwezesha matumizi ya mfumo wa stakabadhi kwa

mazao ya mpunga na pamba. Bodi ya Leseni za Maghala imeanza kutoa elimu ya mfumo katika mikoa hiyo ili kuwezesha uanzishaji wa matumizi ya mfumo wa stakabadhi kwa zao la mpunga ambalo linazalishwa kwa wingi katika eneo hilo.

Mfumo wa stakabadhi kwa hivi sasa unatekelezwa katika mazao ya korosho, kahawa, ufuta, alizeti, mahindi na mpunga. Ikumbukwe kuwa, mfumo huo utakuwa nguzo kuu ya uanzishwaji wa Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange)* kwa kuwa unawezesha upatikanaji wa mazao katika maghala kwa kuzingatia viwango vya ubora na wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendeleza miundombinu ya masoko ya Mikoa na kuanzisha masoko mpakani kama vile Karagwe, Kigoma, Holili, Horohoro, Namanga, Sumbawanga, Taveta na Tarakea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, ujenzi wa miundombinu ya masoko ya mazao kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* inayopangwa katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans - DADPs)* na miradi kama vile *DASIP* unaendelea katika Wilaya za Tarime (Sirari), Misenyi (Mtukula), Karagwe (Murongo na Mkwenda), Ngara (Kabanga), Kigoma (Manyovu) na Kahama (Isaka – Bandari kavu). Miundombinu kama masoko, maghala, machinjio na barabara za vijijini imejengwa. Wizara inaendelea na uhamasishaji wa kuibua miradi ya kuimarisha na

kujenga masoko ya mazao katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,vile vile, kazi ya kuandaa Mpango Kabambe *(Master Plan)* wa ujenzi wa masoko katika miji ya Segera na Makambako iliyofanywa na Chuo Kikuu cha Ardhi imekamilika. Maeneo ya ujenzi wa masoko haya yamepimwa na kuwekewa alama za mipaka kwa kushirikiana na Halmashauri husika ili kuzuia uvamizi maeneo hayo. Wizara imeanzisha majadiliano na Benki ya Rasilimali *(TIB)* ili kufanikisha ujenzi wa masoko haya muhimu.

Aidha, maandalizi ya kujenga masoko saba ya mipakani katika mikoa ya Kagera, Mara, Shinyanga na Kigoma kupitia mradi wa *DASIP* yanaendelea vizuri. Masoko haya yatajengwa katika mipaka ya Mtukula, Murongo, Mkwenda, Kabanga, Manyovu, Sirari na Isaka (bandari kavu). Mradi wa *DASIP* unakamilisha mpango wa kumpata Mshauri Mwelekezi wa usanifu na usimamizi wa ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kufanya tafiti za masoko ya mipakani na kuzishauri Halmashauri za Wilaya husika ili kufanikisha ujenzi wa masoko hayo. Timu ya Wizara imetembelea Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kasulu kubainisha maeneo yanayofaa kuendelezwa kimasoko ili kukuza biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani ya Burundi. Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri husika kufanikisha ujenzi wa masoko ya mipakani. Aidha, Wizara imekagua masoko yaliyoko kando kando mwa barabara kuu kati ya Dar es Salaam na Dodoma ili

kuandaa mpango wa kuendeleza masoko kando kando ya barabara hiyo. Wizara itashirikiana na Halmashauri husika ili kufanikisha ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni na kutekeleza Mikakati ya Masoko ya Ndani, Kikanda na Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushirikiana na Sekta Binafsi kupitia Jukwaa la Wadau wa Masoko ya Mazao ya Kilimo *(Agricultural Marketing Forum)* ambalo huwakutanisha wadau ili kujadiliana maendeleo ya masoko ya mazao ya kilimo na mifugo. Kupitia jukwaa hilo Wizara imeweza kushirikiana na Taasisi zifuatazo:-

Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania *(MVIWATA), Tanzania Horticultural Association (TAHA), Horticultural Development Council of Tanzania (HODECT), Agricultural Council of Tanzania (ACT), Rural Livelihood Development Company (RLDC), Tanzania Agricultural Market Development Trust (TAGMARK),* Bodi za Mazao na Vyama vya Ushirika. Mafanikio ya ushirikiano huo ni pamoja na kuandaliwa kwa andiko la kuanzisha Soko la Bidhaa *(commodity exchange); Mkakati wa Masok*o ya Mazao na bidhaa za Kilimo, Mkakati wa Leseni za Udhibiti, mapendekezo ya kuboresha mazingira ya biashara, kufanya mapitio ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwalinda wajasiriamali wa ndani kwa kutoingiza bidhaa mbalimbali kutoka nje ambazo zinaua Soko la Ndani la Bidhaa

Mheshimiwa Mwenyekiti,katika kuimarisha udhibiti wa bidhaa duni *(substandard)* kutoka nje ya nchi, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) tangu tarehe 01 Februari, 2012 imeanza kutekeleza utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinakotoka kabla ya kuingiza nchini *(Preshipment Verification of Conformity to Standards – PVoC).*

Katika kuwalinda wajasiriamali, Wizara kupitia Tume ya Ushindani imeendelea kufanya ukaguzi wa bidhaa bandia katika bandari Kuu ya Dar es Salaam na bandari kavu *(Inland Container Depots).* Vilevile, Tume imeendelea kufanya ukaguzi katika maghala na maduka ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti,katika kuendeleza utoaji wa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi na ubora wa bidhaa za viwanda ikiwa ni pamoja na uzalishaji unaozingatia hifadhi na kulinda mazingira, Wizara inaendelea kupata ushirikiano mzuri kutoka Serikali ya Japan, kupitia Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* ambapo imeendelea kupata wataalam wa kusaidia katika kuendeleza viwanda. Hii inajumuisha msaada wa kuanzisha Programu ya *Kaizen* itakayotoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi, usimamizi wa shughuli za viwanda na kuongeza ubora wa bidhaa. Mradi huo unatekelezwa kufuatia mafanikio ya majaribio *(pilot project)* ya mwaka 2010/2011 yaliyohusisha

wajasiriamali 113 wenye viwanda vidogo vya nguo na mavazi katika mkoa wa Dar es Salaam.

Aidha, makampuni kutoka Japan yenye nia ya kuwekeza nchini katika sekta ya viwanda yameendelea kujitokeza kutokana na kuimarika kwa ushirkiano na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara. Makampuni hayo ni pamoja na *NITORI HOLDINGS Ltd* linalotaka kuwekeza katika pamba na bidhaa za pamba na *SUMITOMO* katika uzalishaji wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya kukamilisha Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* ikizingatia maslahi ya nchi na mapendekezo ya Sekta Binafsi. Vilevile, Wizara iliendelea kushirikiana na Sekta Binafsi kwa kuandaa vikao vya kisekta kujadili maendeleo na changamoto na kutoa mapendekezo husika Serikalini. Sekta hizo ni pamoja na nguo na mavazi; ngozi na bidhaa za ngozi; chuma na uhandisi; kemikali; chakula na vinywaji; karatasi na vifungashio; mafuta ya kula na sabuni.

Wizara ilishiriki katika mikutano ya *UNIDO LDC* na *UNIDO General Conference* iliyojadili maendeleo na changamoto za Sekta ya Viwanda na iliwezesha majadiliano kati ya viongozi wa Wizara na *UNIDO* na kukubaliana juu ya miradi ya kutekelezwa kwa ushirikiano. Miradi hiyo ambayo imeanza kutekelezwa ni pamoja na *Industrial Policy Analysis, Industrial*

*Upgraging and Mordernisation* na *Africa Agribusiness and Agroprocessing Development Initiative (3ADI).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *National Bureau of Statistics (NBS), CTI* na *UNIDO* imekuwa ikifanya Tathmini ya Maendeleo ya Viwanda (*Industrial Survey*) nchini ambapo tathmini ya mwaka 2010 inakamilishwa. Aidha, kwa kuzingatia kuwa sensa ya viwanda ilifanyika mara ya mwisho mwaka 1989, Wizara kwa kushirikiana na *NBS*, Sekta Binafsi na wadau wa maendeleo itaendelea na majadiliano ya kuona namna ya kutekeleza kazi hii ifikapo mwaka 2013.

Wizara tayari imeandaa andiko la kufanya sensa hiyo ambalo litagharimu takribani jumla ya Shilingi bilioni nane. Mazungumzo na *UNIDO* na *NBS* yanaendelea ili kupata wahisani wa kufadhili zoezi hilo. Kufanyika kwa sensa inayokusudiwa itawezesha kupata taarifa na takwimu sahihi zikiwemo idadi ya viwanda vilivyopo, bidhaa zinazozalishwa, ajira, mchango wa sekta katika Pato la Taifa, matumizi na mahitaji halisi ya umeme, maji na huduma nyinginezo. Aidha, taarifa hizo zitaiwezesha Serikali na wadau wengine kuweka mipango ya sekta kwa usahihi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,utekelezaji wa Mradi wa Kasi Mpya unaendelea vizuri. Kampuni ya Maganga Matitu *Resources Development Limited (MMRDL)* ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya *NDC* na *MM Steel Resources Company Ltd* imekamilisha kazi ya uchorongaji ili kuhakiki wingi na ubora wa mashapo ya chuma cha Maganga Matitu. Mashimo 58 yenye urefu wa jumla ya mita 11,298 yalichimbwa kwa ajili hiyo.

Aidha, uchorongaji katika eneo la makaa ya mawe ya Katewaka umekamilika na jumla ya mashimo 28 yenye urefu wa mita 4,547 yamechimbwa. Ujenzi wa migodi ya chuma na makaa ya mawe na kiwanda cha kuzalisha chuma ghafi unatarajiwa kuanza mwaka 2013. Uzalishaji wa chuma ghafi unatarajiwa kuanza mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Mradi wa Ngaka Kusini wa kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe unatekelezwa na Kampuni ya *TANCOAL ENERGY Ltd* ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya *NDC* na kampuni ya *Intra Energy Ltd.* Mradi huo tayari umeanza uchimbaji wa makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi viwandani na unatarajiwa kuzalisha umeme wa MW 400 hadi MW 600 kwa ajili ya kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *NDC* linamiliki asilimia 30 ya hisa na *Intra Energy* asilimia 70. Upembuzi yakinifu wa kuanzisha mgodi wa makaa ya mawe wa Ngaka Kusini umekamilika na kuthibitisha kuwepo kwa mashapo kiasi cha tani milioni 251. Ujenzi wa mgodi wa makaa ya mawe ulianza Agosti, 2011. Kampuni ya *TANCOAL* imeanza uzalishaji wa makaa ya mawe na kiasi cha tani 85,000 kimechimbwa na kuuzwa kwa viwanda vya saruji vya Mbeya, Tanga na kiasi kimeuzwa nchini Malawi na kuingiza jumla ya Dola ya Marekani milioni 3. *TANCOAL* ina mpango wa kujenga kituo cha kuzalisha umeme wa *MW 200* kwa kuanzia ifikapo mwezi Desemba 2015 hadi MW 400 mwaka 2017/2018 na kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

Sambamba na ujenzi huo, *TANCOAL i*mepanga kujenga njia ya msongo mkubwa wa umeme (Kilovoti 220 hadi 400) kati ya Ngaka na Songea (Kilometa 100) kwa ajili ya kupitishia umeme utakaozalishwa. Hivi sasa, *TANCOAL* inafanya mazungumzo na *TANESCO* kuhusu mkataba wa mauzo ya umeme *(Power Purchase Agreement-PPA)* utakaozalishwa na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umeme wa Upepo unaotekelezwa na Kampuni ya ubia kati ya *NDC, TANESCO* na Kampuni ya *Power Pool East Africa Limited (PPEAL)* iitwayo *Geo Wind Power Tanzania Ltd.* unategemewa kuzalisha umeme wa Megawati 50 kwa kuanzia na kufikia MW 300 ifikapo 2018/2019 kwa kutumia upepo huko Singida. Aidha, mkataba wa ujenzi *(EPC Contract)* umesainiwa kati ya NDC na Kampuni ya *China Dalian International Economic & Technical Cooperation Group Co. Ltd (CDIG)*. Vilevile, maombi ya awali ya mkopo nafuu *(Concession Loan)* wa Dola ya Marekani milioni 136 yamewasilishwa Benki ya Exim ya China. Mazungumuzo yanaendelea kati ya Kampuni ya ubia na *TANESCO* ili kupata mkataba wa kuuza umeme *(PPA)* wakati uzalishaji utakapoanza. Ujenzi wa mradi unategemewa kuanza mwezi Agosti, 2012 na kukamilika mwezi Septemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza viuadudu *(biolarvicides)* wa kibaiolojia wa kuua viluwiluwi vya mbu wanaoeneza Malaria katika eneo la *TAMCO*-Kibaha, unaendelea vizuri. Wizara kupitia *NDC* inasimamia na kugharimia ujenzi wa kiwanda hicho ambacho ujenzi unafanywa kwa

kutumia teknolojia na utaalam wa kiufundi kutoka nchi ya Cuba.

Kiwanda kitakapoanza kazi kitakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni sita za viuadudu kwa mwaka. Gharama za ujenzi wa kiwanda hadi kukamilika ni Dola ya Marekani 22,307,688.00. Asilimia 75 ya fedha hizo imekwishalipwa hadi sasa. Aidha, *NDC* inatafuta wadau kutoka kwenye mashirika na Sekta Binafsi ili kugharimia asilimia 25 iliyobakia ambayo ni sawa na Dola ya Marekani 5,576,922. Ujenzi wa kiwanda unatarajiwa kukamilika Desemba, 2012. *NDC* inaendelea na mazungumzo na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu kuingia mkataba wa ununuzi wa viuadudu hivyo pindi uzalishaji utakapoanza, mwanzoni mwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* imejipanga kutekeleza miradi ya usindikaji wa mazao ya kilimo ya mpira, michikichi na nyama kwa njia ya ubia kati yake, na wawekezaji, na kushirikisha wakulima wadogo. Juhudi za uongezaji thamani nyama zimeendelea ambapo *NDC* imebainisha eneo la Themi Arusha kuwa ni muafaka kujenga kiwanda hicho. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi inayomiliki eneo hilo imekubali *NDC* kulitumia. Aidha, *NDC* imefanikiwa kumpata mwekezaji, Kampuni ya Kichina ya *China Dalian International Economic & Technical Cooperation Group Co. Ltd (CDIG)* na makubaliano ya awali *(Memorandum of Understanding-MOU)* yalisainiwa mwezi Julai, 2011. Majadiliano yenye nia ya kusaini Mkataba wa Ubia yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Vilevile, upembuzi yakinifu wa mazao ya muhogo, mtama mtamu na mchikichi *(palm)* ulifanyika na kuchagua mafuta ya mawese kama kipaumbele kati ya mazao hayo matatu. Juhudi za *NDC* kupata ardhi ya kuanzisha kilimo cha michikichi Wilaya ya Kisarawe na Kibaha zinaendelea. Mwekezaji, Kampuni ya *Nava Bharat African Resources PVT Ltd* ya India kwa kushirikiana na *NDC* katika kilimo cha michikichi amepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa zao la mpira kwa mashamba ya Kalunga, Kilombero na Kihuhwi, Muheza yanaendelea vizuri na uzalishaji umeongezeka kutoka tani 120 mwaka 2010 hadi tani 202 mwaka 2011. Upanuzi wa shamba la Kalunga umeanza katika eneo ambalo lilikuwa halijaendelezwa. Kwa upande wa shamba la Kihuhwi bado upandaji miche haujaanza katika eneo ambalo halijaendelezwa kutokana na uvamizi uliojitokeza. Juhudi za kupata ufumbuzi kwa kushirikiana na Wilaya ya Muheza zinaendelea. Pia, juhudi za kupata ardhi zaidi kwa ajili ya mashamba mapya ya mpira katika Wilaya ya Kilindi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa kanuni za kusimamia mfumo wa *SEZ* ili usajili wa wawekezaji uanze kutumika umeanza na rasimu ya kanuni za *SEZ* tayari imeandaliwa na utaratibu wa kutangaza kanuni hizo katika Gazeti la Serikali uko katika hatua za mwisho. Vilevile, uandaaji wa Mpango Kabambe (*Master Plan*) wa eneo la kipaumbele la Bagamoyo *SEZ* unaendelea. Tayari maandalizi ya upembuzi yakinifu,

uthaminishaji mali na kulitangaza eneo la mradi katika Gazeti la Serikali yamekamilika. Ujenzi wa miundombinu ya msingi kwa kushirikiana na Sekta Binafsi utaanza mara Mpango Kabambe wa Bagamoyo *SEZ* utakapokamilika. Makampuni 16 yameshawasilisha maombi ya kuendeleza miundombinu na kujenga viwanda katika eneo hilo. Aidha, taratibu za uendelezaji wa maeneo ya bandari huru na *SEZ* katika eneo la uwekezaji Mtwara na Kigoma zimeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia *EPZA* imeendelea kuhamasisha wawekezaji kujenga miundombinu na viwanda vya kuzalisha bidhaa katika maeneo maalum ya uwekezaji. Makampuni 19 yamepewa leseni kama yalivyobainishwa katika Kitabu cha Mafanikio ya Sekta ya Viwanda na kuanzisha viwanda katika maneneo maalum na kufanya Makampuni yanayozalisha kupitia mfumo huo kufikia 59. Aidha, mtaji katika maeneo ya *EPZ* umeongezeka kutoka Dola ya Marekani milioni 650 na kufikia milioni 792.2 na ajira za moja kwa moja zimeongezeka kutoka 12,500 mpaka 16,105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO* inatekeleza Mradi wa Kuboresha utendaji ili kuongeza ufanisi wa viwanda *(Industrial Upgrading and Modernisation)* hasa viwanda vidogo na vya kati. Mradi huu unalenga zaidi kutoa ushauri katika kuboresha maeneo ya menejimenti/utawala, matumizi mazuri ya rasilimali *(wastes reduction),* matumizi sahihi ya nishati, mpangilio wa mitambo ya uzalishaji *(plant layout),* ubunifu *(innovation)*, matumizi ya teknolojia sahihi na kushauri juu ya ukarabati unaohitajika na

hatimaye kuunganisha viwanda husika na masoko hasa ya nje. Kitengo cha kutekeleza mradi huo kimeanzishwa na *UNIDO* imekwishatoa mtaalamu atakayetoa mafunzo kwa Watanzania watakaotoa mafunzo na ushauri viwandani *(trainer of trainers)*. Kwa kuanzia viwanda 15 vitanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO* inatekeleza Mradi wa Kujenga uwezo wa Wizara na wadau wa kuchambua Sera ya Maendeleo ya Viwanda. Aidha, chini ya mradi huo, ripoti *(Industrial Competitiveness Report)* imeandaliwa ili kuwezesha Serikali kutoa maamuzi sahihi. Mafunzo ya awali yalifanyika mwezi Machi 2012 na kuhusisha Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais - Mipango, Wizara ya Fedha, Vyuo Vikuu (*UDSM* na Mzumbe), Sekta Binafsi na Asasi Zisizo za Kiraia. Ripoti hiyo inatarajiwa kuzinduliwa mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia sera za uwekezaji ikiwa ni pamoja na Sera ya *PPP*, Tanzania imeendelea kuvutia wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali duniani. Baadhi ya wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuwekeza hapa Tanzania hivi karibuni ni Kampuni ya *NITORI HOLDINGS Ltd.* ya Japan. Nia yao ni kuwekeza katika kilimo cha pamba, viwanda vya nguo na mavazi, kauri *(ceramics),* bidhaa za vioo *(glass)* na ngozi na bidhaa za ngozi. Tayari Kampuni hiyo imefanya tafiti za awali kwa ajili ya kubainisha malighafi zilizopo nchini na kiasi kinachoweza kupatikana kwa ajili ya matumizi ya viwanda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani kwa wajasiriamali hasa vijijini, Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa *SIDO* kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye ujuzi, kuwapa mafunzo watumishi wake ndani na nje ya nchi na kuwapatia vitendea kazi. Kutokana na juhudi hizo, *SIDO* imeweza kutoa huduma za ugani kwa wajasiriamali 16,138 katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Serikali imezingatia umuhimu wa kuhakikisha kuwa teknolojia zinazofaa zinatafutiwa utaratibu wa kuzizalisha kwa wingi *(commercialization of proven technologies)*, na kuzisambaza kwa watumiaji. Utekelezaji umefanywa hatua kwa hatua kwa kutumia vituo vya kuzalisha na kuendeleza teknolojia vya *SIDO* na vya wajasiriamali wadogo. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, teknolojia 142 zilitafutwa kwa ajili ya matumizi ya wajasiriamali pia, wajasiriamali wabunifu waliweza kutengeneza teknolojia mpya 76. Aidha, kwa kutumia baadhi ya teknolojia hizo, jumla ya mashine 396 zilizalishwa na kusambazwa kwa watumiaji mbalimbali hasa katika usindikaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha Manispaa na Halmashauri za Miji na Vijiji kutenga maeneo kwa ajili ya kujenga viwanda vidogo ambavyo vitasaidia kuongeza thamani mazao. Aidha, Wizara imeanzisha mpango wa kuhamasisha ujenzi wa kongano *(industrial clusters)* katika Mikoa kwa lengo la kusindika mazao na kuongeza thamani.

Katika Mkoa wa Singida, eneo la ekari 20 limetengwa katika Wilaya ya Singida Vijijini kwa ajili ya

kujenga kongano la kusindika na kuongeza thamani ya zao la alizeti. Ramani na michoro katika kijiji cha Mtinko, Singida Vijijini imekamilishwa. Eneo hilo ni mojawapo kati ya maeneo ambayo Shirika la Ushirikiano la Japan *(JICA)* limeonyesha nia ya kusaidia ujenzi wa makongano ya usindikaji wa zao la alizeti katika Mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida. Aidha, kwa Mikoa ya Kilimanjaro na Morogoro yataanzishwa makongano ya shughuli za chuma *(metal works).* Usindikaji na uongezaji thamani wa mazao unaongeza tija kwa mjasiriamali na bidhaa zinazozalishwa zitapata soko na kutoa ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujenga misingi na kusaidia uzalishaji wa bidhaa mpya kutokana na ubunifu wa wajasiriamali binafsi, utaratibu wa kulea wabunifu *(incubator Programu)* unaosimamiwa na Wizara na kutekelezwa na *SIDO*, umeendelea kuwawezesha wajasiriamali kuendeleza ubunifu. Aidha, ukarabati umefanyika kwa majengo sita ili kukidhi haja ya ubunifu na wabunifu wapya 32 wamewezeshwa kwa kupewa sehemu ya kufanyia shughuli zao katika majengo hayo. Vilevile, jengo la kudumu kwa ajili ya kutoa huduma za ushauri, teknolojia na mawasiliano *(ICT)* katika mikoa ya Shinyanga, Mbeya, Arusha, Dar es Salaam, Tanga, Kigoma na Kagera limekamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* imetoa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa wajasiriamali 8,880 katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Maarifa na ujuzi waliopata washiriki umewasaidia kuongeza uelewa na ufanisi wa kuendesha miradi ya uzalishaji na

biashara. Vile vile, wazalishaji wadogo wamewezeshwa kupata masoko ya bidhaa na huduma zao kwa kutengeneza miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara na kutengeneza sehemu za kuoneshea bidhaa za wazalishaji wadogo. Katika kufanikisha lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO*, imetoa fursa kwa wajasiriamali kutangaza bidhaa zao na kupata habari za masoko, kupitia maonesho matatu ya kanda za Mashariki, Kusini na Nyanda za Juu Kusini ya bidhaa za wajasiriamali yaliyofanyika na kutoa fursa kwa wajasiriamali 649 kutangaza na kuuza bidhaa zao ambapo mauzo ya Shilingi milioni 316. 5 yalifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapojidhihirisha kuhitajika, hadi kufikia Machi, 2012, Serikali imeipa *SIDO* kiasi cha Shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuongeza fedha za mfuko wa *NEDF* na kufanya kiasi kilichotolewa na Serikali kwa ajili ya Wajasiriamali kufikia Shilingi bilioni 5.326 toka mfuko huo ulipoanzishwa mwaka 1994. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, jumla ya mikopo 4,387 yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.181 ilitolewa kwa wajasiriamali. Jumla ya ajira 8,719 zilitengenezwa kutokana na mikopo hiyo na asilimia 51.6 ya ajira hizo ilienda kwa wanawake. Aidha, ili kuhakikisha kuwa wajasiriamali wadogo wanatumia mikopo waliyopewa inavyotakiwa, Wizara kupitia *SIDO* imetoa mafunzo na ushauri wa mikopo kwa wajasiriamali 14,688 katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uwezo wa uzalishaji wa zana za kilimo, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* kupitia vituo vyake vya uendelezaji wa teknolojia vilivyopo Mbeya, Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Shinyanga na Kigoma, iliwezesha utengenezaji wa zana mpya za aina tofauti 604. Zana hizo ni pamoja na jembe la kukokotwa na wanyama kazi, mashine ya kupandia, pampu za maji, mashine ya kuvunia, mashine ya kupura mtama na mashine za kupukuchua nafaka. Zana hizo zimerahisisha kazi ya kilimo na hatua za awali za usindikaji wa mazao ya shamba kwa ajili ya mahitaji mahsusi kwa uzalishaji mali. Aidha, vipuri 2,472 vilizalishwa na kusambazwa kwa watumiaji ili kuhakikisha kuwa shughuli za uzalishaji haziathiriki kwa kukosa vifaa hivyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kusimamia na kutekeleza Mikataba na Itifaki mbalimbali ambazo Tanzania imeridhia, Tanzania inatekeleza makubaliano ya kibiashara na uwekezaji baina yake na nchi mbalimbali zikiwemo Vietnam, Comoro, Uturuki, India, China, Canada na Marekani. Aidha, Tanzania inatekeleza Itifaki za biashara ya kikanda kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika; na mikataba ya kibiashara chini ya Shirika la Biashara la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa mafunzo kwa Maafisa Biashara wa Wilaya, Manispaa na Miji kuhusu fursa za masoko ya nje ikiwa ni pamoja na Sheria na kanuni za kuingia masoko hayo, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Misaada ya *Southern Africa*

*Trade Hub-SATH* imetoa mafunzo kwa wadau 100. Fursa za masoko hayo ni pamoja na yale ya upendeleo maalum yanayotolewa chini ya mpango wa *AGOA* na *EBA*, China, Japan, Canada na India; na yale ya kikanda ya *SADC* na *EAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliunda Kamati za Kitaifa za Wataalamu kwa ajili ya kujadili na kuishauri serikali kuhusu masuala ya biashara ya kimataifa. Kamati hizo ni pamoja na *National Monitoring Committee on NTBs (NMC – NTBs), National SPS Committee, Technical Barriers to Trade (TBTs) na Trade Facilitation Committee*. Kamati hizo zinajumuisha wadau kutoka Serikali na Sekta Binafsi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Kamati hizo zimekuwa zikifuatilia kwa ukaribu majadiliano yanayoendelea ya Duru la Doha kwa maeneo husika na kuishauri Serikali. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo *(UNCTAD)* katika kuboresha mazingira ya biashara kama njia mojawapo ya kuleta maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imefanya mapitio ya Sheria ya *Anti Dumping and Countervailling Measures*. Rasimu ya mapitio hayo ipo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuwasilishwa ngazi za juu kwa ajili ya kupitishwa. Sheria hiyo itakapoanza kutumika itatusadia kukabiliana na changamoto za uingizaji wa bidhaa kutoka nje zinazouzwa kwa bei ya chini kuliko gharama zake za uzalishaji ambapo itatuwezesha kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa makubaliano ya Shirika la Biashara la

Dunia *(WTO)* ili kuleta ushindani wa haki katika biashara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *WITO* chini ya mwavuli wa *EAC*, inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara kwa lengo la kuhakikisha kwamba inatangamana na matakwa ya *WTO* na hasa katika suala la uwazi na urahisishaji biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuimarisha mahusiano kati ya nchi na nchi, kikanda na yale ya Kimataifa kwa lengo la kuendelea kukuza fursa za masoko kwa bidhaa zetu na kuvutia wawekezaji, Tanzania ilisaini Mkataba wa kulinda na kuendeleza uwekezaji baina yake na Uturuki. Aidha, Wizara iko katika majadiliano na Serikali ya China kwa lengo la kuanzisha Kituo cha Biashara *(Logistics Center)* jijini Dar es Salaam. Kituo hicho kitawezesha wajasiriamali wa Tanzania hususan wanawake kupata maeneo ya kufanyia biashara. Kituo hicho kitawezesha upatikanaji wa teknolojia ya kisasa katika uongezaji thamani wa bidhaa za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia inaendelea kushiriki katika majadiliano yatakayowezesha Jumuiya za *COMESA, EAC* na *SADC* kuanzisha Eneo Huru la Biashara *(Tripartite Free Trade Area).* Majadiliano hayo yanalenga kupanua fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania na kurahisisha biashara kwa kuondoleana vikwazo visivyo vya kiushuru, kuimarisha miundombinu, kuvutia wawekezaji na kuleta maendeleo ya Viwanda. Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 ili iweze kuendana na mfumo wa utandawazi na mabadiliko yanayojitokeza katika nyanja ya biashara duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuviimarisha Vituo vya Biashara vya Tanzania vilivyopo London na Dubai kwa kuviongezea uwezo kifedha ili kutekeleza majumu yake kikamilifu. Vituo hivyo vimekuwa vikitangaza vivutio mbalimbali vilivyoko Tanzania kwa lengo la kuvutia wawekezaji na vile vile kutoa taarifa za fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania. Kituo kwa ushirikiano na Bodi ya Utalii na Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar zinazoratibu Maonesho ya Kimataifa ya London huwezesha makampuni zaidi 60 kushiriki ili kupata masoko ya bidhaa zao na wabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeandaa Mfumo Mpana na Unganishi wa Taarifa za Masoko. Mfumo huo utaunganishwa na mifumo ya wadau wengine katika kutoa taarifa za masoko ya ndani na nje. Hadi sasa Mfumo wa majaribio umekamilika kama ilivyoelezwa katika aya ya 73. Katika kuwajengea uwezo wazalishaji na wafanyabiashara kuzalisha zaidi na kuuza katika masoko yenye bei shindani, Wizara imeendelea kukusanya, kuhifadhi, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko kwa wadau kupitia ujumbe wa simu za kiganjani, mtandao wa kompyuta na vyombo vya habari. Taarifa hizo hukusanywa mara tatu kwa wiki kwa mazao makuu ya chakula na mara moja kwa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuleta ufanisi wa biashara mipakani, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inakamilisha taratibu za ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi Mipakani *(OSBP)* katika

Vituo vya Tunduma/Nakonde na Kabanga/Kobero. Makubaliano ya ujenzi wa vituo hivyo kati ya Tanzania na nchi za Zambia na Burundi kuhusu ujenzi wa Vituo hivyo yamesainiwa. Kwa upande wa Kituo cha Tunduma/Nakonde, maandalizi ya awali ya ujenzi wa kituo hicho yamekamilika ikiwa ni pamoja na utafiti wa mahitaji na michoro, chini ya uratibu wa Wizara ya Fedha na ufadhili wa Taasisi ya *Trade Mark East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini, Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BARA 2007), ambayo ilihitaji marekebisho zaidi ya yale yaliyofanywa kupitia Sheria ya Fedha Na. 5 ya Mwaka 2011. Lengo ni kuwezesha utekelezaji wa sheria hiyo hususan kuruhusu utozaji wa ada za leseni. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa mapendekezo ya marekebisho husika kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusogeza huduma ya usajili wa majina ya Biashara na Makampuni karibu na Jamii ya wafanyabiashara, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni, *(BRELA)* wameendelea kuwasiliana na Chama cha Wafanya Biashara wenye Viwanda na Kilimo *(TCCIA)* ili ofisi zao zitumike kutoa huduma ya usajili wa majina. Aidha, *BRELA* wametembelea ofisi za *TCCIA* za Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Kilimanjaro na Manyara ili kuona uwezekano wa kutoa huduma hiyo. Wafanyabishara wadogo 70 Mkoa wa Tanga na 35 Mkoa wa Pwani na wadau wengine wameelimishwa kuhusu huduma za usajili wa majina ya biashara na Makampuni zinazotolewa na *BRELA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, matumizi ya *TEHAMA* katika usajili wa majina ya biashara na uandikishwaji wa makampuni imewezesha upatikanaji wa taarifa na utoaji wa huduma za usajili kwa urahisi. Taarifa zote zinazohusu *BRELA* zinapatikana kupitia tovuti *www.brela-tz.org*. Huduma zinazopatikana ni pamoja na fomu za maombi ya kuandikisha makampuni, fomu za usajili wa majina ya biashara, fomu za maombi ya usajili wa alama za biashara na huduma, fomu za kuomba hataza na fomu za maombi ya leseni za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa leseni za Biashara kwa mujibu wa Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya Mwaka 1972 na marekebisho yake. Jumla ya leseni za Biashara 1,612 zimetolewa kwa kipindi cha Julai, 2011 – Machi 2012.

Pia, marekebisho ya baadhi ya Sheria za biashara zinazosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara imefanyiwa marekebisho na kupitishwa na Bunge ili kuboresha mazingira ya biashara nchini. Sheria hizo ni Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 *(CAP 212)*, Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara *(CAP. 213), "Merchandise Act, R.E. 2002"*; na Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)*. Vilevile, mapendekezo ya kutungwa Sheria Mpya inayoruhusu kuanzisha Kampuni za Ubia *(Limited Liability Partnership)* yamekamilika. Aidha, Wizara imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Leseni za Udhibiti pamoja na mkakati wake. Sera hiyo inatoa mwongozo wa utoaji wa leseni za uthibiti ambazo kwa

hivi sasa hutolewa na taasisi mbalimbali za udhibiti na hivyo kuongeza gharama za kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha lengo la kukuza matumizi ya mfumo wa utambuzi wa bidhaa kwa kutumia nembo za mistari *(bar codes)* unaoratibiwa na Shirika la Kimataifa la *GSI* lenye ofisi zake huko Brussels Ubelgiji, Wizara inaendelea kuhamasisha wenye viwanda juu ya matumizi ya mfumo wa utambuzi wa bidhaa kupitia vikao mbalimbali vya wadau wa sekta.

Aidha, Wizara imekuwa ikisisitiza wajasiriamali na wenye viwanda wadogo juu ya umuhimu wa kutumia mfumo wa utambuzi wa bidhaa zao kwa kutumia nembo za mistari *(Bar Codes).* Tangu mwezi Agosti, 2011, utaratibu huo ulipoanzishwa, jumla ya Makampuni 151 yamejisajili kutumia huduma hiyo na takriban bidhaa 3,000 zimepata alama ya *GS1*. Aidha, baadhi ya viwanda vikubwa kama vile Kampuni ya Chai ya Kagera, Kampuni ya Bia Tanzania *(TBL)*, Tanzania *Distilleries Co. Ltd* yameanza kutumia nembo ya Tanzania. Vilevile, baadhi ya wasanii wa muziki wameanza kutumia nembo hizo na Wizara inaendelea pia kushirikiana na Wizara ya Habari na Maendeleo ya Vijana ili kuwashawishi wasanii zaidi kutumia huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, ufuatiliaji wa ununuzi wa zao la Korosho kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani umefanyika katika Mikoa yote inayozalisha zao hilo (Pwani, Mtwara, Lindi, Ruvuma na

Tanga). Changamoto kubwa iliyojitokeza katika msimu huu wa ununuzi wa zao la korosho ni kushuka kwa bei ya zao kulikosababisha korosho nyingi kutouzwa kwa wakati. Hadi kufikia Juni, 2012, takriban tani 14,000 za korosho kutoka mkoa wa Pwani na wilaya ya Tunduru zilikuwa hazijapata mnunuzi. Hata hivyo, Serikali imekamilisha taratibu za kuhakikisha kuwa wakulima wote wanalipwa sio chini ya Shilingi 1,200 kwa kilo ya korosho za daraja la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TanTrade* iliendelea na utafiti wa mifumo ya masoko na bidhaa zinazozalishwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga. Utafiti huo ni mwendelezo wa utafiti uliofanyika mwaka 2010/2011, katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Kigoma, Tabora na Singida unaokusudia kuweka Mfumo wa Mnyororo wa Thamani *(value chain)* kwa kuanzia na bidhaa za asali, ngozi na bidhaa za utamaduni. Wizara inategemea kukamilisha zoezi hilo mwaka ujao wa fedha kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TanTrade* iliendelea kuimarisha ofisi ya Zanzibar kwa kuweka vitendea kazi na mtumishi mmoja kwa lengo la kukuza uzalishaji na Biashara Visiwani Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo la kuendeleza uboreshaji, uundaji na uanzishwaji wa uzalishaji kibiashara wa matrekta madogo aina ya *CFT 221* na zana zake; kuendesha mafunzo kwa mafundi, waendesha matrekta na wasimamizi wao, Wizara kupitia *CAMARTEC* imekwishatengeneza matrekta

nane yaliyobuniwa ambayo yana matumizi mbalimbali *(multipurpose).* Kati ya matrekta hayo, matatu yalitumika katika majaribio Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Upungufu uliojitokeza kaika zoezi la majaribio ulifanyiwa marekebisho.

Aidha, matrekta mengine sita yapo katika hatua za matengenezo na yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Augosti 2012. Uzalishaji huo unatumia fedha za mkopo za utafiti chini ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambazo zitakiwezesha Kituo kutengeneza matrekta 14 na zana zake. Zana zitakazotengenezwa ni plau, jembe la matuta *(ridger)*, *harrow* na vifungasho *(attachments)* kama vile pampu za maji, mashine za kupukuchua, kukoboa na kusagisha nafaka. Mkopo fedha za utafiti kutoka Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia wa Shilingi milion 225 wa riba nafuu ya asilimia 0.25 kwa mwezi na utalipwa kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Juni 2012. Matrekta yatakayotengenezwa kwa kutumia mkopo huo yatakapokamilika, itakifanya Kituo kuwa kimetengeneza jumla ya matrekta 20. Matrekta yanayoendelea kutengenezwa na Kituo *(pre-commercial stage)* yanauzwa moja kwa moja kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuendeleza uzalishaji wa trekta la *CFT 221* na zana zake kibiashara, *CAMARTEC* itaanzisha kampuni ya ubia ya kutekeleza jukumu hilo. Mazungumzo kati ya *CAMARTEC* na *NDC* yanaendelea kwa nia ya *NDC* kuipatia kampuni hiyo eneo la kufanyia uzalishaji katika eneo la *Kilimanjaro Machine Tools Co. Ltd (KMTC)*, Moshi. Vilevile,

*CAMARTEC* wameongea na Benki ya Rasilimani Tanzania *(TIB)* kwa ajili ya kuipatia mkopo kampuni hiyo na *TIB* imeonesha utayari wa kutoa mkopo kwa kampuni hiyo itakapokuwa tayari. Takribani kiasi cha Shilingi billion tatu kinahitajika kwa ajili ya kuanzisha uzalishaji kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo la kuendeleza utafiti wa ufuaji umeme jadidifu kwa kutumia teknolojia ya biogesi, Wizara kupitia *CAMARTEC* imeendelea na majaribio ya kufua umeme kwa kutumia nishati ya biogesi ambapo jenereta kwa ajili hiyo zinatarajiwa kufungwa Chalinze, mkoani Pwani (kwa wakulima wa Msoga) na Wilaya ya Masasi (Gereza la Namajani). Mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na asasi ya *Rural Energy Agency (REA)*. Maeneo mengine yatakayohusishwa katika mradi huo wa ushirikiano na *REA* ni pamoja na Mbinga (Mlale JKT), Bukombe *(Seminari ya Queen of Apostles)* na Kasulu (Shule ya Sekondari St. Bakanja).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara kupitia *CAMARTEC* iliunda na kutengeneza mashine za kusindika mazao ya kilimo kama vile za kukamua nyanya kupata mbegu ambapo mashine tano zimeuzwa kwa wakulima wa eneo la Tengeru Arusha. Aidha, imeboresha mashine ya kupukuchua mahindi inayoendeshwa kwa trekta dogo lililoundwa na *CAMARTEC* na kubainika kufanya kazi vyema. Mashine ya kupukuchulia mahindi iitwayo *Vicon* yenye uwezo wa kupukuchua gunia 200 kwa saa iko katika hatua za mwisho za kuikamilisha na kuizalisha kibiashara kwa kushirikiana na Shirika la Mzinga.

Pia, Kituo cha *CAMARTEC* kimeunda na kutengeneza mashine mpya ya kukatia malisho ya wanyama, kama ng'ombe, inayoweza kuendeshwa kwa injini ya *HP5.* Aidha, Wizara kupitia *CARMATEC* imebuni na kutengeneza mashine za kuvunia mpunga inayoendeshwa na trekta dogo aina ya *power-tiller.* Lengo la ubunifu ni kuwapunguzia wakulima wadogo wadogo suluba ya kuvuna mpunga na kuongeza tija katika kilimo cha mpunga nchini. Utafiti wa mashine hii umekamilika na kituo kinaandaa taratibu za kumpata mbia wa kuzalisha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo la kuendeleza uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali zilizobuniwa na taasisi za utafiti, sambamba na kutoa huduma katika viatamizi vilivyopo kwenye Taasisi za Utafiti; Wizara kupitia *CAMARTEC* imeeneza zaidi ya majiko 335 bunifu ya mkaa ya kutumia kwenye kaya; mashine 5 za kukamua nyanya kupata mbegu, mabomba 700 ya kutolea gesi kwenye mitambo ya biogesi *(dome pipes)*, mabomba 300 ya kuingiza gesi kwenye majiko ya biogesi *(burner pipes)* na majiko 61 ya kutumika kwenye taasisi (majiko 25 ya lita 200, majiko 16 ya lita 100, majiko 10 ya lita 50 na 10 ya lita 25).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo *(TEMDO)* imeendelea na uhawilishaji wa teknolojia ya kiteketezi cha taka ngumu za hospitali *(bio-medical solid waste incinerator)* pamoja na teknolojia ya kutengeneza briketi za mabaki ya mimea kwa kushirikiana na Shirika la Mzinga.

Viteketezi vimefungwa katika hospitali za Kibong'oto, Bagamoyo na Nzega. Kwasasa ufungaji wa kiteketezi unaendelea katika hospitali za Mount Meru. Uhawilishaji wa mashine za kutengeneza bidhaa za ngozi (mashine ya kukata mikanda, kuweka urembo na kukata pateni) umefanyika kupitia *SIDO* kwa ajili ya kuzitengeneza kibiashara.

Vilevile, *TEMDO* imehawilisha teknolojia za kusindika matunda na asali kupitia Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo *(SIDO)*. Aidha, *TEMDO* iliendelea kuboresha mashine na vifaa vya kusindika mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na mashine za kusindika maziwa (*cheese press, cup seal, pasteuriser*); kahawa (kumenya, kukaanga, kusaga); karanga (kukaanga, kumenya, kutoa siagi ya karanga); matunda na vifaa vya kusindika asali *(centrifugal honey extractor, honey strainer, honey press)*. Baadhi ya teknolojia (mashine na vifaa) hizi zimehawilishwa kupitia Shirika la *SIDO* kwa lengo la kuzitengeneza na kuzisambaza kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika hilo, katika kutekeleza lengo la kutoa mafunzo na kuhamasisha wajasiriamali kwa kutumia viatamizi vya teknolojia mbalimbali, wajasiriamali 12 katika nyanja za usindikaji wa vyakula na utengenezaji wa briketi za mkaa waliendelea kupatiwa huduma kupitia Kiatamizi cha Teknolojia na Biashara na *TEMDO*. Vilevile, *TEMDO* imeendelea kubuni na kuendeleza teknolojia mpya zikiwemo mashine na vifaa kwa ajili ya machinjio ya kuku *(slaughtering cones, hot water scalder, chicken*

*plucker);* uendelezaji wa teknolojia za kuongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mabaki ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TEMDO* iliendelea kutoa huduma za kihandisi katika viwanda mbalimbali nchini hususan viwanda vya kusindika vinywaji (bia na mvinyo), kiwanda cha kutengeneza bidhaa za umeme na sukari. Mafunzo juu ya kutambua vihatarishi, ukadiriaji wa hatari, uchunguzi wa ajali na matukio hatarishi pamoja na kutunza na kuweka mfumo wa utawala wa mazingira kwa wajumbe wa Kamati za Usalama na Afya Sehemu ya Kazi yalifanyika kwa viwanda vya kutengeneza sukari *TPC Ltd*., Moshi na kiwanda cha kutengeneza mvinyo cha Banana *Investment* Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda *(TIRDO)* likishirikiana na *TEMDO* na kampuni binafsi liko katika hatua za awali za kuhaulisha teknolojia ya kurejeleza plastiki. Moja ya juhudi hizo ni kugawana majukumu ya usanifu wa mitambo. Hii itafanya mitambo ya kurejeleza plastiki kuzalishwa hapa nchini na inategemewa kusambaza teknolojia hii sehemu nyingi na kupunguza kero za taka za plastiki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* limeendeleza ujenzi wa majengo ya viatamizi vya *TEHAMA* na usindikaji wa mazao ya kilimo kwa ajili ya kuendeleza viwanda na wajasiriamali. Vilevile, *TIRDO* imetengeneza makaushio sita yanayotumia nishati ya jua na kuyasambaza kwenye vitongoji vitatu Wilayani Mkuranga. Wajasiriamali wapatao 116 walipata

mafunzo ya jinsi ya kutumia makaushio hayo kukausha mboga na matunda ili zisiharibike na kuwawezesha kuuza katika masoko ya ndani. Shirika la *TIRDO* lilipata fedha za utafiti chini ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia za kuendeleza utafiti wa kaushio la jua. Aidha, Shirika linafanya majaribio ya kuboresha kaushio hilo kufikia viwango vya kanda ya Afrika. Lengo kuu la mradi huo ni kutengeneza kaushio linaloweza kutumiwa na wafanyabiashara hasa katika kukausha muhogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* limeendelea kutoa huduma za upimaji wa uharibifu wa mazingira unaotokana na uzalishaji wa viwandani na kutoa ushauri wa utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika uzalishaji wa viwandani kwenye sekta ndogo ya chuma, tumbaku, plastiki na ngozi katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Tanga na Iringa. Viwanda vilivyopata huduma hiyo, kwa sasa uchafuzi wa mazingira uko katika viwango vinavyokubalika kimataifa. Vilevile, Shirika la *TIRDO* linaendelea kuhakiki ubora wa vifaa vya kihandisi kama *panton* na matanki ya mafuta. Katika, kutoa huduma hiyo vifaa vya kisasa kama *X-ray machines*, *ultrasonic testing machines* hutumika. Vilevile, wataalamu wamepata mafunzo ya utaalam huo huko Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* kwa kushirikiana na Benki ya Rasilimali (TIB), pia limeweza kufanya ukaguzi wa kitaalamu *(technical assessment)* katika viwanda vitano vya kusindika mazao ya kahawa, maziwa, matunda, nyama na maji vilivyopo Rombo, Bukoba, Sumbawanga, Arusha na Dar es

Salaam ili kutoa ripoti ya kitaalamu itakayowezesha viwanda hivyo kupata mkopo toka Benki hiyo. *TIRDO* pia limetumiwa na *NDC* kuwa mshauri mwelekezi katika kufanya upembuzi yakinifu na kutathmini mitambo iliyopo katika kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools Company Ltd (KMTC)* na kisha kutoa ushauri juu ya hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kufufua uzalishaji katika kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* limetengeneza mashine zinazotumika kusindika vyakula na matunda *(Hammer mill, Juice extractor)*, mashine ambazo zimetumia malighafi zisizo na madhara kwa walaji na zinazokubalika kimataifa kama vile chuma cha pua *(stainless steel)* au *manganese steel*. Bei za mashine hizo ni mara mbili hadi nne za mashine zinazotumika sasa lakini hudumu zaidi ya miaka nane na kukidhi viwango vya Kimataifa, ukilinganisha na mashine za kawaida huchakaa ndani ya mwaka mmoja na kuzalisha bidhaa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kisasa ili viwanda vya ngozi nchini vipunguze uharibifu wa mazingira, Wizara kupitia Shirika la *TIRDO*, linatekeleza mradi wa kurejeleza taka za ngozi viwandani na kuzalisha bidhaa kama *Leather board* katika juhudi za kuimarisha sekta ya ngozi. Kwa kuanzia, mradi utaangalia takwimu za uchafuzi wa mazingira unaotokana na viwanda vya ngozi katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro na Mwanza. Aidha, *TIRDO* iko katika hatua ya kununua vifaa vya maabara baada ya kupata fedha za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukamilisha mchakato wa kuhakiki na kuboresha maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi ili iweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani, Shirika la *TIRDO* limeendelea na shughuli zitakazoiwezesha maabara ya mazingira kupata uhakiki ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa maabara kwa kuagiza vifaa vifuatavyo, *dragger pump with its detectors testing tubes*, *Multi probe system and Dust sample*.

Vilevile, shirika limewapeleka mafunzoni watafiti wawili wa ndani wa maabara ya mazingira kwenye mafunzo ya *Method Validation and Measurement of Uncertainty* kutoka kwa mtaalamu aliyetoka Afrika ya Kusini. Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*. Vilevile, maabara imeweza kujiandikisha katika mfumo wa kuhakiki matokeo ya upimaji kwa ustadi *(Proficiency Testing)* wa hewa ili kuweza kutoa matokeo yenye uhakika zaidi yanayozingatia kiwango cha kimataifa cha *ISO/IEC 17025.* Maabara nyingine ziko katika hatua mbalimbali za uhakiki na kwa sasa taasisi kupitia Wizara inatafuta fedha za kuendeleza uhakiki huo. Shirika linategemea baada ya kuhakiki maabara zake litapata wateja zaidi na matokeo ya majaribio hayo kukubalika ulimwenguni kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa mazao ya kilimo yanaingia katika masoko ya kimataifa, *TIRDO* imekuwa inatekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa mazao *(traceability)*. Mfumo huu ulifanyika kwa mazao

ya chai, kahawa, korosho na samaki wa maji baridi kwa ufuatiliaji wa kujaza taarifa kwenye karatasi *(paper based tracebility system)* katika viwanda vya usindikaji wa mazao hayo. Majaribio (*Mock recall)* yalionesha mafanikio kwa kiwango kikubwa kwani kumbukumbuku zote ziliweza kupatikana na kuhifadhiwa kwa uhakika. Hata hivyo, tatizo la upatikanaji wa fedha lilifanya mfumo huu wa ufuatiliaji kushindwa kuwekwa kwenye mfumo wa kikompyuta *(computerised traceability system)* ili kuboresha zaidi mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa huduma viwandani zinazolenga matumizi ya teknohama, Shirika la *TIRDO* limeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusaidia Wajasiriamali Wasindikaji *(Agro-processors)* katika kupata masoko ya bidhaa zao zinazotokana na usindikaji wa mazao ya kilimo. Shirika pia limeendelea kutoa ushauri wa kiufundi kwa wajasiriamali na wadau wengine kuhusu manufaa ya matumizi ya mifumo ya utambuzi wa bidhaa kwa kutumia nembo za mistari.

Kutokana na juhudi hizo, makampuni 151 yamesajiliwa katika matumizi ya nembo za mistari na bidhaa 3,000 zimepata nembo za mstari. Aidha, Shirika limeweza kuunda tovuti 77 za wajasiriamali katika mikoa ya Pwani, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Lindi na kutoa mafunzo juu ya matumizi ya tovuti hizo kwa lengo la kujitangaza. Jitihada hizo zimewezesha jumla ya wajasiriamali 14 kupata nembo za ubora za *TBS, TFDA* na nembo za mistari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali wadogo ili kuwasaidia

kufanya biashara zao kisasa zaidi, Chuo cha Elimu ya Biashara, kimeendesha kozi tatu za muda mfupi kwa jumla ya wajasiriamali 163. Mafunzo hayo yalikuwa katika maeneo yafuatayo: Namna ya kubuni na kusimamia miradi, Usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine kama watu *(HRM)*, Njia bora za utunzaji wa kumbukumbu za biashara na mbinu za kuimarisha ubora wa bidhaa na huduma zitolewazo na wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo la kuandaa mitaala ya kozi ya ujasiriamali katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada, Chuo kimeanza kutekeleza mpango wa kuandaa mafunzo ya ujasiriamali kupitia mradi wa *'Netherlands Initiatives for Capacity Building of Higher Education'*. Katika mradi huo Chuo kitaandaa mitaala ya ujasiriamali katika ngazi za astashahada, stashahada na shahada. Mitaala hiyo itapitiwa na kupata kibali kutoka kwa Baraza la Ithibati *(NACTE)* kabla ya utekelezaji.

Mradi huo kwa sasa uko katika hatua zake za awali *(Inception Stage)*. Chuo kimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kubadilisha matumizi ya eneo la Nzuguni kutoka kuwa bustani ya wanyama *(Capital Zoo)* kwa mujibu wa taratibu na kuwa eneo la Ujenzi wa taasisi ya Elimu. Chuo kimeweza pia kufuatilia na kufanikiwa kupata hati miliki ya eneo la Nzuguni. Kwa upande wa eneo la Kiseke Mwanza, Chuo kimefanikiwa kulipia gharama za fidia zilizokuwa zikidaiwa. Kati ya Shilingi milioni 243 zilizokuwa zikihitajika, Chuo tayari kimelipa Shilingi milioni 203, kati

ya hizo Shilingi milioni 103 zikiwa zimelipwa katika kipindi cha mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* imeendelea na juhudi za kuziwezesha maabara zake kufikia viwango vya upimaji vya kimataifa *(Laboratory Accreditation).* Lengo ni kuziwezesha maabara hizo kupima sampuli na kutoa taarifa za upimaji *(Test reports)* zinazotambuliwa duniani kote. Maabara hizo ni za Uhandisi Umeme, Uhandisi Mitambo na Uhandisi Ujenzi ambazo miongozo yao ya ubora imekamilishwa kulingana na kiwango cha kimataifa *ISO 17025*. Hatua inayofuata ni kufanyiwa tathmini na Shirika la *SANAS* la Afrika ya Kusini ili kuthibitishwa umahiri wa upimaji katika nyanja za nyaya za umeme, nondo na saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* imekamilisha utaratibu wa upimaji wa ubora wa bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja Tanzania *(Pre-shipment Verification of Conformity to Standards - PVoC).* Utekelezaji ulianza rasmi tarehe 01 Februari, 2012 na makampuni matatu (3) yamepatikana kwa njia ya ushindani wa Kimataifa. Makampuni yaliyofanikiwa kupata zabuni ya kufanya kazi hiyo ni *M/S Intertek International Ltd ya Uingereza; M/S Bureau Veritas Inspection, Valuation and Control (BIVAC)* ya Ufaransa; na *M/S SGS Societe Generale De Surveillance S.A.* ya Uswisi. Baada ya utaratibu huo kuanza, bidhaa zenye ubora hafifu ikiwa ni pamoja na zile za bandia zimeanza kupungua katika soko la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza ufanisi na kuimarisha ukaguzi wa ubora wa bidhaa yakiwemo magari yaliyotumika, Wizara imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha uongozi wa shirika, kuyafungia makampuni ya ukaguzi ya *WTM Utility Services* ya Uingereza, na Jaffar *Mohamed Garage* ya Dubai, ambayo yamekuwa yakikiuka taratibu za ukaguzi wa magari kwa kutokuwa na vifaa na utaalam unaohitajika na kuchelewesha malipo ya ukaguzi.

Shirika pia limeendelea kuimarisha utaratibu wa kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za ukaguzi wa ubora toka kwa mawakala kwa kuzishirikisha Idara za Uthibiti Ubora, Huduma za Shirika na Kitengo cha Fedha (Uhasibu) na kufanya kazi kwa karibu na Mamlaka ya Mapato nchini, Tume ya Ushindani, Jeshi la Polisi na Mamlaka za Miji na Majiji husika. Kwa upande wa ukaguzi wa bidhaa kupitia *PVoC,* mapendekezo ya wadau yatawezesha pia kuangalia uwezekano wa kutenganisha bidhaa zinazohitaji kukaguliwa ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia makundi tofauti ya wafanyabiashara wa Tanzania (wakubwa, wa kati na wadogo) bila kuathiri ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ushauri uliotolewa na Kamati za Bunge, Wizara imeunda Kikosi Kazi kinachowajumuisha Wajumbe kutoka Taasisi za Umma na Sekta Binafsi ili kuishauri Serikali kuhusu utaratibu mzuri zaidi wa kukagua bidhaa nje ya nchi ikiwa ni pamoja na magari.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba nimepokea taarifa ya Kikosi Kazi tarehe 20 Julai, 2012. Taarifa hiyo ina mapendekezo kwa ajili ya kuishauri Serikali kuhusu utaratibu zaidi wa kukagua bidhaa nje ya nchi ikiwa ni pamoja na magari.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Wizara itayafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Kikosi Kazi. Baadhi ya mapendekezo ya Kikosi Kazi ni pamoja na: Kuishauri Serikali kutangaza upya mchakato wa kuwapata mawakala wa ukaguzi wa magari nje ya nchi kwa kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004; Kupata maoni ya wadau kuhusiana na mahitaji ya maboresho ya Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 ili kuangalia uwezekano wa ukaguzi wa magari kufanyika ndani au nje ya nchi au yote kwa pamoja. Tayari baadhi ya Taasisi za Serikali zikiwemo Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)* na *VETA* zimeonesha nia ya kufanya ukaguzi wa magari ndani ya nchi; na kuangalia upya muundo wa *TBS* hususan Idara ya Ubora na Udhibiti na vilevile, kuwa na ratiba ya mzunguko kwa watendaji baada ya muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* hadi kufikia mwezi Machi, 2012 imetoa jumla ya leseni 90 za ubora wa bidhaa mbalimbali kwa wazalishaji wa hapa nchini ambao walitimiza masharti ya ubora wa bidhaa zikiwemo zile zinazogusa afya na usalama wa walaji, mazingira na uchumi wa Taifa. Idadi hii ni sawa na asilimia 75 ya lengo zima la kutoa leseni 120 kwa mwaka 2011/2012. Leseni za ubora zitawezesha bidhaa husika kushindana kikamilifu katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania iliendelea na utoaji wa mafunzo ya ufungashaji bora kwa wajasiriamali wadogo na kati *(SMEs)* wapatao 248 hadi kufikia mwezi Machi 2012 katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya. Mafunzo hayo hutolewa kuwasaidia wajasirimali wadogo ili waweze kupata nembo ya ubora ya *TBS* kwa lengo la kuongeza uwezo wa kushindana katika soko. Aidha, Wizara inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kupimia vifungashio mbali mbali. Vilevile, katika kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi, hadi kufikia mwezi Machi 2012 Shirika la Viwango lilitoa vyeti vya ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje vipatavyo 1,945 sawa na asilimia 69.5 ya lengo la vyeti 2,800 kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania iliendelea na upimaji wa sampuli za bidhaa kutoka viwanda mbalimbali nchini na nchi za nje vikiwemo vya wajasiriamali wadogo na wa kati *(SMEs)*. Hadi kufikia mwezi Machi, 2012 lilikuwa limepima jumla ya sampuli 6,019 katika maabara mbalimbali za Shirika, idadi hii ni sawa na aslimia 65 ya lengo la mwaka la kupima sampuli 9,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Baraza la Ushindani katika mwaka 2011/2012 ilikuwa na kesi kumi na tatu zilizokuwa zinaendelea kusikilizwa ambazo zilisajiliwa mwaka 2010/2011. Aidha, Baraza lilisajili kesi mpya kumi na hivyo kufanya idadi ya kesi za kusikilizwa katika kipindi cha 2011/2012 kuwa ishirini na tatu Hadi kufikia mwezi Aprili, 2012 kesi tisa zilikuwa zimesikilizwa

na kutolewa maamuzi na kumi na nne zilikuwa katika hatua mbalimbali za mchakato wa usikilizwaji. Lengo la Baraza ni kesi kusikilizwa na kutolewa maamuzi katika miezi isiyozidi sita tangu tarehe ya kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uwezo zaidi wa Baraza katika kushughulikia kesi hizo, Baraza limeweza kutekeleza malengo yake ya kujenga uwezo zaidi wa Baraza katika kushughulikia kesi kwa kupata mafunzo mbalimbali. Katika kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza katika Uchumi; Baraza limeweza kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia warsha, semina na vyombo vya habari juu ya kazi zake ili kujenga uelewa na ufahamu wa wadau. Katika mwaka 2012/2013, Tume itaendelea kutoa elimu kwa wadau kikanda. Wizara kupitia Baraza la Ushindani iliweza kuchambua Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003 na kubainisha upungufu unaosababisha Baraza lisifanye kazi kwa ufanisi uliokusudiwa. Aidha, Baraza limefanikiwa kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo ambayo yamewasilishwa Serikalini pamoja na mapendekezo yaliyopendekezwa na Tume ya Ushindani ili yaweze kufikishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo *(WMA)* iliendelea na majukumu ya kukagua, kuhakiki na kusimamia usahihi wa Vipimo vinavyotumika katika biashara ili kumlinda mlaji. Jumla ya vipimo 545,506 vinavyotumika katika biashara vilikaguliwa na wafanyabiashara 5,503 walipatikana na makosa ya kukiuka Sheria ya Vipimo. Katika kuhakiki vipimo vya mita za umeme, mita za maji

na mitungi ya gesi ya kupikia, Wakala imekamilisha taratibu za ununuzi wa vifaa vya kukagua mita za maji.

Aidha, Kitengo cha Wakala wa Vipimo bandarini kimeanza ufuatiliaji wa mfumo wa upimaji, ujazaji na ufungashaji kwenye mitungi ya Gesi inayotoka nje na Gesi Asilia inayozalishwa hapa nchini. Lengo ni kuhakiki usahihi wa vipimo vinavyotumika katika uuzaji wa Gesi bila kumpunja mtumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za Kitengo cha Vipimo Bandarini, Wakala wa Vipimo imewezesha watumishi saba kupata mafunzo ya usimamizi wa biashara ya mafuta na vipimo nchini Marekani. Aidha, vitendea kazi kama *standard densitometer,* kipimajoto kwenye matenki ya mafuta melini na *offshore* vimenunuliwa. Katika kutimiza lengo la kuendelea kukagua usahihi wa bidhaa zilizofungashwa *(quantities in pre-packed goods)* zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini na pia kutoka nje ya nchi, kitengo cha ukaguzi bandarini kwa bidhaa zilizofungashwa *(pre-packed goods)* kimeanzishwa na maandalizi ya hatua za utekelezaji wa majukumu yake unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vipimo imekamilisha ununuzi wa kiwanja eneo la misugusugu, Pwani. Kiwanja hiki kitatumika kwa ujenzi wa kituo cha kisasa cha kupimia ujazo wa matenki *(Calibration Bay)* ya malori ya kusafirisha mafuta ya nishati hapa nchini na nchi jirani. Hati ya kiwanja hicho imekabidhiwa kwa Wakala na kazi ya ujenzi wa uzio imekamilika. Aidha, Wakala wa Vipimo inaendelea kuimarisha ofisi zake

mikoani kwa kuanza kununua viwanja *(plots)* 15 ili hatimaye yajengwe majengo kwa ajili ya ofisi zake mikoani. Hatua hiyo itaiwezesha Wakala kuwa na ofisi zinazokidhi mahitaji ya kitaalamu na pia kupunguza gharama za pango, kwani ofisi nyingi za Wakala hivi sasa zipo katika majengo ya kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vipimo *CAP 240 RE* 2002 yanayolenga kupanua wigo wa matumizi ya vipimo rasmi kutoka sekta ya biashara na kuhusisha pia sekta za afya na mazingira. Aidha, marekebisho yanazingatia maridhiano yaliyofikiwa na nchi kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo inaendelea na kuelimisha umma juu ya masuala ya vipimo sahihi kupitia televisheni, redio, magazeti, vipeperushi, kalenda pamoja na kushiriki maonesho mbalimbali hapa nchini. Jumla ya vipindi 20 vya televisheni viliandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, jumla ya vipindi 10 vya redio, taarifa 37 za magazeti ziliandaliwa. Vile vile, Wakala ilishiriki jumla ya maonesho 5 ya Kitaifa ambayo ni; Sabasaba, Nanenane, *SIDO* na Maonesho ya Mwanamke Mjasiriamali – *Month of Women Enterpreneurs (MOWE).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya mizani ya rula *(steel yard)* katika ununuzi wa zao la pamba, Wizara yangu kama nilivyoahidi katika Kikao cha Bunge la Bajeti la mwaka 2011/2012, ilikamilisha taratibu za kisheria za kuondoa matumizi ya mizani ya rula na kutangazwa kupitia *GN NO. 47* ya mwaka 2012.

Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Juni, 2012, ni kiasi cha mizani 2,460 tu ambazo zilikuwa zimeingizwa nchini ikilinganishwa na mahitaji ya mizani zaidi ya 9,000.

Kutokana na kutokamilika kwa ununuzi wa mizani za dijitali ambazo ndizo zilizopendekezwa na wadau, Serikali baada ya majadiliano na wadau wa zao kupitia vyama vyao vya *Tanzania Cotton Association (TCA)* na *Tanzania Cotton Growers Association (TACOGA)* imeruhusu matumizi ya mizani za rula sanjari na mizani za dijitali kwa msimu huu ili kutoathiri ununuzi wa pamba ambao umeanza tarehe 2 Julai, 2012.

Chama cha Wakulima wa Pamba (*Tanzania Cotton Growers Association* kwa kushirikiana na Chama cha wanunuzi wa Zao la Pamba *(Tanzania Cotton Association)* wameandaa mpango wa kuondoa matumizi ya mizani ya rula hatua kwa hatua kadiri upatikanaji wa mizani za dijitali utakavyokuwa unapatkana. Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imekamilisha uhakiki wa mizani hizo za aina mbili. Aidha, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo, inaendelea kuelimisha umma juu ya masuala ya vipimo kupitia televisheni, redio, magazeti, vipeperushi, kalenda pamoja na kushiriki maonesho mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imekamilisha kazi ya kuingiza taarifa zake zote za Makampuni na Majina ya Biashara yaliyosajiliwa katika mfumo wa kielektroniki na wanaendelea kuunganisha mfumo huo na Mfumo wa Usajili *(Registry Management System-RIMS)*. Mifumo hiyo imeanza kutumika kusajili makampuni (siku tatu) na majina ya biashara kwa muda mfupi zaidi siku moja

iwapo nyaraka zote muhimu zimekamilika. Aidha, utaratibu huo umerahisisha ulipaji kwa kutumia mabenki kupokea ada mbalimbali. Vilevile, *BRELA* na *TRA* inakamilisha utaratibu wa kutoa Hati ya Kumtambulisha Mlipa Kodi *(TIN)* mara tu anaposajili kampuni au jina la biashara. Hatua hiyo inatarajia kuwaondolea adha wateja wa *BRELA* na *TRA* ya kulazimika kwenda *TRA*, baada ya kusajili Makampuni au Majina ya biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua upungufu ya uwezo wa matumizi ya mitandao kwa watanzania wengi hasa wanaojihusisha na biashara ndogo ndogo mijini na hasa vijijini kutokana na changamoto mbali mbali, *BRELA* imekubaliana na Chama cha Wafanya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania *(TCCIA),* kusaidiana na wadau wengine wakiwemo, Mawakili, Wahasibu binafsi ambao hutoa huduma ya matumizi ya mtandao huko huko wilayani ambako hadi sasa *TCCIA* ina mtandao katika wilaya tisini na tano. Aidha, *BRELA* ikishirikiana na *TCCIA* imetoa mafunzo ya kutoa huduma hiyo kwa wadau tajwa. Ushirikiano huo utapunguza gharama za kufanya biashara na kupanua wigo na wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imeendelea kusajili Majina ya Biashara papo kwa papo katika maonyesho mbali mbali yanayofanyika kitaifa. Hadi sasa majina ya biashara 1,408 yamesajiliwa kwa njia hiyo ambayo imeonekana kuwa na manufaa sana kwa wajasiriamali wadogo wadogo waliotapakaa nchi nzima na kuwaondolea gharama isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Miliki Ubunifu BRELA kwa kushirikiana na Miliki la Dunia *(WIPO)* inaendelea na mpango wake wa kuhifadhi takwimu kutoka kwenye majalada na kuziweka katika mfumo wa kielektroniki *(Automated Intellectual Property System (IPAS).* Mfumo huo unakusudia utahusisha pia suala la utoaji wa Hataza, hatua ambayo ipo katika ngazi za mwisho. Aidha, *BRELA* imeendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa wazalishaji bidhaa na watoaji huduma kutumia Alama za Biashara katika bidhaa wanazotengeneza na za Huduma wanazozitoa, ili kuzitofautisha bidhaa zao na au huduma zao na bidhaa na au huduma zinazofanana za washindani wengine. Njia hiyo imekwishaonesha mafanikio ya kuongezeka kwa thamani ya bidhaa na huduma za wafanyabiashara wanazingatia kwa usahihi wa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kupitia *BRELA*, imefanya mapitio ya Sheria za Makampuni ya mwaka 2002, Majina ya Biashara sura 213 ambayo ilijumuishwa katika mswada wa kurekebisha sheria mbali mbali za biashara uliopitishwa na Bunge hili katika kikao chake cha mwezi Aprili, 2012. Marekebisho hayo ni pamoja na kuwezesha mtu mmoja kumiliki hisa zote kwenye kampuni *(Single Shareholder)na* pia itaruhusu matumizi ya mwongozo wa kurahisisha maandalizi ya nyaraka za usajili wa kampuni na fomu inayopatikana katika mtandao. Marekebisho hayo yanaruhusu matumizi ya fomu kwa lugha ya Kiswahili, kupanua wigo wa mawasiliano na wateja kwa kuongeza mawasiliano kwa njia ya nukushi, mtandao wa kompyuta na simu za viganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Leseni za Viwanda sura 46 inafanyiwa mapitio ili kuangalia kama inakidhi matakwa ya sasa ya Uwekezaji. Lengo la sheria hiyo ni pamoja na kuratibu uanzishwaji wa viwanda na kukusanya takwimu zinazohusiana na viwanda. Hamasa zinaendelea ikiwa ni pamoja na ukaguzi elekezi usiolenga udhibiti tu. Nia ni kuhamasisha wazalishaji kwa hiari yao waone umuhimu wa kupata leseni za viwanda na kuvisajili kwani kwa kufanya hivyo, wamiliki wa viwanda hivyo huweza kupata punguzo la ushuru wakati wa kuingiza nyenzo na zana za kuzalishia ikiwa ni pamoja na mali ghafi za uzalishaji zinazotoka nje. Aidha, imebainika kuwa utaratibu wa awali haukuwa na mvuto mkubwa hasa kwa wajasiriamali wadogo kutokana na ada kubwa ya kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imefanikiwa kupata kiwanja eneo la Ada *Estate* katika Manispaa ya Kinondoni – Dar es Salaam ambako inatarajia kujenga ofisi zake na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea. Jitihada za Kazi ya usanifu wa majengo umekwishafanyika na tathmini na mapendekezo yamewasilishwa kwenye Bodi ya Zabuni. Pia, kutokana na utendaji mahiri, *BRELA*, ilitunukiwa tuzo ya *"International Arch of Europe Quality Award 2012, Gold Category* na *Business Initiative Directions B.I.D* katika Mkutano wa 38 uliofanyika *Frankfurt*, Ujerumani, mwezi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza huduma za usajili na utoaji wa leseni za viwanda,

Wakala imesajili Makampuni 7,058 ikiwa ni ongezeko la Makampuni 1,780 ukilinganisha na makampuni 5,278 yaliyosajiliwa 2009/2010, Majina ya Biashara 14,866 yalisajiliwa mwaka 2010/2011 yakilinganishwa na Majina ya Biashara 11,127 yaliyosajili mwaka 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 34. Kwa upande wa alama za biashara na huduma maombi yaliongezeka kutoka 1,259 kwa mwaka 2009/2010 hadi 2,502 kwa mwaka 2010/2011 hili ni ongezeko la asilimia 99. Hali kadhalika, kwa upande wa leseni za Viwanda, *BRELA* ilitoa leseni 105 kwa mwaka 2010/2011 ukilinganishwa na leseni 99 zilizotolewa kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo ililojiwekea la kutangaza shughuli za Tume kwa umma ili kuongeza utekelezaji wa sheria *(compliance),* Wizara kupitia Tume ya Ushindani, imefanya semina katika mikoa mitano kwa lengo la kuelemisha umma juu ya kazi na majukumu yake kama yalivyoanishwa katika Sheria ya Ushindani No. 8 ya 2003 katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Dodoma, Morogoro na Singida.

Tume inatarajia pia kuandaa semina katika mikoa ya Mbeya na Iringa kufuatana na uwezo wa kifedha. Kutokana na semina hizo, Tume imeweka kwa wadau wa masuala ya ushindani na kujua changamoto za ushindani na pia wafanyabiashara kupata hamasa ili kuchangamkia fursa zinazoletwa na ushindani na imeweza kuibua masuala yanayofifisha ushindani, kwa mfano katika semina ziliyofanyika Tume iliweza kuibua masuala ya ushindani kwa sekta mbali mbali, na muungano wa Makampuni ambayo hayakutoa taarifa

na masuala mengine ambayo Tume inaendelea kuyachambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumuelimisha na kumlinda mlaji, Wizara kupitia *FCC* imetoa elimu kwa mlaji kwa kushiriki katika maonesho ya SabaSaba na NaneNane. Pia, Wizara kupitia Tume imetoa elimu kwa mlaji na wafanyabiashara kupitia mpango wa semina kwa wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo unaoendeshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* katika Manispaa za Ilala Karikoo tarehe 19 Aprili, 2012, Segerea tarehe 25 Aprili, 2012; na Temeke Kigamboni tarehe 15 Machi, 2012. Lengo la mafunzo hayo ni kuwa na waelimishaji ambao sambamba na majukumu yao ya kila siku watakuwa tayari kusambaza elimu ya mlaji katika maeneo mbali mbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Tume imefanya tathmini ya mafunzo yaliyotolewa awali kwa waelimishaji wa masuala ya kumlinda mlaji katika mikoa ya Dodoma na Mtwara. Lengo la tathmini hiyo ni kupima mafanikio na changamoto katika utoaji wa elimu ya mlaji katika maeneo yao. Mapendekezo ya waelimishaji hao yatasaidia katika kubuni mikakati itakayoboresha utoaji wa elimu kwa mlaji katika maeneo mbali mbali nchini.

Vilevile, Wizara kupitia Tume imeweza kufanya mchakato wa Tenda ya kutafuta Mshauri Mwelekezi katika masuala ya matangazo ya biashara katika Radio na Televisheni, tenda hiyo imetangazwa na kufunguliwa. Tenda inasubiri kibali cha Tenda Bodi ya Tume kumthibitisha mzabuni aliyeshinda. Lengo la

utafiti huu ni kufahamu jinsi gani matangazo ya biashara yanaweza kuchochea (kwa njia ya upotoshaji) utashi wa mlaji juu ya ununuzi wa bidhaa na huduma pia kufahamu ukubwa wa tatizo hili katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza lengo la kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kama radio, luninga na magazeti kuhusiana na bidhaa bandia na madhara yake kwa binadamu na mali zake, Wizara kupitia Tume ya Ushindani, imerusha hewani matangazo madogo yapatayo 32 kati ya mwezi wa saba 2011 na mwezi wa tatu 2012. Aidha, Tume ilishiriki katika maonesho ya wiki ya utumishi wa Umma Dar es Salaam. Maonesho ya 35 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam, Julai, 2011, maonesho ya Wakulima (Nane Nane) na maonesho ya Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru, Desemba, 2011. Katika maonesho hayo, Tume ilitoa mafunzo kwa vitendo kuhusu namna ya kutambua bidhaa bandia.

Vile vile, Tume imefanya semina kwa wadau mbali mbali katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Mara, Mwanza, Dodoma na Morogoro kati ya Julai na Desemba, 2011. Wadau zaidi ya 600 walifikiwa katika Mikoa hiyo kutoka katika jumuiya za wafanyabiashara (*TCCIA, CTI* na wafanya biashara mmoja mmoja), Wazalishaji viwandani, Wanasheria, Maafisa biashara, Maofisa wa mamlaka ya Mapato *(TRA),* Polisi na Watumishi wa Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume, pia inashiriki katika shughuli na mikutano inayoratibiwa na

Jukwaa la Mlaji Tanzania *(Tanzania Consumer Forum)* ambayo inaandaa Jarida la Sauti ya Mtumiaji na Sera ya Utetezi wa Mlaji Tanzania. Vile vile, Wizara kupitia Tume imeshiriki katika mikutano ya kimataifa kwa njia ya simu *(Monthly Teleconferencing)* kujadili masuala mbali mbali ya utetezi wa mlaji; maandalizi na maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mlaji *"World Consumer Rights Day"* inayoadhimishwa tarehe 15 Machi kila mwaka ambayo mwaka huu 2012 yalifanyika Jijini Mwanza, hivyo kwa mara ya kwanza, yamefanyika nje ya Dar es Salaam.

Maadhimisho hayo yalijumuisha shughuli mbali mbali zilizolenga kutoa elimu kwa mlaji hususan mkutano na vyombo vya habari *(Press Conference),* vipindi na mijadala katika Radio mbali mbali ambazo ni *"Radio Free Africa"," Kiss Live.* Kongamano na Wanafunzi wa Vyuo vya Biashara *(CBE)* na St. Augustine, shule za sekondari na maonesho ya siku nne katika viwanja vya Makongoro-jijini Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Tume imefanya kazi ya Mapitio ya Mikataba baina ya Mlaji na Muuzaji *(review of standard form contracts).* Rasimu ya Kanuni za "*Standard Form Contract*" imeandaliwa. Aidha, Tume imeweza kuandaa kanuni za kumlinda mlaji Tanzania *(consumer protection regulations).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni ya kutafuta Mshauri Mwelekezi *(Consultant)* imetangazwa ambapo jumla ya maombi manne yamewasilishwa na kuchambuliwa.

Kutokana na elimu iliyotolewa katika semina mbalimbali, Wizara kupitia Tume imepokea jumla ya malalamiko 30 kutoka kwa walaji kuhusu bidhaa na huduma mbali mbali ambazo hazijakidhi matarajio au matumizi yaliyokusudiwa *(unmerchatable goods and services).* Tume hutoa ushauri wa kisheria ikiwa ni sehemu ya elimu kuhusu Sheria ya Ushindani hususan vifungu vinavyomlinda mlaji, kwa pande zote mbili (muuzaji na mlaji) za mgogoro na kufanya pande zote mbili kuweza kuafikiana kumaliza mgogoro kwa njia ya amani. Endapo suluhu haijafikiwa, upande usioridhika huwa na haki ya kisheria kufungua kesi ya madai Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, bidhaa zilizolalamikiwa kwa kiwango kikubwa ni bidhaa za elektroniki na vifaa vya umeme, simu za viganjani, komputa *(Laptops)*, luninga, feni, betri za magari na za simu na jenereta. Katika malalamiko yote 30 malalamiko 14 yalitatuliwa kwa makubaliano kati ya mlalamikaji na mlalamikiwa (mlaji na muuzaji) chini ya usimamizi wa Kitengo cha Kumlinda Mlaji, malalamiko yapatayo 12 ya walalamikaji hawakuleta vielelezo na malalamiko yapatayo manne yanaendelea kufuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupambana na kudhibiti makampuni yanayokula njama kwa pamoja kupanga bei, na kwa kudhibiti kiasi cha bidhaa inayopelekwa kwenye soko *(output restrictions between competitors),* Wizara kupitia Tume ya Ushindani inashughulikia lalamiko moja linalohusu

kampuni za mafuta kuthibiti bidhaa za mafuta kuingia sokoni na kusababisha uhaba. Lalamiko hili ambalo lilifikishwa mbele ya Tume liko katika hatua za mwisho za uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha lengo la kufanya uchunguzi wa masoko na kusikiliza kesi za ushindani, katika mwaka 2011/2012, Tume ya Ushindani imefanya uchunguzi wa masoko na kesi nane ziko mbele ya Tume. Kesi hizo zinahusu masoko ya bidhaa za maziwa, sabuni, gesi, Umeme, tumbaku, sukari, vinywaji baridi na saruji. Tume inaendelea kusikiliza kesi tatu ikiwa ni sehemu ya utekelezwaji wa sheria ya ushindani *(enforcement)*. Kesi hizo zimefikia hatua mbalimbali za usikilizwaji. Pia, Tume ya Ushindani inakabiliwa na kesi moja ambayo ipo Mahakama Kuu na rufaa moja ambayo ipo Baraza la Ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2011/2012, Wizara kupitia Tume ya Ushindani, imepokea na kupitia jumla ya maombi 21 ya muungano wa Makampuni. Kati ya maombi hayo 18 yalipitishwa bila masharti. Maombi yaliyobaki bado yanashughulikiwa na yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Maombi yaliyopokelewa yanahusu sekta za fedha, kilimo, huduma, madini, mafuta, mawasiliano, majengo, nguo na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Ushindani iliwezesha watumishi wa Tume kupata mafunzo ya awali ya jinsi ya kutumia mfumo wa *ASYCUDA++* ambayo yaliendeshwa na maofisa wa Mamlaka ya Mapato *(TRA).* Aidha, Wizara kupitia Tume

ya Ushindani imeunda Kikosi Kazi *(Task Force)* ili kuboresha mahusiano na Taasisi nyingine za Serikali zikiwemo *TRA, TFDA*, POLISI, *TBS* na Ofisi ya Mawanasheria Mkuu wa Serikali *(AG's Chamber)* kwa mujibu wa Kanuni ya Alama za Bidhaa ya mwaka 2008. Uteuzi wa wajumbe wa Kikosi Kazi umekamilika na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia maslahi ya Mlaji kwa kupeleka maoni yake kwenye tume ya ushindani na mamlaka za udhibiti na Serikali kwa ujumla, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji limeendelea kutoa elimu na uhamasishaji kwa mlaji/walaji kuhusu haki na wajibu wao, kama inavyoainishwa katika sheria za mlaji. Katika kutekeleza majukumu hayo, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji limewahamasisha vijana na hasa wanafunzi wa vyuo mbalimbali ili wawe chachu ya mageuzi katika kutambua haki ya mlaji. Aidha, Baraza limetoa semina na vipeperushi kwa wadau mbalimbali kuhusu haki na wajibu wa mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji liliendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa kushirikiana na mabaraza ya utetezi wa mlaji/ mtumiaji. Baraza pia kwa kushirikiana na taasisi nyingine za *Fair Competition Commission*, *EWURA, SUMATRA, TCAA, FTC* na *TCRA* tumefanikiwa kuchapisha jarida la utetezi wa mlaji na mtumiaji Tanzania ambalo lengo lake kuu ni kuwaelimisha Watanzania kuhusu haki na wajibu wao. Majarida hayo yamesambazwa katika taasisi mbali mbali vikiwemo vyuo, shule na katika vituo vya mabasi.

Pia, Baraza lilitoa matangazo ya moja kwa moja kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limefanikiwa kuanzisha Kamati mbali mbali za utetezi wa mlaji, katika Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kaskazini (Arusha), Kanda ya Kati (Singida), Kanda ya Mashariki (Morogoro), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Iringa), na Kanda ya Kusini (Mtwara). Vilevile, Baraza limepokea na kushughulikia malalamiko ya Walaji waliouziwa vifaa bandia na kuwashauri kuwasilisha malalamiko yao katika vyombo vya udhibiti kama vile *FCC, EWURA* na *TCRA*. Baraza pia limewaelimisha wadau kuhusu haki na wajibu wao pale wanapokuwa wameuziwa bidhaa bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala, iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ili kuhakikisha mkulima analipwa bei inayolingana na ubora wa mazao aliyoleta ghalani. Kutokana na matumizi ya mfumo huo, wanunuzi wengi wameonesha kuridhishwa na ubora wa mazao yaliyohifadhiwa ghalani kutokana na uthibiti wa ubora katika maghala hayo. Katika msimu wa 2011/2012, Bodi iliratibu matumizi ya mfumo katika mazao ya korosho, kahawa, alizeti, mpunga, pamba na mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Bodi ya Leseni za Maghala imetoa jumla ya leseni 52 za Maghala na leseni 28 za Waendesha Maghala. Aidha, tani zipatazo 158,587 za korosho, 2,800 za alizeti na zaidi ya tani 15,000 za kahawa

zilikusanywa na kuuzwa kwa kutumia mfumo huo. Kutokana na usimamizi thabiti wa Bodi, bei za mazao zilizidi kuimarika na pia ubora wa mazao uliongezeka. Kwa mfano, bei ya kahawa isiyokobolewa iliongezeka na kufikia Sh. 5,000/= kwa kilo wakati bei ya korosho iliongezeka kutoka Sh. 800/= mwaka 2010/2011 hadi Sh. 1,200/= msimu wa mwaka 2011/2012 sawa na ongezeko la asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Bodi ya Leseni ya Maghala, imefanikiwa kutoa elimu katika mikoa ya Kagera na Mwanza kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa wakulima na wadau wengine kupitia mikutano, warsha na vyombo vya habari vikiwemo radio na luninga. Kutokana na uhamasishaji huo, wilaya za Misungwi, Kwimba na Magu walitumia Mfumo wa Stakabadhi ghalani kwa zao la mpunga msimu wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala iliendelea kuwahamasisha Halmashauri za Wilaya na Sekta Binafsi na hivyo kufanikisha ujenzi wa maghala ya Mang'ula – Morogoro, Gendi - Manyara na Malula - Arusha. Vilevile, Benki ya *NMB* imekubali kutoa mikopo kwa vyama vya msingi kwa ajili ya ujenzi wa maghala katika mikoa ya Singida na Pwani. Katika msimu wa mwaka 2011/2012, kiasi cha Shilingi bilioni 33.3 kilitolewa na *NMB* kwa ajili ya malipo ya awali ya wakulima ukilinganisha na Shilingi bilioni 42.9 za msimu 2010/2011. Benki ya *CRDB* walitoa jumla ya Shilingi bilioni 26.4 katika msimu wa 2011/2012, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 66.47 za msimu 2010/2011, na *KCB* Shilingi bilioni

3.8 msimu 2011/2012 ukilinganisha na Shilingi bilioni 12.23 za 2010/2011. Aidha, Bodi inaendelea kukusanya taarifa za wadau wa Mfumo kwa ajili ya kuanza kutengeneza kitabu cha kumbukumbu za wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *COSOTA*, imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999 na imeandaa marekebisho ya sheria hiyo na kuwasilishwa Baraza la Mawaziri kwa maamuzi. Aidha, katika kulinda maslahi ya wasanii, makubaliano yamefanyika kati ya Wizara yangu na Wizara ya Fedha, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ili *TRA* ianze kutoa stika za kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa kazi za muziki na filamu kuanzia mwezi Julai, 2012. Vilevile, kampeni ya uhamasishaji wa masuala ya hakimiliki kupitia vyombo vya habari, kama vile luninga na redio umefanyika. Sambamba na zoezi hilo, *COSOTA* imetoa elimu kwa wauzaji wa kanda na wanunuzi kuhusu *CD* na mikanda bandia kwa Maafisa Ugani na Maafisa Leseni kuhusu Hakimiliki na Hakishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *COSOTA* imesajili jumla ya Makampuni 106 yakiwemo makampuni 38 ya uzalishaji na usambazaji wa kazi za muziki; 19 ya uzalishaji na usambazaji wa kazi za filamu; na 49 ya uzalishaji, usambazaji wa kazi za uchapishaji na maandishi.

Aidha, Wizara kupitia *COSOTA* imeendelea kusuluhisha migogoro na kufungua kesi dhidi ya wakiukaji wa Sheria na wasiotoa ushirikiano kulipia mirabaha kwa kupatia ufumbuzi migogoro 18 kati ya

migogoro 24 iliyopokelewa. Jumla ya Kesi kumi zilifunguliwa dhidi ya ukiukaji wa Hakimiliki, tatu katika Mahakama zilizopo mkoani Dar es Salaam na saba katika mkoa wa Singida. Kati ya hizo, Jamhuri imeshinda kesi sita kati ya saba mkoani Singida na tatu za mkoani Dar es Salaam zinaendelea. Pia, katika mwaka 2011/12, *COSOTA* imetayarisha Kanuni za Utoaji Leseni ya Maonesho kwa Umma na Utangazaji ili iweze kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2011/2012, Wizara imepata kibali cha kuajiri watumishi wapya 42 kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kati ya nafasi 80 zilizoombwa. Hadi kufikia Aprili, 2012 watumishi 10 wameripoti kazini na Sekretariati ya Ajira inaendelea kuajiri watumishi 38 waliobaki.

Vile vile, Wizara imewathibitisha kazini watumishi watano na kuwapandisha vyeo watumishi 65 wa kada mbalimbali ikilinganishwa na malengo ya watumishi 67 kwa kutumia Mfumo wa Wazi wa Upimaji Utendaji Kazi (MWATUKA/*OPRAS*). Aidha, watumishi 20 waliwezeshwa kupata mafunzo katika ngazi ya Shahada, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu na watumishi 25 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara na taasisi imeendelea kutoa elimu kwa watumishi na umma kupitia mikutano ya ndani na maonesho ya biashara katika kupambana na kudhibiti rushwa na kubaini mianya ya rushwa kwa lengo la

kuiziba. Vilevile, Wizara imeshirikiana na Menejimenti ya Utumishi kuendesha mafunzo ya maadili na utawala bora kwa wafanyakazi wote wa Wizara mwezi Aprili 2012. Aidha, Wizara imeanza kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kuboresha taratibu za utoaji huduma kwa umma na kuainisha haki na wajibu wa mteja na wa mtoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika kutekeleza maelekezo ya Serikali kupitia Waraka Na. 2 wa mwaka 2006, imeendelea kutoa mafunzo kwa njia ya vipeperushi, maonesho na mikutano mbalimbali juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari. Aidha, imeendelea kuwawezesha wafanyakazi waishio na virusi vya UKIMWI kupata huduma ya virutubisho *(food suplements),* lishe na usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Mazingira -NEMC ilifanya tathmini ya hali ya uzingatiaji wa masuala ya mazingira *(Enviromental Impact Assessment - EIA)* kwa miradi mipya inayoanzishwa. Wizara, pia imefanya ukaguzi wa mazingira *(enviromental audit)* kwa mitambo ya viwanda vilivyopo ili kushauri wawekezaji na wenye viwanda kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika uzalishaji Viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika kutekeleza majukumu yake imekabiliwa na changamoto kadhaa zikiwa ni pamoja na uhaba wa umeme na maji, ushindani usio haki, miundombinu duni, uhaba wa mitaji na fedha, upatikanaji wa masoko, ukosefu wa

wataalam na teknolojia duni. Katika kukabiliana na changamoto za kisekta, Wizara imechukua hatua kadhaa ikiwemo kuzingatia ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara wa kuweka vipaumbele vichache katika kutekeleza majukumu yake ya kisekta.

Kwa mfano, katika kukabiliana na changamoto za uhaba wa mitaji na fedha, Wizara imetayarisha maandiko mbalimbali yatakayosaidia sekta hiyo kunufaika na mikopo ya kibenki pamoja na Mpango wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi – *Public Private Partnership (PPP).*

Aidha, Wizara imeshirikiana na Taasisi za Serikali kama *Commission for Science and Technology (COSTECH)* na hivyo kuziwezesha Taasisi zifuatazo kufaidika na fedha za Sayansi na Teknolijia: *TIRDO* – kwa ajili ya *accreditation* ya maabara*, solar dryier* na ngozi; *CAMARTEC* – kwa ajili ya uendelezaji wa trekta dogo; na *TEMDO* kwa ajili ya kiteketezi cha taka za hospitali (*Bio-medical incinerator*); na kuwawezesha kuendeleza ubunifu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, jitihada zimefanyika za kuwa na majadiliano *(Setor Dialogue)* na Washirika wa Maendeleo hasa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Benki ya Dunia (WB), Denmark, Jumuiya ya Ulaya *(EU), International Fund for Agricultural Development (IFAD),* Japan, Switzerland, *UNDP*, *UNIDO* pamoja na Washirika Wapya wa Maendeleo hasa Korea Kusini, India na China ili kushirikiana katika kuandaa na kutekeleza mikakati na

Programu za kuendeleza sekta hii ambayo ni moja ya vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa mazingira ya biashara na urasimishaji wa biashara zisizo rasmi, Wizara kwa kushirikiana na sekta nyingine, iliendelea kuboresha mazingira ya biashara na kusaidia kupunguza gharama za kufanya biashara. Kwa mfano, utaratibu wa kupitisha maombi ya leseni za biashara katika ofisi za mipango miji na afya kama sharti la utoaji leseni ya biashara umeondolewa. Aidha, *BRELA* imerahisisha taratibu za usajili wa Makampuni kwa kuweka fomu zote za maombi ya usajili kwenye tovuti yake *(www.brela-tz.org),* kufupisha muda wa kusajili kutoka siku tano hadi kufikia siku tatu. Wizara kupitia *SIDO* inahamasisha ujasiriamali na kuelimisha umma kuhusu kufanya shughuli rasmi na kuunda vikundi ili kuwezesha upatikanaji wa mitaji na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya elimu ya biashara na ushindani usio wa haki, Wizara kupitia *CBE, COSOTA, FCC, NCAC, SIDO, TBS, TWLB, TanTrade* na *WMA*, imetoa elimu na mbinu za kufanya biashara kiushindani, kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa bandia na pia kusimamia matumizi sahihi ya vipimo na viwango katika biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* inaendelea kukabiliana na uhaba wa upatikanaji wa umeme wakati huo huo inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe na upepo ambayo ipo katika hatua za awali. Hii ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa mawe wa

Ngaka Kusini na Mchuchuma na mradi wa umeme wa upepo Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo na mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2012/2013, ni kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo; kuongeza ubunifu katika utendaji; kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi kupitia mfumo wa *PPP*; kutafuta mitaji na fedha zaidi ili itoe mchango zaidi katika Pato la Taifa kama ilivyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Uendelezaji Viwanda nchini unaohusisha sekta ndogo ya nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi, korosho, na nyama kwa kuhamasisha uwekezaji zaidi ili kupanua wigo wa soko la mazao hayo ndani na nje ya nchi. Hatua hiyo itaboresha bei ya mazao ambayo ni changamoto inayojitokeza mara kwa mara.

Pia utekelezaji wake utaenda sambamba na utekelezaji wa Programu za *Africa Agribusiness and Agroprocessing Development Initiative (3AD)*, *Industrial Upgrading and Modernisation na Programu ya* Mafunzo ya Kuongeza Tija, Ufanisi na Ubora wa Bidhaa *(Kaizen Programume).* Vilevile, Wizara itaendelea kufuatilia ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu vya Mazalia ya Mbu waenezao malaria kinachojengwa katika eneo la *TAMCO*-Mkoani Pwani. Matokeo ya mradi huo ni pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa wa malaria na kupunguza

matumizi ya fedha za kigeni kuagiza dawa za kutibu Malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itafuatilia utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga unaoendeshwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania kupitia *NDC* na Kampuni ya Sichuan Hongda ya nchini China. Aidha, Wizara itafuatilia miradi ya *TANCOAL*, Kasi mpya na Umeme wa Upepo (Mkoani Singida) inayoendeshwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na Sekta Binafsi. Lengo ni kuhakikisha kuwa miradi hii inatekelezwa kwa wakati ili kuhakikisha uzalishaji wa umeme na uchimbaji wa chuma unakamilika ili kuongeza uzalishaji viwandani na kupunguza utegemezi wa chuma chakavu unaochangia uharibifu wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *EPZ* itaendelea kuhamasisha uwekezaji, ujenzi wa miundombinu katika maeneo ya *EPZ/SEZ* na kutoa fidia kwa maeneo ya *EPZ/SEZ* nchini likiwemo la ujenzi wa kituo cha biashara - *Tanzania – China Logistic Centre*, ili kuwezesha hatua za awali za ujenzi kuanza. Ujenzi wa maeneo ya *EPZ/SEZ* pamoja na *Tanzania – China Logistic Centre* yataongeza ajira, soko la malighafi nchini pamoja na kuvutia uwekezaji na biashara. Aidha, *Tanzania – China Logistic Centre* itakuwa kitovu *(hub)* cha biashara cha kutangaza fursa ya bidhaa za Tanzania kwa soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kukamilisha hatua zilizokwishaanza za kushughulikia viwanda vyenye changamoto maalum ikiwa ni

pamoja na viwanda vilivyobinafsishwa, Viwanda vya *General Tyre* na Urafiki, biashara ya vyuma chakavu na biashara ya ngozi ghafi nchini. Lengo ni kuhakikisha ufufuaji na uendelezaji wa viwanda nchini, kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa, kuongeza ajira na mapato yatokanayo na mchango wa sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kujenga na kuhamasisha Halmashauri kutenga maeneo ya kufanyia kazi wajasiriamali wadogo. Katika kufanikisha hilo, Wizara itaandaa mwongozo utakaosaidia Halmashauri kutenga maeneo yanayohamasisha sekta kupanuka. Hii itasaidia wajasiriamali kukua na kurasimisha biashara zao ili kuwawezesha kukopesheka. Wizara kupitia *SIDO* na Halmashauri itaratibu uanzishwaji wa kongano *(cluster)* za uzalishaji na teknolojia katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro na Singida. Kongano hizo zitachochea uzalishaji na ubora wa bidhaa na hivyo kuongeza kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *SIDO* na wadau wengine itaendelea kutoa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara na huduma za ugani kwa wajasiriamali hasa vijijini. Aidha itawezesha upatikanaji, uzalishaji na usambazaji wa teknolojia hasa za usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo na hivyo kuongeza tija katika uzalishaji. Hii itasaidia bidhaa za wajasiriamali kushindana katika soko la ndani na la Afrika Mashariki na hivyo kuongeza ajira, pato la mjasiriamali na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *SIDO* na taasisi nyingine, itaendelea kubuni mbinu mbalimbali za kuwezesha wajasiriamali wadogo kupata mitaji na fedha za kuendeshea shughuli zao. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa *NEDF*. Upatikanaji wa mitaji na fedha utaongeza ajira na ukuaji wa wajasirimali wadogo na hivyo kupanua wigo wa kodi. Wizara itaendelea na juhudi za kutafuta na kuwaunganisha wajasiriamali na masoko ya ndani na nje ya nchi kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa na sekta. Hii ni pamoja na kuwawezesha wajasiriamali kushiriki katika maonesho ya ndani na nje ya nchi ambapo watapata fursa ya kutangaza bidhaa, kupata miadi ya biashara na kujifunza kutoka kwa wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na majadiliano baina ya nchi na nchi *(bilateral)*, ya kikanda *(Regional)* na yale ya kimataifa *(Multilateral)* kwa lengo la kupanua fursa za masoko kwa bidhaa na huduma na hivyo kuvutia wawekezaji. Majadiliano hayo yatazingatia maslahi ya nchi yetu na kutetea masuala yanayohusu vikwazo visivyo vya kiushuru *(NTBs)* na Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin)*. Majadiliano hayo yanazingatia kulinda viwanda vyetu, kupata fursa za masoko kwa masharti nafuu (mfano China na India), masoko ya upendeleo (mfano Marekani - *AGOA, EU – EBA*, Japan na Canada) na kuleta ushindani wa haki. Katika fursa hizo tunalenga kuongeza uuzaji bidhaa na mazao yaliyoongezwa thamani katika masoko hayo hususan katika zao la korosho, pamba, tumbaku, bidhaa za ngozi, maua, matunda na mboga *(horticultural produce)* na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Utatu *(Tripartite Free Trade Area - FTA)* linalojumuisha Kanda za *COMESA – EAC - SADC* ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa *Lagos Plan of Action* wa mwaka 1980 wenye lengo la kukuza mtangamano wa kiuchumi na biashara katika nchi 26 za Afrika. Pia majadiliano ya Eneo Huru la Utatu yanalenga kurazinisha sera zinazokinzana kutokana na baadhi ya nchi ikiwemo Tanzania kuwa na uanachama wa zaidi ya kanda moja. Katika majadiliano yanayoendelea kuhusu Ubia wa Uchumi kati ya *EAC* na *EU*, Wizara itaendelea na majadiliano ili kuhakikisha maslahi ya Tanzania na ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vya biashara vilivyopo London na Dubai ili kuendelea kukuza masoko ya bidhaa za Tanzania na kuvutia wawekezaji na watalii nchini. Aidha, vituo hivyo vitaendelea kuratibu ushiriki wa makampuni ya Tanzania katika maonesho ya kimataifa yakiwemo maonesho ya bidhaa za chakula yatakayofanyika mwezi Machi 2013 London, Uingereza. Vituo vitaendelea kufanya utafiti wa soko *(market intelligence)* kwa bidhaa za Tanzania na kuunganisha wazalishaji na wanunuzi. Ili kuongeza upanuzi wa masoko katika nchi zinazoibukia kiuchumi *(emerging economies)* zikiwemo Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusini *(BRICs),* Wizara inakusudia kuanzisha vituo vya biashara kwa kuanzia nchini China na Afrika Kusini.

Vilevile, Wizara inakusudia kupeleka Waambata wa Biashara nchini Marekani na Ubelgiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuendeleza miundombinu ya masoko nchini hususan masoko na maghala ya kuhifadhia mazao. Masoko ya kipaumbele ni yale ya mipakani ambayo ni Sirari, Mtukula, Murongo, Mkwenda, Kabanga, Manyovu na Isaka (bandari kavu).

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Kasulu, Nanyumbu na Songea imelenga kuendeleza masoko katika mipaka ya Kilelema, Mtambaswala, Daraja la Mkenda, Mtawalia. Kwa masoko ya Segera na Makambako, Wizara itahimiza kufikia makubaliano kati ya *TIB* na Halmashauri za Mikoa husika ili kuanza ujenzi wa masoko hayo mapema. Masoko hayo yatawahakikishia wakulima soko la uhakika ikiwa ni hatua muhimu ya kutekeleza mkakati wa kukuza biashara ya ndani na nje na kurasimisha biashara nchini.

Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wengine kufanikisha uendelezaji wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja Mipakani *(One Stop Border Post - OSBP)* na kuanzisha Kamati za Kufanya Kazi Pamoja Mipakani *(Joint Border Committees – JBCs)* ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara *(Doing Business)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeweka lengo la kufanya mapitio ya sheria ili kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa masoko ya mazao na

mifugo na kuendeleza soko la ndani. Sheria zilipangwa kufanyiwa marekebisho ni pamoja na Sheria ya *The Export Control Act, Control of Movement of Agricultural Product Act*, Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara, *The Limited Liability Partnership Act*, *The Warehouse Receipt Act 2005,* na *The Weight and Measure Act Cap 340 RE 2002.* Aidha mabadiliko ya sheria ya *Warehouse Receipt Act (2005)* inalenga kuwezesha uanzishwaji wa Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange)* ambalo litatumia Mfumo wa *WRS*.

Mfumo huo utawezesha kuanzishwa kwa *Tanzania Commodity Exchange (TCX)*, kupanua wigo wa biashara na kutoa bei shindani kwa wakulima. Wizara imefanya maandalizi ya kuanzisha Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange)* ili kuwahakikishia wakulima soko la uhakika. Maandalizi yaliyofanyika ni pamoja na kuunda Kikosi Kazi cha kuratibu uanzishaji wa Soko la Bidhaa. Kikosi hicho kilipata fursa ya kujifunza Ethiopia, China na India ili kupata uzoefu. Aidha, andiko la mpango *(concept note),* Mpango wa utekelezaji *(road map)* vimeandaliwa na Waraka wa Baraza la Mawaziri umewasilishwa ili kupata maamuzi ya kuanzishwa kwa soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na Bodi ya Stakabadhi za Maghala, Uongozi wa Mkoa wa Kagera na Vyama vya Ushirika ili kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi kwa zao la kahawa kwa msimu wa ununuzi wa 2013/2014. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kutoa elimu na kufuatilia utekelezaji wa Mfumo huo

katika maeneo ambayo yanautumia ili kuendeleza manufaa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Masoko, Wizara itaendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya simu ya kiganjani na mtandao wa kompyuta ili kupata taarifa za masoko hususan taarifa za bei kwa wakati muafaka ambazo zitaunganishwa na mifumo ya taarifa za masoko ya mipakani. Wizara itaanza kwa majaribio *(piloting)* kutekeleza Mfumo Mpana na Unganishi wa Masoko kutegemeana na upatikanaji wa rasiliamali fedha. Hii ni moja ya hatua muhimu katika kukuza masoko ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kusimamia, ubora wa bidhaa na huduma, ushindani wa haki na matumizi ya vipimo rasmi ili kulinda maslahi ya walaji. Usimamizi huo hufanywa kupitia mashirika ya Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* Tume ya Ushindani *(FCC),* Baraza la Ushindani *(FCT),* Wakala wa Vipimo *(WMA),* Baraza la Utetezi wa Haki ya Mlaji *(NCAC)* na Chama cha Hakimili Tanzania *(COSOTA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizojitokeza kuhusu ukaguzi na udhibiti wa ubora wa bidhaa kutoka nje ikiwa ni pamoja na magari kwa mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania katika mwaka 2012/2013, itafanyia kazi changamoto zote na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na

Biashara; Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC).* Vilevile, Wizara itaendeleza jitihada za kuijengea uwezo *TBS* kwa kuwezesha ajira za wataalam wa kutosha na kuwapa vitendea kazi ili kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, *TBS* itaendelea kuimarisha utaratibu wa kukagua ubora wa bidhaa ukiwemo ukaguzi wa magari kabla ya kuingia nchini. Hii ni pamoja na kuwashirikisha wadau mbalimbali ili kupata maoni yao yatakayowezesha kufanywa marekebisho ya Sheria ya Viwango ya mwaka 2009, kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kufanya ukaguzi wa magari ndani ya nchi. Kwa upande wa ukaguzi wa bidhaa kupitia *PVoC*, mapendekezo ya wadau yatawezesha pia kuangalia uwezekano wa kutenganisha bidhaa zinazohitaji kukaguliwa ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia makundi tofauti ya wafanyabiashara wa Tanzania (wakubwa, wa kati na wadogo) bila kuathiri ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara pia itahakikisha kuwa *TBS* inashirikiana kwa ukaribu na vyombo vingine vya serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania *(TFDA),* Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA),* Tume ya Ushindani Halali *(FCC),* Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini ni zenye ubora unaokubalika. Wizara pia

itaendeleza juhudi za kutoa elimu na kuhakikisha kwamba maabara zote za Shirika zinapata vyeti vya umahiri *(laboratory accreditation)* ili kuwezesha kukubalika kwa bidhaa nyingi zaidi za Tanzania katika soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Baraza la Ushindani *(FCT)* litasikiliza kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa Udhibiti na Ushindani wa Biashara kwenye Soko; kujenga uwezo zaidi wa Baraza katika kushughulikia kesi hizo kwa kuimarisha rasilimali watu na Wajumbe wa Baraza; kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza na umuhimu wake katika Uchumi; na kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati *(Strategic Plan-SP)* wa Baraza wa miaka mitano.

Aidha, Tume ya Ushindani itadhibiti na kupambana na uingizaji na uzalishaji wa bidhaa bandia; uchunguzi wa usikilizaji wa kesi za ushindani; utafiti wa masoko ili kubaini matatizo ya masoko husika na kama hatua za kurekebisha; na kumlinda na kumwelimisha mlaji. Vile vile, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji litasimamia maslahi ya mlaji kwa kupeleka maoni yake kwenye Tume ya Ushindani, Mamlaka za Udhibiti na Serikali kwa ujumla; kuendelea kupokea na kusambaza habari na maoni yenye maslahi kwa mlaji; kuanzisha Kamati za Mlaji za Mikoa na Sekta na kushauriana na kamati hizo; wenye viwanda, Serikali na jumuiya nyingine za walaji katika mambo yenye maslahi kwa mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wakala wa Vipimo itaendelea kuimarisha kaguzi za matumizi ya vipimo nchini kwa kutoa elimu ya matumizi ya vipimo na ufungashaji wa bidhaa kwa wananchi sambamba na kuongeza weledi kwa watumishi wa Wakala na kuwaongezea vitendea kazi. Aidha, itaimarisha Kitengo cha Vipimo Bandarini *(WMA Ports Unit)* na kuhakiki usahihi wa vipimo vitumikavyo katika biashara ya gesi na mafuta ili kulinda mapato ya Serikali na haki ya mlaji. Wakala itakamilisha kazi ya upembuzi yakinifu kwa mradi wa ujenzi mpya na wa kisasa (eneo la kupimia magari yanayo safirisha mafuta) katika eneo la Misugusugu, Pwani, na kukamilisha taratibu za utungaji wa Sheria mpya ya Vipimo *(Legal Metrology Act)* ili kukidhi matakwa ya sasa ya biashara na pia kuzingatia maridhiano yaliyofikiwa na nchi kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika kulinda haki za wasanii dhidi ya uharamia wa kazi zao, Wizara kwa kupitia *COSOTA* katika mwaka 2012/2013, inatarajia kukamilisha marejeo ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999. Hatua hii itawezesha sheria hiyo kuendana na *Standard Act* ya Afrika iliyozingatia makubaliano ya mikataba iliyofanyika baada ya mwaka 1999. Makubaliano hayo yanatenganisha shughuli za udhibiti wa Hakimiliki na zile za Vyama vya Usimamizi wa Pamoja wa Hatimiliki. Aidha, *COSOTA* itaendelea kupanua wigo wa utendaji kwa kufungua ofisi mjini Arusha na Dodoma; kukusanya mirabaha kutoka kwenye mashirika ya utangazaji; na

kuhamasisha wanunuzi wa *CD*, kanda za miziki na filamu kununua kanda na *CD* zenye Hakigram.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kukuza na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA),* Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara *(TanTrade)* na Bodi ya Leseni ya Maghala *(TWLB).* Katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia *BRELA* itaboresha usajili wa makampuni na majina ya biashara kwa kutumia mfumo na mashine za kisasa zijulikanazo kama *'special machine readable certificates'* ili kuondoa wimbi la kughushi vyeti na kuleta uthibiti.

Aidha, *BRELA* itaendeleza jitihada za kupunguza muda unaotumika kusajili kampuni na majina ya biashara kwa kutumia mifumo Programu ya kompyuta inayowezesha kufanya usajili kwa mtandao *(On line registration systems),* kuboresha Masijala za kisheria zinazosimamiwa na Wakala ili kuendana na mifumo ya kitekinolojia na hivyo kurahisisha utoaji huduma; kufanya marekebisho ya sheria zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kwenda na wakati; na kutoa elimu kwa umma kuhusu taratibu za usajili wa makampuni na majina ya biashara kwa kuzingatia taratibu za sheria na kanuni zilizopo. Pia Wizara itatoa msukumo wa kuanza ujenzi wa ofisi za *BRELA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* itaendelea kuboresha biashara ya ndani na nje kwa kuongeza wigo wa masoko ya kikanda na kimataifa. Wizara

kupitia *TanTrade* itaboresha maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam *(DITF)* na kuhamasisha ushiriki wa wajasiriamali kwenye maonesho ndani na nje ya nchi kwa lengo kutangaza bidhaa za Tanzania na kutumia fursa za masoko mbalimbali. Aidha, Wizara kupitia *TanTrade* itaimarisha Kituo cha Zanzibar na kutoa huduma ya taarifa za biashara kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao na bei shindani kwa wakulima, katika mwaka 2012/2013 Bodi ya leseni ya Maghala itasimamia uanzishwaji wa utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika zao la kahawa mkoani Kagera na kupanua matumizi ya mfumo katika mazao mengine na kufanya maandalizi ya kuwezesha mfumo huo kutumika katika Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange).* Aidha, Bodi itasimamia utekelezaji wa mfumo huo katika maeneo yote yanayotekeleza mfumo hapa nchini, kuboresha mfumo wa ukaguzi wa maghala na kutoa elimu ya mfumo kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya *EPZA* kwa mwaka 2012/2013 ni kulipa fidia na kuanza uendelezaji wa eneo la kipaumbele la Bagamoyo SEZ utakaohusisha ujenzi wa miundombinu ya msingi katika eneo la awamu ya kwanza (*phase one*). Aidha, kufanya uthamini na ulipaji fidia katika eneo la mradi wa *Tanzania - China Logistics Center,* Kurasini, Dar es Salaam na kuanza utekelezaji; kulipa fidia kwa maeneo ya *EPZ* na *SEZ* ya Mara, Ruvuma, Tanga na Kigoma ambayo yameshathaminiwa na kuthibitishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Vile vile, kwa kushirikiana

na uongozi wa mikoa mipya ya Geita, Njombe, Katavi na Simiyu; itakamilisha zoezi la ubainishaji wa maeneo ya *EPZ* na *SEZ* katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *EPZA* itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa kujenga miundombinu na wale wa kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* ikiwemo kujenga mfumo wa maji taka katika eneo la Benjamin William Mkapa *SEZ*; kufanya *detailed design* ya ujenzi wa miundombinu ya msingi katika maeneo ya Kigoma *SEZ* na *Mtwara Freeport Zone*. Vilevile itafanya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* na kuandaa mpango mpana *(Master plan)* kwa ajili ya uendelezaji wa Mtwara *SEZ*, Tanga *SEZ*, Ruvuma *SEZ* na Mara *SEZ*; na kuandaa mpango mkakati mpya wa miaka mitano wa *EPZA* *(Five Years Strategic Plan 2013-2018)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* litaendelea na utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga; kuendeleza utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe iliyoko Katewaka na mradi wa Chuma ulioko Maganga Matitu kuzalisha chuma ghafi (Mradi wa Kasi Mpya), kujenga kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe (Ngaka Kusini, Songea), kujenga Kituo cha kuzalisha umeme wa upepo (Singida) na kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha Viuadudu (*biolarvicides*) kwa ajili ya kuua viluwiluwi kwenye mazalia ya mbu wa malaria (*TAMCO*, Kibaha).

Vilevile, *NDC* itaendelea na ukarabati wa Kiwanda cha General Tyre, Arusha ili kukifufua na kuanza uzalishaji wa matairi; kujenga maeneo ya viwanda (*Industrial parks*) sehemu za *TAMCO, KMTC* (Moshi) na Kange (Tanga); kuanzisha viwanda vya kusindika nyama, mpira na mazao mengine ya Kilimo; Kukamilisha tafiti na kuanzisha kiwanda cha kuzalisha magadi *(soda ash)* katika Ziwa Natron na Engaruka, Arusha; kuratibu uendelezaji wa kanda za maendeleo za Mtwara, Tanga, Kati na Uhuru; na kuwajengea uwezo wananchi wa maeneo ya miradi kufaidika na fursa zinazotokana na miradi hiyo inayotekelezwa na *NDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kusimamia maendeleo ya ujasirimali ambalo linatekelezwa na *SIDO*. Katika mwaka 2012/2013, *SIDO* imepanga kuimarisha uwezo wa kuzalisha na kusambaza mashine ndogo za kuongeza thamani mazao na kuwezesha usambazaji wa teknolojia vijijini kupitia Programu ya Wilaya Moja bidhaa Moja *(ODOP).*

Vilevile, *SIDO* itasaidia uanzishaji wa kongano za viwanda vidogo vya kusindika alizeti; kuchochea ubunifu na utengenezaji wa bidhaa mpya kupitia Programu ya kiatamizi na kutoa elimu ya ujasiriamali, na uongozi wa biashara. Pia *SIDO* itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya *SIDO* Mkoa wa Manyara na kuwezesha Vyuo vya Mafunzo na Uzalishaji vya *SIDO* kufanya kazi, kupanua wigo wa masoko ya wajasirimali wadogo, kutafuta na kusambaza taarifa za kuboresha biashara na kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri. Malengo hayo yataongeza idadi ya

wajasirimali, ajira na kipato na hivyo kuchangia katika kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina majukumu ya kufanya utafiti, kutoa mafunzo mbalimbali ya kisekta na kuendeleza teknolojia mbalimbali kwa kushirikisha Taasisi za *TIRDO, TEMDO, CAMARTEC* na Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* ili kuongeza ubora na ufanisi wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda mbalimbali na kujipatia teknolojia rahisi na yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TEMDO* katika mwaka 2012/2013 itaboresha miundombinu ya kiatamizi cha teknolojia/biashara *(Technology/Business Incubator)* na kuwezesha wajasiriamali watano wanaosindika vyakula na kutengeneza mashine na vifaa kwa matumizi ya viwanda vya kati kwa kuwapatia teknolojia na mafunzo. Aidha, *TEMDO* itaendeleza utoaji huduma na ushauri wa kihandisi pamoja na mafunzo kwa viwanda kumi kwa lengo la kuongeza tija, uzalishaji, kulinda afya na usalama pamoja na kuhifadhi mazingira sehemu za kazi. Vilevile, *TEMDO* itaendelea kubuni, kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji wa chasili *(prototypes)* za vifaa vya hospitali *(hospital equipment and devices)* kama vile mashine za kufua nguo, majokofu ya kuhifadhi dawa au maiti *(hospital refrigerators or mortuary facilities),* vitanda na viti maalum ili kupunguza uagizaji wa vifaa hivyo kutoka nje ya nchi kwa kutumia fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TEMDO*, itabuni na kuendeleza chasili za teknolojia za kutumia upya au kurejesha *(re-use or re-cycle)* taka za mijini na

kutengeneza umeme, kutengeneza vifaa vya plastiki na karatasi *(Municipal Solid Waste recycling technologies*. Halikadhalika, *TEMDO* itafanya majaribio ya chasili za machinjio ya kisasa yenye gharama nafuu pamoja na teknolojia za kuongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mabaki ya mifugo na kuendelea na maboresho pamoja na uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali zilizothibitishwa ikiwa ni pamoja na teknolojia ya kuteketeza taka za hospitali *(bio-medical waste incineration).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIRDO* katika mwaka 2012/2013 itatekeleza mradi wa kurejeresha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama *leather boards* kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na viwanda vya kusindika ngozi na kuimarisha uzalishaji katika viwanda vya kusindika ngozi na viwanda vya bidhaa za ngozi. Aidha, itashughulikia umahiri *(accreditation)* wa maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi ili iweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani; *TIRDO* pia, itatekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa mazao *(traceability)* kwa kutumia kompyuta na pia kutoa ushauri wa kiufundi kwa viwanda vikubwa na vidogo katika sekta ya uzalishaji bidhaa zitokanazo na mazao ya kilino *(agro-processing industries)* kupitia benki ya rasilimali *(TIB)* na; kujenga tovuti ili kusaidia wazalishaji wadogo na kati kutangaza bidhaa zao ili wapate masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAMARTEC* katika mwaka 2012/2013 itaendeleza uzalishaji wa trekta ndogo lililobuniwa na *CAMARTEC* na kuharakisha

uzalishaji wake kibiashara *(commercialisation)* kupitia Sekta Binafsi; itabuni na kutengeneza, vipandio vya mbegu za mahindi na jamii ya mikunde vinavyoendeshwa kwa trekta, mashine ya kufyatua matofali ya udongo saruji inayoendeshwa kwa injini, teknolojia za nishati jadidifu, mitambo ya kuchemsha maji kwa kutumia nishati ya mionzi ya jua na mashine za kukatakata majani ya kulishia wanyama zinazoendeshwa kwa injini. Teknolojia hizi zitapunguza suluba na kurahisisha utendaji kazi kwa wananchi vijijini na hivyo kuongeza uzalishaji na tija.

Vile vile *CAMARTEC* itanunua na kusimika mashine na vifaa kwa ajili ya maabara ya kisasa (kupima tabia za udongo, majaribio ya mashine na teknolojia za nishati ya mionzi ya jua na *biogas*), kuendesha mafunzo ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Aidha, itakarabati na kuboresha majengo ya ofisi na karakana ya Tawi la *CAMARTEC* lililoko Nzega na kukamilisha ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo la Kituo huko Themi (Arusha) kwa ajili ya usalama wa mali za Kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Chuo Cha Elimu ya Biashara kitaimarisha mafunzo yenye mwelekeo wa kiutendaji katika nyanja za biashara yaani Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi, Utawala na Uongozi wa Biashara, Uhasibu, Menejimenti ya Masoko, Taaluma ya Mizani na Vipimo, Taaluma ya Habari na Mawasiliano na Taaluma nyingine zinazohusiana na hizo katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili.

Aidha, Chuo kitaandaa mitaala mipya ya shahada ya kwanza katika Ujasiriamali, Menejimenti ya Rasilimali Watu na Elimu ya Biashara. Vile vile Chuo kitaandaa mitaala ya Shahada ya Uzamili, kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wakati ili kuwasadia wafanye biashara zao kwa ustawi mkubwa zaidi. Pia Chuo kitaandaa mpango kabambe wa Chuo *(Master Plan)* katika Kampusi zake tatu yaani Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza kwa ajili ya upanuzi wa chuo; kukarabati majengo ya Chuo na kupeleka watumishi katika mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada za Uzamivu *(Ph.D)* na shahada ya uzamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 53 wa kada mbalimbali ili kuziwezesha idara na vitengo kupata rasilimali watu wa kutosha ili kutoa huduma nzuri na kwa ukamilifu. Pia, Wizara inatarajia kuwathibitisha kazini watumishi 42 na kuwapandisha vyeo Watumishi 28. Pia Wizara inatarajia kuwapeleka watumishi 15 mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali nchini na watumishi 20 kwenye mafunzo ya muda mfupi ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi wake kwa kutoa mafunzo ya Sheria mbalimbali za kazi, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sheria ya Fedha ili kuwawezesha kufanya kazi na kutoa maamuzi kwa kuzingatia matakwa ya sheria tajwa. Ili kuweza kutoa huduma bora zinazokidhi viwango vilivyoainishwa katika

Mkataba wa Huduma kwa Mteja, Wizara itaendesha mafunzo ya elimu ya huduma kwa mteja kwa watumishi 50 ili kuwapatia mbinu mbalimbali za kuhudumia wateja. Vilevile wizara inatarajia kuimarisha dawati la kushughulikia malamiko ya Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ili kuweza kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na jitihada za kuwawezesha watumishi waliojitokeza na watakaojitokeza wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupata huduma ya virutubisho, lishe na usafiri. Pia Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari. Aidha, Waelimishaji rika watapewa mafunzo ili kuwawezesha kupata mbinu mpya ambazo zitawawezesha kuwaelimisha watumishi wenzao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati inayohusu utunzaji wa mazingira pamoja na Programu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira Viwandani na taasisi za Sekta za Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani za dhati kwa nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa na yanaendelea kutoa misaada mbalimbali kusaidia Wizara yangu. Misaada na michango hiyo

imechangia kwa kiasi kikubwa Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija. Nchi rafiki ni pamoja na Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na: Benki ya Dunia, *DANIDA, CFC, ARIPO, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA*, Jumuiya ya Madola, *KOICA*, Sida, *UNCTAD, UNDP, UNIDO, USAID, WTO* na *WIPO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara na Taasisi zilizo chini yake inaomba kutengewa jumla ya Sh. 170,199,842,000/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Kati ya fedha hizo, Sh. 38,819,055,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 131,380,787,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Sh. 43,974,000/= kutokana na faini zitokanazo na kukiuka Sheria ya Leseni, uuzaji wa nyaraka za tenda pamoja na makusanyo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Sh. 38,819,055,000/= zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Sh. 31,378,315,000/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara *(PE)* na Sh. 7,440,740,000/= zimetengwa kwa ajili ya matumizi mengine *(OC).* Aidha, kati ya fedha za mishahara *(PE)* Sh. 2,443,590,000/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Sh. 28,934,725,000/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara ya Taasisi. Vile vile,

kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengine *(OC),* Sh. 6,143,859,000/= zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Sh. 1,296,881,000/= zimetengwa kwa ajili ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha Sh. 123,713,139,000/= kati ya Sh. 131,380,787,000/= zilizotengwa kwa shughuli za miradi ya maendeleo katika Wizara na Taasisi zake ni fedha za ndani, na Sh. 7,667,648,000/= ni fedha za nje zitakazotoka kwa Washirika wa Maendeleo. Sh. 60,000,000,000/= kati ya Sh. 123,713,139,000/= zilizotengwa kutokana na fedha za ndani, zitatumika katika uanzishaji wa *Tanzania – China Logistic Centre* na Sh. 50,200,000,000/= zitatumika katika kulipa fidia na kuendeleza maeneo huru kwa ajili ya uzalishaji bidhaa za mauzo nje na ndani ya nchi *(Special Economic Zones – SEZ/EPZ).* Sh. 7,960,000,000/= zitatumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kuendeleza viwanda mama katika Shirika la NDC na Sh. 5,553,139,000/= zitatumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Wizara na Mashirika mengine chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara *www.mit.go.tz. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 99(7) na 114(11) Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha maoni ya Kamati. Kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adimu ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu naomba nitoe pole kwa ndugu na jamaa wote walipoteza maisha yao kwa ajili ya meli iliyotokea Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema Roho za Marehemu. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Gregory George Teu kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa tutashirikiana vizuri katika

kuendeleza na kuimarisha sekta hii ya viwanda hasa kwa kuzingatia uzoefu wao katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Nachukua fursa hii pia kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote walioteuliwa kushika nafasi hizo. Aidha, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kushika wadhifa huo. Nawapongeza pia Wenyeviti wote waliochaguliwa kuongoza Kamati mbalimbali za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru sana wapiga kura wangu kwa kuniunga mkono na kuniamini katika kutekeleza majukumu yangu katika Jimbo la Mufindi Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri Waislam wote popote walipo duniani katika Mfungo Mtukufu wa Mwezi wa Ramadhani. "*Ramadhani Mbarak!*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha uliopita 2011/2012 Kamati yangu ilitoa maoni, ushauri na maagizo 10. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza baadhi ya ushauri wa Kamati. Hata hivyo Kamati itaendelea kushauri na kuagiza Serikali, kuongeza juhudi katika kutekeleza ushauri ambao haujatekelezwa au kutekelezwa kwa sehemu ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha Sh. 57,728,718,000/=. Kati ya Fedha hizo Sh.

30,052,589,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 27,676,129,000/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inasikitishwa na tabia ya Serikali kutokutoa fedha zote na kwa wakati kama zilivyoainishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hii inasababisha Wizara pamoja na Taasisi kushindwa kutekeleza mipango yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Tarehe 5 - 7 Juni, 2012 Jijini Dar es Salaam, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda - Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hiyo, Mheshimiwa Waziri alieleza kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara;

(ii) Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya mwaka 2011/2012;

(iii) Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2011/2012;

(iv) Utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010;

(v) Utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo;

(vi) Changamoto zinazoikabili Wizara;

(vii) Maombi ya Fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2012/2013; na

(viii) Malengo na Mikakati ya Wizara itakayotekelezwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Makadirio hayo, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba jumla ya Sh. 167,199,842,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 38,819,055,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na Sh. 128,380,787,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Sawa na asilimia 77%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majukumu makubwa ya Wizara ya Viwanda na Biashara na kutokana na upungufu wa watumishi pamoja na ukosefu wa wataalam, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara, kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili mapema kwa kuajiri watumishi wa kutosha na wenye utalaam unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na shughuli za Wizara ya Viwanda na Biashara kutegemea Wizara nyingine ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, mfano Wizara ya Miundombinu, Nishati na Madini, Kilimo, Maji na Mifugo, Maliasili na Utalii na

kadhalika, na kwa kuwa vipaumbele katika Wizara hizi hutofautiana kunasababisha kukosekana kwa muunganisho wa Mipango ya Utekelezaji. Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati na mipango ya pamoja kabla ya kuwekeza katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati wa kuomba Wizara kuongezewa bajeti na kuiongezea kutoka Sh. 57,728,718,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mpaka Sh. 167,199,842,000/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali kuzitoa fedha hizo zote kama zilivyopangwa na kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara imekuwa ikitumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kulipia kodi ya Ofisi. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 imetenga Sh. 720,000,000/= kwa ajili ya pango sawa na Shilingi milioni 60 kwa kila mwezi. Kiasi hiki ni kikubwa. Ili kuepuka upotevu wa fedha hizi, Kamati inashauri Wizara kuweka mkakati mahsusi wa kujenga Ofisi yao wenyewe. Hii itasaidia siyo tu kupunguza gharama bali pia itaipatia hadhi Wizara hii ambayo ni ya kibiashara na inatembelewa na wafanyabiashara wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tatizo la *TIRDO* kutopatiwa Hati miliki kwenye eneo wanalolimilikikwa muda mrefu, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kulimaliza tatizo hili. Aidha inashauri Serikali kushughulikia mapema matatizo ya

hati miliki kwa Taasisi zake zote kama *TANTRADE, SIDO* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuweka vipaumbele ndani ya Wizara. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013 Wizara imeweka kipaumbele katika Taasisi ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa ajili ya Mauzo Nje *(EPZA)* kwa kuitengea Shilingi bilioni 60 kwa ajili ya maendeleo. Kiasi hiki cha fedha kitaiwezesha *EPZA* kulipa fidia kwa wananchi, kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika eneo la Benjamini Mkapa, Bagamoyo na Kigoma hii itaharakisha kupata wawekezaji, italiongezea Taifa pato la Fedha za kigeni, ajira itaongezeka pamoja na kuongeza kipato na hivyo Maisha Bora kwa kila Matanzania yatawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri *EPZA* kuzitumia fedha hizi kama zilivyokusudiwa na hii itaweza kuwa mwanzo mzuri wa *EPZA* kujitegemea na kuepukana na utegemezi wa bajeti ya Serikali unaojitokeza kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa mengi Duniani yameweza kuendelea kiuchumi na kuondokana na umasikini kwa kuweka kipaumbele kwa wajasiriamali wadogo kupitia *SIDO*. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 *SIDO* imejiwekea mipango na mikakati ifuatayo:-

(i) Kujenga na kuendeleza miundombinu ya uzalishaji na biashara;

(ii) Kujenga msingi na mbinu za ujasiriamali kwa kupata mafunzo ya elimu ya biashara na ujuzi maalum;

(iii) Kuzalisha bidhaa kutokana na malighafi zilizopo; na

(iv) Kuongeza huduma za fedha kwa kutoa mitaji kwa wajasiriamali ya kununulia mitambo na kukidhi gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu kwa kutambua umuhimu wa *SIDO* ilishauri Wizara kuipa kipaumbele kwa kuitengea bajeti ya kutosha. Lakini kwa masikitiko makubwa, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya *SIDO* kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha Sh. 4,003,408,479/= kwa ajili ya maendeleo ni ndogo sana kiasi kwamba haitaweza kutekeleza hata mpango mmoja. Baada ya majadiliano Kamati iliitaka Serikali kuongeza bajeti hiyo ili iwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayofuraha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ilikubali kuongeza bajeti hiyo na kufikia Sh. 10,001,000,000/=. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itatekeleza jambo hili kwa vitendo kwa kuipatia fedha hizo zote na kwa wakati na kwamba *SIDO* itatumia vizuri fedha hizo kutekeleza mipango yake kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa wakati Waziri wa Fedha akiwasilisha Bajeti ya Serikali, alilieleza Bunge hili kuwa Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 4.5 kwa bajeti hiyo na kufikia Sh. 10,001,000,000/=. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itatekeleza jambo hili kwa vitendo kwa kuipatia fedha hizo zote na kwa wakati na kwamba *SIDO* itatumia vizuri fedha hizo kutekeleza mipango yake kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili limekabidhiwa majukumu mazito ya kuibua miradi mikubwa nchini ikiwemo kuendeleza Miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Ngaka, Chuma cha Liganga, kujenga kiwanda cha kuzalisha dawa kwa ajili ya kuua mazalia ya mbu, kuzalisha umeme Ngaka kusini na kufufua kiwanda *General Tyre Arusha*. Endapo miradi hii itatekelezwa nchi itaweza kutekeleza miradi mikubwa ambayo ni chachu ya uanzishwaji wa viwanda vikubwa, kati na vidogo kutokana na upatikanaji wa mali ghafi muhimu ya chuma na upatikanaji wa umeme wa uhakika. Miradi ya Ngaka na Mchuchuma itakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa Mw 600 ifikapo 2014, na kutengeneza chuma tani 1,000,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa kiwanda cha kutengeneza dawa za kuangamiza mazalia ya Mbu chenye uwezo wa kuzalisha lita milioni sita kwa mwaka. Utekelezaji wa kiwanda hiki utaleta suluhisho la kudumu la ugonjwa sugu wa Malaria kwa Watanzania na kuondoa tatizo la kupoteza nguvu kazi inayopotea kila mwaka kutokana na vifo vya Malaria. Aidha, mradi huu

utaweza kuiondolea Serikali aibu ya kuendelea kupata msaada wa vyandarua ambavyo hata hivyo, siyo suluhisho la kudumu la tatizo la Malaria, kwani tumeendelea kuona na kushuhudia Watanzania wakiendelea kufa kutokana na ugonjwa wa Malaria pamoja na juhudi za Serikali za kugawa vyandarua kila kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *NDC* kulundikiwa miradi hii mikubwa na yenye maslahi kwa Taifa, bado Serikali haionyeshi nia ya dhati *(commitment)* kwa vitendo katika kutekeleza miradi hii. Hii ni kutokana na kiasi kidogo cha bajeti Sh. 7,960,000,000/= kutengwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo yote. Kamati inaishauri Serikali inapoweka mipango iwe tayari kutekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyefahamu kuwa tatizo la umeme nchini limekuwa kero na kusabababisha kuporomoka kwa uchumi. Lakini ni kweli pia kwamba *NDC* kupitia miradi ya makaa ya mawe Ngaka na Mchuchuma ni jibu na suluhisho la kudumu la tatizo la umeme. Kinachoshangaza ni kwamba Serikali imekuwa na juhudi mbalimbali za kutafuta ufumbuzi wa tatizo la umeme kwa njia za dharura na kuingia gharama kubwa sana kila mwaka. Utafiti uliofanywa na wataalamu unaonyesha kuwa endapo Serikali itaingia gharama ya kujenga mtambo *(Transmission line)* kutoka Makambako hadi Songea ambao unagharimu kama Dola za Kimarekani 64, tatizo la umeme litaweza kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mwekezaji katika miradi ya makaa ya mawe Mchuchuma na Ngaka yuko tayari kutengeneza umeme kwa kutumia makaa ya mawe ifikapo mwaka 2013/2014, lakini cha kushangaza ni kwamba Serikali haijatenga fedha yoyote kwa ajili ya kuendeleza mradi huu wa umeme ambao utaleta nafuu sana kwa watumiaji (senti 10-11 kw.) Kamati inashauri Serikali kulichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili kwa kuisaidia *NDC* namna ya kupata fedha za kuweza kuzalisha umeme wa uhakika kutokana na makaa ya mawe. Hii ni pamoja na Serikali kufanya mazungumzo ya kimkakati na Kampuni ya *TANCOL* inayomiliki mgodi wa makaa ya mawe ya Ngaka, *TANESCO* na Mashirika ya Fedha ili kuharakisha upatikanaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kufufua hata viwanda vingi vilivyokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu pia inashauri kuwa umeme wa makaa ya mawe utakapowekwa kwenye *Grid* ya Taifa, wananchi wanaolizunguka eneo la mradi wafikiriwe kupatiwa umeme. Aidha, fidia kwa wakazi wa Ngaka iangaliwe upya ili iendane na hali halisi ya maisha ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inashauri kuwa utekelezaji wa mradi wa chuma cha Liganga uende sambamba na uanzishaji wa viwanda vinavyotumia chuma, kama viwanda vya magari, Nondo, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inajua kuna Madini ya Makaa ya Mawe mengi nchini maeneo ya Mchuchuma, (Ludewa) Ngaka (Mbinga) na yanamilikiwa na *NDC* pamoja na Wabia wake. Kwa kuwa hili ni muhimu sana kwa uchumi wa taifa letu, Kamati inaishauri kuwepo na sera ya Madini ya Makaa ya Mawe kama ilivyo kwa wenzetu wa Boswana, kuliko utaratibu unaotumika sasa. Bila kuwa na sera hii tani nyingi za Makaa ya Mawe zitauzwa nje ya nchi bila kujali matumizi muhimu ya makaa ndani ya nchi kama vile uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* ni muhimu sana kwa afya na usalama wa maisha ya Watanzania, kwa maana ya kudhibiti bidhaa zisizo na ubora zinazoingia nchini kutoka nje ya nchi. Pamoja na *TBS* kutoa vyeti 1,945 sawa na asilimia 69.5% ya lengo la vyeti 2,800 kwa mwaka 2011/2012 vya ubora wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje, Kamati yangu imesikitishwa sana na bidhaa zisizo na ubora/duni zinavyoshamiri katika maduka mengi tena zikiuzwa kwa uwazi bila hofu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa bidhaa hizi zimeenea kiasi kwamba ukifika madukani kupata mahitaji unaulizwa unataka bidhaa halisi *(original)* au bandia. Hali hii ni hatari kwa maisha ya Watanzania kwani mara nyingi bidhaa hizi duni madhara yake ni makubwa sana. Kwa mfano, kumekuwepo na ajali nyingi za pikipiki na kusababisha ulemavu na hata vifo kutokana na matumizi ya mipira isiyo na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja nchini *(Pre- shipment Verification of Conformity – PvoC)* ya mwaka 2009. Kamati yangu inaungana na Kamati za Hesabu za Serikali (*PAC*) pamoja na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC)* kuona kwamba utekelezaji wa Sheria hii una upungufu kubwa na inatakiwa kuangaliwa upya haraka iwezekanavyo. Aidha, Kamati yangu inampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda - Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hatua za awali alizoanza kuchukua katika Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* kwa kumsimamisha kazi Mkurugenzi Mkuu - Ndg. Charles Ekelege. Aidha, Kamati yangu inaitaka Serikali kuangalia upya uwezo wa utendaji kazi katika Idara ya Udhibiti wa ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inashauri pia kuwa ni wakati muafaka sasa Serikali kupitia *TBS* kuwa makini na ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini na pia ukaguzi usiishie pale tu bidha zinapoingia kuwepo na utaratibu wa kupita madukani kuona bidhaa zinazouzwa kama zina ubora unaostahili na zinapobainika hazina ubora hatua kali zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuwa nchi pekee yenye Sheria nzuri ya Ushindani katika nchi za Afrika Mashariki. Aidha, kutokana na uzuri wa Sheria hii, hata Sheria ya Ushindani ya Afrika Mashariki wameiga kutoka Sheria ya Tanzania. Hata hivyo, majukumu ya Tume ya Ushindani bado hayajaeleweka vyema kwa wananchi. Kamati yangu inashauri *FCC* kujitangaza na

kutoa elimu kuhusu majukumu yake. Aidha, Kamati inashauri *FCC* kufanya kazi kwa karibu sana na *TBS* kwani mara nyingi bidhaa duni zinaendana na bidhaa bandia, hivyo kwa kushirikiana wataweza kumaliza tatizo la bidhaa duni na bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala Wa Vipimo Na Mizani – *Weights And Measures Agency (WMA);* Kamati inaupongeza uongozi wa Wakala wa Vipimo na Mizani kwa juhudi walizozifanya hadi kuwa na uwezo wa kujitegemea. Aidha, Kamati inashauri elimu ya Vipimo itolewe katika ngazi zote hasa kwa watumiaji wa ngazi za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuisaidia Serikali kuongeza mapato na kusimamia vyema ukusanyanji wa mapato ya Serikali katika Sekta ya Gesi. Kamati yangu inaishauri Serikali kutumia Wakala wa Vipimo katika kukagua ujazo wa vipimo vya gesi, kwani eneo hili lina udanganyifu mkubwa kwa Serikali na hata kwa watumiaji wa gesi majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kukabidhi kiwanda cha Matairi kwa Shirika la Maendeleo la Taifa baada ya kusimamisha uzalishaji kwa muda mrefu. Pamoja na pongezi hizi, Kamati inaiomba Serikali kuiwezesha *NDC* kifedha ikiwa ni pamoja na kutafuta Mbia makini ambaye atashirikiana na *NDC* katika kukiendeleza kiwanda hiki. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa kiwanda hiki kiendelee kuzalisha matairi kama ilivyokusudiwa tangu awali. Hii itasidia kuhamasisha wakulima wa

mpira kufufua mashamba ya mpira ambayo yalianza kufa kutokana na kukosa uhakika wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo yaliyojitokeza katika kiwanda hiki siku za nyuma, Kamati inashauri kuwa, ni vizuri Serikali ikawa makini wakati wa kusaini Mkataba na Mbia atakayepatikana ili kutorudia kosa la awali na kusababisha kiwanda kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo na kuelezwa matatizo yanayokikabidhi kiwanda hiki tangu kuanzishwa kwake kuwa ni malipo ya waliokuwa wafanyakazi wa *Southern Paper Mills*, upatikanaji wa mali ghafi (magogo) na matatizo ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo ya wafanyakazi walioachishwa kazi wakati kiwanda kinabinafsishwa pamoja na Ardhi ya Kiwanda cha Karatasi Mgololo. Kamati yangu inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwalipa waliokuwa wafanyakazi wa *Southern Paper Mills* ambao walifukuzwa kazi tangu mwaka 2005 ili kumpa nafasi mwekezaji mpya kuendelea na shughuli zake za uzalishaji bila kubugudhiwa kwa sababu Mkataba unaonyesha kuwa yeye (mwekezaji mpya) hahusiki na malipo yoyote kwa wafanyakazi hao;

(ii) Kuhusu tatizo la Ardhi, Wizara ya Maliasili na utalii, zikutane ili kuona namna ya kulimaliza tatizo hili

kwani limechukua muda mrefu sasa na hivyo kukwamisha maendeleo ya kiwanda; na

(iii) Wizara ya Maliasili pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara zikae pamoja na kutafuta suluhisho la kudumu ili tatizo hili la upatikanaji na bei kubwa ya magogo likasababisha ukosefu wa mapato kwa Serikali na ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini changamoto zinazoikabili sekta hii. Kabla ya Sera ya Ubinafsishaji, tulikuwa na viwanda 21 baada ya ubinafsishaji viwanda vingi vimekufa vimebaki viwanda vitano tu na kati ya hivyo ni vitatu tu vinavyofanya vizuri vingine vinasuasua na viko mbioni kufungwa. Kufungwa kwa viwanda hivi kumeathiri dhana nzima ya ubinafsishaji ambayo ililenga kutoa ajira kwa wananchi, kununua pamba inayozalishwa nchini na hivyo kuboresha maisha ya wakulima wa pamba.

Kwa sasa tuna tatizo kubwa sana la uuzaji wa pamba yetu. Pamba inayotumika kwenye uzalishaji hapa nchini ni kati ya 20% hadi 30% tu na 70% inauzwa nje ya nchi kwa taabu sana. Kama viwanda vya nguo vitaendelea kuzalisha kwa kiasi kidogo na vingine kufungwa vitasababisha kero kubwa kwa wakulima wa pamba. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa karibu Viwanda vya Nguo ili kuwahakikishia Wakulima wa Pamba uhakika wa Soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imesikitishwa na hali mbaya na mwenendo mzima wa

Kiwanda cha Urafiki. Hii ni kutokana na hali halisi iliyopo sasa kiwandani hapo ikiwemo:-

(i) Matumizi mabaya ya fedha kiasi cha USD milioni 27 zilizotolewa na Serikali;

(ii) Kung'olewa kwa mashine na kuuzwa kama vyuma chakavu;

(iii) Wafanyakazi kufukuzwa kwenye nyumba za kiwanda na kuwapangisha watu wa nje;

(iv) Baadhi ya majengo ya kiwanda kupangishwa kwa wafanyabiashara na kuyafanya maghala ya kuhifadhia na kuuzia magari;

(v) Uzalishaji hauridhishi ni kama kiwanda kimesimama kuzalisha;

(vi) Wafanyakazi wengi kusimamishwa kazi na waliopo kulipwa mafao duni sana; na

(vii) Dhamira ya Serikali kuingia ubia na mwekezaji mwingine kabla ya kupata suluhisho la matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakati Kamati ilipotembelea kiwanda hiki iliishauri Wizara kusitisha mpango wake wa kuingia ubia na mwekezaji mpya, ikiwa ni pamoja na kumaliza matatizo yaliyobainishwa hapo juu. Kutokana na matatizo hayo hapo juu, Kamati inapenda ipate maelezo ya kina namna Serikali

ilivyojipanga ili kukinusuru kiwanda hiki muhimu ambacho Serikali ina Hisa ya 49%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaomba uridhie ombi letu la kuunda Kamati Ndogo ya Uchunguzi ili kuweza kubaini matatizo yaliyojitokeza katika kiwanda hili kwa lengo la kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea kiwanda cha kutengenezea chuma na kubaini upungufu wa vitendea kazi kwa ajili ya kujikinga na moto. Kamati iliagiza Serikali kufuatilia Kiwanda hiki na kuhakikisha kinanunua vifaa vya kujikinga na moto haraka iwezekanavyo kwa lengo la kunusuru maisha ya wafanyakazi. Kamati inapenda kupata maelezo na ufafanuzi wa namna ilivyoshughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imebaini matatizo makubwa kwenye Sekta ya Ngozi ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha sekta hii kutoendelea. Kwa mfano viwanda vingi vya ngozi vinazalisha kwa kusuasua na vingine kufungwa kabisa na hivyo wafanyakazi wengi kupoteza ajira, Serikali kupoteza mapato na wafugaji kukosa mahali pa kuuza ngozi zao. Aidha, lipo tatizo la mgongano wa kimaslahi kati ya wenye viwanda vya kusindika ngozi, wanunuzi wa ngozi kutoka kwa wafugaji na wauzaji wa ngozi ghafi nje ya nchi. Kamati yangu pia imegundua kuwa kuna udanganyifu mkubwa katika eneo hili kwa baadhi ya viwanda na wauzaji ngozi ghafi nje

kukwepa kodi *(Tax evasion)* na kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo haya, Kamati yangu inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwasaidia Umoja wa wanunuzi wa ngozi Tanzania *(UWANGOTA)* kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika ngozi vitakavyoweza kuboresha thamani ya ngozi na baadaye kuja kuzuia kabisa uuzaji wa ngozi ghafi nje ya nchi;

(ii) Kamati yangu inazishauri Wizara za Viwanda na Biashara pamoja na Uvuvi na Mifugo kuwa karibu na Viwanda ili viweze kujua ukweli wa uzalishaji halisi na mahitaji halisi ya ngozi. Hili litasaidia kuwafanya wenye viwanda kutokujiingiza katika biashara ya uuzaji ngozi ghafi nje ya nchi ambapo kwa sasa wamekiri wanafanya hivyo; na

(iii) Kamati yangu imekusudia kuunda Kamati ndogo kwa ajili ya kupata ukweli wa mambo haya ili iweze kuishauri Serikali ipasavyo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia utekelezaji wa mfumo wa soko huru kumekuwa na uingizwaji wa bidhaa zisizo na ubora na bandia na ambazo huuzwa kwa bei ndogo na kusababisha ushindani usio wa haki katika biashara kwa viwanda vyetu vya hapa nchini.

Aidha, ukwepaji wa ulipaji wa kodi unaotokana na *under invoicing, under declaration, tax evation* na kadhalika, vimeongeza tatizo la ushindani usio wa haki kwa viwanda vya ndani. Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kulinda viwanda vyetu ili viweze kuhimili ushindani. Hii ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa uzalishaji, upatikanaji wa mali ghafi ikiwemo magogo kwa ajili ya mbao kumaliza matatizo ya miundombinu, kuweka kodi kubwa kwa bidhaa zinazoingia nchini ambazo viwanda vyetu vya ndani vinatengeneza na viwanda vilivyobinafsishwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Mikataba *(MoU).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dhamira ya Serikali ya kupandisha ushuru wa mafuta ya mawese yasiyosafishwa *(crued palm oil),* Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa makini sana katika suala hili ili kuwe na ushindani wa haki na viwanda kama hivi vilivyoko katika nchi nyingine za Afrika Mashariki kama Kenya na Uganda ambako wameondoa kabisa ushuru katika bidhaa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na maelezo ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika taarifa yake ya utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa fedha 2011/2012 kuhusu Serikali na Taasisi zake kununua bidhaa ikiwemo Samani kutoka kwa wazalishaji wa ndani. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huo wa busara na wenye kujali maslahi kwa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji wa ndani. Hata hivyo, Kamati inashauri

kuwa ni wakati muafaka sasa wa kuweka kauli hizi katika Sheria ili kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uhaba mkubwa wa sukari na kupanda kwa bei ya bidhaa hii muhimu, Kamati yangu imefuatilia kwa ukaribu kufahamu mikakati kabambe itakayoondoa kero ya sukari hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa ili kutatua tatizo Bodi ya Sukari ilitoa Leseni za kuagiza sukari kutoka nje ya nchi kiasi cha tani 200,000 mpaka sasa tani 91,000 zimekwishaingia nchini, tani 25,000 zipo Bandarini na tani zilizobakia zitaingia hivi karibuni. Hata hivyo, ongezeko hili la sukari bado halijaleta nafuu kubwa ya upatikanaji wa sukari kwa bei nafuu. Sababu kubwa ni kwamba nchi za jirani nazo zina uhaba wa sukari, hivyo sehemu ya sukari inayoingizwa inatoroshwa na kuvuka mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha nchi inakuwa na sukari ya kutosha ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo wa uwajibikaji kwa Askari wetu wanapokamata sukari inayovuka mipaka. Kamati inaona upo umuhimu mkubwa kwa Serikali kuhamasisha wananchi kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya sukari hii ikiwa ni pamoja kuja na mfumo utakaowavutia wakulima wadogo wadogo kuanzisha viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imepata malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabishara na

wenye viwanda kuhusu utaratibu mzima unaotumika kutoza na kukusanya kodi. Kamati inashauri *TRA* – kuwa rafiki na kutoa elimu kwa wananchi ili wapende kulipa kodi. Kwa sasa baadhi ya Maafisa wa *TRA* huwa wanaonekana kama aina nyingine ya Polisi kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Maonyesho ya 36 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo ilifarijika sana na kazi nzuri inayofanywa na Mamalaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzanaia *(TANTRADE),* licha ya kuwa na rasilimali watu kidogo ukilinganisha na majukumu yao. Mamlaka hii ilianzishwa mwaka 2009 kwa lengo la kuratibu na kusimamia biashara ya ndani na nje. Ikiwa katika viwanja vya Mwalimu Nyerere Kamati yangu iliweza kushiriki uzinduzi wa Maonyesho uliofanywa na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Balozi Seif A. Idd uliofanyika tarehe 3 Julai, 2012. Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Panua Wigo wa Biashara yako."

Mheshimiwa Mwenyekiti, maonyesho ya mwaka huu hayakutangazwa vya kutosha kama mwaka uliopita na hivyo kufanya ushiriki wa wa Wizara, Taasisi na hata wafanyabiashara kutoka nje kuwa kidogo. Kamati yangu inashauri maandalizi ya maonyesho yafanywe mapema ili kupata washiriki wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inasikitishwa na urasimu uliopo bandarini ambao unakwamisha utoaji wa mizigo kwa wakati, hivyo kuongeza gharama za uzalishaji na hivyo kusababisha

upandaji bei wa bidhaa na kuwaumiza walaji. Kwa mfano, wapo wafanyabiashara ambao walileta bidhaa zao kwa ajili ya maonyesho ya Saba Saba ambao bidhaa zao zimekaa sana bandarini na hivyo kuchelewesha maandalizi kwa ajili ya kuzionyesha na kuziuza kwa muda uliotakiwa. Kamati inaishauri Serikali kusimiamia kwa makini Mamalaka hii ili wafanyabiashara waendelee kuitumia bandari yetu la sivyo wengi wa wafanyabiashara wanalazimika kusafirisha mizigo yao kwa kutumia bandari ya Mombasa na hii inapoteza mapato ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza washiriki wote katika maonyesho hayo hasa washiriki kutoka nchi za nje ambao wamekuwa chachu na kivutio kikubwa kwa washiriki wa ndani na nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kama nilivyoeleza hapo awali kuhusu majukumu ya yanayofanywa na Taasisi /Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, Kamati inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa kuweka vipaumbele ndani ya Wizara ili kuziwezesha kwa mwaka huu Taasisi za *SIDO, NDC, EPZA* ziweze kutekeleza vyema majukumu yake na baadaye kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru tena wewe binafsi, Naibu Mwenyekiti Mheshimiwa Job Ndugai, pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Azzan Zungu, na Mheshimiwa Silvester Mabumba kwa kuendesha Vikao vya Bunge vizuri kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Naibu Waziri - Mheshimiwa Gregory George Teu, Katibu Mkuu - Bibi Joyce Mapunjo, pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zake kwa maelezo na ufafanuzi walioutoa mbele ya Kamati, wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wao katika kuchambua Bajeti ya Wizara na kutoa Maoni haya ya Kamati. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo – Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe ni Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, Mheshimiwa Chiku Aflah Abwao, Mheshimiwa Conchesta Leons Rwamlaza, Mheshimiwa Ester Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Naomi A. Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa

Salim Hassan Abdallah Turky, Mheshimiwa Mohamed Dewji, na Mheshimiwa Omari Rashid Nundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashilillah na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nimshukuru Katibu wetu Bibi Angelina Langisi Sanga kwa kazi nzuri ya kuihudumia Kamati wakati wote ikiwa ni pamoja na kuandaa Maoni haya ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kiidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mgimwa.

Waheshimiwa Wabunge, nitaomba wenzetu wanaotusaidia kuweka kumbukumbu ya vikao vyetu waichukue taarifa hii kwa ujumla wake kama ilivyo na kuingiza kwenye orodha ya kumbukumbu ya vikao hivi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, niwataje Waheshimiwa Wabunge watakaoanza kuchangia kama hawako katika ukumbi huu ili waweze

kujiandaa na kusogea ndani ya ukumbi. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Magalle John Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Mussa Zubeir.

Baada ya kuwataja hao wachangiaji wa mwanzo naomba sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu hoja hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaomba kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa na marafiki wote wa Marehemu waliofariki kutokana na kuzama kwa meli ya Skagit karibu na kisiwa cha Chumbe huko Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipigania siku zote na kwa kunirejeshea afya yangu na sasa nimesimama hapa ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Ofisi ya Bunge kwa ujumla kwa huduma zote za msingi za matibabu kuanzia pale Hospitali ya Bugando, kisha kunisafirisha

mpaka *Muhimbili Hospital* na hatimaye kunipeleka nchini India kwa matibabu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru madaktari wote na wauguzi walio nihudumia kipindi chote cha matibabu, kwa kweli mwenyezi Mungu awabariki. Hali kadhalika napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wote wa Jimbo la ilemela na Jiji la Mwanza kwa ujumla kwa kazi nzuru waliyo ifanya kwa kuhakikisha kuwa ushindi unapatikana katika uchaguzi wa udiwani kata ya Kirumba uliofanyika tarehe 1st April 2012 pamoja na kuwa walipata taarifa ya tukio la kutekwa kwangu katika jaribio la kutaka kuniua usiku wa kuamkia siku ya kupiga kura, lakini waliamka mapema asubuhi na kwenda kupiga kura na kisha kuja hospitali ya Bugando kunijulia hali jambo ambalo lilionyesha imani kubwa walionayo kwangu na kwa kweli ilikuwa ni sala tosha na ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wabunge wote walionitembelea hosptali na Watanzania wote kwa maombi yao, naamini Mwenyezi Mungu atawabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nitoe shukrani kwa viongozi wangu wa Chama changu CHADEMA Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuhakikisha umoja na mshikamano kwa wananchi wa Jimbo la Ilemela unaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto zote ninazokutana nazo, napenda kutumia fursa hii kuishukuru familia yangu kuendelea kuwa nami bega kwa bega bila kukata tamaa, sote tukiamini kuwa Mungu akiwa upande wetu, hakuna jambo litakalotushinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini kwa namna ya kipekee, namshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa kunipa dhamana ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Viwanda na Biashara pamoja na changamoto zote ilizo nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira ya Biashara, mazingira ya kufanyia biashara na uendeshaji wa biashara nchini bado ni magumu na yanaweza kuonekana wazi kutokana na ubovu wa miundombinu, hususan reli, umeme, maji, rushwa, barabara za vijijini na ufisadi katika maeneo mbalimbali ya utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira haya yanakuwa magumu zaidi kutokana na urasimu uliopo Serikalini na mlolongo mrefu ambao mfanyabiashara anapaswa kuufuata kabla ya kuweza kupata leseni kwa ajili ya kuweza kufanyia biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za *Doing Business Report*, inayoandaliwa na Benki ya Dunia, pamoja na ile ya *Global Competitiveness Report*, inayoandaliwa na *World Economic Forum*, zinaonyesha kuwa Tanzania

haifanyi vizuri katika kujenga mazingira ya kuvutia wawekezaji.

Hali hii inachangiwa sana na urasimu wa Taasisi za Serikali katika kuwahudumia wawekezaji ili kutoa huduma bora na za haraka, ukosefu wa miundombinu kama maji, barabara, umeme, usafiri na hasa ikizingatiwa kuwa ikishafika saa kumi na mbili jioni uchumi wa nchi yetu huwa unalala, kwani hakuna usafiri ama wa ndege au mabasi kwa muda wa usiku, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama Rais angekwenda nje kila siku, kama hatujaboresha mazingira ya uwekezaji katika nchi yetu tutakuwa tunaendeleza matumizi mabaya ya rasilimali za Taifa letu tu.

Pamoja na Mheshimiwa Rais kwenda G8 na kurejea akisema kuwa tumepata mafanikio makubwa, lakini Taarifa ya Benki ya Dunia ya mazingira ya kufanya biashara, inaonyesha kuwa Tanzania mwaka 2011 ilikuwa ya 125 na mwaka huu 2012 iko nafasi ya 127. Huku ni kurudi nyuma, na hii ni dalili ya wazi kuwa kwenda nje ya nchi siyo suluhisho la kupata wawekezaji, bali njia pekee ni kuboresha mazingira yetu ya uwekezaji hasa kwa kuimarisha miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na *World Investment Report 2011,* mitaji kutoka nje imeongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 646 mwaka 2009 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 700 mwaka 2010. Hii ni

sawa na ongezeko la Dola milioni 53 kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii imekuja wakati ambapo nchi yetu imekuwa na wawekezaji kwenye Sekta ya Gesi na Mafuta ambao wamejitokeza katika kipindi husika. Huu ni ushahidi wa wazi kuwa mazingira ya biashara nchini ni mabovu. Ndiyo maana mitaji inaongezeka kwa kasi ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inahoji kama kwa mwaka mzima mitaji inaongezeka kwa kiwango hicho, kuna haja gani ya Serikali kuendelea kusisitiza kuwa ziara za Rais nje ya nchi zimekuwa na mafanikio makubwa ya kuvutia wawekezaji? Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika katika mwaka husika kwa ajili ya ziara za Rais na viongozi wengine nje ya nchi kwa ajili ya kutafuta wawekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Biashara ndogo nchini; mwaka jana wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya *Doing Business* ya Benki ya Dunia huko Arusha, baadhi ya Watanzania walinukuliwa katika vyombo vya habari wakilalamika kuwa kama tatizo hili la ugumu wa mazingira ya kufanyia biashara hapa nchini halitafanyiwa kazi ipasavyo kama moja ya masuala ya dharura katika kukuza uchumi na kupambana na umaskini, basi tutaendelea kuwa nyuma ya nchi nyingine, zikiwemo wanachama wenzetu wa *EAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo vya ufanyaji biashara nchini vinakwenda katika maeneo mbalimbali, hadi kugusa eneo la masoko kwa

wafanyabiashara wetu hapa nchini. Wananchi wanaendelea kulalamikia juu ya manyanyaso wanayoyapata katika eneo la kutozwa ushuru mkubwa kwenye masoko mbalimbali na hii inakwaza ufanyaji wa biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni wafanyabiashara wauzaji wa matunda na mbogamboga katika Soko Kuu la Majengo, Dodoma. Waliwahi kumwandikia barua Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, zaidi ya mara kadhaa, wakimlalamikia mambo mawili, kwanza kutozwa ushuru wanapoteremsha bidhaa zao sokoni licha ya kwamba zinakuwa zimeshalipiwa ushuru husika katika maeneo walikonunua bidhaa hizo wakati ushuru huo ulikwishafutwa na Serikali.

Pili, walilalamika juu ya matumizi ya Polisi na Mawakala wanaokusanya ushuru yanayoandamana na unyanyasaji pamoja na kuwekwa rumande na kushtakiwa Mahakamani wakati jambo wanalolalamikia kuhusu kutozwa ushuru mara mbilimbili ni suala la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wafanyabiashara hao wa Majengo (ambao ni mfano tu wa manyanyaso wanayofanyiwa wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali nchini) kuiandikia Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI mara tano bila ofisi hiyo kuchukua hatua zozote, huku Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, wakati huo akiwa Alhaji Musa Nkhangaa, naye ikionekana kupuuza maelekezo

kutoka Wizarani, mpaka leo wanaendelea kunyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya barua ya maelekezo kutoka Wizarani iliyoandikwa na aliyekuwa Naibu Waziri wakati huo, Mheshimiwa Mizengo Pinda, yenye Kumbu. Na. *HB*.42/387/01 ya tarehe 15 Julai, 2005, ambayo inadhihirisha pasi na shaka kuwa malalamiko ya wafanyabiashara hao ni ya msingi lakini Serikali bado inaonesha uzembe wa hali ya juu kutatua matatizo yanayowakabili wananchi wake, nanukuuu:

"Tarehe 8/2/2005 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais alipokea barua ya malalamiko ya Wafanyabiashara hawa kuhusu ushuru unaotozwa katika soko hilo. Tarehe 11/2/2005, Ofisi hii ilikuletea maelekezo ya kuitaka Ofisi yako ishughulikie suala hili. Tarehe 22/2/2005 Wafanyabiashara hao walimwandikia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, barua nyingine .Tarehe 14/4/2005 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, aliandikiwa tena barua na ikafuatiwa na barua yao ya tarehe 26/5/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipoona hilo liko kimya tarehe 11/7/2005 wamemletea Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nakala ya barua yao ya tarehe 26/5/2005 kukumbushia suala lao. Kwa kuwa kwa bahati mbaya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI bado maelekezo yake hayajapata maelezo kutoka Ofisi yako imetuwia vigumu kuwajibu ipasavyo kwa kuwa licha ya barua wamekuwa wakija hapa ofisini na hata Bungeni kumtafuta Waziri wa Nchi au mimi, tujulisheni utekelezaji wa maelekezo ya Waziri wa Nchi,

TAMISEMI ili tujue namna ya kuwasaidia wafanyabiashara hawa. Natumaini sasa jambo hili litapatiwa ufumbuzi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nukuu ya barua hiyo hapo juu mbali ya kuonesha namna ambavyo Serikali hii ya CCM isivyokuwa sikivu kwa vitendo wanavyovifanya vya kuwanyanyasa wananchi wake ambao ni wafanyabiashara wadogo. Pia inadhihirisha namna ambavyo mamlaka iliyo chini inavyoweza kupuuza mamlaka ya juu yake na hii ni dalili ya Serikali ambayo haina nidhamu na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali inayodhihirisha kuwa Serikali hii ya CCM si sikivu, mpaka sasa tunavyozungumza hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu ameendelea kupuuzwa na watumishi walioko chini yake, ambapo wafanyabiashara hao wanaendelea kukumbana na manyanyaso hayo waliyoyaandikia tangu miaka 10 iliyopita. Huu ni mfano mdogo tu kati ya mifano mingi, mingine yenye manyanyaso ya kutisha ambayo kwa kweli inawakandamiza wafanyabiashara wadogo, wa kati na wale wakubwa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni uliojengeka nchini kwa Serikali za Mitaa kutunga sheria ndogo ndogo (Kanuni) katika masuala yanayohusu biashara ambayo Bunge lako linakuwa limefikia maamuzi ya kuyafutia kodi ni dharau kwa Bunge hili kwani wenye wajibu wa kutunga sheria ni Bunge na kama linafuta kodi ni lazima mamlaka za Serikali za Mitaa ziheshimu maamuzi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wadogo wadogo wanaojulikana kama "Wamachinga" na akinamama na baba lishe wamekuwa wakikumbana na manyanyaso mengi kutoka kwenye vyombo vya dola kama vile Polisi na Mgambo wa Miji na Majiji mbalimbali na wengine huishia kupoteza mitaji yao midogo ambayo wameitafuta kwa jasho jingi kwani Serikali haijaweka utaratibu wa kuwakopesha ama kuweza kuwapatia mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haikubaliani na unyanyasaji huu unaofanywa na vyombo vya dola kwa wafanyabiashara wadogo waliopo nchini na tunaitaka Serikali kueleza Bunge ni kwa nini manyanyaso hayo yanaendelea? Ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wale wanaochukua mitaji ya wafanyabiashara wadogo na hatimaye kuwafilisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi wa bidhaa za nje na viwango vya ubora kwa muda mrefu sasa Tanzania imekuwa moja ya nchi inayoweza kufananishwa na jalala la kutupia bidhaa zilizo chini ya viwango au zilizokwisha muda wake wa matumizi. Hali hii imekuwa ni moja ya vigezo vinavyotumika kuonesha utendaji dhaifu wa Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajulikana vyema kuwa kuruhusu nchi yetu kuwa dampo la bidhaa zilizopitwa na wakati au zile zilizo chini ya viwango ni kuua uchumi wetu na kuhatarisha maisha ya wananchi wetu na ni tishio kwa usalama wa Taifa vile vile. Serikali makini

ambayo inasema kuwa mipaka ya nchi iko salama na hakuna hatari yoyote inayowakabili wananchi wake, haipaswi kuachia wananchi wake wakaendelea kutumia bidhaa ambazo zinahatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa visingizio mara kwa mara kuwa ukubwa wa mipaka ya nchi iliyosambaa ndiyo unasababisha kuwepo kwa njia nyingi za panya ambazo zimekuwa ni vichochoro vinavyofanya kazi usiku na mchana kupitishia bidhaa hizo, ingawa wakati mwingine bidhaa za namna hiyo pia zinapitishwa katika njia ambazo zina ulinzi mkali na ukaguzi kama kwenye viwanja vya ndege, bandari zetu na kwa usafiri wa magari. Kwa vyovyote vile, hali hii ya ukubwa wa nchi haiwezi kuwa sababu tena hapa, bali ni uzembe wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo kulinda raia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kuwa kila mwananchi anao wajibu wa kuhakikisha nchi hii haiwi dampo la bidhaa mbovu, hasa kwa kuhakikisha wanazitambua, kutozinunua na kisha kutoa taarifa kwa mamlaka husika, bado hiyo haiwezi kuondoa wajibu wa msingi kwa Serikali yoyote makini kuhakikisha usalama wa nchi na raia wake wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kuwa suala hili linadhihirisha kuwa mipaka ya nchi yetu haiko salama, bidhaa zilizo chini ya kiwango zinaathiri uchumi wa Taifa, kwa namna mbalimbali ikiwemo kupunguza au kuikosesha Serikali mapato, kukosesha ajira vijana wetu kwa sababu bidhaa hizo zinaua viwanda vyetu vya hapa nyumbani kutokana na kuzidiwa na ushindani

kwani siku zote bidhaa hizo mbovu, hasa zinazotoka nje ya nchi huuzwa kwa bei ndogo. Hali kadhalika, uwepo wa bidhaa feki hukimbiza wawekezaji makini ambao hawako tayari kufanya kazi katika nchi inayokubali kuwa dampo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mpango wa Serikali wa *Pre-shipment Verification of Conformity (PVoC)* ambao ni mpango wa kukagua bidhaa zikiwa nje ya nchi ambao Serikali imeamua kuutekeleza kwa sasa umeingia kwenye msafara uleule wa kutoa zabuni kwa kampuni ambazo hazina uwezo wala sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kampuni tatu zilizopewa kazi ya kufanya ukaguzi huu mojawapo ni ya *M/S Bureau Veritas Inspection, Valuation and Control (BIVAC)* ya nchini Ufaransa. Taarifa zilizopo ni kuwa Kampuni hii ilishindwa kazi nchini Uganda na Japan ambako ilikuwa inakagua magari yaliyokuwa yanasafirishwa kuja Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni vigezo gani vilitumika kuipatia mkataba kampuni hii na kama Wizara ilifanya jitihada za kujua kuwa iliondolewa kwenye nchi hizo kwa sababu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunataka kujua kuna hatua gani za makusudi ambazo zinachukuliwa na Serikali dhidi ya nchi na makampuni ambayo yamekuwa yakizalisha na kusambaza bidhaa feki hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini. Suala lingine ambalo mpaka sasa linaonekana kuwa ni kikwazo kwa wazalishaji/wafanyabiashara hasa wale wa kati na wadogowadogo nchini ni vifungashio vya bidhaa zao, ambavyo ni moja ya vigezo muhimu katika kupima ubora wa bidhaa husika, kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kupunguza gharama za usafirishaji, kuongeza thamani na wakati huo huo kupunguza uwezekano wa kuharibika zinapokuwa katika hatua mbalimbali za usambazwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao wajibu wa kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wetu wote, wadogo, wa kati na wakubwa, wanafungasha bidhaa katika viwango vya Kimataifa ili kuweza kushindana katika soko la ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu. Hali hii pia imeendelea kuwa kikwazo pamoja na *TBS* kuanzisha teknolojia ya kukagua vifungashio *(PTC*), ambayo inapaswa kuwa nafasi muafaka kwa wazalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kuhusu Serikali kutekeleza wajibu wake wa kuhamasisha wananchi wawekeze katika viwanda vya kusindika mazao, ikiwa ni moja ya vigezo vya kuongeza thamani, kisha kuongeza bei zetu katika soko la dunia na hatimaye kuongeza pato la Taifa, imeelezwa kuwa kati ya miradi 173 iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC)*, kwa mwaka 2011, miradi 18 ni ya uongezaji thamani mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile, kiwango cha miradi 18 kwa ajili ya kuongeza thamani mazao ya kilimo kwa nchi kama yetu ambayo imerudi nyuma sana katika masuala ya viwanda na hasa vile vinavyohusika na bidhaa za kilimo, ni kiwango kidogo sana. Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa Serikali kuwa kama kweli tuna nia ya kushindana katika soko la Afrika Mashariki, *SADC* na lile la Dunia, hatuna budi kuwa na mpango kabambe wa kuziongezea thamani bidhaa zetu.

Kambi ya Upinzani inaitaka serikali itoe maelezo ya kina mbele ya Bunge lako Tukufu, juu ya kuwepo kwa vituo vinne vya atamizi ambavyo vinapaswa kuwa maalum kwa ajili ya kuwaweka wajasiriamali pamoja na kuwapatia huduma zinazostahili ili kuendeleza ubunifu wao, ni wajasiriamali wangapi wamewezeshwa kuongeza thamani kwenye bidhaa zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ni vyema Serikali ikatoa maelezo ya kina kuwa vituo hivyo vinavyoelezwa kuwa vina jumla ya wajasiriamali 56 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Rukwa, viko katika maeneo gani hasa na kwa kiwango gani vimeweza kufikia malengo yaliyotarajiwa na iwapo kuna mkakati wowote ule wa kuwafuatilia na kuwafanyia tathmini wajasiriamali hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* na ukaguzi wa magari nje ya nchi; Shirika la Viwango Tanzania limekuwa na utaratibu wa kukagua bidhaa mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuweza kubaini ubora wake na

kutoa hati maalum za ubora kabla ya bidhaa hizo kuruhusiwa kuingia kwenye soko la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa kitengo maalum kwa ajili ya kufanikisha kazi hiyo, shirika hili limeonesha udhaifu mkubwa sana katika kufanya ukaguzi wa magari unaofanywa na kampuni mbalimbali nje ya nchi kwani waliopewa kazi hiyo ni makampuni ambayo hayana uwezo wala sifa ya kuweza kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kampuni ambazo zilipewa kazi ya kufanya ukaguzi bila hata kupitia utaratibu wa zabuni kutangazwa kama ilivyofanyika kwa kampuni ya *VOSA* ya nchini Uingereza kupewa zabuni ya kufanya ukaguzi bila utaratibu kufuatwa. Kambi ya Upinzani inataka kujua zimechukuliwa hatua gani kwa wale ambao wamevunja sheria kwa kutofuata taratibu za zabuni na kama kampuni hiyo inafanya kazi zake kisheria ama la na kama ukaguzi utakuwa halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Serikali ni kuwa tangu mwaka 2002 ni kuwa kiasi cha dola 18 milioni kiliweza kutumika kama ada ya ukaguzi wa magari na fedha zilizoingia nchini ni kiasi cha dola 2.2 milioni tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni kwa nini Serikali ilipata kiasi kidogo namna hiyo cha fedha na kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa tunaweza kukusanya mapato zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo makampuni ambayo yalifungiwa na *TBS* kufanya kazi ya ukaguzi kutokana na makampuni hayo kutokufikisha fedha Serikalini, makampuni hayo ni pamoja na *Jaffer Al Garage (Dubai), Planet Automotive (Singapore), Quality Garage (Hong Kong)* na *WTM* ya (Uingereza). Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ni hatua gani zaidi zimechukuliwa dhidi ya makampuni hayo na fedha zimerejeshwa ama la? Vile vile ni kiasi gani cha fedha kilichokusanywa kutokana na faini wanazopigwa wamiliki wa magari ambao wanaingiza magari yao bila kukaguliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wakati wa Bunge la Mwezi Aprili zilipowasilishwa taarifa za Kamati za Bunge za *POAC, PAC* na ile ya CAG wakati mjadala ulipokuwa mkali na baada ya Bunge kuahirishwa ipo timu iliyosafiri kwenda Japan kuhusiana na suala la ukaguzi wa magari ilimhusisha Waziri wa Viwanda na Biashara wakati huo Mheshimiwa Cyril Chami (japo tunajua kuwa hakuweza kusafiri), Wabunge akiwemo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Mahamood Mgimwa na Mheshimiwa George Simbachawene wakiambatana na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa *TBS* Charles Ekelege, Mwenyekiti wa Bodi ya *TBS,* Oliver Mhaiki na Mrs Kezia Mbwambo ambaye ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa barua ya *TBS* iliyosainiwa na Mhandisi J. Katabwa kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa *TBS* ya tarehe 17.4.2012 iliyotumwa kwa Mkurugenzi wa Kampuni hiyo ya *East*

*Africa Automotive Service* yenye kumb. Na*. QA/QCC-A/825/118* ilionesha kuwa ujumbe huo ulikuwa unawakilisha Kamati ya Bunge hili na ulitumwa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kuwa hakukuwa na taarifa zozote ambazo ziliachwa na ujumbe huo Wizara ya Mambo ya Nje wala kutumwa kwa Balozi wetu ambaye angekuwa na jukumu la kuwapokea. Ila barua hiyo ilimwelekeza Mkurugenzi wa kampuni hiyo ndugu Prosper kuhakikisha kuwa anawatafutia malazi wajumbe hao kwenye hoteli. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kuhusiana na mambo yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa barua ya mwaliko ilionesha kuwa Wabunge walikwenda kuwakilisha Kamati ya Bunge, tunataka kujua walikwenda kuwakilisha Kamati gani na kama walipewa jukumu hilo na Ofisi ya Spika na ripoti yao iko wapi. (*Makofi*)

(ii) Kama hawakutumwa ni hatua gani zitachukuliwa na Ofisi ya Spika dhidi yao kwani huku ni kulivunjia heshima Bunge. (*Makofi*)

(iii) Nini tamko la Serikali kuhusiana na ziara hiyo na ni nani aligharamia ziara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuboresha ukaguzi wa magari unaofanywa uwe na ufanisi unaotakiwa na kuondoa ujanja ujanja unaofanywa na kampuni hizi na kuepusha magari ambayo yanaingia

nchini bila kukaguliwa na hasa yale ambayo yanapitia njia za barabara kama vile kutokea Afrika ya kusini kupitia Tunduma na kadhalika Kambi ya Upinzani ina mapendekezo yafuatayo:-

(a) Magari yawe yanapangwa kigredi badala ya kuangalia umri wa gari kwani yapo ambayo umri ni mkubwa lakini yametumika kidogo na ambayo umri ni mdogo lakini yametumika sana.

(b) Magari yawe yanakaguliwa nchini moja kwa moja na hii itaongeza fursa ya ajira kwa vijana waliomaliza *VETA* na Jeshi la Polisi waliohitimu masomo ya ukaguzi. Hii ni kwa sababu magari sasa yanaagizwa kwa njia ya intaneti na hata mmiliki anakuwa hana taarifa za uhakika kama yamekaguliwa ama la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda, Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2012/2013, iliyosomwa hapa Bungeni na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Daktari William Mgimwa, katika ukurasa wa 34 imeeleza: "Kadhalika, Serikali imefanya uhakiki wa mashirika 170 yaliyobinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hayo, mashirika 41 yalikutwa yanajiendesha kwa faida, mashirika 66 yanajiendesha kwa hasara na mashirika 63 yalikuwa Mfilisi. Kwa yale ambayo yanaendeshwa kwa hasara, yatawekwa chini ya Mfilisi kwa lengo la kuyachambua na kupendekeza hatua za kuchukuliwa. Aidha, kwa yale yaliyokuwa Mufilisi hatua za kuyafilisi zinaendelea."

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo viwanda vingi sana vilibinafsishwa na kushindwa kutekeleza masharti ya mkataba na sasa ama vimekufa kabisa, vingine vimegeuzwa maghala ya mazao au havifanyi kazi kabisa. Viwanda vilivyobinafsishwa na sasa havifanyi kazi kutokana na wawekezaji walionunua viwanda hivyo kushindwa kutekeleza masharti ni pamoja na Viwanda vya nguo vya Urafiki, *Mwatex, Sungura tex, Mutex* na kadhalika, Viwanda vya zana za kilimo, Viwanda vya Korosho, Viwanda vya Mkonge, Viwanda vya Pamba, Viwanda vya Kukoboa Kahawa na Viwanda vya Kusindika Ngozi, mfano, Mwanza *Tanneries* na kadhalika. Orodha ni ndefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuwa pamoja na bajeti kuu ya Serikali kuendeleza hadithi kama nilivyonukuu hapo juu, lakini katika randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwenye sehemu ya malengo na mikakati ya Wizara itakayotekelezwa mwaka wa fedha 2012/2013, hakuna mahali popote katika sekta ya viwanda ambapo imeelezwa nini hatma ya viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ivirejeshe Serikalini viwanda vyote ambavyo vilibinafsishwa na kushindwa kutekeleza masharti ya mkataba, kwani ndivyo Sheria inavyotaka na sio vinginevyo na hii itaongeza pato la Taifa na ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viwanda vya Korosho vilivyobinafsishwa; Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iweke wazi hapa Bungeni juu ya hatma

ya Viwanda vya Korosho vilivyokuwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, ambavyo viliuzwa katika zoezi la ubinafsishaji kuanzia miaka ya tisini. Ni vyema sasa Serikali kupitia Wizara hii, ikatoa maelezo ya kina yatakayoweza kuwaelewesha vizuri wananchi wa Mikoa ya Kusini juu ya Viwanda vya Likombe, Lindi, Mtama, Newala I na Newala II.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Kamati ya *POAC* na taarifa yake kuwasilishwa katika Bunge lako, ilibainika kuwa zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma katika Sekta Ndogo ya Viwanda vya Korosho limesababisha kilio na kuongeza machungu kwa wakulima wa Mikoa ya Kusini na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hiyo ilibaini viwanda vyote vya kubangua korosho ambavyo vilijengwa kwa Mkopo wa Benki ya Dunia kwa thamani ya shilingi bilioni 426, havifanyi kazi, huku wawekezaji waliovinunua, wakijiamulia kufanya watakavyo kinyume na masharti ya mikataba na kuvigeuza kuwa maghala ya kuhifadhia korosho, huku nchi yetu, hususani kupitia Wizara ya Biashara na Viwanda, ikiendelea kupata hasara kubwa kwa kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani ilielezwa na *POAC* kuwa Kiwanda cha Likombe kilichoko Mjini Mtwara kilichouzwa mwaka 2004, kwa Kampuni ya *Micronix System Limited*, mbali ya kwamba kiwanda hicho hakijawahi kuzalisha tangu kilipobinafsishwa

mwaka 2004, mwekezaji hajawahi kufanya ukarabati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilibainika kuwa sehemu ya ghala imekodishwa kwa kampuni binafsi ambayo inaendesha zoezi la kutunza korosho kwa mtindo wa stakabadhi ghalani na pia amekodisha sehemu ya Kiwanda kwa Kampuni ya *Olum* ambayo inafanya shughuli za ubanguaji wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati viwanda vinakufa Bodi ya Korosho inaonekana kujikita zaidi katika kutafuna fedha za posho badala ya kushughulikia maslahi ya wakulima wa korosho kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara kama tulivyoonesha kwenye hotuba ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutekeleza mapendekezo na maazimio ya Bunge ya kurejesha Viwanda hivyo Serikalini na kutengeneza mkakati wa namna ya kuvifufua na kuviendesha kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba suala la *General Tyre* imesemwa limekabidhiwa kwa *NDC*, bado Serikali inawajibika kuliambia Bunge lako juu ya hatua gani zinachukuliwa kukinusuru Kiwanda hicho ambacho taarifa zinasema hali yake ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na madeni kiwanda hiki kilifikia hatua ya kutaka kupigwa mnada na taarifa ilitolewa hapa Bungeni. Kambi ya Upinzani tunataka kujua ni hatua gani imefikiwa katika kuyalipa madeni hayo?

Aidha, Kambi ya Upinzani inahoji kuhusu mustakabali wa waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha *General Tyre*. Katika suala hili, ni vyema Bunge hili likajulishwa hatma ya utekelezaji wa ripoti ya Kamati Ndogo ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (*POAC*) iliyoundwa kufuatilia suala la Kiwanda cha *General Tyre,* hasa kuhusu kuifufua kampuni hiyo na namna ya kurejesha mikopo iliyochukuliwa na kampuni hiyo kwa dhamana ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Samaki, kuna uhusiano mkubwa sana kati ya tatizo la kushuka kwa bei ya samaki linaloendelea kuwakabili wavuvi hivi sasa nchini, hususan katika Ziwa Viktoria na mwenendo mbovu wa wawekezaji, ambao wanamiliki viwanda vya samaki hapa Tanzania na katika nchi jirani, zinazotumia ziwa hili, mathalani Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Kamati iliyoundwa kuangalia bei ya samaki aina ya sangara katika nchi tatu zinazotumia Ziwa Victoria za Tanzania, Kenya na Uganda imegundua kuwepo kwa tofauti kubwa ya bei ya kununua samaki mwaloni na kiwandani. Kati ya nchi zote hizo tatu, imebainika kuwa Tanzania ndiyo pekee ambayo bei za bidhaa hiyo ziko chini kwa kilo moja ya samaki, sehemu zote, mialoni na viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya bei nzuri kwa kila kilo ya samaki katika viwanda vya Kenya, wavuvi wengi wa Tanzania wamekuwa wakilazimika kwenda kuuza bidhaa zao katika nchi hiyo jirani, hali

ambayo inaendelea kuviimarisha viwanda hivyo huku vya hapa nchini vikionekana kutofanya kazi na wavuvi kuendelea kupunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la bei kuwa tofauti kuna kila harufu ya hila, kwa sababu wamiliki wa viwanda nchini Kenya ni hao hao ambao wanamiliki viwanda Tanzania sasa inakuwaje upande mmoja wanunue kwa bei kubwa na upande wa pili wanunue kwa bei ndogo? Kwani Kenya bei ya kununulia kilo moja kiwandani ni sawa na shilingi 4,300 mpaka 5,000 na huku Tanzania ni kati ya shilingi 2,500 hadi 3,000 kwa kilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haikubaliani na hoja kuwa hali hii inasababishwa na kushuka kwa bei kwenye soko la dunia kwani samaki wanaozalishwa na viwanda vya Kenya wanauzwa kwenye soko lipi la dunia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa watu wanaofanya kazi katika viwanda hivyo vya samaki, hususan katika viwanda vya Tanzania na Kenya inaonekana wazi kuwa sheria za Tanzania hazina meno katika suala hili, kwani Kambi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa viwanda vingi vya samaki nchini Tanzania havijaajiri watu, hivyo Watanzania wengi wanaofanya katika viwanda hivyo wanafanya kazi kama vibarua, lakini kwa nchini Kenya hali ni tofauti ambako wamiliki hao hao, wamewapatia ajira za kudumu wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ndio inasababisha bei upande wa Kenya ipande kwani wanataka kutoa ajira kwa wananchi wao na kulinda viwanda hivyo visifungwe ilhali huku hawajali kutokana na Serikali kushindwa kuwasimamia kikamilifu wawekezaji wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua, kwa nini Serikali imeendelea kuachia hali hii ambayo kwa kiasi kikubwa imechangia katika mgogoro mkubwa unaoendelea katika biashara ya samaki, bila kuchukua hatua zozote za msingi kuwanusuru wavuvi wa Tanzania na watu wanaofanyishwa kazi za vibarua kwa miaka mingi katika viwanda hivyo, kinyume kabisa na sheria za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viwanda vya Ngozi, kutokana na ongezeko la asilimia 50 kwa wasafirishaji wa ngozi ghafi nje kumekuwepo na mgongano mkubwa wa kimaslahi kuanzia kwa wazalishaji wa ngozi mpaka kwa wasafirishaji wa ngozi ghafi nje. Jambo hili limesababisha mrundikano wa ngozi katika maghala yote kuanzia kwa wazalishaji na kwa wanunuzi wa kati ambao ni mawakala wa viwanda vya kusindika ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna viwanda vinane tu vya kusindika ngozi, lakini vinavyonunua ngozi ni viwanda vitatu tu, ambavyo ni *Moshi Leather, Himo Tanneries* na *Lake Tanneries*, navyo vinanunua ngozi kwa kiwango cha chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na uchache wa viwanda na uwezo mdogo wa viwanda hivi kwa sasa na kwa kulinganisha na wingi wa ngozi unaopatikana nchini, ni dhahiri kuwa tatizo hili linahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka ili kunusuru mapato ya Taifa na ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ifanye yafuatayo:-

(1) Ilieleze Bunge ni hatua gani za haraka inazichukua ili kuhakikisha kuwa ngozi yote iliyo kwenye maghala ya wazalishaji na wanunuzi wa kati inanunuliwa; na

(2) Kwa kuwa viwanda vinavyofanya kazi ni vichache, Serikali ieleze ni hatua gani inachukua ili kuhakikisha kwamba viwanda vyote vya ngozi vilivyopo nchini vinafanya kazi na kuwa na uwezo wa kununua ngozi zote nchini kabla ya kuchukua hatua ya kupandisha ushuru wa asilimia 50 kwa usafirishaji wa ngozi ghafi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo hapa Bungeni namna ambavyo itaondoa tatizo hili, ili sekta hii sasa ichangie kwa ukubwa unaostahili katika pato la Taifa na uchumi wa Watanzania wanaohusika na biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nguo Urafiki, Serikali ya Tanzania inamiliki hisa 49% na Serikali ya watu wa China wanamiliki hisa 51% katika kiwanda

hiki. Kiwanda cha ubia kilianza kazi rasmi tarehe 1/4/1997. Asilimia 49% zinazomilikiwa na Serikali ni nyingi hivyo kukosekana kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara katika masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji ni kosa ambalo limesababisha Serikali kupata hasara kubwa. Katika hatua ya kukiimarisha kiwanda, Serikali ya China ilitoa mkopo wa *USD* 27,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni kwamba fedha hizo zilitumika kununua mitambo mikuu kuu. Aidha, wafanyakazi waliendelea kupunguzwa badala ya kuongezwa kutokana na kufufuliwa kwa mitambo, jambo ambalo kama kweli mitambo ingelikuwa ni mipya ajira zingeongezeka na sio kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inafahamu kuwa baadhi ya mitambo imekuwa ikiuzwa kama vyuma chakavu? Aidha, Waziri alieleze Bunge ukaribu wa Serikali katika uendeshaji wa Kiwanda chetu ukoje kwani Serikali ndiyo iliingia ubia na Serikali ya watu wa China?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, msuguano mwingine unatokana na ukweli kwamba wakati Bodi ya Pamba ilivitaka viwanda vyote vinavyotumia bidhaa ya pamba kama malighafi muhimu katika uzalishaji wa bidhaa zake kuipelekea mahitaji yao ya pamba kutokana na kupanda kwa mahitaji ya pamba kwenye soko la dunia, menejimenti haikupeleka mahitaji ya kiwanda kwenye Bodi . Matokeo yake ni kiwanda hicho kukosa malighafi ya kutosha na hivyo

kupunguza wafanyakazi kwa kisingizio cha kutokuwa na malighafi (pamba) ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na wimbi kubwa la ukosefu wa ajira, hivyo basi, tunaiomba Serikali kupitia kwenye Bodi ya Mamlaka ya Pamba kuweka kipaumbele katika mauzo ya pamba kiwe ni viwanda vya ndani kwanza kabla ya kuuza nje ya nchi. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa mtafaruku wa bei ya pamba ulioko hivi sasa na kuongezeka kwa bei ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inataka kujua kuna mkakati gani wa kufufua kiwanda hiki ambacho kwa sasa hakizalishi na badala yake kinaagiza nguo kutoka nje ya nchi. Hata Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara ilipotembelea ilikumbana na adha ya kuzuiliwa kuingia kuweza kukagua baadhi ya mitambo na mashine za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi kubwa na uuaji wa Viwanda, mfumo wetu wa kodi hapa nchini sio rafiki katika kuweza kukuza viwanda vyetu kwani umekuwa haukuzi badala yake umekuwa ukitishia uhai wa viwanda vyetu na hali hii imekuwa ikijirudia kila mwaka na mfano ni kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kuwa Serikali ilipaswa kuwa mstari wa mbele katika kulinda viwanda vya ndani ili kuweza kukuza ajira na kupunguza tatizo la ajira lililopo nchini na kukuza uzalishaji kwenye malighafi

mbalimbali ambayo viwanda hivyo vitatumia kutoka nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha Serikali imeamua kuongeza kodi kwenye malighafi ya mafuta ambayo yanaagizwa kutoka nje ya nchi kutoka shilingi sifuri hadi kufikia asilimia 10 *(crude palm oil)* wakati nchi nyingine za Afrika ya Mashariki hususani Kenya na Uganda wakiwa hawajaongeza kodi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipoondoa kodi kwenye mafuta ghafi uzalishaji wa zao la alizeti uliongezeka kutoka tani 50,000 hadi kufikia takribani tani 300,000 mwaka huu na hii ni kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Kilimo. Hii ilitokana na ukweli kuwa viwanda viliweza kuwekezwa nchini na hivyo kuwa na uhitaji wa bidhaa hiyo kwa wingi na kuweza kuwafanya wakulima kuwa na soko la uhakika na hivyo kuvutika kulima kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yake, Waziri wa Kilimo alikiri kuwa uzalishaji wa mbegu zote za mafuta hapa nchini ni asilimia 40 tu ya mahitaji yote yanayohitajika na hivyo kuna upungufu wa asilimia 60. Hii maana yake ni kuwa tunapaswa kuagiza mafuta ya kula kutoka nje kwa asilimia 60. Hivyo, kitendo cha kuongeza kodi kwenye mafuta ghafi ni dhahiri kuwa kitasababisha kupanda kwa bei kwa mafuta ya kula na huu ni mzigo kwa mwananchi wa kawaida. Pia ni kufungua soko la nchi jirani ambazo hazitozi kodi kwenye mafuta ghafi kuweza kuuza bidhaa hiyo hapa nchini na itaathiri viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwa kama lengo ni kulinda wakulima wetu, basi tuongeze kodi kwenye mafuta ya alizeti yanayoagizwa kutoka nje ya nchi na kufikia asilimia 25 badala ya asilimia kumi za sasa, ila mafuta ghafi yasiongezewe kodi kwani yatasababisha viwanda vya mafuta kuzorota, ajira kupungua na hata bei ya mafuta kupanda na hivyo kuendelea kumuumiza mwananchi ambaye mpaka sasa ana wakati mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kodi kubwa utaikuta pia kwenye viwanda vya kuzalisha saruji, sigara, pombe, sukari na bidhaa nyingine mbalimbali hapa nchini, hali ambayo haichochei kumwezesha mwananchi kumudu bei ya kununua bidhaa hizo na hivyo kuwafanya wanunue bidhaa kutoka nje ya nchi kwani zinauzwa bei nafuu zaidi ya za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA*, kwa namna ya utendaji wa Shirika la Usajili wa Kampuni na Biashara *(BRELA)* hatuwezi kushindana na nchi nyingine kwa utendaji, hata kama tutalazimika kuweka sheria mpya kila siku. Urasimu uliopo sasa hivi katika *BRELA* unachangia sana kushusha ushindani wa Tanzania na nchi zingine, lakini pia unashusha ufanisi na ari ya wafanyabiashara wetu wanaotaka kurasimisha biashara zao kutokana na muda mrefu na urasimu uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfanyabiashara yeyote anayetaka kusajili jina la kampuni, hatua ya kwanza ni kujua kama tayari lipo ama la. Kwa kupitia

mtandao wa *BRELA* mteja anaweza kutafuta na akajua kama jina analotaka kutumia lipo au halipo. Lakini kumekuwa na tatizo la kutopata taarifa sahihi kupitia huduma hii ya mtandao kwani mteja anapata jibu kwamba jina hilo halipatikani, lakini akienda kwenye Ofisi za *BRELA* anaambiwa jina hilo linapatikana. Wakati mwingine pia hata pale mteja anapobadilisha jina la kampuni, *BRELA* wamekuwa wazito kuweka mabadilisho hayo. Majibu mara nyingi yanayotolewa ni kwamba bado hawajaingiza taarifa zote kwenye mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi pia kuwa si Watanzania wote wanatumia huduma ya mtandao, hivyo kwa wale ambao kwa sababu mbalimbali hawana huduma hiyo, basi wanaweza kwenda kwenye ofisi za *BRELA* na kufanya hicho kitu kinachoitwa *name-search*, inasikitisha kuona kuwa kwa mteja anayetumia njia hii anatakiwa asubiri kwa siku tatu kuweza kupata majibu kuhusiana na jina analolitafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kujiuliza hapa ni je, kama *BRELA* wanatumia mfumo wa kielektoniki katika kufanya hiyo *name-searching* kwa nini ichukue siku tatu kwa mteja kujua kama jina la kampuni au biashara analotaka kutumia linapatikana ama la?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania watakumbuka kuwa mapema mwaka huu Bunge lilipitisha sheria iliyohusu pamoja na mambo mengine kupunguza muda wa kukamilisha usajili wa

kampuni/biashara na sheria hiyo inasema zoezi hilo liwe limekamilika ndani ya siku saba (7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo ni kuwa suala hili nalo bado ni kizungumkuti kwani wateja wanalazimika kuchukua zaidi ya wiki nne kukamilisha usajili wa kampuni au biashara. Ikumbukwe kuwa ili mfumo wowote ukubalike kuwa unafanya kazi sawasawa ni lazima kuwepo na nguvu za ziada. Kwa mfano, kwa maana ya hapa, wale wote ambao hawana uwezo wa kuajiri mwanasheria basi zoezi la kusajili jina la biashara au kampuni limekuwa la kusuasua sana na baadhi ya mambo yanayosababisha hii hali ni pamoja na:-

Lugha; fomu ambazo wateja wanatakiwa kujaza zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza tu. Tunapenda kujua hivi wafanyabishara wote Tanzania wanajua kusoma na kuandika kwa lugha hiyo ya kigeni au *BRELA* inahudumia wasomi peke yake?

Wingi wa fomu na taarifa kwenye fomu; kwa wale wanaotumia mtandao katika kusajili, *BRELA* wameweka fomu si chini ya 53! Mteja anatakiwa achague ni fomu gani inamfaa, lakini mtu huyo hawezi kujua aina ya fomu unayotakiwa kutumia mpaka kwanza analazimika kupitia fomu hizo kwani zimewekwa kwa namba tu! Mara mteja akishapata fomu anayoitaka baada ya kusota bila sababu yoyote, akisumbuka kujua kwa nini ajaze fomu mfano namba 437 na si fomu 305 au namba 10, anakutana na maswali ambayo hayana msingi wowote katika ujazaji wa fomu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo sasa, kama hatutabadilisha utendaji wa *BRELA*, wafanyabishara wengi wataendelea kufanya shughuli zao nje ya mfumo rasmi kwa sababu mchakato wa kurasimisha biashara na kusajili kampuni si rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi jirani zimepiga hatua na zinaendelea kuboresha utaratibu wa usajili. Nchi ya Rwanda, wako mbioni kupunguza muda wa usajili ili uwe saa moja wakati sisi bado tunazungumzia siku kadhaa na katika utekelezaji tunatumia wiki kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

(a) *BRELA* wakae chini na kujitathmini ili kujua aina ya wateja wake na kujipanga vizuri. Sio kila mfanyabiashara ana uwezo wa kuajiri Mwanasheria ili asajili biashara yake.

(b) Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa na ndiyo inayotumiwa na Watanzania wengi. *BRELA* waweke taarifa kwenye mtando na fomu zake kwa kutumia lugha zote mbili; hivyo, kila mtumiaji anaweza kuchagua lugha anayotaka kati ya Kiingereza na Kiswahili.

(c) *BRELA* wanapaswa kuweka mfumo wa ufuatiliaji *(tracking system)* itakayoonesha nani alipokea fomu, aliifanyia kazi kwa muda gani, sehemu

gani ilikuwa sahihi na sehemu gani haikuwa sahihi na wawe na utaratibu wa kutoa risiti kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo na nataka ku-*declare interest* mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Viwanda na Biashara. Kabla ya yote, napaswa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kutupa afya njema na mfungo wetu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niwafariji waliofiliwa wote katika meli ya *MV. Skagit* kule Zanzibar, niwaambie kwamba tuko pamoja, msiba huo ni wetu sote, sote umetukabili na tunawaombea Marehemu wote Mungu awalaze pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nisije nikasahau naunga mkono hoja. Nianze kwa kuja moja kwa moja kwenye suala la ngozi. Sipingani na hoja ya *total ban*, lakini ninachoiomba Serikali kupitia Wizara hii, iwe makini na mpango huu wa *total ban*. Kwa sababu tusiwe tunakwenda tu kwa kufuata mkumbo kwamba Afrika sasa hivi nchi zinazotuzunguka zote zimekwenda huko kwa hivyo na sisi twende. Tujiandae, halafu ndiyo twende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe tuna vigezo vyenye kukidhi kwenda huko na vigezo vyenyewe kwanza

tuhakikishe kwamba je, tuna viwanda vya kutosha hapa nchini kabla hatujaamua. Nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumza kuwa, tuna viwanda sita na ameeleza *capacity* kwamba sasa hivi vinafanya kazi chini ya kiwango. Lakini cha kushangaza viwanda hivi hivi vinauza nje malighafi ambayo wao wanaipigia kelele kwamba haiwatoshi. Sasa hili ni jambo la kwanza la kukaa na kufikiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tusije tukawaangusha wafugaji wetu wanaolima ng'ombe zao huko Vijijini, ngozi zao wakawa hawana pa kuzipeleka na huko ndiko tunakoelekea. Naona tuna nafasi nzuri ya kukaa na kulitafakari hili, halafu tufikie hatua basi ya kusema kwamba sasa tuna nafasi ya kuweka *total ban* kwamba hatuna tena sababu ya kuuza nje ngozi zetu hususani zikiwa ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona jambo la msingi la kufanya sasa hivi ni kuongeza viwanda hususani kwa wale wafugaji wanaokusanya zile ngozi, wanaochinja, wakawa na nafasi na wao ya kuweza kusindika ngozi wao wenyewe. *Otherwise* kwa kutegemea viwanda hivi, vitawaangushia bei na watakuwa hawana pa kuzipeleka hizo ngozi, itabidi wauze tu, wakiambiwa 200/= wauze au 300/= wauze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kushangaza, hivi Tanzania hii tuko milioni 46, kuna *Board* ya kupitisha au kuruhusu hawa watu kupeleka ngozi nje, huyo Mwenyekiti awe mzungu, sisi Watanzania wote tuliokuwemo humu, hakuna mtu

anayeweza kutosheleza, akatosha akawa Mwenyekiti, lazima awe mzungu? Mzungu huyo, yeye mwenyewe binafsi ana viwanda na kazi yake kusafirisha sio kwamba anafanya hiyo kazi vizuri ya kusindika hizo ngozi bali na yeye anauza hizo hizo ngozi ghafi nje. Hivi atawakagua wenzie kwa uhakika, halafu ajikague na yeye mwenyewe kwa uhakika kama anavyowakagua wenzie kabla ya hizo ngozi kuzisafirisha, hapa patakuwa na haki kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la viwanda. Suala la viwanda, mimi nasema kubinafsisha tumethubutu, tumeweza, hatukusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sioni aibu, najisikia *proud* kusema hivyo, kwa sababu kuthubutu ni jambo la ujasiri, kuweza ni jambo linalotaka mtu lazima awe ameamua kufanya jambo ndiyo aweze. Sasa kushindwa ni hatua ya tatu. Tumefanikiwa mbili, tumeshindwa ya tatu, yaani tumeshindwa moja. Tuna nafasi nzuri na hili nimesema kwamba sisemi wala sioni aibu, juzi Korea walithubutu, wakaweza, lakini baada ya dakika moja *rocket* waliyorusha ilianguka. Sijui wale watasema kwamba hawakuweza na Mataifa makubwa yalikuwa yakipiga kelele kwamba wasifanye lile jambo, lakini wamethubutu, wamerusha, *rocket* yao ikaanguka. Hivi sasa hivi nafikiri wanakaa na kutafakari kwa nini baada ya dakika moja ile *rocket* ya masafa marefu imeanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndiyo la kukaa na sisi kutafakari kwa nini tumethubutu, tumetoa nanihi kwa wawekezaji, tumeweza, lakini hatukusonga mbele.

Lakini huku tukikaa na kutafakari suala hili, naona tuna nafasi nzuri vile vile ya kurejea viwanda vyetu vidogo vidogo. Huu ndiyo ukombozi kwamba Taifa hili, litaondokana na hapa tulipo na kwenda huko mbele, kwa sababu nilichokigundua, kwenye wawekezaji wakubwa, tatizo linalotusumbua ni kwamba wanamiliki kila kitu, halafu kazi yao kukaa na kuwafisidi wafugaji wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa na utaratibu wa viwanda vidogo vidogo, hili jambo naona litaepukika na ajira nyingi kwa vijana zitapatikana na kuondosha huu ukiritimba unaofanywa sasa hivi. Kwa sababu kwenye suala kama la sukari, amezungumzia hapa miwa inauzwa mpaka tani moja sh. 54,000/= mpaka kwenye 60 na inashuka mpaka kwenye shilingi 35,000 yaani inategemea na Mikoa. Sasa tujiulize tunawauzia nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hawa tunaowauzia, ndiyo wanaokaa wakapanga hizi bei, sisi hatupangi hizi bei hata kama tunaingia humo, wanatupangia. Tukiwa na viwanda vyetu vidogo vidogo na mifano tunayo, nendeni China, kila siku si Mawaziri mko China, nendeni India, kila siku Mawaziri mko India. Waangalieni watu walivyokuwa wako *busy* na masuala ya kulima pamoja na viwanda vidogo vidogo. Mtu ana kiwanda kwenye upenyo wake wa nyumba ana kiwanda anatengeneza sukari. Hivi sisi tunashindwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano umeshaonekana kwamba kufuatana na maelezo tayari tumeshakuwa

na viwanda vidogo vidogo vitano, tumeshatengeneza. Hivi tena tunashindwa nini? Naona sasa hivi Mheshimiwa Rais wetu, yale mabilioni yake, baada ya kutoa kwa lengo thabiti la vijana, lakini fedha zile zikachukuliwa na watu wanaojulikana, wenyewe wanawaelewa. Sasa naona fedha zile zielekezwe kwenye *small scale industry* kwa ajili ya kuleta faida kwa vijana na kutoa ajira kubwa kwa vijana na kuepukana na kunyanyaswa kwa kazi kubwa wanayoifanya wakulima hususani wa miwa, halafu wakaenda wakapangiwa bei, sasa bei watakuwa wamejipangia wenyewe na sukari katika nchi yetu inaweza ikashuka bei, vinginevyo, hatutafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la umeme, huwezi kuzungumzia viwanda kama hujazungumzia umeme. *NDC* wana uwezo mkubwa sana wa kuleta umeme, lakini bado nina wasiwasi kwa sababu hata *TANESCO* wana uwezo mkubwa sana wa kuleta umeme, lakini naona kuna *sabotage* ya makusudi inayofanywa kwa maslahi ya watu maalum, wanajielewa. Kwa hiyo, hata tukienda huko kwenye, wapi tunapokuzungumzia sijui hiyo migodi ya mkaa wa mawe na nini, hali itarudi kuwa ni hii hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi labda sasa hivi nitoe rai au nihamasishe wananchi huko nje, kwa kuwa sasa hivi tuko kwenye mchakato wa Katiba, basi tupitishe na Sheria ya kuua hawa watu wote wanaohujumu uchumi. Tena wauliwe kwa risasi na risasi hiyo wailipie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Wizara hii muhimu katika uchumi wa nchi yetu. Nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na bajeti nzuri waliyotuletea hapa katika Bunge la Bajeti la mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia maeneo machache kwa haraka sana. Naomba bado kunukuu na kusema kwamba, viwanda ni sekta mojawapo inayochangia pato la Taifa na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla. Nchi zote ulimwenguni zilizoendelea zimesaidiwa kwa kiwango na viwanda. Napenda kutamka kwamba hatuna njia nyingine yoyote kama nchi za wenzetu zilivyoendelea bila viwanda. Hata tukipata mafuta, dhahabu, tutumie utalii, gesi, bila viwanda, bado uchumi utakuwa kwa taratibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tunaweza kuwa na mafuta na madini kama tuliyonayo sasa hivi na tukapata fedha nyingi. Lakini kama hatuna viwanda ambavyo vitazalisha vitu, hizo pesa tutakazopata tutatumia kununua bidhaa kutoka nje na hatutakuwa na bidhaa zetu wenyewe ambazo tunaweza tukanunua. Bidhaa muhimu kabisa kwa binadamu, vyakula, sabuni, maziwa, siagi, juisi, nguo, viatu, *furniture* hata vifaa vya ujenzi bado itabidi kununua nje kwa bei watakayoiweka wao ambayo

itafanya uchumi wetu uwe uchumi tegemezi badala ya kuwa uchumi wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo bado nasisitiza viwanda ni muhimu sana. Tutazame mfano wa Nigeria ambao walipata mafuta na hatimaye wakapata matatizo ya uchumi kwa sababu waliachilia vitu vyao, hawakuweka mkazo kwa vitu vingine. Tusifike huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetengeneza Sera ya Viwanda Vidogo, safi na nzuri sana, hata huu mkakati wa 2025, Sera ya *EPZ* ni nzuri. Inapita miaka kumi sasa kwa sababu wakati inatengenezwa na mimi nilikuwepo. Naomba niseme, Sera nzuri lakini utekelezaji umekuwa mgumu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niipongeze Serikali, mafanikio yapo, Sera ya Ubinafsishaji pamoja na kuweka mazingira mazuri, imewezesha wawekezaji wamekuja na tumeona viwanda vizuri vikubwa kama *Breweries, TCC, SUBMILLERS, LOVO, Cement Factories, Uniliver, Shellchemicals* na vingine, lakini bado safari ni ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri wangu sasa kama ifuatavyo:-

Serikali itangaze *industrialisation strategic*, mkakati wa *industrialisation*, kuifanya nchi yetu iwe nchi ya viwanda. Hiyo lazima tutangaze, tena tutangaze sio kisiasa, tutangaze kiutekelezaji na mkakati uwepo, tu-*sacrifice*, tujitolee Serikali na wananchi kwa ujumla ili nchi yetu iweze kusonga mbele. Kwenye hotuba ya

Mheshimiwa Waziri nimefurahi sana ametaja hiyo na nilishaanza kuandika kabla sijaisikia, lakini naomba niongezee ameongelea amesema viwanda mama na mimi naviita hivyo hivyo *Basic Morden Industries.* Kuna vya chuma, *textiles*, kuna *glass, cement, wood, plastics leather*, karatasi na *machineries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbushane viwanda vya nyuma hapo vilivyokuwa chini ya *NCI, TLI* (*Tanzania Leather Industries), TEXCO, NDC* na kadhalika. Hivyo, ndivyo inapashwa turudi kule kwenye viwanda vya miaka ya 70. Kwa sasa havitakuwa na faida ya haraka haraka kwa sababu huwezi ku-*invest* hapo bilioni labda 800 kiwanda kimoja na upate hapo hapo, lakini kwa manufaa ya nchi kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivyo vikubwa vitasaidia sana uanzishwaji wa viwanda vidogo, tutapata *machinery* ya kuanzisha viwanda vingine vidogo, tutapata malighafi na itasaidia sana katika ukuaji wa hivyo viwanda ambavyo tunavitaka viwe kwa wingi. *Intermediate and production of local goods* pamoja na *tools* za *machinery used to make other goods,* kutengeneza hivyo viwanda vingine. Hivyo, ndivyo wenzetu wa China na India walivyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, hapa naona imetengwa bilioni 131 kwa maendeleo na sio kwa viwanda hivyo ninavyosema viwanda mama ni maendeleo yote kwa ujumla ya viwanda. Naomba kusema ni kidogo sana, tuisaidie Wizara huo mkakati wa Serikali yote pamoja na wananchi, tuweze kusaidia huu mpango wa *industrialisation* wa nchi yetu. Serikali

yote kwa ujumla wake, tukubaliane na tuweze kuwasaidia. Hivyo ndivyo tu tutakavyoweza kuvianza hivi, vizae vingine vidogo na nchi yetu iweze kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona sitoeleweka ninaposema bilioni 131 ni kidogo, hazipatikani, kwa sababu bajeti yenyewe tunaijua na tumeshajua ni trilioni ngapi. Lakini Serikali tukope, tuna uwezo huo, tunakopesheka. Hapo ndipo ninaporudia kusema kwamba ile dhana niliyosema wakati ule kwamba tumuachie Waziri na akili zake, tumpe *free hand* atazame, aone atatufikisha wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akishapewa hiyo sekta na Rais aachiwe sasa tumwambie lete *Basic Morden Industries* ili tuweze kuendeleza viwanda katika nchi yetu. Mabenki duniani yana pesa sana. Naomba kudiriki na kwa kujiamini kabisa kusema kwamba Serikali imetumia pesa nyingi sana kunisomesha na kunipeleka nchi nyingi sana duniani nikiwa kama mfanyakazi wa Serikali. Nimeona nchi zote, nimejifunza na haya yanawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea kuchangia vile vile katika sekta hiyo hiyo ya viwanda kuhusu kuanzisha viwanda. Viwanda vinaweza vikaanzishwa nchi nzima na hivi viwanda vidogo vidogo. Wafanyakazi wa Wizara watoke nje ya Wizara, waende huko Mikoani wa- *identify* au wabaini Mkoa upi una malighafi ipi kwa kiwanda kipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pale pale muwasaidie. Kwa mfano, unaweza kusema Kusini tuwasaidie korosho, Mikoa yenye ng'ombe nyingi tuwasaidie Viwanda vya Ngozi, yenye pamba viwanda vya nguo, halafu Serikali tuweke miundombinu pale na pia tuwasaidie fedha viwanda vianze. Hii ni kama Sera naweza nikasema nairudia kila siku lakini bado nitasisitiza kwamba bila mkono wa Serikali, hatuwezi kufika popote. (*Makofi*)

Mheshimia Mwenyekiti, tunaona kabisa kwamba viwanda vingi au mali nyingi ukiingia *supermarket*, ukitazama kila kitu unakuta ni *imported*. Unaweza kwa mfano, ukatazama *Blue Band*, hebu tujiulize kuna *Margarine* yeyote ambayo inatoka hapa nchini kwetu, si tunatumia za nje, *Blue Band* za Kenya*, Flora* za nje. Ebu tufikirie hivi vitu vidogo vidogo, hivi ndiyo tunaita viwanda vya kati ambavyo tunaweza tukavianzisha hapa nchini kwetu. Ningeomba sana hilo lisaidiwe na ili tuweze kuwa na viwanda vikubwa pamoja na hivyo vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea kuhusu kulinda viwanda vyetu. Serikali, tufanye mkakati wa kulinda viwanda vyetu. Hatutaweza kabisa kushindana na ushindani wa nje kwa sababu, *cost of production,* ama niseme ile gharama za uzalishaji hapa kwetu ni kubwa sana. Kwa hiyo, tujaribu kuongeza kodi, lakini kwa bidhaa zile ambazo zinazalishwa hapa nchini na ndio hapo hapo narudia kusema kuna umuhimu bado wa kuzalisha kila bidhaa na Serikali, tuingie katika huu mpango wetu wa *industrialization.* Hii inawezekana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutamka tofauti kwamba, tupige marufuku ngozi isiende nje. Tukishapiga marufuku, hakika hivi viwanda vilivyopo, vitaongezewa *production* na tutazalisha. Sijui kwa nini, mpaka sasa hivi bado Serikali, inakuwa na kigugumizi katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuongelea kuhusu Sera za *WTO, Regional Intergration* kama *SADC, EAC* na *COMESA.* Jamani, zipo na sisi ni wanachama, lakini, mmh, tunafanya biashara na wenzetu ambao ni miamba, wenye *big economic base,* wana viwanda vingi na vikubwa. Sisi tuko pale kama mtoto mdogo, halafu bado tunasema sawa, tuingize kila kitu *free* na nini; siwezi kusema kwamba, tukatae, lakini ningeomba tutumie busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Vile vile kabla sijachangia hii, naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe pole kwa ndugu zetu waliopoteza maisha katika Boti iliyopata ajali kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri. Naanza na *EPZ.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZ* ni eneo ambalo nchi nyingi sana duniani zimepata faida kwa kupitia Mfumo wa *EPZ.* Ilianzia Shanon, kule Ireland, mwaka 1959, leo nchi zaidi ya 120 ziko kwenye mfumo huu. Tanzania, tuko na mafanikio makubwa sana yameanza kuonekana, zaidi ya ajira 13,500. *Investment* ya dola milioni karibu 700 imefanyika na bado kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka huu katika *EPZ* ni nzuri, lakini natarajia sana hata katika Mpango wa Maendeleo wa 2025, hakuna eneo ambalo linaonekana litasaidia nchi hii ya Tanzania na nchi zote duniani, kama sekta ya viwanda. Maana ukiwa na kiwanda, ndio ina-*transform,* kununua rasilimali za wananchi wanaolima kule, wanapata soko lao, linaingia viwandani, halafu wanakuwa na uwezo wa kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Shinyanga, kuna mifugo zaidi ya 4,000,000. Nimemshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amesema hapo kwamba, kitakuja Kiwanda cha Ngozi, Shinyanga,. Ni habari njema sana kwa watu wa Mkoa wa Shinyanga. Juzi tu nilikuwa na maongezi na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Mheshimiwa Waziri, kuna Viwanda vya Nguo vinakuja katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio mambo ambayo tunayahitaji sasa, kwa sababu, ukiwa na viwanda katika Mikoa ambayo ina *advantage* kama Shinyanga; leo, 60% ya pamba, inatoka Shinyanga na ng’ombe 4,000,000 wanatoka Shinyanga. Kwa kweli,

ilikuwa ni aibu sana kusema kwamba, Shinyanga, ilikuwa haina viwanda. Sasa tukishakuwa na viwanda hapa, tayari mambo yanakuwa mazuri sana kwa nchi yetu, kwa maana ya kupata *foreign currencies,* ajira na masoko ya uhakika katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ngozi tusikurupuke kufanya *total ban,* tusikurupuke kabisa. Juzi tulikuwa tunawasikia wadau pale, wafanyabiashara wadogowadogo hawa wanaonunua kule kwa wafugaji kuwaletea viwandani, wanasema wana *stock* kubwa kwelikweli na viwanda hawataki kununua ile *stock* yao na wa viwanda nao wana malalamiko yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili, tuna viwanda nane, katika viwanda nane vya ngozi ni vitatu tu vinafanya kazi na katika vitatu, viwili vinafanya kwa kusuasua. Sasa wewe unafanya *total ban*. Kabla ya kufanya *total ban* katika Mkoa wa Shinyanga, ngozi zilikuwa zinaoza huko, sasa leo unafanya *total ban,* ndio kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala hata Mheshimiwa Rais Mkapa, Rais Mstaafu, alisema huna haki ya kuongea kama hujafanyia utafiti. Naamini kabisa katika Kamati yetu ingefanya kazi ya kuunda Tume ambayo itakwenda kulifanyia kazi hili na kuja na mapendekezo mazuri, yatakayotupa fursa nzuri ya kufanya maamuzi mazuri katika eneo hili. Ni pamoja na kuwasaidia wafanyabiashara wadogowadogo wa ngozi, ili na wenyewe wawe na kiwanda kitakachoweza kuwasaidia mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *EPZ,* viwanda na *SIDO,* ndio maeneo ambayo hata *Far East,* Nchi za China na Nchi za Thailand na wapi, wamepata mafanikio makubwa sana kupitia hili eneo. *SIDO,* hata kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alisema wametengewa bilioni 4.5, lakini kwenye vitabu sijaziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala hili, wasije wakairuka *SIDO,* wakakosa fedha hizi. Wakikosa fedha hizi, maana yake umenyima fursa ya *SIDO* kwenda kufundisha vijana wetu kuwa na *skills* za kutengeneza viatu, mkanda, na kadhalika na ndio ajira yenyewe huku, fedha zisipopatikana, kwa kweli hatutaelewana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madudu yako kwenye Kiwanda cha Urafiki. Viwanda hivi ni vikubwa, vina historia kubwa sana katika nchi yetu na ni moja katika eneo ambalo limesababisha hata wakulima wetu wa pamba kutopata bei nzuri. Leo ingekuwa Urafiki inafanya kazi vizuri, *MWATEX* na viwanda vingine vikubwa ambavyo Baba yetu wa Taifa aliviacha, Hayati Mwalimu Nyerere, tusingekuwa na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipata mkopo wa dola bilioni 27, kutoka Benki ya *Exim,* zimepotea, hatujui zimekwenda wapi? Kuna eneo, wameuza mashine za Urafiki, hatujui wameuza wapi? Kuna *sabotage* kubwa sana katika kiwanda hiki. 49% Serikali, 51% Wachina, kwa maana ya historia ilivyokuwa pale; mimi pia

napendekeza na nashauri kwamba, mapendekezo ya Kamati, kwenda kuchunguza eneo hili, Serikali, ikubali na Mheshimiwa Spika, akubali hili, ili tuje na maeneo makubwa sana. Tungekuwa na kiwanda hiki, leo bei ya pamba tusingekuwa tunalalamika, sisi wadau wa pamba, katika Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya Afrika Mashariki; wafanyabiashara wengi sasa hivi, wameacha kupeleka bidhaa Afrika Mashariki; hii *East Africa,* Muungano ni uwongo mtupu. Wafanyabiashara, wamepeleka bidhaa kule Kenya, wakifika pale *border,* wanasumbuliwa na watu wa Kenya. Bidhaa za Kenya, zikija Tanzania, tunawapokea kama maua. Hii ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Waziri, mwenye dhamana hii, afanyie kazi hii. Viwanda vingi sana vimeacha na vimesema usumbufu mkubwa, wamekuja kwenye Wizara husika, kuleta malalamiko, hakuna msaada wa aina yoyote unaofanyika, wameacha. Viwanda vya ngano wamekwenda kule, wamestopishwa *(Stop)* pale, wamesumbuliwa, kuna malori yamekaa pale zaidi ya miezi minne, pale *border* mpaka wameacha, makampuni ya *Bakhresa, Azania* na wengine wengi tu. Wamesema tume-*stop* kabisa na tume-*give up* kufanya biashara na *East Africa.* Sasa hebu niambie, hii *East Africa* hii, faida yake nini kwa Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee *TBS* kuhusu ukaguzi wa magari nje ya nchi, na ndio lilimuondoa Mheshimiwa Waziri, Chami. Ni *scandal* kubwa tu. Suala

la ukaguzi wa magari, si kweli kwamba, unapoikagua gari nje ya nchi, eti unaitengeneza au unaifanya kuwa na hadhi nzuri ya kuingia nchini, uwongo. Tufanye kama Kenya tu, unaweka umri wa gari, miaka nane *standard,* nje na miaka nane gari usiingize Tanzania, kwisha, unaondoa kabisa hizi *loophole* za rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa hivi, kama mnataka tu kutengeneza Tanzania, magari yakaguliwe Tanzania, kwa maana ya kutengeneza ajira ni sahihi, wala sipingani na hilo. Tufanye tu utafiti mzuri, tuone kama lina maslahi na nchi yetu, yakaguliwe ndani ya Tanzania, hapo sina matatizo nalo. Lakini kukagua nje ya nchi, ni njama tu za kutengeneza fedha, watu wanakula fedha nje, zinakuja kwa mlolongo ambao unaleta mambo ambayo yanaiingiza Serikali yetu katika aibu kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pamoja na *PVOC,* ukaguzi wa bidhaa kutoka nje. Naungana kabisa na rai ya Kamati ya Viwanda na Biashara kwamba, kuna umuhimu wa kuitazama Sheria hii. Sasa hivi ukaguzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi kuja Tanzania, umeingia kwenye sura mpya kabisa, vurugu tupu. Yaani ukiwa *on the ground* kutazama hali hii, unaona kabisa kwamba, sasa kama ni bidhaa *fake* za bandia, ndio zitaingia sana kuliko ilivyokuwa kwanza. Mazingira ya kufanya bidhaa zisiingie *fake* hapa ni mazingira mazuri tu, ushindani wa biashara ndani ya soko. Kwa sababu, huwezi kuleta bidhaa *fake* au bandia, kama unajua kabisa mwenzako kaleta bidhaa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari. Simenti tuliachia na mpaka sasa hivi bado kuna *demand.* Sukari achieni tu, achieni kwa muda wa miezi sita, mwaka mmoja, tuone *impact* yake itakuwaje. Ukiachia hivi kwa miezi sita, mwaka mmoja, bei itashuka; lakini kwa vibali vibali, mara rushwa, mara sijui nini, tuachie kama tulivyoachia simenti. Simenti sasa hivi hakuna kibali, watu wanaleta tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sehemu ambayo inaudhi kama Bandari, inaongeza *cost* ya *production* ama kuuza bidhaa au kuzalisha. Nitoe mfano mmoja tu, hivi viwanda vya ngano, ukiwa na *storage* pale, kwa siku moja wanalipa dola 100,000. Sasa ile 100,000 sidhani yeye anailipa kwa huruma, anakuja kuongeza kwenye *cost of production,* ambayo anakuja kuilipa mlaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari tatizo lake ni urasimu tu. Mfanyabiashara, hana tatizo na kulipa ushuru. Unamchelewesha siku 20, halafu mwisho unamwambia 15,000,000/=. Sasa 15,000,000/= anakwambia angeniambia siku ya pili tu, ningelipa hata 17,000,000/=. Unampeleka mlolongo mlolongo, mpaka mwisho kule, unamwambia leta 20,000,000/=; anakwambia ungeniambia siku ya tatu, ningelipa nikatoa mzigo wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya, wanatupiku, bandari moja tu ya Mombasa pale; sisi tunayo ya Mtwara, tunayo sijui Bagamoyo tunajenga mpya, tunayo Tanga, tunayo Dar-es-Salaam hapa, bandari moja tu ya Mombasa, imeshatuzidi na sasa hivi

wanajenga Lamu, kwa maana ya kuchukua soko la Sudan ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, suala la Bandari, sio suala la mzaha mzaha kwa kuwa lina *impact* kubwa sana kwenye biashara, kwa maana ya biashara yenyewe na viwanda. Lifanyiwe kazi na nashauri kabisa, ikiwezekana hata lingekuwa na Wizara yake kabisa, Wizara ya Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, iichukue Bandari hii, leo wewe katika *common sense* tu ukicheleweshe *container* siku 15, unapata 15,000,000/=. Lakini katika siku 15 hizo hizo, ukatoa *container* nne, unapata 60,000,000/=, nani aliyechelewa ku-*collect revenue?* Serikali, mnajichelewesha wenyewe tu kupata fedha; Serikali, mnajichelewesha wenyewe tu kutoa mali ama *product* au *raw material* katika viwanda, mnasababisha bei kupanda, mnasababisha vitu kupanda katika soko, mnasababisha kuchelewa wenyewe. Leo, katika Bandari kwa mfano, Bandari peke yake…

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, ili nami nichangie kwenye hoja hii, inayoihusu Wizara ya Biashara na Viwanda. Hii Wizara, ni muhimu sana

katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu maana inajipambanua, kuna viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana kama hii Wizara, Serikali, ikiiangalia kwa makini na kuipa kipaumbele, hii Wizara inaweza ikatunufaisha Watanzania na kutoa ajira kwa Watanzania. Yaani kuleta ajira nyingi kwa Watanzania na kuzalisha bidhaa ambazo, kama walivyosema wachangiaji wengine kwamba, tukiona bidhaa za nje tunapapatika, za kwetu hapa ndani tunazidharau. Ni kwa sababu, gani zinadharaulika? Ni kwa sababu, hii Wizara, haijafanya kazi yake vizuri kuboresha viwanda, kuboresha bidhaa zilizoko viwandani na kuboresha biashara, ambapo sisi Watanzania wenyewe, tungekuwa tunajivunia nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana, mimi natokea Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro, enzi ya Mwalimu, ulikuwa na viwanda vingi na ikasifika, ndio maana Mkoa wa Morogoro, kuna *guest house* nyingi kwa sababu, wageni wengi, wanafika Mkoa wa Morogoro, kibiashara na yaani *weekend* watu wanakwenda kupumzika kwa sababu, ni eneo ambalo lina mzunguko wa pesa. Lakini kadiri na tumethubutu sisi Mkoa wa Morogoro kuchimba mpaka Bahari, ni Mji kasoro Bahari, lakini kuna Bahari pale pembeni; wanaotaka kuogelea watakwenda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mkoa huu kadiri tunavyozidi kwenda, unazidi kurudi nyuma. Mkoa wa Morogoro ulikuwa na viwanda, lakini hivyo viwanda leo ukiuliza viko vingapi? Lakini hata vinavyofanya kazi, nenda kaangalie kwenye hivyo viwanda, watu

wanateseka, hakuna mishahara inayokidhi, watu wamekuwa vibarua ndani ya nchi yao, kwa hiyo, Morogoro badala ya kusonga mbele, tunarudi nyuma. Sasa kama hii Wizara ya Viwanda na Biashara, inafanya kazi gani kuboresha hiyo hali ili nchi yetu au na Mikoa yetu ipate maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku nauliza hapa swali na nashindwa kupata majibu sahihi. Kilichokuwa Kiwanda cha *Polytex* pale Morogoro, pamoja na kuwa kiwanda kimebinafsishwa, lakini wafanyakazi wametupwa pembeni, wanahangaika, hawana mbele wala nyuma. Hivyo viwanda pamoja na ubinafsishaji wake, sasa hivi tunazungumzia kuweka viwanda vipya, hivyo vya zamani mmevifanyia kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda anamiliki ndugu yangu hapa, ndugu yangu hapa jirani yangu, sitaki kumtaja maana wanasema hamna kutaja; kiwanda kilichokuwa kinaitwa cha *Moproco,* leo twende mkaangalie, Wizara, mkakiangalie *Moproco* kinafanya kazi? Kama hakifanyi kazi ni kwa nini? Wakati alizeti inalimwa, eeh, kile kiwanda si kingekuwa kinazalisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilivyomdodosa kwa karibu, akasema bwana ni tatizo kwa sababu, wale wanaoagiza mafuta kutoka nje, wanasema mafuta hayajapembuliwa. Lakini wanaagiza mafuta ambayo yameshakuwa yamepembuliwa, yanakuja hapa mafuta yakiwa mazuri, kwa hiyo, yeye akinunua alizeti, akienda kuzalisha kiwandani, anashindwa kushindanisha bei na wale wanaoagiza kutoka nje,

ambao hawalipi ushuru Serikalini. Kwa hiyo, sasa tunaoua viwanda vyetu ni sisi wenyewe Watanzania, tuliopewa dhamana na wananchi. Matokeo yake badala ya kuangalia ni namna gani tutapata maendeleo, watu wanarudisha nyuma maendeleo kwa sababu wanazojua wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nipate majibu. Ni kwa nini kiwanda cha *Moproco,* hakifanyi kazi wakati Watanzania, wameendelea kuzalisha alizeti ufuta na karanga katika mashamba yao? Nipate majibu kutoka kwa Serikali. Ni kwa nini, kiwanda cha mazulia Kilosa, kimekufa? Mabati, mashine, yanang'olewa, Mkoa wa Morogoro. Nataka nipate majibu kutoka kwa Serikali, kile kiwanda, hatima yake ni nini? Kiko pale Kilosa, Magomeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate majibu ya Serikali, ni kwa nini kiwanda cha *Spare Parts,* Mang'ula, mpaka leo, kilichokuwa kinatengeneza *spare parts* za kila aina, kipo pale na mashine zimeng'olewa? Nataka nipate majibu ya Serikali. Ni kwa nini, mnatudidimiza Watanzania, katika mali hii? Tunakosa pesa, tunakosa ajira, tunakuwa maskini, tunaomba majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka huko nakwenda kwenye biashara, nakwenda Kilombero kwenye lile shamba kubwa la *KPL,* wanasema la kuzalisha mpunga; hivi lile ni biashara au kilimo? Yule amezalisha mpunga kuanzia mwaka 2008 mpaka leo. Anazalisha magunia kwa magunia pale ya mpunga, anafanya biashara. Watanzania, wanafaidika vipi na ile *KPL?* Biashara pale ikoje? Viwanda vya kusindika ule

mpunga, mchele unaotoka pale, viko wapi katika Wilaya ya Kilombero? Matokeo yake, malori yanakusanya mpunga, yanapeleka yanakopeleka huu mchele, barabara zinabomoka, barabara zenyewe hazijengwi, Watanzania tumebaki tunaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate majibu kutoka kwa Serikali. Ile *KPL* pale Kilombero, ni biashara au ipo ipo tu, bado inafanya majaribio mpaka baada ya miaka 10 ndio waseme sasa tumeingiza faida au tumekosa faida. Anamwita mjomba wake, anaingia tena halipi kodi; wakati ukilima mwaka mmoja mpunga, umelima vizuri, unafanya biashara ya uhakika na umerudisha gharama zako zote. Mpaka leo, ameshalipa kodi shilingi ngapi Serikalini? Ni lazima tupate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Sukari, Kilombero. Mpaka leo, mnasema hapa kuna *TIB,* watawezesha wakulima wadogowadogo, kila siku hapa naihoji Serikali, wale wakulima wadogo wanaozunguka wenye mashamba ya miwa, wanadhulumiwa kila kukicha na yule Mwekezaji wa Kiwanda cha Kilombero Sukari; wakipeleka miwa pale hakuna mtu wa kuwasimamia kwamba, sukari katika miwa kiasi gani? Kwa hiyo, yeye ndio mnunuzi, yeye ndio mpimaji, yeye ndio anayetoa bei, kwa hiyo, Mtanzania wa kawaida anateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka majibu ya Serikali, hii *TIB* mmewawezesha vipi wakulima wadogowadogo wa miwa, Wilaya ya Kilombero, ili waweke viwanda vidogovidogo vya kutengeneza

sukari? Lakini mbaya zaidi katika suala la biashara, sukari inatengenezwa Kilombero, mmeanzisha makampuni ya kwenda kubeba sukari Kilombero, yanapeleka Dar-es-Salaam, mfanyabiashara wa Kilombero, anatakiwa aende Dar-es-Salaam, akachukue sukari airudishe Kilombero. Matokeo yake, mlaji wa Dar-es-Salaam anapata sukari kwa bei ya chini, kuliko aliye Kilombero; kuna faida gani ya kuwa na kiwanda Kilombero? Hamisheni hicho kiwanda, hamisheni, hakuna faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mimi niko jikoni napika ugali, halafu mimi nisile, wanakwenda kula watu wengine, ni biashara gani mnafanya hizo? Kwa nini hamboreshi? Nataka majibu ya Serikali, kwa nini mnatufanyia hivi? Tumewakosea nini kama Watanzania? Lakini wafanyakazi, ona wanavyopunjwa, wale wakata miwa pale wa nje, ambao wanakodishwa na wale watu wa tenda, wanalipwa 7,000/=. Yule Mwekezaji, anawalipa wale wakata miwa 3,000/=, huoni kama hii biashara kichaa? Kwa nini huyu anawadhulumu Watanzania? Nendeni mkaangalie na nataka majibu ya Serikali, ni kwa nini mnatufanyia biashara ya namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amewawezesha wakulima wangapi pale waweke viwanda vidogo vidogo, maana msituwekee takwimu tu kwenye vitabu kila mwaka hivyo hivyo, lakini utelekezaji hakuna. Tunataka utekelezaji, mje hapa na takwimu mmewawezesha Watanzania wangapi, mmeweka viwanda vingapi, wamekopeshwa wangapi kama mmeshindwa kulipa mje hapa mtuambie lakini

siyo kila siku hadithi hadithi, kitabu mnamaliza makaratasi hamna kitu, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia uchungu watu wanateseka ndani ya nchi yao, hiyo nimeizungumzia tu Morogoro na Kilombero ambako mimi nakujua vizuri, lakini karibu viwanda vyote Tanzania ni mateso makubwa. Naomba viwanda vyote vya Katani, vya Mazulia Kilosa vifufuliwe, nataka mpango wa Serikali ni namna gani watavifufua. Leo mnasema *General Tyre* mnafufua Arusha, lile shamba la mpira pale Mang'ula mnalifanyaje, mnalifufua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jamaa pale anafanya ujanja ujanja tu, anakaa anachukua ule sijui anapeleka Kenya, wafanyakazi wa pale waliokuwepo hawajui hatima yao imekuwa kama shamba lake binafsi, hii nchi mnaipeleka wapi? Kwa nini Nyerere aliitengeneza hii nchi, ninyi kazi yenu ndiyo kama hivi mnasema mmeweza, mmethubutu, hamsongi mbele, mnarudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnasema tena mnataka kuweka viwanda vingine vile vya zamani mmevifanyia kazi gani, boresheni kwanza vile vilivyoko, halafu anzishe hivyo viwanda vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usindikaji, sisi Wilaya ya Kilombero tunalima mpunga, mmetuwekea mbunga, leo tunabeba kwenye magunia malumbesa, lakini tungependa mpunga wetu, mchele wetu tuukoboe vizuri, tuweke kwenye package na unasema kabisa Kilombero *Rice Mill Grade One, Grade Two,*

mmewawezesha vipi wafanyabiashara kule wadogo wadogo ili wafanye hiyo yenye uhakika angalau hata mkifanya maonesho yenu ya Nana Nane huku Dodoma waje na bidhaa zao muone mchele unavyonukia. Kwa hiyo, lazima Wizara biashara iboreshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niende sehemu nyingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Sasa naomba nimwite mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na nafikiri huyu atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mchana wa leo, kwanza kabisa na nitoe pole kwa wafiwa wote katika ajali ya meli. Lakini vilevile nitoe pole kwa wananchi wa Geita kwa ajali mbaya sana iliyotokea tarehe 15 Julai, watu kumi na mbili wakapoteza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali hii ilipelekea usafiri wa vigari vidogo vidogo aina ya mchomoko kuzuiwa kufanya kazi. Kimekuwa ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa Geita, lakini nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri Mkuu kwa kuruhusu michomoko kufanya kazi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia kwa karibu sana kilio cha wananchi hawa kutokana na kuzuiliwa michomoko au magari madogo madogo yanayotoka Geita Katoro, yanatoka Geita kwenda Rwamgasa, Nyarugusu, kwenda Butundwe kote huko kwa sasa yanafanya kazi. Naishukuru sana Serikali kusikiliza kilio cha wananchi, lakini pia kusikiliza kilio changu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa katika mchango wangu, kwanza kabisa niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hotuba nzuri sana ambayo amewasilisha hapa Bungeni. Katika hotuba hii nimefurahia sana kutokana na kwamba Serikali ina mpango wa kuanzisha masoko ya kuwezesha wananchi kufanya biashara kubwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na kufanya watu wa nchi za nje kununua bidhaa zetu hapa Tanzania. Katika Kanda ya Ziwa nimeona kwamba watajenga soko Isaka katika bandari kavu. Nichukue nafasi hii kwa kweli kupongeza sana uamuzi huo na niiombe Serikali sasa suala hili la kujenga soko pale Isaka ihakikishe kwamba linatekelezwa kama lilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niombe pia kwa Jimbo langu pale Katoro ambapo kwa kweli kwa wale ambao wamefika Katoro wanaona jinsi ambavyo panavutia sana kibiashara, niombe wajenge soko la Kimataifa na nafaka kama lililopo Kibaigwa pale, soko hili litawezesha wananchi wa Geita kwa ujumla lakini pia na mikoa jirani kama ya Mwanza, Kagera, pamoja

na Mara na Shinyanga kuweza kuleta bidhaa zao pale kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wananchi wa Geita watanufaika kwa wingi zaidi kwa sababu wananchi wengi watapata nafasi ya kufanya biashara vizuri kabisa, kwa sababu mahali pale pamechangamka vizuri halafu vile vile ni mpakani nchi ya Rwanda iko karibu, nchi ya Burundi iko karibu kabisa, ni jirani mahali pale. Kwa hiyo, niombe kwa kweli kwa Katoro tuweze kuanzisha soko la Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika masuala ya viwanda, katika Wilaya ya Geita na Jimbo la Busanda kwa ujumla, tunashukuru kwamba sasa hivi wanaleta umeme wa *grid* ya Taifa, umeme huu ambao sasa wanaweka nguzo sehemu mbalimbali katika Jimbo langu, hasa pale Bukoli na Nyarugusu na Rwamgasa wameshaweka nguzo, tunasubiri umeme kuwaka tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sasa Serikali pamoja na wawekezaji mbalimbali wajitokeze kuja kuwekeza Geita. Geita sasa ni mkoa na tunahitaji viwanda vya kutosha katika Mkoa mpya wa Geita ili kuweza kutengeneza ajira kwa watu wetu ambao wanahitaji ajira. Sasa hivi kutokana na shule za Sekondari, watoto wengi sana wanapata ujuzi katika sekondari. Kwa hiyo, wataweza kupata ajira katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuomba Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla waje wawekeze Geita, tuna maeneo ya kutosha kabisa kuweza kujenga viwanda. Lakini pia niombe Serikali sisi katika Kanda ya Ziwa hatuna Kiwanda cha Saruji, Viwanda vya Saruji, viko Mbeya, Tanga, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitumie pia fursa hii kuomba Serikali itutafutie wawekezaji waje wawekeze katika Viwanda vya Saruji, tena itafurahisha pale wakiweka kiwanda Geita, watu watafurahia sana, wataweza kufanya kazi zao vizuri na wananchi wataweza kunufaika kwa sababu vifaa vya ujenzi hasa hasa saruji, kwa sasa ni ghali sana kwa sababu ya gharama za usafirishaji. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwa kweli ituangalie sana Kanda ya Ziwa kuweza kuanzisha Kiwanda cha Saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Kiwanda cha Saruji, niombe kwamba kwa vile katika Mkoa mpya wa Geita tumezungukwa na Ziwa Victoria ambapo tuna samaki wa kutosha pia tuwezeshwe kuanzisha Viwanda vya Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bukondo tumezungukwa na Ziwa Victoria, tunapata samaki wa kutosha, Kasamwa na sehemu mbalimbali pamoja na kwa Mheshimiwa Magufuli katika Wilaya ya Chato, pia tumezungukwa na Ziwa Victoria. Kote huko tunahitaji wawekezaji waje kuwekeza katika sekta ya samaki ili basi wananchi waweze kuuza samaki hao katika

viwanda vyetu na pia tuweze kunufaika zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika Wilaya ya Geita na Mkoa mzima tunashughulika na kilimo cha matunda, mananasi yako kwa wingi sana, nadhani ukitoa Kiwangwa, nadhani Geita itakuwa ni ya kwanza kwa uzalishaji wa mananasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia wawekezaji wa viwanda vya kutengeneza *juice* pale Geita ili wananchi tuweze kunufaika na mazao yetu haya kwa sababu ilivyo sasa mananasi yanapoiva kwa wingi kwa kweli wananchi wanauza kwa bei ya chini sana. Lakini tukiongeza thamani kwa kutengeneza *juice*, nina uhakika *juice* hizi tutaweza kuuza nchi za nje lakini pia hata ndani ya nchi, kwa sababu ndani ya nchi yetu tuna watu wengi sana zaidi ya milioni 40. Kwa kweli ni watu wengi sana, tutaweza kupata soko kubwa ndani ya nchi, lakini vile vile na nchi za nje, nchi za Rwanda na Uganda, ambazo jirani na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuomba Serikali itutafutie wawekezaji katika maeneo haya ili kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii kushukuru sana kusema ukweli *TIB,* inafanya kazi nzuri, mwaka huu au mwezi huu tumeweza kufanikiwa, katika Jimbo langu pale Katoro tumepata mkopo, kuna *SACCOS* moja inaitwa *Kasemi Mababa SACCOS* wamefanikiwa kupata mkopo wao kutoka *TIB* na

vilevile wamepewa matrekta mawili. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niombe waongeze zaidi kwa sababu siyo Katoro tu, Narwamgasa kule, Nyarugusu, Bukoli na sehemu mbalimbali za nchi hii ambapo wananchi wako vijijini wanahitaji msaada mkubwa; tuongeze fedha na mtaji kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuendelee kutoa elimu ya ujasiriamali, bila ya kuwapa ujuzi wafanyabiashara hawa hawawezi kufanya kazi zao vizuri. Kwa hiyo, niombe Serikali kweli iendelee yaani iangalie uwezekano mzuri na mkakati wa kuweza kuwafikia hasa wananchi walioko vijiji kuweza kuwapa elimu ya kutosha kwa sababu ujasiriamali unahitaji elimu bila ya kuwa na elimu haiwezekani kufanikiwa katika ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali kusema kweli isiangalie tu mijini, mijini kuna *NGOs* nyingi ambazo zinatoa elimu tu-*concentrate* sasa vijijini ili tuweze kuboresha maisha ya wananchi walioko vijijini. Tukitoa elimu, sambamba na elimu tuweze pia kuwaongeza mtaji, kwa sababu bila ya mtaji haiwezekani kabisa kuweza kuendesha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vile vile Serikali iweke mazingira mazuri ya kuwawezesha wananchi kuwapa elimu wafanyabishara ndogo ndogo kama

hao unaowazungumzia wa Mchomoko pale Katoro, wanahitaji kuwezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana naona kipindi cha asubuhi cha shughuli za Bunge na ni wajibu kikomee hapa na muda hauturuhusu kwenda zaidi ya hapo kwa kuwa hatutamtendea haki mchangiaji yeyote. Tutakaporudi hapa mchana wa leo mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa *Engineer* Athuman Mfutakamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, hao ndiyo watakuwa wachangiaji wetu wa mwanzo na orodha yangu ninayo kabisa iko tayari hapa, tutaendelea kuangalia namna gani tutaendelea kuwataja wachangiaji wachache kabla hatujaingia kwenye mafungu. Naomba nirejee tena katika maelekezo ya mwongozo wangu pale saa tano asubuhi wakati wa matangazo.

Naomba Kamati ya Bunge ya Uongozi tukutane saa saba na robo saa hizi tukishasitisha shughuli za Bunge ili tuweze kushauriana kwa pamoja jambo lile ambalo lilikuwa limeletwa ndani ya Bunge litafanyiwaje kazi na linaweza likawasilishwa namna gani. Kwa hiyo tunakutana saa saba na robo sasa baada ya kusitisha shughuli hizi Bunge, kwenye ukumbi wetu wa Spika kwa ajili ya kikao hicho.

Natangaza hivi kwa sababu mara ya kwanza ilikuwa kikao hiki tukifanye saa saba kwa kuwa

Mheshimiwa Spika alikuwa kahudhuria mazishi kule alikosema, lakini mazishi yamesogezwa mbele, yatakwenda mbele zaidi ya saa kumi na mbili. Kwa hali hiyo, ni bora tufanye kabisa hiki kikao chetu saa saba hii ili Mheshimiwa Spika apate nafasi ya kwenda kushiriki mazishi yale ambayo alikuwa ametupa taarifa hapa Bungeni.

Baada ya kutoa tangazo hili, Waheshimiwa Wabunge nawashukuruni sana na naomba sasa nisitishe shughuli hizi, tutakutana tena hapa ukumbini saa kumi jioni kama tulivyobadilisha kanuni yetu.

*(Saa 07.15 mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika kipindi cha jioni na kama tunavyojua tunaendelea na hoja hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Tulipositisha mchana basi tulishaweka utaratibu wa kuanza. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Athuman Mfutakamba na nilisema Mheshimiwa Peter Msolla ajiandae.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya

Mkoa wa Tabora, tuna viwanda Tabora yaani Tabora *Textile* au Kiwanda cha Mbao. Hivi viwanda ni rasilimali kubwa kwa Mkoa na kwa Taifa kwa ujumla, tungeomba Serikali ifanye mikakati ili vianze kuzalisha kama vilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sera ya ulinganifu pamoja na ujumuishaji wa matumizi ya raslimali za nchi, *backward* na *forward linkages* hasa kwenye eneo la chuma pamoja na makaa ya mawe sijui sera ya Wizara ikoje ili kuweza kuwa na viwanda vya msingi yaani *basic industries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yoyote iweze kuendelea uhitaji wa *basic industries* ni muhimu, lakini tunaweza kuiga hata nchi zinazoendelea kama China na Japan waliiga kutoka nchi zilizoendelea. Basi na sisi tufanye utaratibu huo ili tuweze kutumia chuma hiki na kukiongeza thamani na pia kwa sababu umeme utapatikana kutoka kwenye makaa ya mawe, nafikiri tutapiga vita umaskini kwa hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye viwanda vidogovidogo yaani *cottage industries*. Jimbo la Igalula na Mkoa wa Tabora kwa ujumla uzalishaji wa embe ni mkubwa sana. Naamini Wizara ya Viwanda na Biashara vikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula pamoja na Ushirika, kama tutaweza kutumia mbegu bora inayozalishwa Sokoine, miembe hii inaweza kuzalisha embe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Tabora sasa hivi unawekwa lami, kwa hiyo kunaweza

kuwa na ndege zikachukua maembe na kupeleka sehemu mbalimbali ambapo hakuna embe kama Uarabuni na sehemu nyingine. Hilo likifikiriwa naamini uchumi wetu utakuwa kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lipo suala ambalo tunaamini linaweza kusaidia sana katika viwanda vya Maji. Kuna maeneo mengi Masasi wanazalisha maji na nimewaeleza wajaribu kuleta hata Tabora viwanda vya kutengeneza maji, kama utaratibu huo watashirikiana na Wizara Maji nafikiri viwanda hivyo vitatusaidia kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Sera ya Viwanda na Biashara inaweza kutusaidia tukaongeza ajira na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa machache hayo, napenda niishie hapo, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mfutakamba na sasa nitamwita Mheshimiwa Profesa Msolla, naona Mheshimiwa Msolla hayupo basi naomba nimwite Mheshimiwa Chiku Abwao atafuatiwa na Mheshimiwa Shibuda.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza katika viwanda vyetu tulivyovibinafsisha na hasa Kiwanda cha Urafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yanashangaza sana, ambayo mtu unashindwa kuelewa. Kiwanda cha Urafiki kilikuwa ni kiwanda ambacho kimetuletea faida kubwa sana Tanzania. Ni kiwanda ambacho kilikuwa kinatengeneza nguo nzuri na nzito, Khanga za maana na Vitenge. Ni kiwanda ambacho hata baada ya kubinafsishwa tukawa na hisa 49%. Kwa hiyo, tuna umiliki mkubwa, kama Serikali ingefuatilia kuona utendaji wa kiwanda hiki unavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, tulipotembelea kiwanda hiki baadhi ya Wajumbe tulitokwa machozi na baada ya kuulizia matatizo zaidi tukaambiwa viongozi wetu wengi wanajua tatizo hili, wakatueleza hata Mheshimiwa Frederick Sumaye wakati akiwa Waziri Mkuu alishafika pale na baadhi ya viongozi wengine wengi tu wanajua matatizo ya pale. Lakini cha kushangaza haichukuliwi uzito unaostahili ili kuhakikisha kwamba kile kiwanda kinafanya kazi ipasavyo hata kama baada ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoonesha hapa Serikali baada ya kuamua Sera ya Ubinafsishaji ikawa kama imetua mzigo kwamba haiwezi tena kufuatilia masuala hayo, vile wamebinafsisha shauri yao, kama kitafanya kazi ama hakitafanya kazi kiwanda chochote liwalo na liwe, kitu ambacho kinashangaza sana hasa ukiangalia jinsi hali ya uchumi wa nchi yetu unavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipofika pale tulishangaa kuona kiwanda vumbi tupu ingawa tumeoneshwa nguo mbili au tatu pale, lakini ukweli ni kwamba uzalishaji hakuna, ilikuwa tu ni kudanganywa kwamba kuna uzalishaji pale. Wafanyakazi wenyewe baadhi yao ndiyo waliitwaitwa tu kwa simu kufika pale na kibaya zaidi maeneo mengine wakatuzuia hata tusiingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa purukushani kubwa mpaka tukatishia kuita Polisi ndipo Ma-*godown* yakafunguliwa mengine ambayo walikuwa wanatuzuia. Baada ya kuingia ndani tulishangaa, kumbe walikuwa wanaogopa kuturuhusu tuingie kwa sababu ya baadhi ya mitambo imeng'olewa na inauzwa kama vifaa chakavu kama Mwenyekiti wangu wa Kamati alivyowasilisha, kitu ambacho kinasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lawama chungu nzima wafanyakazi; wafanyakazi wanahamishwa kwenye nyumba za kiwanda, wanahangaika makazi, nyumba za kiwanda zinapangishwa watu binafsi, bidhaa ambazo zilitarajiwa zizalishwe hazizalishwi, kuna maeneo ambayo yamegeuzwa stoo. Kimsingi hali inatisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo kuna ubadhirifu mkubwa wa bilioni 27 ambazo zilikopwa kwa kutegemea labda kufufua hicho kiwanda lakini pesa hizo mpaka leo hazijulikani zipo wapi na Kamati tuliomba iundwe Kamati ndogo ili ifuatilie suala hili. Cha kushangaza maana mimi ilibidi nimuulize

Mwenyekiti mara mbili au tatu baada ya kusema kwamba eti Mheshimiwa Spika amezuia isiundwe Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala nyeti kama hili hasara kubwa kama hii Kamati imeona na imeshuhudia na inataka kupata ukweli wa mambo ulivyo ili tujue hizi pesa zote zimetumika kwa kazi gani. Ukiangalia kama nilivyoeleza juzi kwamba kiwanda kimekosa kabisa mwelekeo hakifanyi kazi ambayo imetarajiwa, lakini Kamati inatakiwa iundwe lakini inazuiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza hii tunafanya kwa maslahi ya nani? Hizi dola bilioni 27 zimekwenda wapi? Ni swali ambalo tunajiuliza, lakini hatupati majibu. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri leo atueleze pengine ameweza kujua hizi pesa zimetumika vipi maana nasikia alikwenda na yeye akashuhudia mambo aliyoyakuta huko. Nadhani atakubaliana na mimi yote niliyoyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujue hizi pesa zote zimefanya kazi gani? Hili ni suala la msingi kabisa, tunaomba mtusaidie sisi Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Kamati yetu ya Viwanda na Biashara tunafanya kazi kwa umoja sana. Katika masuala ya maslahi ya Kitaifa hakuna chama wala hakuna atakayesema mimi ni CHADEMA labda ndiyo nina uchungu sana au mimi CCM nina uchungu sana, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakuwa na kauli moja na nina hakika kwa suala hili tulikuwa na kauli moja na tukamuomba Mwenyekiti wetu naye akatupokea kauli ile bila ubishi wowote. Akasema kwamba nitahakikisha kweli namweleza Mheshimiwa Spika na ninaeleza dhamira yetu ya kuunda Kamati ndogo ili tupate ukweli wa hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa msititizo sana na kwa maombi makubwa sana kwa uchungu wa pesa zetu Watanzania ukizingatia tuna hisa 49% katika kiwanda hiki, kwa hiyo sisi ni wadau wakubwa, naomba sana meza yako iweze kuzingatia suala hili la kuunda Tume ili tuweze kupata ukweli wa pesa hizi zimefanya nini na zilikwenda wapi na wahusika ni akina nani. Kama ni ubadhilifu na wizi, basi wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria. Hatuwezi kuacha raslimali za Watanzana wakati tuna hali ngumu sana ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina matatizo na Mheshimiwa Kigoda kwa sababu katika Wizara hii yeye ni mgeni ameingia juzi, hata haya tunayolalamikia na yeye ameyakuta. Lakini bado ana nafasi kubwa kuhakikisha naye anasaidia tatizo hili ili liweze kutatuliwa kwa sababu hatuwezi kuwa tunazembea wakati rasilimali zetu zinapotea bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naliwekea msisitizo na hili pia ni msimamo wa Kamati yetu, tulikuwa tunaomba sana ushuru katika mafuta ghafi utolewe. Kwa mafuta ghafi wenzetu nchi kama Uganda na Kenya hawajaweka ushuru na sasa hivi

viwanda vyetu vilikuwa 21, lakini vimebaki vitano na katika vitano hivyo ni viwanda vitatu tu ndiyo vinafanya kazi na vingine bado vinasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongeza ushuru wa mafuta ghafi tutasababisha bidhaa zinazotengenezwa viwandani kwetu kupanda bei. Matokeo yake kukosa soko na hatimaye kuzidi kuwapa faida wenzetu majirani ambao hawana ushuru wa mafuta ghafi wakapata biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta ghafi pamoja na kwamba yanasaidia kusafisha mafuta lakini pia yanasaidia kutengeneza bidhaa za sabuni mbalimbali ambazo sasa hivi tumeshuhudia katika ziara yetu ya Viwanda unakuta kuna wageni wengi wanakuja kununua sabuni hapa kwetu wanapeleka Uganda, Kenya na hata Kongo kwa sababu kuna unafuu fulani kutokana na kutoa ushuru huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushuru huu ukirejeshwa kama ilivyoonekana dhamira ya Serikali kwamba kuongeza kodi katika ushuru wa mafuta ghafi, itabidi viwanda vyetu vitengeneze bidhaa zake kwa gharama na kufidia ushuru huo ambapo vitakuwa na gharama kubwa ukilinganisha na majirani zetu, kwa hiyo, itapelekea sisi kukosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara sasa hivi ushindani uliopo ni mkubwa na hawa wawekezaji wa ndani ambao wanaendesha viwanda vidogo tunatakiwa kuwasaidia ili kuhakikisha viwanda vyote

havifi kwa sababu mpaka sasa hatuna viwanda, kwani viwanda vimekufa, wanashindwa kufanya kazi. Kwa hiyo, tufanye jitihada za makusudi ili kuwawezesha kufanya kazi angalau kusaidia kuinua uchumi wetu na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine pia tulilikuta la kutisha katika Kiwanda cha Kamal ambacho wanahusika na masuala ya vyuma, wanatengeneza Nondo. Kwa kweli tulihuzunika sana, hadi nikajiuliza hivi hii Wizara ya Viwanda na Biashara kazi yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kiwandani unakuta mazingira ya ajabu, tuliwakuta wafanyakazi wamefunga magunia, wamefunga ma-*box* miguuni ili kuzuia wasiungue, kazi ambazo zingeweza kufanywa kwa mashine yaani wanafanya watu wanachochea moto kuyeyusha vyuma, yaani hali tuliyoikuta ni ya kutisha na kushangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungekuwa na uwezo sisi kama Kamati siku ile kusema hiki kiwanda kifungwe mara moja, tungeweza kufanya hivyo. Lakini kwa kuwa hatukuwa na uwezo ilibidi lazima turudi tena tukae, tutoe taarifa yetu Bungeni na hali kadhalika Serikali iangalie namna gani itafanya, lakini ukweli ni kwamba, huu mimi nahesabu kama ni udhaifu mkubwa sana wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunabinafsisha viwanda tunaweka wawekezaji wanafanya kazi na watu wetu wanapata ajira pale, hatufuatilii hata wanafanyaje kazi zao, usalama wao

kazini, kama wanapata vitendea kazi, tunawaacha tu wafanye vyovyote itakavyokuwa. Kwa kweli hiki ni kitendo cha kusikitisha ambacho hakitakiwi Wizara hii ikifumbie macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri naomba uwe na utaratibu mpya wa kutembelea...

*(Hapa Kengele Ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiku hiyo ni kengele ya pili!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Ni ya pili?

**MWENYEKITI:** Ndiyo!

**MHE. CHIKU A.ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda!

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kwanza kabisa kutoa shukrani kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa pole za dhati kwa msiba mkubwa wa kufa maji ndugu zetu na raia wa nchi ya Zanzibar. Nawapa pole wafiwa wote pamoja na viongozi wote wa Serikali Mola awajaalie moyo wa subira na wafiwa wote

wapate moyo wa subira. Hivyo hivyo, nawatakia mfungo mwema na Mola awajaalie yote dhidi ya mitihani mtakayokabiliana nayo katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo mbele yetu ni ya kuhusiana na masuala ya viwanda na biashara na napenda kusema kwamba, viwanda na biashara viko karibu sana na vina uhusiano mkubwa na masuala ya kilimo kwa sababu bila kilimo baadhi ya viwanda haviwezi kuwepo na hapawezi kuwepo biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika changamoto ambazo nitachangia, basi nitachangia katika masuala ya viwanda vya mafuta, viwanda vya nguo pamoja na biashara ya Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na masuala ya viwanda vya mafuta vilivyopo hapa nchini changamoto iliyopo na iliyopo mbele yetu ni kwamba viwanda vingi vinakuwa vinazungumzwa kwa hisia potofu kwamba huenda wanatumia malighafi ya mafuta ambayo tayari yana usafi wa kuwa chakula. Kwa hiyo, naomba Serikali itusaidie na iondoe dhana potofu ya kuhusiana na viwanda hivyo kwa kuleta mchanganuo na mpambanuo wa kuhusu viwanda vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hadhi ya viwanda hivyo ni kweli vinatumia malighafi ya mafuta ambayo ni nusu au ambayo hayajatengenezwa? Tuna viwanda vya mafuta ya alizeti na mafuta ya pamba, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri apate nafasi atuletee mchanganuo, ndiyo hisia hasi ambazo zipo dhidi ya

viwanda hivi na uweze kutakasa mawazo ya Watanzania wanaohisi kwamba wenye viwanda wanadhulumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viwanda vya Pamba ambavyo vipo sambamba na biashara ya pamba napenda kusema ifuatavyo:-

Wakulima ndiyo kiwanda cha kuzalisha biashara ya pamba, kwa hiyo, wakulima hivi sasa wana ghadhabu kubwa sana kutokana na ukimya wa Serikali ambao haujafafanua na kuelezea mwelekeo na mwegemeo wa bei ya pamba. Wakulima tangu enzi ya *TANU* waliamini sana urafiki wao na siasa ya Chama cha Mapinduzi ya Nyerere, lakini hivi sasa umma wa wakulima una mgutuko mkubwa. Una fikra za kutangatanga na wana ghadhabu kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wanaomba majibu kuhusu majibu kifo cha viwanda vya nguo kwa sababu kila siku wanaahidiwa kwamba kuna mchakato na upembuzi, je, mchakato huu ni hatima ya mauti ya siku gani, kwamba sasa mauti ya mchakato yamefika viwanda vinaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Nguo viliuzwa kwa bei tupatupa, hivi sasa nguvujasho ya wakulima wa pamba na yenyewe inauzwa kwa mfumo wa tupatupa kwa sababu hawajui thamani ya bei yao. Je, Serikali ya CCM ni ufunguo wa jela kwa maisha bora na afya bora kwa wakulima wa biashara ya pamba? Je, ghadhabu hizi za wakulima na hila za

ukimya wa Serikali unaibua ushawishi wa kuomba nembo za CCM za jembe na nyundo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo jembe liondolewe kwenye kuwa nembo ya Chama cha Mapinduzi katika bendera yake kwa sababu kama kweli CCM nembo yake ni jembe na nyundo basi wangekuwa siku wanaamka kuzungumzia maslahi ya wakulima. Mbona mna ukimya sijasikia kikao chochote cha Chama cha Mapinduzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona haya niwaase kwa sababu mtoto mdogo habembelezewi nyimbo za mashetani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ghadhabu za mdororo wa biashara ya pamba ni ufu wa Viwanda vya Nguo, viarifu na vihusisho vya kuambiwa wakulima CCM ni rafiki yao vinaanza kutoweka. Nashukuru kwamba Waziri pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu, kwa hiyo, napenda kusema kwamba wakulima kutokana na ghadhabu zao wanauliza wahamie chama gani? Wananiuliza wahamie chama gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia hamieni chama mnachopenda wenyewe, msinifuate kule niliko kwa sababu hamjui, hamjui kwani wa kale husema ya kwamba mpangaji ndiye anayejua siri ya ubora wa sakafu na ubora wa mwenye nyumba na nyumba inavuja vipi! Wahenga husema mpangaji ndiye anayejua hayo, vivyo hivyo mpangaji ndiye anayejua ustaarabu wa mwenye nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM inapukutisha imani ya marafiki zake wa biashara wa pamba, je, fadhila za kudai uhuru na ahadi za *TANU* sasa zimekufa? Ubatilishi wa fikra potofu kuhusu Serikali ya CCM na tatizo la viwanda na tatizo la biashara ya pamba, naomba kusema kwamba ni sawasawa na dua la kuku halimpati mwewe. Ahadi mnazotoa kila siku Serikali hazitabiriki. Mko kwenye mchakato, mna mawazo, tumeyapokea, Serikali sikivu, hivi nyinyi usikivu wenu ni wa nusu kaputi au uko namna gani? Uongozi na utawala wa nchi usipoeleweka, siasa ya Chama hicho hufa kama *UNIP* ilivyokufa Zambia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaandaa vivutio kwa wawekezaji, tambueni bei ya pamba kwa biashara ya pamba ndiyo kivutio kwa mkulima. Bei ya biashara ya pamba hivi sasa siyo kivutio tena, hivi sasa wawekezaji wanaaminika zaidi. Kwa hiyo, wakulima wa pamba wanakuja na hisia ya kwamba wawekezaji kwanza wakulima mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Bunge hili litambue mambo yafuatayo ambayo ni changamoto kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakulima wa pamba wanaelewa kwamba Wabunge walisema hapa ‘bila buku hakuna pamba’. Hoja ya pili, Wabunge haohao wakaenda kwa Mheshimiwa Rais wakaomba bei ya Sh.725, wakulima walipokutana na Mheshimiwa Rais tarehe 25 akazungumzia bei ya Sh.745. Hivi Serikali ina bei gani hasa kwa wakulima wa pamba? Namwomba Mheshimiwa Rais Kikwete azungumze na atoe kauli ya mwisho tuelewe ili pamba iuzwe na tuelewa kwamba

matatizo yapo namna gani? Uongozi wa wakulima unataka kupata ukweli wa uhalisia, wamechoka kuambiwa ‘bila buku hakuna pamba’ lakini Wabunge walipokutana na yeye Rais wakazungumza Sh.725, hapa Bungeni hapajakanushwa ‘bila buku hakuna pamba’. Naomba sana wakulima wapewe uwazi na ukweli. Waheshimiwa wakulima nimejitahidi, tumekutana na Mheshimiwa Waziri wa Mkuu, tumekuta na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tumekutana na Mheshimiwa Rais lakini mambo yamekuwa kimya. Ndugu zangu wa CCM ukimya ni mchwa utakaowatafuna hadi mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyohivyo kuongoza ni kutambulisha mazingira ya ukweli kwa waongozwa. Hivyohivyo maana ya uongozi ni kuelezwa mabaya na mazuri, kwa nini Chama cha Mapinduzi mnakaa kimya? Namwomba Mheshimiwa Rais Kikwete atambue bei Sh.660 waliopewa wakulima ilikuwa ni shinikizo, hii siyo ahadi waliyokubaliana Ikulu. Mheshimiwa Rais namwomba sana na wakulima wanaomba ongezeko la bei ya pamba la Sh.100 ambayo itakuwa ni shilingi bilioni 30 au shilingi bilioni 60. Wakulima wa pamba hawataki ruzuku, wanataka bei ambayo watapewa kutokana na mkopo kama alivyofanya Rais Obama kwa kufufua uchumi wa Marekani. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Fedha na tumeongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa namwomba Rais awaite hawa wawili wazungumze, mtoe kauli muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu naomba litambue kwamba tozo za pamba zimesaidia shilingi

bilioni 34 kwenye Halmashauri na mzunguko wa shilingi bilioni 660 zinaathiri maeneo ya Mikoa ifuatavyo: Shinyanga, Mwanza, Simiyu, Geita, Tabora, Mara, Kagera, Kigoma, Singida, Morogoro, Manyara, Tanga, Pwani, Iringa na Kilimanjaro. Athari kwa jamii ya wakulima wa pamba sasa ni kifo cha MKUKUTA, maisha bora hakuna, afya bora hakuna, mfumuko wa bei ni aibu kubwa, sasa waende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvundo wa yai moja bovu ni mkali kuliko harufu ya mayai mazuri. Hivi sasa uvundo wa bei ya pamba ni mkali sana na utaangamiza na wale wasiopenda kuangamizwa, unazaa kwikwi la kisiasa. Kifo cha viwanda ni kichocheo cha biashara ya pamba kufa. Kunguru hafugiki. Je, imani ya Watanzania itafuga vipi imani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, katika sekta ya pamba kuna suala ambalo limejitokeza. Naomba kauli ya Serikali kuhusu kutokea tatizo la Mkurugenzi kusimamishwa kazi, Bwana Mtunga. Wananchi wanaopenda haki wanataka waambiwe kauli ya Serikali ya kutambulisha makosa ambayo ameyafanya Bwana Mtunga, je, alifanya makosa gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natahadharisha matumizi ya vikao vya Bunge kuwa ni machinjio ya watumishi kwa kutumia hisia za shutuma na tuhuma ambazo si za kweli na hazina upembuzi, tutavunja heshima ya kuaminika Bunge letu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda ni kengele ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tunajaribu kupitia muda tuliobakiwa nao hapa kwa kweli inabidi sasa kusitisha michango ya Waheshimiwa Wabunge wengine waliobakia. Muda ni mchache.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia makadirio ya matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka 2012/2013, nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya viwanda na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo vina uwezo wa kutoa mchango mkubwa kwa ukuaji uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo ili viwanda hivi viweze kutoa mchango wake kikamilifu kwa ukuaji wa uchumi lazima yawepo mazingira wezeshi yatakayosaidia viwanda hivyo kufanya kazi kwa ufanisi. Nchi kama India imefanikiwa kuwa na sekta madhubuti ya viwanda vidogo kutokana na kuweka mazingira wezeshi. Leo hii sekta ya viwanda vidogo nchini India inachangia sana katika kutoa ajira, ikizidiwa tu na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu hapa nchini uzoefu unaonesha kuwa pamoja na kuwa kilimo ndicho kwa muda mrefu kimeongoza katika utoajia ajira kwa Watanzania, viwanda navyo vimekuwa vikibeba mzigo wa changamoto ya ajira mijini, changamoto ambayo inatokana na wimbi la ongezeko la watu wanaokimbilia mijini. Hata hivyo, kufuatia kufungwa kwa viwanda vingi, mzigo huo sasa unabebwa na sekta isiyo rasmi. Ili kuweka uwiano mzuri utakaotuhakikishia kuongezeka kwa uzalishaji kupitia kilimo, kuongezea mazao yetu thamani na kuondoa tatizo la ajira, ni vyema tukaangalia uwezekano wa kuvutia uwekezaji wa viwanda nchini kwa kuingiza teknolojia ya viwanda vidogo na vya kati ambavyo vilishamiri katika nchi za Asia lakini kwa sasa vinafungwa kutokana na kupanda kwa gharama za uzalishaji katika nchi hizo. *SIDO* ambayo imefanya kazi kubwa katika kuendeleza viwanda vidogo nchini iwezeshwe kifedha na kushirikishwa kikamilifu katika kusimamia uingizwaji wa teknolojia na uanzishwaji wa viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maziwa ina fursa kubwa ya kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Tanzania tuna fursa kubwa ya kukuza uchumi na kuwaondolea wananchi umasikini. Hata hivyo, kama Taifa bado hatujaitumia vyema fursa hii kutokana na mazingira mabovu yaliyopo, ambayo yamezuia ukuaji wa sekta ya maziwa. Takwimu zinaonesha kuwa wakati ambapo Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa wingi wa mifugo kwa kuwa na ng'ombe wapatao milioni 221.3 na kuzalisha kiasi cha lita za maziwa zipatazo milioni tano, ni lita 112,500 tu ndizo zinasindikwa. Cha

kushangaza zaidi ni kwamba ni 3% ya maziwa yanayozalishwa nchini ndiyo yanaingia katika soko rasmi ikilinganishwa na asilimia 30 Kenya na asilimia saba (7%) nchini Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu vya usindikaji wa maziwa vimekuwa vikitumia sehemu ndogo ya uwezo wake kusindika kwa takribani asilimia 26.7 tu wakati ambapo viwanda vya Kenya vinatumia asilimia 85.7 na Uganda asilimia 45.5 ya uwezo. Kwa hali hii usindikaji Tanzania unatoa bidhaa chache za maziwa ikilinganishwa na nchi jirani zetu hivyo kuathiri uwezo wa usindikaji na kiushindani kwenye soko la *EAC*. Mojawapo ya sababu zinazochangia hali hii ni gharama kubwa za uzalishaji wa bidhaa hizi nchini ikilinganishwa na nchi jirani. Utafiti uliofanywa na *RLDC* (2010) unaonesha gharama za kusindika maziwa (*pasteurized milk)* kwa lita moja kwa kiwanda kilichopo Tanzania inagharimu kiasi cha shilingi za Tanzania 778 ikilinganishwa na shilingi 526 kwa Kenya. Aidha, takwimu zitokanazo na utafiti huu zinaonyesha kuwa tuna changamoto kubwa kwani lita nyingi za maziwa hazikusanywi toka kwa wafugaji na kusindikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha vilevile kuwa kiwango cha unywaji wa maziwa Tanzania ni kidogo sana. Kwa wastani Mtanzania anakunywa lita 40 tu za maziwa kwa mwaka ikilinganishwa na lita 100 kwa Mkenya na lita 55 kwa Mganda. Aidha, changamoto nyingine inayodumaza ukuaji wa sekta ya maziwa na maziwa yaliyosindikwa (*VAT* asilimia18); mfumo ambao hautoi ushindani ulio sawa ikilinganishwa na majirani zetu wa Kenya ambao

katika kuifanya sekta ya maziwa kuwa *competitive* mwezi Machi mwaka huu ilipitisha uamuzi wa kutotoza kabisa kodi katika bidhaa za maziwa na maziwa yaliyosindikwa. Ili Taifa linufaike na fursa zilizopo katika sekta ya maziwa nchini, ni lazima kama Taifa tuhakikishe tunakuwa na mkakati wa kuvilinda viwanda vichache vilivyopo ili viweze kushindana na viwanda vya nchi jirani. Aidha, lazima tuje na mkakati wa kuongeza idadi ya viwanda vya kuyasindika maziwa yetu hapa nchini na vilevile kuwahamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kunywa maziwa. Kwa kufanya hivi, tutapunuza tatizo la ajira na kuongeza kipato cha watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo kama Taifa tunaweza kulitumia kikamilifu katika kukuza pato la Taifa ni katika sekta ya uvuvi. Sekta hii inafursa kubwa sana ya kuweza kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu katika nyanja za kukuza pato la wananchi, ajira na hata katika kuboresha lishe na usalama wa chakula kwa watu wetu. Ili sekta hii iweze kutupatia mchango mkubwa kiuchumi, ni vyema sasa tukawa na mkakati unaotoa miongozo ya uwekezaji wa kibiashara katika sekta hii *(investment policy for aquaculture parks);* mkakati ambao utatuwezesha kuingia katika ufugaji wa samaki kisasa kwa kuanzisha maeneo maalum ya biashara ya ufugaji wa samaki (*aquaculture value chain parks).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa maeneo maalum ya biashara ya ufugaji wa samaki, *(aquaculture value chain parks),* utatusaidia kuongeza kwa haraka mchango wa sekta ya uvuvi katika uchumi

wa nchi yetu. Hii inatokana na ukweli kuwa asilimia 46 ya samaki wanaopatikana katika soko la Dunia wanapatikana kupitia ufugaji wa samaki katika bahari ya kina kifupi, mabwawa na mito. Jirani zetu wa Uganda, Kenya na Rwanda tayari wamepiga hatua kubwa katika hili. Wakati ambapo mauzo ya samaki nchini Uganda yanafikia tani 550,000 kwa mwaka kati ya hizo tani 90,000 zinatokana na ufugaji wa samaki. Hii inaifanya Uganda kuwa nchi ya tatu katika Afrika kwa ufugaji wa samaki ukiziacha Misri na Naigeria. Uganda kwa sasa wanakusudia kuongeza idadi ya samaki wanaotokana na ufugaji hadi kufikia tani 300,000 ifikapo mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa idadi kubwa ya Watanzania hawajafaidika na mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuwawezesha kiuchumi. Ili lengo la kuwasaidia na kuwawezesha wananchi wengi wenye kipato cha chini liweze kufikiwa, lazima *targeting* na utekelezaji wa mikakati hii isimamiwe ipasavyo. Mfuko wa Taifa wa kuendeleza Wafanyabiashara Wadogo *(NEDF)* unaosimamiwa na *SIDO*, mtaji wake ni mdogo sana kuweza kutosheleza mahitaji ya wananchi. Ni vyema Serikali ikaangalia uwezekano wa kuongeza mtaji katika mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo tetesi kuwa Serikali imekuwa ikipoteza zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa mwezi sawa na wastani wa shilingi milioni 20 katika kila kontena la ngozi linalosafirishwa na ukwepaji kodi ya mapato na usafirishaji wa kinyemela nje ya nchi. Kama jambo hili ni kweli, ni lazima Serikali ichukue hatua za makusudi kukomesha jambo hili. Njia nzuri ya

kukomesha jambo hili na wakati huohuo kuongeza mapato na ajira nchini ni kupiga marufuku uuzwaji wa ngozi ghafi nje ya nchi. Kama Uganda na Ethiopia wamepiga marufuku uuzwaji wa ngozi ghafi nje ya nchi yao na kupata mafanikio makubwa sisi tunashindwa nini? Lazima tuamue kwa haraka kupiga marufuku suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nikiamini kwamba Serikali itazifanyia kazi changamoto nilizoainisha na ushauri nilioutoa.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chumvi nyingi sana inavunwa huko Meatu – Simiyu. Naiomba Serikali ianzishe kiwanda cha kusindika chumvi ili kuongeza kipato kwa Wilaya na nchi kwa ujumla. Aidha, naomba sasa Serikali itoe fedha kwa ajili ya mikopo kwa wajasiliamali wa chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika mambo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ni ukweli usiopingika kuwa Sekta ya Viwanda na Biashara ndio inayoinua uchumi wa nchi yoyote. Leo hii sekta hii haipewi kipaumbele ili iweze kutekeleza majukumu yake na kibaya zaidi hata kibajeti bado haipewi fedha zote inazoomba. Tatizo hili la kutotoa fedha zote linaathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa mipango yake. Hii ina maana kuwa bado uchumi wa nchi yetu

utakuwa unabakia palepale kama si kurudi nyuma. Imefika wakati sasa kama nchi kuhakikisha bajeti inayoombwa katika Wizara hii inatolewa yote ili kunusuru uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma kulikuwa na viwanda vingi sana ambavyo vilipunguza hata tatizo la ajira, leo hii hakuna hata kiwanda kimoja kinachofanya kazi. Viwanda kama *General Tyres, Tanganyika Parkers,* Kiwanda cha Maziwa (Kilosa na Morogoro) pamoja na viwanda vya ngozi. Viwanda vyote hivi vilikuwa vinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuleta ajira nyingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waziri katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2012/2013, ameliambia Bunge kuwa itaongeza viwanda vingine pamoja na kuvifufua vilivyokufa, hili ni suala zuri na linatia moyo kwa vile vijana walioko kwenye maeneo husika watapata ajira. Je, Serikali itatoa fedha yote katika bajeti yao ili Wizara iweze kutekeleza suala hili? Wasiwasi wangu ndio huo. Tumekuwa na mikakati mizuri lakini hatutekelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumefunga viwanda vya nguo ambavyo vilivyokuwa vinanunua pamba ya wakulima, hivyo viliongeza mapato na hali ya uchumi ya wakulima. Leo hii pamba imejaa majumbani mwao hawana sehemu ya kuipeleka, matokeo yake watu wachache wamekuwa wakiwanyonya wakulima hawa kwa kuwauzia pamba kwa bei ya kutupwa. Hali hii inafanya mkulima akate tamaa kabisa na mwisho wa siku zao hili la pamba

litapotea ndani ya nchi yetu. Naiomba Serikali ilinde viwanda vyetu kwani ndio vinavyosaidia kuleta ajira na kuongeza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiona bidhaa nyingi zikiingia nchini chini ya kiwango. Hii inaonyesha ni jinsi gani *TBS* haifanyi kazi yake kikamilifu. Matokeo ya bidhaa hizi ni kuwaacha wananchi wakibakia maskini kwani wananunua vitu ambavyo viko chini ya kiwango na hivyo haviwezi kudumu, hivyo inampasa anunue tena kingine, hali hii inarudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa magari nje ya nchi na *TBS* kwa kutoa hati maalum za ubora kabla ya bidhaa hizo kuruhusiwa kuingia kwenye soko la nchi yetu. Makampuni haya mbali na kutokuwa na sifa bado yalipewa kazi bila kupitia utaratibu wa zabuni. Matokeo yake kazi ya ukaguzi haifanyiki ipasavyo na kuinyima Serikali mapato kwani kiwango kinachoingizwa nchini ni tofauti na zinazotumika kama ada ya ukaguzi. Naiomba Serikali ipitie upya mikataba hii ikiwezekana utaratibumpya wa kutumia zabuni ufuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Serikali kwa kupata mwekezaji atakayejenga kiwanda katika Kata ya Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga. Naelewa fika kabisa kiwanda hiki kitaleta tija katika Mkoa wa Shinyanga na kuongeza ajira nyingi kwa vijana waliokuwa wanakosa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa juhudi zao za kutaka kuibadilisha Wizara hii isimamie vizuri sera za viwanda na biashara nchini, naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sekta ya viwanda. Tanzania ina fursa ya kuwa nchi ya "*agro-industry*" kwa sababu ina malighafi nyingi zitakazotosheleza viwanda vyetu vyote. Katika viwanda vilivyobinafsishwa, viko vinavyofanya kazi vizuri, tunavipongeza, lakini viko vinavyofanya kazi tofauti na makubaliano na viko vile ambavyo havifanyi kazi kabisa. Je, Serikali inachukua hatua gani ya haraka kwa vile viwanda vilivyofungwa na vile vinavyolegalega katika kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa uwepo wa viwanda vingi tunaongeza thamani ya mazao yetu ya kilimo hivyo ni faida kwa mkulima, lakini pia viwanda vinaongeza ajira hivyo kutatua tatizo la ajira nchini. Naiomba Serikali ishawishi uanzishwaji wa viwanda vingi zaidi nchini kwa kuandaa mazingira bora ya uwekezaji. Bidhaa za korosho, ngozi na kadhalika zinatumika kutoa ajira kule zinakopelekwa na kutuacha Watanzania tuwe na ukame mkubwa wa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya biashara. Tanzania hatujazitumia vizuri fursa za biashara kama vile soko la *AGOA*. Aidha, bidhaa zetu nyingi hazijafikia viwango vya Kimataifa katika usafirishaji kwa mfano

zao la embe ambalo sasa limekumbwa na magonjwa, lingeweza kuwapatia wakulima wa Tanzania fedha nyingi za kigeni, vilevile bidhaa za kilimo hai (*organic farming*) zina soko zuri nje ya nchi. Je, ni kwa kiasi gani Serikali inashawishi ulimaji na upatikanaji wa bidhaa za aina hii ili ziongeze kipato cha mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bidhaa feki. Inashangaza kuwa nchi yetu inapokea kwa wingi kutoka nje bidhaa zisizo na ubora wakati tuna *TBS* kwa mfano vifaa vingi vya umeme havina viwango kabisa na hivyo kusababisha hasara na hatari katika nyumba zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Wizara hii ijitahidi sana kukamilisha malengo yake ili nchi yetu isafirishe mazao ya kilimo yaliyoongezewa thamani.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninashauri Wizara iwe na Waambata Biashara katika Balozi zote za Tanzania zilizopo nje ya nchi. Tanzania inatekeleza Diplomasia ya Uchumi, suala hili ni muhimu, linatakiwa lisimamiwe na Wataalam wa Wizara, lisiachiwe Wizara ya Mambo ya Nje pekee. Jeshi la Ulinzi (TPDF) limeweza kuendelea kubakiza Waambata Jeshi (*Military Attaches*). Wizara ya Viwanda na Biashara nayo ihakikishe inao Wataalm wa Viwanda na Biashara katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja ya *EPZA*. Naomba Serikali iweke mkazo kuendeleza *EPZ*. Wapeni mamlaka na pesa za kufanya kazi. Mtendaji ni mzuri sana na ana uwezo, chukueni mfano wa Lesotho, nchi hiyo ilianzisha viwanda 200 kwa pamoja kwa mkopo wa *World Bank*, kisha ikawapa *private sector* kuviendesha, ajira iliongezeka na kuwa 600,000. Wizara/Serikali ikope na ku-*fast track* ukuaji wa *EPZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kuwa na viwanda ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa lakini vilevile hutoa ajira kwa vijana na wananchi wengi, wanaoajiriwa kwenye sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Uwekezaji imejikita sana kwenye uwekezaji kwenye sekta ya kilimo, kwa maana ya ardhi, kwa nini tusielekeze sana kwenye uwekezaji wa viwanda? Kilichofanyika katika sekta hii ya viwanda ni kuwapa wawekezaji viwanda vilivyokuwepo ambavyo navyo sehemu kubwa wawekezaji waliovichukua wameshindwa kuviendeleza, kwa nini wasihamasishwe wawekezaji kutoka nje na ndani kuwekeza viwanda vipya? Mfano viwanda vya mbolea, nguo, magari, matrekta, simenti, mabati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa asilimia kubwa, wawekezaji walio wengi wanapenda kujiingiza kwenye

rasilimali za Kitaifa kama madini, kwa maana ya migodi au katika kilimo kwa maana ya ardhi ambazo ni rasilimali za Taifa. Hii ni hatari kwa Taifa kuachia rasilimali muhimu kwa uchumi wa Taifa kuwa mikononi mwa wageni, ni hatari. Umakini unahitajika sana katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri uwekezaji katika viwanda utiliwe maanani kwa maslahi ya Taifa letu linalokuwa kiuchumi. Aidha, napenda kujua ni viwanda vingapi vipya vimeanzishwa hapa nchini na viwanda vyetu tulivyovibinafsisha ni vingapi vinaendelea vizuri na ni vingapi havijaendelezwa na ni sababu zipi zimefanya/zimesababisha viwanda hivyo visiwe na tija hata baada ya kuwapa wa wawekezaji? Ni hatua zipi zimechukuliwa kwa wawekezaji ambao wameshindwa kuendeleza viwanda vilivyobinafsishwa, ni manufaa gani tumepata kutoka kwenye viwanda tulivyobinafsisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani haiwezi kuendelea kama hatuna viwanda. Nchi hii ina rasilimali kubwa ambazo hatuzitumii kwa kukosa viwanda. Viwanda vingeweza kutengeneza ajira hapa nchini na kuepuka kilio cha vijana wengi ambao hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iandae mpango wa kufufua viwanda ambavyo havifanyi kazi na kwa vile viwanda ambavyo vilibinafsishwa na kutoendelezwa, Serikali ivichukue kwani walio wengi

waliobinafsishiwa viwanda wamebadili matumizi yao. Viwanda vya kuchambulia pamba ni muhimu vikaimarishwa, sambamba na viwanda vya nguo, viwanda hivi vya nguo vikiimarishwa vinaweza kutoa ajira kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na viwanda vya korosho, eneo lingine ni kuimarisha viwanda vya kubangua korosho, tutakuwa tumewasaidia sana wakulima wa korosho wa Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara ambao wanategemea sana zao hilo ambalo linazalishwa kwa wingi sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya samaki, eneo lingine linalotakiwa liangaliwe kwa umuhimu ni Viwanda vya Kusindika Samaki. Tanzania ni nchi ambayo imezungukwa na maji ya Bahari na Maziwa makubwa na Mito ambayo yote ina mazao ya uvuvi. Tukiwawezesha kuweka mazingira ya viwanda vya kusindika samaki, tutazalisha ajira nyingi na kuwafanya wananchi wanaoishi katika maeneo hayo waimarike kiuchumi, nashauri Serikali iwekeze zaidi katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Kusindika Maziwa na Ngozi. Serikali iandae mpango wa kufufua viwanda vya kusindika nyama ambavyo vitasaidia sana kupunguza idadi ya mifugo kwa sababu haina soko. Tukiimarisha viwanda hivi, tutakuwa tumeisaidia jamii ya wafugaji.  Serikali pia iangalie umuhimu wa kuimarisha viwanda vya kusindika maziwa ambayo yatakuwa ni soko la ndani na nje. Tukiimarisha viwanda

hivi hata tatizo la wafugaji wenye asili ya kuhamahama linaweza kutoweka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba Serikali iimarishe viwanda vidogovidogo ambavyo vitajishughulisha na kusindika matunda na kukamua matunda ambayo karibu kila eneo hapa nchini yanazalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii adhimu kwangu kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema mwenye kurehemu. Nawatakia Ramadhani njema wote wenye kushikamana na Mwezi huu Mtukufu. Mwenyezi Mungu azikubali Ramadhani zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza mchango wangu kwa kuzungumzia viwanda. Viwanda ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na watu wake, kama itasimamiwa na kufanya kazi ipasavyo. Tanzania tunazo rasilimali nyingi sana ambazo zikitumiwa vizuri ni mchango mkubwa kwa viwanda. Mfano wa rasilimali ambazo tunazo na zingefaa katika viwanda vyetu badala ya kusafirisha mali ghafi nje ya nchi, ni pamba, ngozi, samaki, nyama, tunayo matunda mbalimbali ambayo ni mengi sana. Ukiangalia matunda mengi tuliyonayo ni matunda ya msimu ambayo yanakuwa mengi katika msimu wake na ukimaliza msimu wake yanatoweka yote na hasara kubwa inapatikana wakati wa msimu wa matunda, yanakuwa mengi hakuna wateja na yanaoza na sio kwa matunda tu bali

na samaki na mengineyo. Kama Serikali ingeweka kipaumbele ingesaidia sana Taifa letu, tungeondoa tatizo la ajira kwa vijana wetu. Wakulima, wavuvi, wafugaji, tungekuza vipato vyao na kuwanusuru kupunjwa bidhaa zao. Nashauri turejeshe viwanda vyote vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi mfano viwanda vya korosho, viwanda vya nguo, viwanda vya ngozi na vingine vyote, huu ni ushauri wa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia biashara, biashara ni mhimili mwingine kwa pato la nchi kama usimamizi mzuri na utekelezaji mzuri utafanywa. Serikali yetu imekuwa na mtazamo wa kuwajali sana wafanyabiashara wakubwa na ambao wengi wao wamekuwa wajanja wa kukwepa kodi, hivyo naiomba Serikali iwe makini juu ya hili. Pia Serikali iwezeshe wafanyabiashara wadogowadogo kwa kuwapatia mikopo ya masharti nafuu itakayoendeleza biashara zao, wapatiwe elimu katika shughuli zao za biashara ili wafanye kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambatanisha mchango kuhusu masuala ya *COSOTA*. Mchango huo ni taarifa ya wadau waliokutana mwaka 2010, naomba nipate maelezo ya utekelezaji wa suala hilo. *COSOTA* inapaswa kuwa *reformed* na sheria iletwe haraka. *TV* na *Radio stations* zianze mara moja kulipa wasanii kwa kazi wanazotumia. Wizara isimamie jambo hili kwa haraka na Sheria ya *COSOTA* ya mwaka 1999 kwenye eneo hili itumike mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya umma wakiwemo wasanii wenyewe hawajui chochote kuhusu *COSOTA* wala Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi, hivyo basi washiriki waliiomba *COSOTA* kuendesha kampeni kabambe nchi nzima ili kuelimisha umma pamoja na wasanii kuhusu Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki. Vyombo vya habari (luninga, redio, na magazeti) navyo pia viliombwa kufanya kazi hiyo kama mojawapo ya majukumu ya vyombo hivyo katika kuelimisha umma. Elimu hiyo pia ijumuishe masuala ya madhara ya kununua kazi feki za wasanii, muziki, filamu na machapisho mbalimbali ambayo mbali na kutokuwepo na ubora wa viwango, lakini pia husababisha kukosekana kwa mapato stahiki (kodi) kwa upande wa Serikali na (mrahaba) kwa upande wa wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* ishirikishwe katika Vituo vya Forodha (bandarini na mipakani) katika uingizaji bidhaa za kazi za sanaa nchini kama vile zinavyoshirikishwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (*Tanzania Food and Drug Authority*) kwa bidhaa za chakula na dawa, Shirika la Viwango Tanzania (*Tanzania Bureau of Standards*) kwa bidhaa zenye viwango vinavyotambulika kimataifa, pamoja na Tume ya Ushindani wa Biashara *(Fair Competition Commission - FCC*) kwa bidhaa bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* au BASATA wasajili na kutoa leseni kwa maduka/maktaba yanayouza/kukodisha *CD/DVD* za muziki/filamu, vibanda vya kileo vinavyoonesha sinema na majumba ya starehe/kumbi zinazopiga muziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Tanzania Revenue Authority*), imepata mafanikio makubwa katika kukusanya kodi kwa upande wa sigara na pombe kali kutokana na kuamuru matumizi ya ukanda wa lakiri (*Bandroll/hologram*) kwa watengenezaji/waagizaji wa bidhaa hizo. Washiriki walipendekeza ama *TRA* au *COSOTA* waanzishe utaratibu huohuo kwa kazi za sanaa. Hii itasaidia kupambanua kati ya bidhaa (*CD/DVD*) halisi na zile feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na vitisho dhidi ya maisha ya watendaji wa Serikali na Taasisi zake *(COSOTA/TRA/FCC)* wakati wa kufanya misako ya bidhaa feki, Serikali ihakikishe inawapatia ulinzi madhubuti na wa kutosha watendaji hao na isiwe na huruma kwa maharamia hao wanaodiriki hadi kuwatishia Maafisa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Tanzania Revenue Authority*) ilipendekeza wasanii wote wasajili kazi zao pamoja na thamani ya kazi hizo na Mamlaka hiyo ili wakati wa kufanya msako iwe rahisi kutambua bidhaa zilizosajiliwa na zile zisizosajiliwa pamoja na thamani ya kazi hizo. Hii itawezesha *TRA* kupata thamani halisi ya kazi hizo kwa ajili ya kutoza kodi na pia kutoa adhabu kwa wale wanaoiba kazi za wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wote wasajili kampuni au Taasisi zao kisheria ili iwe rahisi kutambuliwa na Serikali pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuishajiisha Serikali kuhuisha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ili adhabu kali zitolewe kwa wezi wa kazi za sanaa kwani kwa sheria ilivyo sasa, adhabu zinazotolewa ni ndogo sana kiasi kwamba maharamia wanaoiba kazi hizo hawashindwi kumudu kuzilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuihimiza Serikali kuhakikisha kwamba Jeshi la Polisi na Mahakama wanasimamia sheria hizo kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii, watengenezaji na wasambazaji wa kazi za sanaa walihimizwe kupunguza gharama za uzalishaji bidhaa hizo ili bei nayo ipunguwe kwa mlaji wa mwisho katika kukabiliana na ushindani wa bidhaa feki ambazo kutokana na ubora wake hafifu, bei za bidhaa hizo nayo huwa chini. Bidhaa feki pia husababisha wasanii kukata tamaa kwani huona jasho lao halilipi na hivyo huacha shughuli hizo na kuua vipaji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi lisiwe linawakamata wetengenezaji na wa sambazaji wa kazi feki tu, bali pia liwakamate watumaji (walaji) wa kazi hizo pale wanaponunua bidhaa hizo ili kupunguza kama siyo kuondoa kabisa mahitaji (*market demand*) pia bidhaa feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tume ya Ushindani wa Biashara (*Fair Competiton Commission - FCC*), inaweza kukamata makontena kwa makontena ya bidhaa bandia wakati yakiingizwa nchini kupitia vituo

vya forodha (bandarini na mipakani) kwenye maghala ya kuhifadhia mizigo na mpaka madukani na kuziteketeza bidhaa hizo, kwa nini wasifanye hivyo kwa bidhaa za kazi za sanaa (*DVD* na *CD*) za filamu na muziki? Suala la bidhaa feki limesambaa sana katika kazi za sanaa kwa mfano *DVD* na *CD* za filamu na muziki zinazoingizwa nchini kutoka nchi za Mashariki ya mbali. Wasanii watengenezaji na wasambazaji wa kazi za sanaa wanahimizwa kushirikiana kwa karibu sana na Tume ili kukabiliana na wizi wa kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko mipakani. Naomba mpaka wa Kagunga katika Kata ya Kapuga (mpaka na Burundi) uingizwe kwenye mipango ya Wizara. Nilizungumza suala hili na Katibu Mkuu, mpaka huu ni muhimu sana kwa vile *TPA* wanajenga bandari pale, Wizara itazame suala hili la mpaka wa Kagunga Mkoani Kigoma.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha ombi la wakulima wa zao la zabibu wa Wilaya za Chamwino, Bahi na Dodoma Mjini na hususani wakulima wa mradi mkubwa wa shamba la zabibu la Chinangali wenye ekari 300 ambao hivi sasa wameshaanza kukabiliwa na tatizo la kulipwa bei ndogo na zabibu nyingine kukosa soko. Bei hii ndogo inatolewa na mnunuzi pekee wa kiwanda cha *CETAWICO* kilichopo Hombolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha zabibu katika Mkoa wa Dodoma kilishamiri sana miaka ya nyuma wakati kukiwa na soko la uhakika la kiwanda cha *DOWICO*. Kufuatia kufilisika kwa *DOWICO,* wakulima

wa zabibu wakakosa soko na kilimo cha zabibu kikafifia sana. Kutokana na jitihada za Serikali za kuwatafutia zao la kudumu la biashara wakulima wa Mkoa wa Dodoma, alitafutwa mwekezaji wa kiwanda cha mvinyo cha *CETAWICO* ili kuwapatia soko la uhakika wakuilma wa zao la zabibu. Kiwanda cha *CETAWICO* hivi sasa kimeshachukua na kuvimiliki viwanda vingine vidogo vya usindikaji wa zabibu vilivyoko Hombolo, Bihawana pamoja na kiwanda cha zamani cha *DOWICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ya kiwanda cha *CETAWICO* ya kumiliki viwanda vyote vya usindikaji wa zabibu ndiyo inayoipa *CETAWICO* ukiritimba wa kuwa mnunuzi mkubwa na pekee wa zabibu za Dodoma. Mwekezaji huyu wa kiwanda cha *CETAWICO* pamoja na ukiritimba (*monopoly*) alionao pia ananufaika na unafuu wa kodi unaotokana na kulinda uzalishaji wa zao la zabibu zinazozalishwa hapa nchini, lakini pia mwekezaji huyu *CETAWICO* anavyo vibali vya kuagiza malighafi toka nje ya nchi kwa ajili ya kusindika mvinyo na malighafi nyingine anaziuza kwa makampuni mengine ya hapa nchini kama *Tanzania Distileries Limited* (*TDL*). Unafuu huo pamoja na mvinyo anayouza ni kwa jina la zabibu za Dodoma ambazo anazinunua kwa bei ya chini na nyingine kukosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe ya kwamba kwa sasa, mkulima anawekeza zaidi ya shilingi millioni sita kwa ekari moja ya shamba la zabibu katika kuliandaa hadi kufikia hatua ya uzalishaji. Cha kusikitisha ni kuwa bei ya zabibu ghafi tangu mwaka 2007 imebakia kati ya shilingi 500 mpaka 1000 kwa kila,

bei inayopangwa na kulipwa na mnunuzi huyu pekee bila kuzingatia gharama kubwa anazozitumia mkulima kuzalisha zao la zabibu. Hali hii inaliweka zao la zabibu katika hatari ya kufifia tena kama ilivyowahi kutokea nyuma wakati wakulima walipokosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara iwasaidie wakulima wa zabibu wa Mkoa wa Dodoma kwa kufuatilia kwa karibu sana mwenendo wa mwekezaji wa Kiwanda cha *CETAWICO* kwani ananufaika kwa jina la zabibu za Dodoma bila kuwajali wakulima wa zabibu hizo. Kwa ujumla, Serikali isimamie soko la zabibu za wakulima wa Dodoma. Pia Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia wakulima wa zabibu kuanzisha kiwanda cha kusindika zabibu pale kwenye mradi mkubwa wa shamba la zabibu lililopo Chinangali II kwenye Jimbo langu la Chilonwa, Wilayani Chamwino ambako zabibu ndiyo zao letu la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya uingizwaji wa bidhaa feki kutoka nje ya nchi. Je, Serikali imejipangaje kuzuia tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa viwanda Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma unafuga nyuki, unalima muhogo, ndizi, kahawa, maharage, mchikichi, lakini viwanda vidogovidogo vilivyopo hata havitoshelezi mahitaji ya uzalishaji. Katika Ziwa Tanganyika kuna samaki wadogo na wakubwa,

ukosefu wa dhana za uvuvi unasababisha uvuvi kuwa hafifu lakini pia ukosefu wa viwanda vya kusindika samaki kama vile vilivyopo Mwanza na maeneo mengineo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uhuru, Mkoa wa Kigoma kulikuwa na *ginnery* ya Pamba eneo la Kasuku ijulikanayo kama Kigoma *Ginnery* na aina ya pamba iliyokuwa inalimwa ilikuwa ni ya kipekee yenye urefu wa nchi moja na robo yaani *Grade B*; ya Kigoma ndio ilokuwa *Grade A,* ya Mwanza na ya Shinyanga, hivyo ni lini Serikali itafufua Kigoma *Ginnery* ili wakulima wa pamba Mkoani Kigoma waweze kutengeneza mafuta na vitu vingine Mkoani hapo?

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaunga mkono hoja hii ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Miaka ya nyuma, Serikali ilibainisha viwanda vya kubangua korosho Mkoani Mtwara na maeneo mengine nchini. Baadhi ya waliouziwa viwanda hivi hawavitumii au hawaviendelezi kwa matumizi yaliyokusudiwa na wengine wamegeuza kuwa maghala au wanavitumia kwa matumizi mengineyo. Hivyo naomba Serikali iwanyang'anye wakuhsika viwanda hivi na wauziwe wale ambao wana nia madhubuti ya kubangua korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Nanyumbu hakuna kiwanda cha aina yoyote, ingawa Serikali imejiondoa katika kumiliki viwanda, naiomba Wizara hii iwawezeshe vijana wa Wilayani ya Nanyumbu kwa kuwapatia viwanda vidogovidogo vya kubangua

korosho. Vijana hawa wakiwezeshwa kwa kupatiwa viwanda hivi, wataweza kujikimu kwa maisha na pia kuchangia pato la Taifa. Aidha, nitashukuru kupitia mchango wangu huu Wizara ikaniambia ni taratibu gani za kufuata ili kuweza kupata viwanda hivi kwa njia ya msaada au vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wengine kwa kuandaa hotuba nzuri na mpango wa bajeti wa mwaka 2012/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Wizara iandae mpango mkakati wa viwanda Tanzania. Mkakati ulenge kufufua viwanda vya nguo, nyama, ngozi, korosho, kahawa, chai na mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuwe na *Vallue addition* kwa kila kinachozalishwa nchini ili kiuzwe kwa faida ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara iandae *Human Resource Development Plan,* ili vijana waandaliwe, wapate *skills* na *exepertise,* waweze hata kufanya kazi kwenye *assembly plant* na magari ya Toyota tunayotumia sana nchini yatafutiwe uwekezaji na Toyota kuombwa kufungua Kiwanda cha ku-*assemble* magari Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Wizara ikamilishe na kufungua *EPZ* chache hata mbili tu kwa kuanzia ili thamani ya *EPZ* ionekane. Aidha, *potential* iliyopo katika sekta na viwanda vya ngozi iwe *tapped* na manufaa yaonekane kwa wafugaji, wadau wa zao hili na kwa Taifa. Wizara ya Viwanda na Biashara ikishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kuongeza ushuru wa ngozi ghafi iuzwayo nje kutoka asilimia 40 mpaka 90 na hatimaye kupiga marufuku kuuza ngozi nje ili kujenga uwezo wa viwanda vya ndani na kuongeza mchango wa sekta katika pato la Taifa.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Viwanda na Biashara. *Concern* yangu kwa suala la viwanda hapa Tanzania ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hasa vya kusindika mazao, ni muhimu sana kwa Taifa letu kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao yetu na kutengeneza ajira kwa makundi mbalimbali. Viwanda vya pamba kule Mikoa ya Kanda ya Ziwa, viwanda vya kusindika chai, viwanda vya kubangua korosho vilivyoko kule Mtwara, Lindi na Tunduru na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani na viwanda vya kusindika bidhaa nyinginezo, vyote hivi ni muhimu sana kwa Taifa letu, ni vema Wizara ya Viwanda na Biashara sasa ijipange kuhakikisha kwamba, viwanda vyote hivyo vikubwa na vidogo vinafanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao yanaposindikwa, huongezwa thamani na hivyo kuongeza hata bei ya zao hilo kwa wakulima wenyewe kule vijijini. Viwanda vingi hapa nchini vilibinafsishwa na vingine viliuzwa kabisa na vingine kukodishwa na vitu vya namna hiyo. Hali hii imeleta shida zaidi katika maeneo mengi, wananchi wamekosa ajira, mazao yetu hayapati bei nzuri na mambo mengine kadha wa kadha ambayo yote hayo ukiyahesabu ni hasara kwa wakulima na Watanzania wengine waliokuwa wanatarajia ajira kutoka katika viwanda hivyo na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya korosho vya Mkoa wa Lindi na Mtwara viliuzwa (kwa maana ya kubinafsishwa) kwa makubaliano kwamba viwanda hivi vitaendelea kufanya kazi hiyohiyo ya kubangua korosho. Tangu viwanda hivi vibinafsishwe miaka ya 2000 mpaka sasa viwanda hivi havijaweza kufanya kazi iliyotarajiwa na hivyo kupoteza ajira ya wakazi wengi wa Mikoa hiyo na kusababisha pia bei ya zao la korosho katika Mikoa hiyo kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali ni kuwa isimamie viwanda hivi kuhakikisha kwamba vinarudia kufanya kazi yake kama mwanzo, ama zaidi ya mwanzo. Visingizio vingi vinavyotolewa na hawa matajiri walionunua viwanda hivi vya kubangua korosho ni vema vipuuzwe na badala yake Serikali iwahimize na kuwasimamia kwa karibu kuhakikisha viwanda hivyo vinafanya kazi yake ya kubangua korosho. Kama kuna mfanyabiashara amenunua Kiwanda cha Korosho na imeonekana hawezi kufanya kazi hiyo ya ubanguaji wa korosho hivyo ni vema

viwanda hivyo virudishwe Serikalini na Serikali iangalie utaratibu mwingine wa kuendesha viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya korosho Mikoa ya Kusini vikiweza kufanya kazi, nina imani asilimia 100 ya bei ya zao la korosho litapanda sana na ajira itapatikana kwa vijana wetu na wananchi wengine na hivyo kuwafanya wananchi wa maeneo hayo kujikwamua kiuchumi. Mpango huu wa kufufua viwanda utekelezwe nchini kote kwenye viwanda mbalimbali. Kama haya yatafanyika, nina imani *impact* yake kwa wakulima wengi na wananchi wengine itaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia Wizara iliyo mbele yetu. Kwanza napenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Rais kuendesha Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nathubutu kusema sasa ni wakati muafaka kwa Waziri na Naibu Waziri kuimarisha viwanda vilivyopo na kufufua viwanda vilivyokufa kwani kama tutafufua viwanda vilivyokufa ni wazi kwamba vijana wengi watapata ajira na kupunguza idadi ya vijana ambao hawana ajira. Pia vitamkomboa mkulima wa Tanzania na kuongeza thamani ya mazao yake na pia nashauri kwa vile walioua viwanda wapo na wanatesa huku nchi inapata hasara, wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama Kiwanda cha nguo cha Urafiki, tayari Serikali iliweka pesa katika kiwanda hicho baada ya kufilisika, lakini hivi karibuni Serikali inaamua kutaka kutafuta mwekezaji mwingine hata deni bado halijaisha kulipwa. Namwomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, anifahamishe suala la kumpa mwekezaji kiwanda cha nguo cha Urafiki umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Watanzania jambo kubwa ni kufufua viwanda, angalia Kiwanda cha Ngozi, Mwanza, kiliuzwa kwa sababu zisizo za msingi na baadaye kugeuzwa ghala la mnunuzi. Napenda kujua ni lini Kiwanda cha Ngozi kilichoko Mwanza kitarudi na kuanza kufanya kazi pamoja na Chuo cha Ngozi kilichopo hapo, sasa kitaanza kazi lini Ili wafanyabiashara wa ngozi waweze kuuza ngozi hapo kiwandani kuliko kuuza ngozi ambazo hazijasindikwa. Kiwanda kipo karibu na ziwa na mashimo ya maji taka yapo hapohapo karibu na Ziwa Victoria. Haya ni matokeo ya ubinafsishaji ambao tulidhani yatatukomboa kumbe ni kuwafaidisha, angalia kiwanda cha nguo cha Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa ni lazima Serikali ichukue hatua za makusudi kutafuta mashine ndogondogo na kuzifunga katika Mikoa ambayo inazalisha matunda zaidi kama Mkoa wa Mwanza na Geita, kuna matunda ya kutosha ambayo kama tutapata viwanda vidogo vya kukamua juisi, vijana watapata ajira na wakulima watapata pesa za kuendeleza maisha yao. Hivyo kauli mbiu ya Chama cha Mapinduzi ni “Maisha Bora kwa kila Mtanzania”

yanaweza kupatikana na sio hadithi tu bila vitendo. Ni lazima tuamini Wizara hii ndiyo yenye ajira za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi yoyote ile hutegemea viwanda, Serikali imezingatia ama kujenga ama kufufua viwanda mijini bila kufikiria kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wako vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya vijiji nchini wana mifugo mingi ikiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika, pamoja na matunda kama maembe, mananasi na kadhalika, kwa nini Serikali haijengi viwanda vidogovidogo vijijini kwa ajili ya kukausha nyama na matunda, *technology* ambayo ni rahisi kufanyika na vilevile inaweza kutupatia fedha za nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna soko kubwa la nyama na matunda yaliyokaushwa nchini Marekani, kwa nini Serikali yetu isitumie nafasi hii kuwapatia vijana ajira na vilevile kulipatia Taifa letu fedha za kigeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kutumia muda huu kuchangia kwa maandishi Wizara hii nyeti katika Taifa letu. Aidha, nimshukuru Mungu kwa mema yote aliyonijalia kwa siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda katika nchi yetu vimeshuka sana kiasi cha kuufanya uchumi wa nchi yetu sasa kuyumba na kutegemea vya wenzetu. Tanzania tulikuwa na viwanda vingi, lakini mpaka sasa hivi vingi havifanyi kazi mfano *General Tyre*, *Urafiki, Mwatex*, *Sunguratex* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa upana wa ajira umekosekana na uchumi mkubwa sasa tunapeleka nje, suala hili ni pana limepotezwa na dhana ya ubinafsishaji. Hakuna kitu kizuri kama kuwa na viwanda nchini vinavyofanya kazi, vinavyozalisha na vinajiendesha, mfano kama tukiwa na umeme unaozalishwa nchi nzima na Serikali ikafungua viwanda vidogo vidogo vingi nchini tatizo la umaskini litapungua kwa kiwango fulani na ajira zitakuwepo nyingi. Tunahangaika Tanzania kwa sababu hatuna ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa kuwa na maarifa ya ziada (ubunifu) kwani tunazo rasilimali za kutosha, mali tumezikalia huku tunaziangalia tu, vijana ili wapate ajira ni wakati sasa wa Serikali yetu kupitia Wizara hii iweke viwanda vidogovidogo kwa kuishirikisha *SIDO*. Mfano tuna ng'ombe Mikoa mingi ya Tanzania lakini Watanzania hatuna utamaduni wa kutumia maziwa kuzalisha bali tunakunywa kidogo kwa mzaha. Lakini viwanda vidogo vikizingatiwa, tutasindika ngozi na kutengeneza wenyewe viatu, mikoba ya kisasa, mikanda na vinginevyo bila kutamani vya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa ya kusindika, pia nyama za kusindika tutazalisha badala ya kutamani nyama za kopo toka nje, kupitia kilimo nchi yetu

tumejaliwa matunda kila Mkoa, tuna embe kwa wingi (Katavi) tuna miwa, tuna machungwa na mengine mengi, vivyo hivyo Mikoa mingine mingi nchini kwa nini tusizalishe *juice* kwa wingi na kwa ubora, mpaka tutamani juice za nje kwa kudhani kuwa ndiyo bora? Hapana, Tanzania tukiamua tunaweza sana na tunaweza kuokoa wimbi kubwa la vijana wasio na ajira wakapata ajira kwani wimbi hili la vijana wasio na ajira baadaye watalitesa sana Taifa hili la Tanzania watakapobadilika na kuwa vibaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Wizara hii sasa iamue kufungua viwanda vidogovidogo hasa Mkoa mpya wa Katavi ambao hauna kiwanda hata kimoja na una rasilimali nyingi kama madini dhahabu, shaba na kopa. Kuna matunda kama miwa, embe na machungwa, je, tukipata kiwanda hatuwezi kuliingizia pato Taifa letu? Je, hatuwezi kupunguza kero ya ajira kwa vijana? Mali tunazo lakini tumezikalia, tunanunua *juice* kutoka nje huku matunda yetu yanaliwa na ndege na kuoza bure. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kwa hali hii? Naomba anijibu wakati wa majumuisho suala la kuanzisha viwanda vidogovidogo, hatuoni ni busara kuwa maskini wa kutupwa huku maziwa tunayo, bahari tunayo, mito tunayo na inazalisha samaki wa kutosha lakini tunanunua samaki wa kwenye makopo toka nje, tuna mimea ya mianzi kwa wingi lakini *stick* za kuchokonolea meno tunanunua makopo yake yana chata ya china, ni aibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa kujipanga sasa kwani nchi yetu bila uchumi imara hatuendi.

Tunahitaji sasa baadhi ya wanawake tuliopitia mafunzo ya usindikaji wa vyakula mbalimbali tusibweteke, bali tutumie elimu tuliyoipata kuzalisha bidhaa kupitia malighafi tulizonazo pia viwanda vidogovidogo vya Tanzania yetu hatutaki kununua kitu kama *jam* ya kupaka kwenye mkate kutoka nje na wakati machungwa na manasi tunalima wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe Waziri/Serikali kwamba Mkoa wa Katavi tunaomba kuletewa *SIDO* ili tubadilishe mfumo wetu wa uchumi ili kupunguza umaskini au kuuaga kabisa, uwezo tunao, nia tunayo ila mwanzo mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu katika Sekta ya Viwanda. Nchi zote zilizoendelea ziliwekeza ipasavyo katika viwanda vikubwa, vya kati na viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya maji. Moja ya sababu ya kuwa na nguvu kazi imara yaani watu ni lazima tuwe na watu wenye afya nzuri. Kwa sasa hivi hapa nchini sio sehemu zote zenye kuweza kupata maji safi na salama ya kunywa tukianzia hata na Jiji letu la Dar es salaam ambalo lina wakazi zaidi ya milioni tatu. Kwa sasa hivi watu wengi wamekuwa wakinunua maji ya chupa kwa matumizi ya kunywa siyo wengi wanaochemsha na hii inasaidia kuondokana na magonjwa ya mlipuko ya kuhara kama kipindupindu,

*typhoid* na kadhalika. Hivyo Wizara hii ni wajibu wao kulisimamia hili, viwanda vinavyozalisha maji ya kunywa viondolewe kodi ili watu wengi zaidi waweze kutumia huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha *General Tyre* Arusha. Mpaka sasa hivi ni nini hatua ya kiwanda hiki ambacho kilikuwa kinazalisha matairi yenye ubora? Ajali nyingi Tanzania zinatokana na matairi yanayoingia nchini yasiyo na ubora na hivyo kupasuka ovyo na kuleta ajali. Kamati ya *PAOC* iliunda Tume na kutoa ripoti yake, je, ni kwa kiasi gani ripoti ilifanyiwa kazi? Nini hatua ya wafanyakazi wa kiwanda cha *General Tyre*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa na havifanyi kazi. Kuna baadhi ya viwanda vilibinafsishwa na havifanyi kazi kabisa na vingine vimebadili kabisa kazi ya awali na kufanywa stoo za kuhifadhia bidhaa. Mpaka sasa hivi ni nini hatua ya kiwanda cha Tanganyika *Parkers,* kilikuwa kinazalisha vigae vizuri, nyumba za wafanyakazi zilijengwa nzuri kwa sasa hivi inasikitisha pale kiwandani pamekuwa ni uwanja wa michezo tu sijui vile vipuri vilivyokuwa ndani vimeishia wapi? Pia kuna migogoro ya ardhi (kiwanja) cha Tanganyika *Parkers,* kuna wavamizi waliojenga pale, je, zile nyumba mpaka sasa hivi nani anazimiliki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Magunia, Moshi. Je, nini hatua ya kiwanda hiki pamoja na kiwanda mama cha *Machine Tools* kilichopo Hai, kwa sasa vipuli vimeshapitwa na wakati hivyo lazima vipandishwe hadhi au kununua kila kitu kipya lakini

Serikali imekuwa ikitafuta mwekezaji zaidi ya miaka 10, je, mchakato huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora. Bado limekuwa ni tatizo kubwa kwa bidhaa zisizokidhi viwango kuingia nchini na hii imepelekea baadhi ya viwanda vyetu hapa nchini kufa au kupunguza mauzo na hatimaye wananchi wetu kukosa ajira na juu ya hapo hata baadhi ya bidhaa hizo kuleta madhara kwa watumiaji mfano kiwanda cha viberiti cha *KIBO MATCH*, kilichopo Moshi. Kiwanda kile hali yake ni mbaya kimauzo kwa sababu vipo viberiti vingi vinaingia nchini tena havikidhi viwango, vinauzwa kwa bei nafuu sana, sasa wanakuwa hawawezi kushindana na wafanyabiashara hao. Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda viwanda vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika yaliyo chini ya Wizara - *SIDO*. Shirika hili limekuwa ni mkombozi kwa wajasiliamali wadogo kwa kuwawezesha kupata mitaji na vitendea kazi lakini bado Serikali inahitajika kuwawezesha *SIDO* kwa kuwapa bajeti ya kutosha kutimiza malengo ya kuwawezesha wajasiliamali kufungua viwanda vidogovidogo kulekule vijijini, mazao yanakozalishwa ili yawe *processed* kule (kuongezea thamani) kule ili wakulima wapate faida zaidi na hii kwa kiasi kikubwa itapunguza vijana wengi kutoka vijijini na kukimbila mijini kutafuta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS,* pamoja na juhudi za *TBS* kujitahidi kukagua bidhaa zisizokidhi viwango bado tunaona katika maduka kuna bidhaa zisizokidhi

viwango. Ni jambo la kusikitisha katika Maonyesho ya Sabasaba kuna baadhi ya waliokuwa na bidhaa walikuwa wanauza pasipo na woga bidhaa zenye viwango na zisizo na viwango. Kama wafanyabishahara hawa waliweza kuuza bidhaa hizo pale uwanjani na *TBS* walikuwa pale, je, *TBS* wataweza kweli kudhibiti bidhaa hizi feki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lako Tukufu Serikali kupitia Wizara hii iliwahi kutoa majibu hapa Bungeni wafanyabiashara wanaouza mitumba hawaruhusiwi kuuza mitumba ya nguo za ndani lakini bila aibu nguo hizo bado zipo sokoni tena vijana wanaziuza mitaani waziwazi kabisa. Hivi *TBS* wanakuwa wapi, ina maana hawaoni watu hawa wasiofuata sheria?

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma kuna kiwanda cha Tumbaku ambacho kilikuwa kinaajiri watu 3000, kilisimama kwa ajili ya kuingiza mbia ambaye aliahidi kukiendeleza kiwanda hiki lakini hakutimiza ahadi na kukitelekeza kiwanda. Hivyo wenye hisa wakulima kwa kushirikiana na Bodi ya Tumbaku kuchukua hatua mbalimbali za kisheria hadi kurudisha kiwanda kwa wakulima sasa wapo katika mchakato wa kukifufua ili waanze kazi ya kusindika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Tumbaku imewasaidia kuwatafutia wataalam wa viwanda vya tumbaku na walikipitia na kutoa gharama ambazo zitakirudisha katika hali ya uzalishaji wa sasa. Pia iliwatafutia *guarantee* ya upatikanaji wa tumbaku

itakayokuwa inasindikwa pale. Sasa wapo katika hatua za kuomba mkopo *CRDB* baada ya kukubaliana wakope katika mkutano wa wana hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba wataalamu wa Wizara wawasaidie katika maandalizi ya andiko la mradi wa mkopo wa kiwanda ili wasiingiliwe na matapeli wakawachaji hela nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Nizungumzie kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la ubinafsishaji lilikuwa na lengo la kuboresha hali ya utendaji na uzalishaji. Baadhi ya viwanda vimeweza kuongeza tija, lakini vingi havijatekeleza mikataba vilivyongia na Serikali ya kuviendeleza. Mfano mzuri ni viwanda vya korosho vilivyopo Mtwara (1), Newala (2), Masasi (1), Lindi (1), Mtwara (1), Tunduru (1), Nachingwea (1), Kibaha (1) na *TANITA* Dar-es-Salaam (1). Jumla yake ni viwanda 10 havibangui korosho na Waziri alivitembelea, vyote havina dalili yoyote ya kufanya kazi iliyolengwa. Naiomba Wizara ya Viwanda na Biashara, kutekeleza Azimio la Bunge lililopitishwa la kuvirejesha viwanda hivyo kwa Serikali, ili kuweka mazingira mengine yatakayoviwezesha viwanda hivyo kufanya kazi. Uzalishaji wa viwanda hivi utatoa tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya mazao ya biashara. Kwa sasa wakulima wamekuwa wakiteseka kwa kukosa soko la uhakika la mazao ya biashara kama ufuta, korosho, pamba na kadhalika. Naishauri Wizara kufanya kazi kwa karibu na Wizara ya Kilimo ili juhudi za pamoja zifanyike kunusuru kuyumba kwa masoko ya mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri anayoifanya. Naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kubuni Soko la Kimataifa la Njia Panda (soko la mbogamboga) na Lokolova (soko la nafaka). Naipongeza Serikali, kwa mpango wake wa *EPZ* katika mradi wa Lokolova, mpango huu utasaidia sana kuleta maendeleo ya viwanda katika Jimbo langu la Vunjo na kuajiri vijana wengi wasiokuwa na ajira. Naomba wakati wa majumuisho, Waziri aeleze mpango kabambe wa Serikali wa kujenga soko hilo la Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Himo, kuna Kiwanda cha Ngozi cha *Himo Tinneries*. Kiwanda hiki kimekuwa kero sana kwa sababu kinatoa harufu ambayo inasumbua sana wakazi wa pale. Namwomba Waziri, atembelee kiwanda hiki aone jinsi anavyoweza kutupa ushauri wa kuondokana na kero hiyo. Wananchi wa Vunjo wanataka kiwanda hicho, lakini hawataki harufu yake.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa bajeti nzuri. Kwanza, nieleze masikitiko yangu kuwa viwanda ambavyo ni muhimu sana vimepewa siku moja tu ya kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, imeleta Sera nzuri ya Kilimo Kwanza ambayo imekubalika vizuri na wananchi lakini Serikali pia imebaini kuwa ili wakulima wapate mafao yanayofaa kwa ajili ya kurudisha nguvu za wakulima na kupata faida, ni lazima mazao hayo yatengenezwe ili kuongeza thamani. Kwa hiyo, hakuna ubishi kuwa ni lazima Wizara ya Kilimo, iwe *"linked"* na Wizara ya Viwanda na Biashara. Viwanda vidogovidogo vimekuwa muhimu sana katika kusaidia wakulima kuwaongezea kipato lakini bado wananchi wengi wamekuwa hawana uwezo wa kuwa na viwanda hivyo. Serikali ni lazima ibuni mbinu za kuwawezesha wananchi kupata mashine ndogondogo kwa bei nafuu na masharti rahisi. Mazao mengi sana yamekuwa yakiharibika, kama vile matunda na mbogamboga ambazo zingeweza kusindikwa, zingetoa mapato mazuri kwa wananchi na kutoa msukumo kuongeza uzalishaji kwa sababu sasa hivi bidhaa hizo huoza na kuleta hasara kwa wakulima. Tatizo kubwa ni pamoja na vifaa pia na utaalamu wa kuwafundisha wakulima wadogowadogo jinsi ya kusindika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi vya kati nchini vimekufa kwa kukosa masoko. Sheria ya Manunuzi imekuwa mbaya sana na inakandamiza viwanda nchini. Imeweka kima cha mwisho kwa fedha

za manunuzi kwa viwanda vya ndani shilingi milioni 800 bila kujali aina ya bidhaa. Hii imedidimiza viwanda, kwani kabla ya hapo manunuzi kutoka viwanda vya ndani ilikuwa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Hii inamaanisha, Sheria hii ya Manunuzi inatoa fursa zaidi ya uagizaji bidhaa nje kuliko bidhaa za kutoka kwenye viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji nchini umekuwa na vikwazo vingi sana ikiwemo kukosekana kwa umeme wa uhakika, bei kubwa ya umeme na maji, vyote havipatikani kwa urahisi. Kumekuwa na kodi nyingi kwa malighafi zinazoagizwa kwa ajili ya viwanda vyetu kuliko uagizaji wa bidhaa zilizokwishatengenezwa kutoka nje. Hii inasababisha bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini kuwa ghali kuliko zile zinazotengenezwa na kuletwa kutoka nje. Hali hii imevikumba viwanda vya madawa. Inasikitisha kuwa viwanda hivyo sasa vinauzwa na vingine kugeuza matumizi. Viwanda hivyo ambavyo vilikuwa vinachangia asilimia 30, sasa vinachangia asilima 20 tu; vingi viko kwenye hatari ya kufungwa. Tumeshindwa kutumia *"trips flexibility"* ambayo sasa wanaokuja kununua viwanda hivyo watanufaika na kupeleka faida hiyo inayopewa Tanzania kwenda kwenye nchi zao.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa uteuzi wao. Pia kwa kuweza kuwasilisha hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2012/2013 na kwa ushirikiano mzuri na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kutoa ushauri, maoni na maswali juu ya utendaji katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ujenzi wa Soko la Matunda la Segera – Tanga. Bado wananchi wanasubiri ujenzi wa soko la Kimataifa la Matunda la Segera, kama ilivyodhamiriwa na Serikali zaidi ya miaka nane iliyopita. Je, mkakati huo umefika wapi hadi sasa? Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, imetenga eneo kwa ajili ya matunda muda mrefu bila kuwepo uhakika wa ujenzi. Soko la aina hiyo litasaidia kusimamia mauzo ya matunda nje, litasaidia ubunifu wa vifungashio (*packaging)* kwa usafirishaji wa matunda na pia kusimamia mfumo wa bei na kuwezesha nchi kupata mafao makubwa. Jitihada za kutafuta wawekezaji na kujenga uwezo wa Kitaifa uimarishwe ili kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Matunda – Muheza (Ahadi ya Mheshimiwa Rais). Napenda kufahamu kama Wizara ya Viwanda na Biashara inafahamu kuwepo kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya kuisaidia Muheza kuwa na Kiwanda cha Kusindika Matunda tangu mwaka 2005? Napenda kurudia kuthibitisha kwamba ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwapeleka wawekezaji wakatembelea mashamba ya machungwa, walitaka kujenga kiwanda kikubwa sana lakini hawakuridhika na kiwango cha uzalishaji kwa uwezo wa kiwanda chao. Je, Wizara inafuatilia ahadi

ya Rais na/au kumkumbusha Mheshimiwa Rais, juu ya dhamira ya kuisaidia Muheza na wakulima wa matunda wa Muheza kupata kiwanda kwa usindikaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* walisaidia kikundi cha akina mama kusindika matunda lakini kwa kiwango kidogo na mashine nyingine kutofanya kazi. Napenda kuikaribisha Wizara ya Viwanda na Biashara kufika Muheza, ili kuona mazingira ya kiwanda kidogo kilichopo na kupata mwanga wa kuendeleza jitihada za kuwepo kwa kiwanda cha usindikaji Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, miradi ya mashine za kukamua miwa. Tarafa ya Amani inazalisha miwa mingi sana na inasafirishwa kwenda Dar es Salaam. Naiomba Wizara ya Viwanda na Biashara, itume wawakilishi kuona maeneo ya mashamba hayo ya miwa na kushauri vikundi vya wakulima kutambua kuwepo kwa mashine ndogondogo zenye uwezo wa kusindika/kukamua miwa ili kutengeneza sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, uendeshaji wa shamba la mpira Kihuhwi *(Kihuhwi Rubber Plantation Muheza)*. Baada ya wawekezaji wa Kisomali kuingia mikataba ya kuendeleza shamba hilo kushindwa, *NDC* imekuwa ikisimamia shamba hilo na yupo mwekezaji mpya tangu mwaka 2009/2012. Kwa kweli mwekezaji huyo kama wale wa awali ni wavunaji tu wa mpira na uwekezaji kwa upandaji wa miche mipya ni wa kiwango kidogo sana. Pamoja na hali hiyo, mwekezaji amekuwa hatoi takwimu sahihi za uvunaji na kuvutana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza juu ya ulipaji wa ushuru halali. Tunaiomba Wizara kupitia *NDC*, iisaidie

Halmashauri kwa kuipa malipo yake na kuisaidia kujenga mahusiano mazuri kati ya mwekezaji, wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, madai ya mafao ya wafanyakazi wa shamba la mpira Kihuhwi. Inasikitisha sana kuona amri ya Mahakama ya kutaka wafanyakazi wa shamba la mpira Kihuhwi kulipwa, haijatekelezwa tangu mwaka 2001/2002. Wizara ya Viwanda na Biashara imekuwa inatoa ahadi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu mwaka 2005-2011, kuwa itafuatilia malipo hayo na kumtafuta mwekezaji Msomali aliyekuwa akiendesha shamba hilo kwa mkataba kati yake na Serikali bila hata kutoa taarifa ya hatua zilizofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho Wizara iliniandikia barua mwaka 2010/2011 kuwa Wizara imewasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje, ili kufuatilia mwekezaji huyo nje ya nchi, lakini hakuna taarifa ya maendeleo. Wizara, iliahidi kuwalipa wafanyakazi hao ili kutekeleza amri ya Mahakama lakini hadi leo hakuna utekelezaji. Nashauri tuwatendee haki wananchi kwa kuwa hawana uwezo wa kuvuka mipaka ya nchi kwenda nchi jirani kumtafuta mwekezaji aliyeingia mkataba na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ekta ya Viwanda na Biashara ni sekta muhimu sana kwa maisha ya kila siku lakini hadi sasa Tanzania, hatujatoa kipaumbele katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na viwanda vya kutosha na masoko yenye uhakika ili kutoa ajira za kutosha kwa akina mama na vijana na kuingiza pato kwa Taifa na kuongeza kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie viwanda vya korosho ambavyo viliuzwa kwa watu binafsi tukitarajia kuwa wangeweza kuendeleza ubanguaji wa korosho na kuuza nje na kupata fedha za kigeni ambazo zingeweza kunufaisha shughuli za maendeleo nchini na kukuza uchumi. Lakini matarajio yetu yamekuwa kinyume, viwanda hivi havibangui tena korosho bali wamegeuza maghala ya kuhifadhia mazao. Wanatoza fedha nyingi hivyo kujinufaisha wao wenyewe na Serikali hakuna manufaa yoyote ambayo inayapata. Lakini si hivyo tu, hata vipuri vingi vimeng'olewa katika viwanda hivi na kuuzwa kama vyuma chakavu. Katika suala hili, naomba kuishauri Serikali ichukue jukumu la kuyarejesha majengo haya mikononi mwake kuliko kuyaacha kwa watu wachache kwani wamekiuka makubaliano na nia ya Serikali ya kuuza majengo au viwanda hivi kwa lengo la kuendeleza ubanguaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mtwara, akina mama wengi wamekuwa wakiendeleza ubanguaji wa korosho kwa teknolojia duni sana, lakini wengi wamejiajiri kwa ubanguaji na wamekuwa wakiuza korosho zao ndani na nje ya Mkoa, japokuwa

masoko ya korosho zilizobanguliwa ni mengi sana. Lakini akina mama hawa wanashindwa kuzalisha zaidi kwani mitaji yao ni duni na hawana nyenzo za kisasa za kuweza kuzalisha vya kutosha. Naiomba Serikali iwawezeshe akina mama hawa wajasiriamali vifaa pamoja na mashine za kubangulia korosho na mashine za kufungia korosho ili waweze kumudu soko la ndani na la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia biashara za bidhaa zinazotoka nje na kuingizwa hapa nchini. Bidhaa nyingi zilizopo sokoni, nyingine hazina ubora hivyo nchi yetu imekuwa kama ni *dampo*. Hivyo, naomba tuangalie sana suala hili maana linaua soko la bidhaa zetu za ndani. Wakati umefika sasa kwa Serikali kuwa na mipango madhubuti ya kufufua viwanda vyetu na kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa bei nafuu ili kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba niunge mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuzungumzia viwanda vidogo vya *SIDO*, ambavyo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa wananchi. Hivi ni viwanda vinavyosaidia kufanyika kwa *processing* ya bidhaa zetu nyingi zinazozalishwa nchini. Pesa wanazotengewa *SIDO* ni kidogo mno ukilinganisha na umuhimu wake kwani mbali na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kuhusu uzalishaji wa bidhaa zenye ubora ili kuhimili ushindani, lakini pia jukumu lingine ni kuendelea kuviboresha

viwanda hivyo vidogo vinavyotoa ajira kwa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS*. Jukumu la *TBS* ni udhibiti wa bidhaa zisizo na ubora. Bado udhibiti wake ni mdogo, vitu vingi visivyo na ubora vimejaa sokoni vikiwemo vyakula, vipodozi na vifaa vingine vya umeme. Hali hii ni hatari kwa nchi yetu na madhara makubwa yanatupata sisi wananchi tunaotumia bidhaa hizo. *TBS* wafanye kazi yao kwa umakini ili wanusuru maisha yetu. Kuna tabia iliyojengeka ya kumuuliza mteja kama anataka bidhaa halisi *(original)* au feki (zisizo na ubora).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa viwanda vyetu. Serikali inatakiwa kuvilinda viwanda vyetu vya ndani kwa kuweka kodi kubwa kwenye bidhaa zinazotoka nje ili bidhaa zetu zinazozalishwa nchini zipate soko la uhakika nchini. Hali hii itasaidia viwanda vyetu kuendelea. Vilevile bidhaa zisizo na ubora zinazoingia nchini zitakosa soko, hivyo zitapungua kuingia. Kwa mfano, sasa hivi Tanzania inaagiza asilimia 60 ya mafuta ya kula kutoka nje; kama kodi kubwa ikiwekwa kwenye mafuta hayo kutoka nje, hali hii itasaidia wakulima wa Tanzania kuzalisha kwa wingi karanga, ufuta, mchikichi, alizeti na mbegu zingine zinazotoa mafuta na viwanda vyetu vitaendelea, hivyo ajira pia itapatikana nchini kwetu pamoja na ulinzi wa viwanda vyetu kupatikana. Tuanze sasa inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha *General Tyre.* Ni vema sasa *NDC* waliopewa kusimamia kiwanda hiki wawezeshwe ili kifufuliwe haraka kianze

uzalishaji, kwani walikuwa wazalishaji wa matairi bora Afrika Mashariki. Hali hii itasaidia kupunguza tatizo lililopo sasa la matairi hafifu kutoka China, yanayosababisha ajali kila kukicha na Watanzania wengi wanaendelea kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha nguo cha Urafiki na viwanda vingine kama *MWATEX.* Kwanza Serikali, ieleze juu ya matumizi mabaya ya *USD* millioni 27 zilizotolewa na Serikali za kuboresha kiwanda hiki na ieleze ni nini hatma ya kiwanda hiki pamoja na viwanda vingine ambavyo sasa havifanyi kazi, mashine zimeng'olewa na kuuzwa kama vyuma chakavu? Ni nini hatma ya nyumba za viwanda hivyo na majengo kugeuzwa maghala na kupangishwa watu wafanyie biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, haioni kuwa pamba inazalishwa nchini, ni vema tufufue viwanda ili tuzalishe nguo nchini badala ya kuuza pamba ghafi na matokeo yake tunategemea mavazi kutoka nchi nyingine? Hivyo tunaendeleza viwanda vya nje na ajira nje, wakati Tanzania tuna tatizo la ajira na viwanda.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Sekta ya Viwanda na Biashara. Ni sekta muhimu ambayo inaweza kukuza uchumi wa nchi kwa ajili ya pato la Taifa lakini pia ajira kwa vijana na pato la mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha kiwanda kinachoitwa *Kilimanjaro Machine Tools*. Kiwanda hiki

kilikuwa kinatengeneza vipuri kwa ajili ya mashine za viwanda vingine nchini. Ni miaka zaidi ya 15 kimefungwa na hakifanyi kazi. Eneo lililopo kiwanda hicho ni ekari 627; nina taarifa isiyo rasmi ya Serikali kwa kupitia *CARMATEC* ya Arusha kufanya sehemu ya eneo hili iwe *Assembly line* ya matrekta. Naipongeza Serikali kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kabisa eneo litakalobakia, likatengwa eneo moja likawa *foundry* kwa ajili ya kutengeneza spea za *tractor* zitakazotengenezwa katika kiwanda cha *tractor*. Hata hivyo, majibu ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara juzi kuwa mashine ziko *intact,* yanaweza yasiwe ya tija kwa sababu mashine nazo zinachoka, zina-*depreciate.* Mashine zile zimepitwa na wakati na tukumbuke mahitaji ya Watanzania yanabadilika, mahitaji ya soko na kadhalika. Naishauri Serikali atafutwe mbia tajiri, ambaye pamoja na mambo mengine atabadilisha mashine zile aweke mpya kwa ufanisi zaidi. Ukiwepo ufanisi katika uzalishaji, ajira na pato la Taifa vitapatikana. Eneo la pili litakalobaki, Serikali, pia itafute mbia ajenge viwanda vidogovidogo ili vijana wetu wapate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine ni Kiwanda cha Magunia Mjini Moshi. Kiwanda hiki kimefungwa miaka mingi. Uwezo wa mwekezaji wa kiwanda hiki wa kutengeneza magunia ya katani ni magunia milioni tano na laki (5,500,000/=). Mahitaji ya magunia nchini ni milioni 62 (62,000,000) kwa mwaka. Hata hivyo, mahitaji ya magunia hayako *uniform*, yapo mazao yanaweza kutumia *Jute* na *Sulphate*. Kuna

mengine yanaweza kutumia magunia ya katani, mfano kahawa, mahindi, korosho na maharage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, mwekezaji huyu apewe dhamana ya Serikali *(monopoly)* atengeneze magunia kwa ajili ya *National Food Reserve Agency.* Tukifanya hivyo, viwanda vyote vya magunia Morogoro, Moshi na kwingineko vifunguliwe, pato la Taifa lipatikane, ajira ipatikane, lakini pia *promotion*/hamasa kubwa ifanyike kwa wakulima wa katani nchini; Serikali ilinde viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha tatu, ni *Kibo Match* kilichoko Moshi. Kiwanda hiki kinatengeneza viberiti kwa kiwango kidogo. Sababu za kutengeneza kiwango kidogo ni Serikali kuwaruhusu wafanyabiashara kuagiza kutoka nchi za nje (wanachoita *raw material*) yaani njiti na baruti, ambao kwa kiwango kikubwa wanadanganya wanaagiza mali ambazo ni *almost refined/finished.* Wafanyabiashara hawa wanalipa *import duty* asilimia 10 badala ya asilimia 25 wakati *Kibo Match* wakitengeneza bidhaa wanalipa *VAT* asilimia 18. Kwa mtindo huu, *Kibo Match* inashindwa kutokana na ushindani mkubwa unaotokana na punguzo la kodi kwa wafanyabiashara. Naishauri Serikali, irudishe *import duty* ya kuagiza njiti na baruti ya asilimia 25 badala ya asilimia 10, ili kulinda kiwanda ambacho kikifanya kazi kwa *full capacity,* kitatoa pato zuri la Taifa, lakini pia ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili linalokwamisha *Kibo Match* ni upatikanaji wa mbao. *Allocation* ya mbao kiwanda hiki kinachopata kutoka Idara ya Misitu Kilimanjaro (Msitu wa Rongai - Rombo na msitu wa West Kilimanjaro – Siha, ni kidogo, *allocation* nyingine wanapewa wafanyabiashara. Kwa *Kibo Match* kwenda kuchukua mbao *Sao Hill,* inakuwa ghali na *production cost* ya kiberiti inaongezeka sana na mwisho wa siku kushindwa kuuza kiberiti hicho. Naishauri Serikali, itoe *allocation* ya kutosha ya mbao kwa *Kibo Match* kutoka misitu hiyo ya Rongai na *West Kilimanjaro*, ambayo iko karibu na kiwanda. Wafanyabiashara waende *Sao Hill* kuchukua mbao kwa ajili ya biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* imekuwa mkombozi wa wafanyabiashara ndogondogo kuwakopesha mashine za biashara ndogondogo. Kwa mfano, mashine za kupasua mbao, mashine za kusaga, mashine za kusindika matunda na kadhalika. *SIDO* inatoa mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu *entrepreneurshisp*, masoko, usindikaji, na kadhalika. *SIDO* inatoa mikopo midogomidogo kwa vikundi vya wanawake wafugaji, wakulima na wafanyabiashara, jambo ambalo linawainua kiuchumi. Kuiwezesha *SIDO* kifedha, ni ukombozi kwa Watanzania na hususan wanawake. Naishauri Serikali, kuangalia namna yoyote kuongeza fedha kwa *SIDO* ili ifanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aki-*wind up,* anipe majibu kuhusu viwanda nilivyovitaja hapo juu na baada ya hapo nitaunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika haya yafutayo:-

(i) Je, Serikali, kupita Wizara hii inasema nini kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havizalishi kuvirudisha Serikalini ili vifufuliwe kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla?

(ii) Kuna mikakati gani ya kufufua viwanda vya nguo kama *MWATEX* ili wakulima wa pamba waweze kuuza pamba yao katika viwanda hivyo na kuondoa migongano na Serikali?

(iii) Je, kuna uhalali gani wa kuwaruhusu watu wenye asili ya Kichina, kuja Tanzania na kufanya biashara ndogondogo ambazo zingeweza kufanywa na Watanzania wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la bidhaa na vifaa feki vya umeme ni jambo baya linalohatarisha maisha ya wanunuzi, kwa nyumba kuungua na mambo mengine mbalimbali, lakini cha ajabu *TBS*, Shirika la Viwango Tanzania, wanaruhusu kero hii kuendelea. Je, tatizo hili ni lini litapatiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya bidhaa za ngozi ambapo vinne vimekufa na vitatu vinafanya kazi kwa kusuasua, inapunguza kasi ya kuzalisha ngozi kwa wafugaji. Ngozi ghafi zinazonunuliwa ni asilimia 30 ya

ngozi zinazozalishwa. Wananunua ngozi ghafi, wanauza ngozi hiyo ikiwa ghafi, jambo ambalo ni tofauti na lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila eneo la maendeleo, Tanzania imekuwa ni wasindikizaji tu. Mfano:-

| Nchi | Viwanda vilivyojengwa | Viwanda vilivyohai |
|---|---|---|
| 1. Ethiopia | 25 | 23 |
| 2. Sudan | 18 | 18 |
| 3. Kenya | 8 | 8 |
| 4. Uganda | 5 | 5 |
| 5. Tanzania | 7 | 3 |

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya bandia vya mabati ya kichina vinafanya kazi kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu. Kwa mfano, kiwanda cha Mabati cha Kichina kilichoko Vingunguti, kinafanya kazi ndani ya Kiwanda cha Korosho; mabati yanauzwa kwa Tshs. 9,700/= hadi 11,200/= kwa bati moja lililo na migongo minne au mitano. Mabati hayana nembo ya *TBS* na hayana geji; inakuwaje unanunua bati haupewi risiti? Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na viwanda vya mabati ambavyo ni feki? Mabati yao yanapauka na yanatoboka haraka. Pia, kuna kiwanda cha mabati cha Wachina, ambacho hakiko rasmi; kiko nyuma ya Chuo cha Diplomasia, Kurasini, naomba Wizara ikifuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Korosho vya Kusini, Lindi na Mtwara, vilibinafsishwa kwa watu

binafsi lakini kwa masikitiko makubwa viwanda hivi vyote havifanyi kazi. Serikali ilikopa dola milioni ishirini katika mwaka 1970 – 1980 kujenga viwanda hivi, lakini vilibinafsishwa mwaka 1996 na kuuzwa kwa bei ya kutupwa. Je, Serikali, inasema nini juu ya kufufua viwanda hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyama Mbeya kilijengwa miaka 30 iliyopita lakini hakuna ng'ombe aliyechinjwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameahidi ikifika Desemba 2012, kitafanya kazi. Je, mkakati huo unaendelea vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimwa Dokta Abdallah Kigoda, Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiuitendaji. Huu ni mfano wa kuigwa, kwa maana hachoki na amekuwa mstari wa mbele katika kuliletea Taifa letu maendeleo. Lakini siachi kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Gregory Teu, kwa uwezo mkubwa aliouonesha kwa kipindi kifupi ambacho ameingia katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sote tunavyofahamu Wizara hii ni kioo na roho ya uchumi wa nchi yetu katika nyanja za kiuchumi. Majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni heri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kurahisisha utendaji wao.

Pamoja na hotuba kubeba karibu kila kitu na kujibu hoja nyingi, napenda na mimi nitoe mchango wangu katika hotuba husika japo kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wageni kuvamia maeneo ya vijijini na kushiriki ushindani wa biashara na wazawa, limekuwa sugu katika nchi yetu. Ni kheri sasa Serikali ikatoa mwongozo kuwa wafanyabiashara wageni waishie katika maeneo ya miji mikuu pekee ili kutoa fursa kwa wazawa ambao hawana mitaji ya kutosha, kumiliki na kuhimili uendeshaji wa biashara katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia sasa Wizara kupitia Balozi zetu wasaidie wafanyabiashara wa Kitanzania kwa kuwaeleza fursa zilizopo maeneo yao huko ughaibuni. Lakini pia watengeneze *link* kati ya wafanyabiashara wa nchini na nje ya nchi wanakotuwakilisha. Bidhaa nyingi ambazo tunazalisha zilikwama kupata soko la uhakika kutokana na kutokuwepo na njia madhubuti za kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya uvuvi yapewe kipaumbele ila napenda Serikali ichukue hatua zaidi kuimarisha viwanda vidogovidogo vya usindikaji mazao hayo ili kuinua thamani ya bidhaa lakini pia kuinua kipato cha wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mfumuko wa bei ni kubwa. Naishauri Serikali ichukue hatua za haraka sana kurekebisha mfumo wa uuzwaji wa bidhaa nchini maana soko linaelekea kumuumiza zaidi mlaji kutokana na ushindani usio na tija. Mfumo wa soko huria lisilo na

ukomo wa bei ni changamoto, hivyo, naishauri Serikali kuweka ukomo wa bei kama ilivyofanya kwa bidhaa za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kufufua viwanda ni mzuri na ninaipongeza sana Wizara ila ni vema sasa tukaiongezea mtaji *SIDO* ili iweze kukidhi mahitaji halisi kwa Taifa, ili kuongeza thamani ya mazao mbalimbali nchini. Pamoja na mpango huu, tuhakikishe tunapata namna bora zaidi kwa kufufua viwanda vyetu bila kutegemea wawekezaji wa nje ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa mzigo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla, hii pia inasababisha kelele nyingi kwa wasiofahamu maana. *SIDO* ipewe uwezo na mtaji kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo vya sukari ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa sukari nchini ambapo bei imekuwa kubwa ukilinganisha na fursa za kijiografia za nchi yetu pamoja na ukubwa wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote Serikali imekuwa ikihimiza sana kulinda viwanda vya ndani. Kimsingi hili ni jambo jema, lakini viwanda navyo viwe na dhamira ya kuwalinda wananchi pia. Katika hili pia, nastaajabu sana pale ambapo viwanda vinalindwa na kupewa upendeleo, lakini hawako tayari kulinda wananchi na wanachangia makusudi mfumuko wa bei nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ambavyo vinatosheleza uzalishaji kama vya chumvi, vinazalisha kwa wingi sana, ila bado tunaruhusu chumvi iagizwe kutoka nje; hii si sawa na tunauwa soko na viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa malalamiko na mkanganyiko usio na lazima, naishauri *TBS* ianzishe vituo vya ukaguzi wa magari hapa nchini, ili kutoa fursa za ajira, lakini pia kuongeza ufanisi katika ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za makusudi zifanyike katika ufufuaji wa viwanda vya korosho nchini, ikiwamo kuangalia namna ya kuiwezesha *SIDO* kutengeneza viwanda vya awali, ili kusaidia wananchi wengi kujifanyia wenyewe ubanguaji, lakini pia kukuza soko la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Mfumo wa Usajili wa Biashara. Ihakikishe sasa unaanzia ngazi ya Halmashauri ili kutoa wepesi na kupeleka huduma karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongezaji wa kodi kwa mafuta ya mitende uchukuliwe kwa uangalifu mkubwa, tukizingatia kuwa, wafanyabiashara wamewekeza nchini kwa kujenga viwanda ambavyo vinasafisha mafuta hapa nchini. Soko la mafuta ni kubwa, lakini wakulima hawawezi kufikia lengo la uzalishaji wa malighafi na kutosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kupokea maoni yangu, kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri, namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai huu nilionao hadi leo hii. Nikushukuru na wewe kwa jinsi ambavyo unaendesha vikao kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu yote, kwa hotuba na mikakati mizuri ya utekelezaji wa mwaka 2012/2013, lakini kwa utekelezaji wa mpango wa mwaka 2011/2012. Hotuba hii ina matumaini makubwa kwa wananchi na hasa wafanyabiashara, wakulima na hata wafanyakazi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa ni tajiri sana lakini ni maskini sana. Hauwezi kujiletea maendeleo ya haraka na makubwa kwa sababu bado haujawezeshwa kimiundombinu na vivutio kwa wawekezaji, hasa kutoka nje ya Mkoa, kuja kuwekeza kwa kujenga/kuanzisha viwanda na biashara za viwango vikubwa. Mkoa wa Rukwa, ni tajiri kwa vile una rasilimali zote ambazo zingewezesha Mkoa kuanzisha viwanda. Rasilimali hizo ni kama zifuatazo:-

| **Na.** | **Rasilimali** | **Aina ya Kiwanda** |
|---|---|---|
| 1. | -Mahindi<br>- Ngano | Kiwanda cha kusaga na kusindika unga |
| 2. | Madini ya kila aina | Kiwanda cha kuchimba madini na kuuza |
| 3. | Samaki wa Ziwa | Kiwanda cha kusindika:- |

| | | |
|---|---|---|
| | Tanganyika na Ziwa Rukwa | -Minofu ya samaki<br>-Samaki wenyewe<br>-Dagaa |
| 4. | Alizeti, Karanga na Ufuta | Kiwanda cha kukamua nakusindikamafuta (hayana *colesterol* |

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa uwezeshwe kwa kuleta umeme wa gridi ya Taifa na barabara zikamilike. Hivi ni vivutio vitakavyoukwamua Mkoa wa Rukwa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia hoja hii kwa kuiomba Serikali kufuta kabisa leseni za usafirishaji chuma chakavu. Biashara hii kwa kiasi kikubwa imekuwa ndio chanzo cha uharibifu wa miundombinu; mfano katika jiji la Dar es Salaam, wizi wa mifuniko ya chemba za maji taka, umekuwa tatizo kubwa na athari zake ni ajali zinazosababishwa na mashimo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa nyaya za umeme, mataruma ya reli na mabomba ya madaraja, yote haya yanatokana na biashara ya chuma chakavu. Hivyo ni ushauri wangu kwa Wizara, kuangalia jambo hili ili tuepukane na hasara ya mali na kukinga ajali ambazo zinasabishwa na biashara hii ya chuma chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara hii imekuwa ikipangisha Ofisi za Wizara katika majengo ya

*Water Front* pale Dar es Salaam, kwa thamani ya shilingi milioni 60 kwa mwezi, ambayo ni wastani wa shilingi milioni 720 kwa mwaka. Hizi ni fedha nyingi, hivyo pamoja na nia ya Serikali kuhamia Dodoma na hivyo kufanya Wizara zisiwe na uhalali wa kuendelea kujenga Ofisi katika Mji wa Dar es Salaam, ni ushauri wangu kwamba, uwepo uwezekano kwa Wizara hii kujenga Ofisi ndogo za Wizara hii katika Jiji la Dar es Salaam. Hii ni kwa sababu, Jiji la Dar es Salaam ndio mji mkubwa wa kibiashara katika nchi hii na itaendelea kuwa hivyo kwa muda mrefu kutokana na jiografia yake, hasa kutokana na kuwepo kwa bandari kuu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inamiliki asilimia 49 ya hisa katika Kiwanda cha Urafiki na kwa sasa kiwanda hiki kiko katika hali ya kuelekea kufa kabisa. Hivyo naishauri Serikali, ifanye juhudi ya kukifufua kiwanda hiki ili Watanzania wanaofaidika na ajira pale waendelee na ajira zao na pia, Taifa liweze kunufaika na pato litokanalo na uzalishaji kiwandani hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dokta Abdalla Kigoda, Mbunge, Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina, ambayo imetolewa asubuhi hii. Natamka kwamba, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Gregory Teu, Mbunge, kwa kazi nzuri anayoifanya Wizarani na hivyo kupata ufanisi wa kutosha, hongera sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikumbushe ombi la muda mrefu kwa Wizara kuhusu kusaidiwa kuanzisha *programme* ya viwanda vidogovidogo katika Wilaya ya Siha, Mkoani Kilimanjaro, ili kusaidia vijiji vyetu na hivyo kuwasaidia vijana na akina mama katika kupata ajira. Sisi kama Wilaya, tupo tayari kushiriki kwa dhati katika kuimarisha mpango huo na hii ni pamoja na upatikanaji wa ardhi ambayo itajengwa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia kusema tena kwamba, naunga mkono hoja hii, ahsante.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri na pia, ninawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizi, ninaomba nichangie machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu bidhaa bandia. Nchi yetu imeendelea kupokea bidhaa bandia kutoka nje, hasa bidhaa hizo zinatoka nchini China na kwingineko. Pia, bidhaa hizi zimeendelea kuuzwa katika maeneo ya Kariakoo na Wachina wenyewe; tulisikia kauli ya Serikali kupitia aliyekuwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa

Lazaro Nyalandu, kuwataka Wachina wote walioko Kariakoo, waondoke ndani ya mwezi mmoja lakini, hadi leo hii Wachina hao hawajaondoka na wanazidi kuongezeka. Serikali, inatueleza nini kuhusu hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, soko la mazao ya kilimo. Wilaya ya Karagwe, ni Wilaya inayozalisha mazao ya kilimo kwa wingi kama vile ndizi, mihogo, viazi, maharage, ulezi, karanga na kadhalika. Tatizo linalowakumba wakulima wetu hawa ni kukosekana kwa soko la uhakika nje ya nchi yetu. Naiomba Bodi ya Biashara ya Nje, itusaidie kutafuta masoko ya uhakika. Pia tunahitaji viwanda kwa ajili ya mazao ya mifugo hasa nyama, maziwa na ngozi. Serikali, ifanye chini juu kututafutia wafanyabiashara wa kuwekeza katika mazao ya mifugo hususan maziwa, kwani maziwa ya Karagwe ni mazuri sana lakini yanakosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, soko la *AGOA*. Soko la *AGOA,* lililenga kuwasaidia wananchi wetu kuuza bidhaa zetu huko Marekani, lakini umma mkubwa wa Watanzania, hawana uelewa wa kutosha kuhusu soko hili na bidhaa gani zinauzwa huko. Pia, utaratibu wa kufikisha bidhaa hizo huko Amerika, haujulikani. Ombi langu ni Serikali, itangaze kupitia Runinga, Redio na Magazeti, kuhusu soko la *AGOA*. Pia, semina itolewe kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu soko la *AGOA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Viwanda ndiyo njia

pekee ya kuweza kuinua uchumi wetu na kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa na sasa havifanyi kazi, virejeshwe Serikalini. Kutokana na kutofanya kazi sasa Serikali ichukue hatua ya makusudi ya kuvirejesha viwanda hivyo na itenge fedha za kuvifufua ili vianze kufanya kazi kwa manufaa ya Watanzania. Kuvirejesha viwanda pia kutafanya wakulima wetu wanufaike katika bei za mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maonesho ya Kimataifa, naungana na Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anatoa hitimisho la hotuba yake, anieleze ni namna gani wakulima wa vijijini wanashiriki maonesho ya kimataifa na wananufaika vipi na maonyesho hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali imeteua viongozi walioshiriki kufilisi nchi hii katika Shirika la Ndege? Mafisadi, watu wasio waadiifu na wasio waaminifu kwa nini wameteuliwa kuwa ndiyo viongozi wa shirika hilo? Hivi Serikali haiwaoni? Naomba maelezo.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania, kuna viwanda vingi vimefungwa bila sababu yoyote, haswa Mkoa wa Tanga; kuna viwanda vya Tembo – Korogwe

Vijijini, Kiwanda cha Chuma, Kiwanda cha Foma, Kiwanda cha Mbao, Kiwanda cha Blanketi na Kiwanda cha Mafuta na Sabuni. Kwa kuwa, tumepata Waziri mchapa kazi katika Wizara hii, ni lini viwanda hivi vitafunguliwa, kwani vimefungwa kwa muda mrefu sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wananchi wengi walikuwa wanapata kazi na Mikoa ilikuwa inaendelea kwa haraka, naiomba Serikali, iangalie viwanda ambavyo vinaweza kufunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa madini ya makaa ya mawe Mikoa ya Njombe na kwingineko nchini, kunaashiria umuhimu wa kisera na kiutekelezaji kuwa na viwanda unganishi kisekta (*backward and forward linkages).* Kilimo kikiunganishwa vizuri na viwanda na madini ya chuma, kitaongeza thamani nchini. Nini mkakati wa Wizara, Kisera, kujenga viwanda vinavyozalisha viwanda vingine (*Basic Industries*) nchini, ili kwa ubia *(PPP)* tuzalishe bidhaa mbalimbali na kuziuza nchini na nchi jirani na uchumi kukua kwa kasi kubwa zaidi, pamoja na kuzalisha umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeweka mikakati ipi kisekta ili kuongeza thamani ya vito na madini yetu hapa nchini kama vile almasi, *tanzanite*, *emeralds*,

*zincon*, zikatwe hapa nchini na kuongeza ajira badala ya kukatwa Japan, India au Thailand na kwingineko? Dhahabu inatumiwa kwa kuwekewa vito *(mounting)*, hivyo basi upo umuhimu wa Wizara hii na Wizara ya Nishati na Madini kushirikiana ili dhahabu nayo iongezewe thamani na ubora hapa nchini na kutumika katika utengenezaji wa vito, kama vile pete, mikufu, bangili na hata shanga na kuziuza hapa nchini ama kuzisafirisha nchi za nje na kupata fedha nyingi za kigeni na kuwezesha ajira kupatikana kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubia na makampuni na maduka makubwa duniani unaweza kufanyika na makampuni ya ndani, kama sera zetu za masoko zitaboreshwa na Balozi zetu kutumika kwa kuunganisha makampuni na wafanyabiashara wa ndani na wa nje. Bodi ya Biashara za Nje, pia ichangamkie fursa hizi na kukuza uchumi wetu, kuongeza ajira na kukua kwa pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* ivisaidie viwanda vidogo kusindika maembe, mapapai na matunda ya asili, ambayo ni mengi na yanaoza katika Jimbo la Igalula. Pia, iongeze mikopo ya vikundi na wajasiriamali, ili kuondoa umaskini na kuongeza pato la Jimbo, Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asali inazalishwa kwa wingi na ubora wa juu Jimboni Igalula. *SIDO* itusaidie kupata mizinga bora na ya kisasa ili asali nyingi izalishwe. Kiwanda cha kuongeza ubora wa asali kijengwe na asali ipate soko la ndani na la nje ili kuongeza pato, ajira na uchumi wa Jimbo uweze

kukua. Kata za Kizengi, Tura, Loya na Lutende, zina misitu ya asili na hivyo uzalishaji wa asali ni mkubwa na hakuna madhara ya *nicotin* kwani tumbaku hailimwi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu alizeti, karanga na ufuta zinazolimwa Igalula, tunahitaji *SIDO* itusaidie mitambo midogomidogo ya kukamua mafuta ya kula na kupewa mafunzo ya usindikaji huo. Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko, washirikiane na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, ili Igalula tuweze kuboresha zao la embe kwa kupanda miembe ya kisasa na pia kilimo cha michikichi ili mbegu bora ziongeze uzalishaji wa mafuta ya kula.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba Waziri, apokee pongezi zangu za dhati kabisa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuwa Waziri katika Wizara hii nyeti ya Viwanda na Biashara. Hakika nina imani kubwa sana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie hotuba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ni nzuri, nampongeza Waziri na naomba katika mipango ya kazi, Wizara iamue kwa makusudi kutembelea viwanda vyote vilivyobinafsishwa kuangalia kama vinafanya kazi nzuri kama ilivyotarajiwa. Kuna hujuma kubwa sana inafanyika kwa baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa kwa baadhi ya Wachina, hususan Kiwanda cha Urafiki ambacho Tanzania tunamiliki hisa 49%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuangalia upya dhamira ya Serikali kupandisha ushuru wa mafuta ya mawese yasiyosafishwa (c*rued palm oil*). Wenzetu wa Kenya na Uganda wameondoa kabisa ushuru wa bidhaa hii. Ushuru huu ukiongezwa, utauwa viwanda vyetu vya ndani kwa kuwa utavifanya kuuza mafuta kwa bei ya juu. Hali hiyo ikifikia, ni wazi kwamba viwanda vyetu itabidi viongeze bei za mafuta na kwa vyovyote vile viwanda vyetu vitakuwa na bei ya juu kuliko ya nchi za jirani zetu kama vile Kenya na Uganda ambako wao hawana ushuru wa *crued palm oil* matokeo yake tutakosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haitoshi. Kama anavyoelewa Watanzania wamehamasika sana kulima alizeti na wengi wao wana mashine ndogo za kukamua mafuta. Mafuta haya huwa yanakuwa ni *semi-refined,* ambayo wanayapeleka viwandani na kuyauza ili yakawe *double refined.* Viwandani wanapata faida na itaboresha Sera ya Kilimo Kwanza na vilevile vijana wetu wataweza kupata ajira na pia wao wenyewe kuajiri na kupata ajira viwandani. *Crued oil* pia inatumika kutengeneza sabuni mbalimbali na hivyo kufanya sasa hivi kusiwe na tatizo la kupata sabuni, ziwe za miche, za unga *(detergent)*, sabuni za kuogea na kadhalika, ambazo zinatengenezwa ndani ya nchi yetu. Kwa kupandisha ushuru huu wa *crued palm oil* utasababisha hata bei ya bidhaa hizi za sabuni kupanda na kuturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya makusudi kuvisaidia viwanda vyetu vya ndani, hasa kama hili la

kuacha ushuru huu wa *crued palm oil,* kwa maslahi ya kibiashara ili kukuza soko kwa bidhaa zetu za ndani. Sasa hivi tuna wateja wengi wanahitaji mafuta yetu ya *sun flower (sundrop)* na inasemekana mafuta haya ni bora sana na yanapendwa sana. Sabuni zetu kama kiboko, Takasa, *Giv*, Guru na nyingine, zina soko kubwa sana Uganda, Kongo na nchi zingine za jirani; wafanyabiashara wao wanakuja kuzinunua hapa Tanzania, kwenye viwanda vyetu. Ni wazi kabisa kwa kukuwa kwa soko hili, tunanufaika kwa kodi na pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pesa za kigeni, nimelisema kwa makusudi, ili Waziri ajue watu hawa wanakuja na *US dollars* jambo ambalo siyo zuri kwa uchumi wa nchi yetu. Ni jambo ambalo namwomba Waziri aliingilie kati ili watumie pesa zetu *(T.Shillings)* ili kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namwomba Waziri aangalie mazingira ambayo vijana wetu wanafanyia kazi viwandani. Kwa kweli, baadhi ya wawekezaji wanawatesa sana vijana wetu, kwa mfano, kiwanda cha KAMAL; tulikitembelea kiwanda hiki, kwa kweli hali tuliyoikuta pale tulilia machozi. Tulikuta vijana wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hawana vitendea kazi, kazi ambazo zingefanywa na mashine wanafanya wenyewe, hawana vifaa vya kujikinga na moto. Wengi wao tulikuta wamejifunga maboksi, matambara na magunia. Hakika hali tuliyoikuta ilikuwa mbaya sana, kama tungekuwa na uwezo tungefunga kiwanda kile cha nondo siku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Waziri aweke utaratibu wa kutembelea viwanda; kwa kusisitiza asitoe taarifa, kwani akitoa taarifa hatayashuhudia hayo ninayoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba sana ushuru wa *crued palm oil* usiwepo. Akiondoa ushuru huu, nitaunga mkono hotuba yake ambayo ni nzuri sana. Namkutakia kazi njema Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, pia nawatakia mfungo mwema.

**MHE. MAULIDAH A. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Abdallah Kigoda kuteuliwa kuwa Waziri na Mheshimiwa Gregory Teu kuwa Naibu Waziri, namwomba Mwenyezi Mungu awape hekima, busara na wawe wabunifu ili waisogeze nchi hii kwenye utajiri kwani nchi ni tajiri, lakini ilikosa viongozi wa kuiondoa kwenye umaskini, naomba tena Mawaziri hawa wapate ujasiri na kutenda kazi zao kwa kuangalia Utaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi bila ya biashara haiwezi kufika popote, itaendelea kuwa nchi maskini kwani biashara ndio chanzo cha utajiri, naomba sana na natoa rai ili tuweze kusogea. Tujitahidi sana kuwasaidia wakulima watoke kwenye kilimo cha kutumia jembe kwani kilimo hicho ni kwa ajili ya chakula tu, si kuweza kuuza nje na kupata fedha za kigeni.

(i) Tukaribishe wakulima wakubwa waje kuwekeza kwenye kilimo ili tuweze kupata mazao yaliyo bora na wananchi wetu wajifunze na wao waige wawe wakulima bora.

(ii) Tuendelee kuondoa kodi kwenye vifaa vyote vya kilimo viwe na bei nafuu ili wakulima waweze kumudu kununua na kuondokana na jembe.

(iii) Tutathmini mazao yetu na kuhakikishe tunaendelea kuweka bei nzuri ya mazao kwa wakulima ili wapate moyo wa kujiendeleza.

(iv) Tuendeleze miundombinu kama barabara ili iwe rahisi kuwafikia wakulima na wakulima waweze kufika kwenye masoko.

(v) Serikali isimamie kwa ukaribu wakulima wasidhulumiwe kwenye soko.

(vi) Tuhakikishe umeme unafika vijijini ili wakulima na wafugaji waweze kutumia umeme huo kwa umwagiliaji na ufugaji wa kuku.

(vii) Tujitahidi kufikiria jinsi ya kurudisha utaratibu wa usafiri kupatikana wakati wa usiku kwa kuhakikisha ulinzi wa kutosha na usafiri madhubuti ili wakulima waweze kufikia masoko mapema iwezekanavyo.

(viii) Kusogeza huduma za kibenki karibu na wananchi vijijini ili waweze kuhifadhi fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni muhimu sana kwani tutakapoviendeleza viwanda vyetu ndipo itakapowezekana kuwa na soko la uhakika wa mazao yetu. Hili halina mjadala kwani leo tunajitahidi kuwapa moyo wananchi wetu washirikiane kuwa na biashara zao za umoja kutengeneza vitu kama achari kwa kutumia mbilimbi zetu na kusindika mboga kuzikausha. Lakini hapo hapo malalamiko ni kukosa vifungashio kwani inawabidi kuagiza chupa kutoka nchi jirani, hii ni kwa sababu viwanda vyetu vya hapa nchini vimekufa vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wadogo wadogo wana malalamiko mengi hasa manyanyaso wanayopata kwa kutozwa ushuru mdogo mdogo mwingi wakati biashara wanazofanya tayari zinakuwa zimetozwa kodi tangu mwanzo, aidha mali hiyo inapoingizwa nchini au wakati wakiuziwa wao ili na wao waweze kuuza. Naomba manyanyaso haya yaondolewe kwani tunawavunja moyo na hawajui wafanye nini ili waweze kumudu familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa hili Mzee wetu Marehemu Julius Kambarage Nyerere alijitahidi kuanzisha viwanda vingi mara tu baada ya nchi kupata uhuru. Viwanda hivyo vilikuwa vinapata malighafi hapa hapa nchini kama pamba, ngozi, kahawa, tumbaku, alizeti, mkonge, nyama ya ngombe na vinginevyo. Leo viwanda hivyo vyote tumejidai kuleta eti wawekezaji kuvibinafsisha leo vyote vimekufa, hakuna kitu ila majengo yanayolaliwa na popo na mengine yakiendelea kula pesa za walipa kodi eti wanavilipia, kuvilinda hii ni ajabu sana

unatumia kidogo ulichonacho na hutaki kutafuta njia ya kukirudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu turudishe viwanda vyetu tuwape uwezo wakulima wetu turudishe heshima ya wafugaji kwa kuwatengea maeneo maalum ili kuepusha ugomvi na wakulima tuangalie upya bahari yetu na kuwawezesha wavuvi ili kupata faida ya maziwa tuliyonayo na bahari inayotuzunguka tuache kuwanyanyasa wafanyabiashara wazawa kwa kuongeza kodi za ajabu ajabu bila ya kufikiria madhara yatokanayo na kodi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaheshimu wawekezaji wa ndani na kurudisha meza ya mazungumzo mara kwa mara kujua kinachowasumbua tusiogope kutafuta fedha za kuangalia haya yote na kurudi kuyaimarisha upya kwani tunaweza kurudisha hali nzuri ya wananchi wetu. Barabara bandari, reli, usafiri wa anga ndio nguzo kuu ya kuimarisha biashara na viwanda na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la viwanda, viwanda vingi vimekufa kutokana na ubinafshaji mbovu, baadhi ya viwanda hivyo vimekuwa ni maghala ya kuweka bidhaa za madukani na vingine vimekuwa maghala ya kuwekea vifaa vya

ujenzi. Baada ya wamiliki hao kuchukua mikopo Benki kwa madhumuni ya kuendeleza viwanda hivyo. Ukizingatia tulikuwa tuna Viwanda ya Kusindika nyama, viwanda vya uzalishaji nguo mpaka sasa hivi hakuna vinavyofanya kazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza kiwanda kilichopo Shinyanga cha kusindika nyama ambacho Serikali imetumia gharama kubwa? Je, Serikali ina mpango gani thabiti wa kuwachukulia hatua wawekezaji walioshindwa kuendeleza viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la ajira kwa vijana; viwanda vingi vilivyobinafsishwa vingekuwa vinafanya kazi ingepunguza tatizo la ajira kwa vijana. Leo hii viwanda vingi vimefungwa, vimebadilishwa matumizi baadhi ya vingine. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha viwanda hivyo vilivyobadilishwa matumizi vinarudi katika matumizi yake? Je, Serikali haioni kuna haja ya kuwanyang'anya hao wabinafsishaji walioshindwa kuviendesha hivyo viwanda na kuvibinafsisha upya kwa watu wanaoweza kuviendeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya usindikaji, kuna Mikoa ambayo inaongoza kwa kilimo cha matunda kwa mfano Tanga, Mkoa wa Pwani na kadhalika kipindi cha msimu wa matunda. Matunda haya yamekuwa yakiharibika shambani na kukosa soko. Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwezesha Shirika la *SIDO* ili liwafikie wananchi waliopo vijijini ambao hawana elimu ya ujasiriamali ili wapate taaluma za usindikaji wa matunda ambayo yamekuwa yakiharibika mashambani. Endapo Serikali itawawezesha wananchi wa Mikoa inayoongoza kwa

matunda tutaweza kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na akinamama kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya ngozi, akinamama wengi wamekuwa wakinunua mikoba kutoka nje ya nchi na kupoteza pato la Taifa. Endapo Serikali ingeboresha viwanda vya ngozi tungeingizia Serikali pato kubwa la Taifa. Vitu vingi vinatoka nje ya nchi kama mikoba, viatu, mikanda na kadhalika. Je, ni lini Serikali itaboresha viwanda vya ngozi vilivyokufa ili pesa nyingi wanazozipoteza Watanzania kununua bidhaa kutoka nje zibaki hapa Tanzania na kuiongezea Serikali pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vituo vya kuuza mafuta, kumekuwa na udanganyifu (wizi) sana katika biashara hii ya kuuza mafuta hasa mafuta ya magari kama *petrol* na *diesel* katika vituo vya kuuzia mafuta hayo. Wizi huo na udanganyifu umekuwa ukifanywa vituoni kwa kupunjwa kwa lita kuchanganya na mafuta mengine vitendo hivi vya wizi na udanganyifu havitokwisha mpaka Serikali imeamua kubadilisha mipira ya pampu za kuweka mafuta kutoka iliyopo sasa nyeusi na kuleta sheria ya kutumia hizo mashine na kuwa nyeupe yenye kuonesha mafuta yanayopita (*Transparent pipes*) ili kuondosha huo wizi na udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuleta sheria ya mipira meupe (*Transparent pipes*) katika pampu. Je, ni hatua gani ambazo zimeshachukuliwa kwa wauzaji wa mafuta ambao wamekutwa na *TBS* wakichanganya mafuta au

kupunjwa kwa lita? Je, ni wauzaji wangapi wa mafuta waliochukuliwa hatua za kisheria katika makosa hayo? Je, ni wauzaji wangapi wa mafuta ambao wameshahukumiwa kwa makosa hayo ya kuchanganya na kupunjwa lita ya mafuta?

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Daktari Abdallah Kigoda; Naibu Waziri, Mheshimiwa Gregory Teu; Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina changamoto kubwa sana, kwa sababu viwanda vingi hapa nchini, vimekufa kabisa. Serikali imebinafsishwa kwa wawekezaji ambao badala ya kuvifufua wameviua kabisa na kusababisha wananchi wengi kukosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali itueleze watakapokuwa wanajibu hoja mbalimbali ina mkakati gani hasa kuhusu suala zima la kufufua viwanda vyetu hapa nchini vikiwemo vya Mkoa wa Iringa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kuainisha maeneo ambayo yametengwa kwa ajira ya miradi ya *EPZ* na *SEZ*. Kutokana na umuhimu huo ni vyema maeneo hayo yakafahamika katika Mikoa yote na tukaambiwa vigezo au vipaumbele vinavyowekwa kwa ajili ya uanzishaji wa miradi hiyo. Sababu Mkoa wa Iringa maeneo hayo yametengwa muda mrefu sana, lakini hakuna maendeleo yoyote ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wimbi kubwa la wafanyabiashara wa kigeni kuja kufanya biashara ambazo wazawa wanaweza kufanya kwa mfano wafanyabiashara wa Kichina kuuza maua, *ice-cream* na vifaa vya plastiki na kadhalika. Kwa nini Serikali isiweke sheria kwa wageni hao kufanya biashara ambazo wazawa hawawezi kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwepo na unyanyasaji mkubwa sana kwa wawekezaji wa viwanda hapa nchini kwa wafanyakazi wazawa na kuleta wataalam wa nchi zao wakati hapa nchini kuna watalaam ambao ni ma-*engineer* ambao tumewasomesha katika vyuo vyetu kwa kuwapatia mikopo. Hivyo, wataalam wetu kukosa ajira na hata waliopata ajira utaona hata maslahi yao yamekuwa tofauti na wafanyakazi waliotoka katika nchi zao na hata kama vyeo vyao ni sawa na wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Wizara iwe na utaratibu wa kufuatilia jambo hili ambalo linawabagua wazawa wenye mali yao kupata shida na wageni kuja kututawala katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa ajili ya kutoa elimu na kuwajengea uwezo wakulima kwa kusindika mazao kabla ya kuyauza. Hapa ningeomba Serikali iweke wazi utaratibu unaotumika kutoa elimu hiyo kwa sababu kuna baadhi ya Mikoa na hasa wananchi wanaoishi vijijini hawaelewi nia hii nzuri ya Serikali ya elimu hiyo na kujikuta fursa hii wanapata wananchi wanaoishi mijini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia elimu na fursa kuhusu uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo itolewe kwa nguvu zaidi ili vijana wetu hapa nchini waweze kupata ajira  za kujiajiri wenyewe kuliko ilivyo sasa, vijana wengi hawana shughuli za kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa sana ya viwanda vya *SIDO* bado hakujawa na Muungano wa Biashara kati yao na Serikali. Ningeshauri Shirika la *SIDO* litumike kuunganisha biashara kati ya Halmashauri zetu na viwanda vyao kwa kutengeneza bidhaa zote zinazotumika mashuleni, kama madawati, vifaa vya ofisini, chaki na kadhalika, iwepo sheria kuwa lazima Halmashauri hizi zitoe *order* katika vyuo vyetu ili vyuo pia viweze kujiendesha venyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kama ifuatavyo kwenye bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC, SICHUAN MONGDA GROUP(SMG),* napongeza kwa kusaini ubia, lakini yafuatayo ni ushauri na tahadhari kwa *NDC.  USD 3B Investment* ni *sid money* au itawekeza kwenye miaka mingapi?  Naomba Wizara inipatie maelezo hayo na pia naomba kujua hiyo kampuni ya ubia. Tanzania *China International Mineral Resource* itaendeshwa na *Board* ya watu wangapi na *management* itasimamiwa

na nani? Pia hii fursa ya kuongeza hisa za Serikali kufikia 49 baada ya kampuni ya *SMG* kulipa deni litakalokuwa limekopwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *statement* inanipa wasiwasi naomba kujua yafuatayo:-

(i) Hilo deni litakuwa limelipwa kwenye miaka mingapi?

(ii) Hiyo 3 *USD* inayowekezwa naomba kujua mchanganuo wake.

(iii) Tuhakiki kama Serikali huo uwekezaji wa *USD* 3 *in value for money* liwe wame-*inflate investment* yao. Tungefanya *International audit* ya huo uwekezaji wa *USD* 3 bilioni. Hayo maelewano au mkataba ningeshauri Serikali ituletee hapa Bungeni tuone na tuwashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya masoko, naomba kujua hii sekta inafanya kazi gani kwani sisi tuna matatizo na bei ya mazao yetu hususan pamba, kitengo hiki kinatakiwa kututafutia masoko na bei nzuri lakini wako kimya. Naomba kujua hii Idara inafanya kazi gani au inashauri vipi wakulima ili waweze kuelewa soko la zao lao likoje hapa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni tuliomba Serikali itupe bei ya pamba kuwa shilingi elfu moja, lakini Idara ya masoko iko kimya na haitoi hata tamko. Idara ya masoko inatakiwa itusaidie maana ukiangalia mazao yetu asilimia kubwa hayapati bei nzuri. Ni

wajibu wa hii Idara ya masoko pia itutafutie bei nzuri ya mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mikono hoja hii.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri bila kumsahau Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara na wajumbe wote wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kutaka Serikali itoe elimu kwa wafanyabiashara wa Temeke na Dar es Salaam kwa ujumla. Mji wa Dar es Salaam ni wa kibiashara lakini wafanyabiashara wetu wanafanya biashara pasipo kupewa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa sabasaba bado hakuna ushirikiano na Manispaa ya Temeke. Kodi za majengo hawalipi na tukiuliza tunaambiwa Temeke tunafaidika na kodi za majengo wanayolipia, wapi? *Tan-trade* wabadilike sasa wananchi wanataka kujua wanafaidikaje. Nashauri tushirikiane na Halmashauri kwa maendeleo ya wananchi na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa njia ya maandishi nichangie bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Awali ya yote nitamke bayana kuwa Wizara hii ni muhimu katika kuongeza kipato na kuchangamsha uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhimiza Serikali ili ielekeze nguvu zake katika viwanda vidogo kwa daraja la familia, Vijiji na Kata (*cottage industry*). *SIDO* pamoja na utendaji wake unaotia moyo, mapendekezo yangu ni kwamba, wapewe nguvu na kubebeshwa jukumu la uongozi katika kuhakikisha Watanzania wanatambua na kuitumia sekta ya viwanda vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Wizara hii pamoja na Wizara nyingine mtambuka kuanza upya kampeni ya kipande chake kinunue ukitumie *Buy Tanzania use your produce, build our economy*. Hii itaokoa mazao yetu kwa kuyapa soko, lakini itapunguza uagizaji nje bidhaa tunazoweza kuzalisha nchini kwa faida za kiuchumi zilizowazi. Katika kampeni hii ni wazi kuwa tutatumia faida ya kijiografia kuzalisha nchini na kuuza nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie utendaji wa Shirika la Viwango nchini *(TBS)*. Shirika hili ni muhimu na hivyo inabidi tuliimarishe. Uzalishaji utakaoweza kuridhisha soko la ndani katika soko huru na utandawazi huu pamoja na ubora, lazima bidhaa ziwe na ubora unaokubalika. Uimarishaji wa *TBS* uanzie kwenye rasilimali watu na muhimu hapa ni kuwa na timu ya watendaji yenye uadilifu wa hali ya juu. Mgongano katika viwango vya mafuta jamii ya *petrol* gasoline yaliyoingizwa nchini na kubainika baadaye viwango vyake vina mashaka vinatia doa nguvu kazi yetu. Pamoja na kasoro hii kukutwa sokoni kwa bidhaa zenye viwango duni ilhali wahusika wana hati za *TBS* ni

ishara ya kututaka tujipime na kujipanga upya. Jukumu la *TBS* ni kubwa sana, wapewe zana za kufanyia kazi na waongozwe ili waweze kuendesha shughuli kwa kujiendesha wenyewe, inawezekana kutokana na mfumo wa biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa gharama za usafirishaji na hatimaye bei kubwa kwa mlaji. Naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha Kiwanda cha Saruji, Kanda ya Ziwa. Utafiti mdogo utakuonesha kuwa nchini Uganda Kasese kuna Kiwanda cha Sementi, Kasese hali yake ya udongo haitofautiani sana na ukanda wa Mikoa ya Kagera, Geita na Kigoma. Rai yangu ni kuwa tujenge Kiwanda cha Saruji, eneo hili tuweze kuwapunguzia gharama ya bei walaji na kutengeneza jukwaa la kuhudumia nchi jirani ikiwemo DRC Congo inayojengwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu kuangalia katika maendeleo ya viwanda na masoko ni hatua ya mwanzo yaani wazalishaji. Uzalishaji wa wakulima wetu bado ni wa gharama kubwa, hali hii ni hatari kwa ukuaji na ustawi wa viwanda vyetu kwani ama watanunua malighafi ya bei kubwa hali itakayopelekea kuuza kwa bei kubwa bidhaa ya mwisho na kukosa ushindani au kununua malighafi kwa bei chini ya gharama halisi ya uzalishaji na kupelekea wakulima kutupwa nje ya shughuli na viwanda kulazimika kuagiza nje malighafi au kufa. Hoja hapa ni kuwa jitihada za kufufua viwanda ziende sambamba na matumizi ya mbinu za kisasa za uzalishaji zitakazopunguza gharama za uzalishaji na hatimaye bei nzuri kwa wakulima na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na hali duni ya maendeleo ya Taifa letu katika nyanja za biashara. Natoa ushauri Serikali kupitia Wizara hii iongeze juhudi za kuwaelimisha Watanzania katika nyanja za ujasiriamali masoko na biashara. Ni muhimu kutambua kuwa Watanzania bado wako chini sana katika nyanja ya biashara na masoko. Wanahitaji kusukumwa na kupewa nguvu ili wazitumie fursa hizi kwa ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu wa maandishi katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lengo la Serikali kuinua viwanda vidogo vidogo hasa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015. Katika randama (ukurasa wa 38) nashukuru kuona Serikali imeazimia kuimarisha uwezo wa *SIDO* kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi katika Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutoishia hapa kwenye wafanyakazi tu bali kuiongezea *SIDO* uwezo kifedha kwani *SIDO* itakapokuwa na uwezo kifedha hata utendaji kazi wake utakuwa wenye uhalisia wa kuinua uchumi wa Mtanzania wa kawaida na hii itakuwa ni njia moja ya kutatua tatizo la ajira nchini na pia itasaidia kufikia malengo yaliyopangwa

kwa wakati kwa sababu kazi zote zitafanyika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo hii itakuwa ni njia mojawapo katika kuboresha viwanda vidogo vidogo kwa sababu fedha hizo zitasaidia katika kununulia vifaa kama vitendea kazi vinavyohitajika katika viwanda hivyo na pia zitasaidia katika kuwalipa wafanyakazi wa kawaida pamoja na wataalam wanaohusika na shughuli za viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuna viwanda vingi ambavyo vina oda kubwa ya bidhaa lakini inakuwa ngumu kutengeneza bidhaa za kutosha kutokana na uchache wa wafanyakazi, vifaa vya kutengeneza bidhaa hizo na pia katika kusafirisha bidhaa kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Katika hili naipongeza Serikali kwa hatua waliyofikia.

Mheshimiwa Spika, katika randama (ukurasa wa 41) Serikali imetoa shilingi milioni 300 kusaidia *NEDF* kwa ajili ya wajasiriamali safi kabisa, hofu yangu kubwa ni kwamba, je, fedha hizi zitawafikia wajasiriamali ambao tumelenga kuwainua hasa wale wa vijijini? Naiomba Serikali ituhakikishie kwamba kweli fedha hizo zitawafikia walengwa hasa vijijini na je, hizo ajira ni ajira za namna gani maana isiwe ni ajira kwa wenye ajira wakati kuna maelfu ya vijana wamejaa kule vijijini na hata mijini hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma za ugani kupitia *SIDO* lipewe kipaumbele zaidi kwa sababu linasaidia kukuza uwezo wa vijana wetu kujiajiri

badala ya kukaa tu vijiweni na kusubiri ajira za kuajiriwa kitu ambacho kimekuwa vigumu kwa wananchi hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maombi yangu kwa Wizara kulisimamia hili katika Mwaka huu wa fedha na ikiwezekana kuvuka kiwango kilichofikiwa mwaka huu uliomalizika cha wajasiriamali 16,138 kwa Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya viwanda, ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia suala la kwamba nchi yetu iko kwenye mapinduzi ya viwanda. Viwanda vyetu vidogo vidogo vimekuwa vikiathiriwa katika uzalishaji wake na tatizo la umeme. Umeme limekuwa ni tatizo kwa sababu umeme umekuwa ukikatika kila baada ya masaa kadhaa. Kutokana na tatizo hilo viwanda vimekuwa vikisimamisha utendaji wake wa kazi kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mapendekezo yangu kwa Wizara kushirikiana na Wizara ya Nishati kutatua tatizo la umeme ili kuweza kuvikomboa viwanda vyetu vidogo vidogo katika randama (ukurasa wa 27) Serikali imetamka wazi kuwa imeandaa mkakati wa kuendeleza sekta ya nguo na mavazi ili kuboresha teknolojia ya viwanda vya nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mkakati huo uweze kufikia malengo yake ni lazima Serikali ifanye juhudi za makusudi za miradi ya umeme wa makaa ya mawe, lakini kwa umeme huu huu wa kukatikatika kila wakati

malengo hayo hayatafikiwa. Hivyo, nashauri mipango na mikakati hii ambayo utekelezaji wake unahitaji mambo mengi kufanyika kwa kutegemea eneo lingine basi mashirikiano katika kufanikisha hili uwekewe mkazo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali na Wizara hii husika kwa kufanikisha ununuzi wa mashine za kuchimbia makaa ya mawe, hii inaweza kutusaidia pengine kufikia mahali ambapo Watanzania wangependa tuwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu *SME*, (*Small and Medium Enterprises*) ya mwaka 2003 ni kujenga mazingira mazuri ya kutengeneza ajira na uzalishaji kipato kupitia uanzishwaji wa *SME* mpya kwa ajili ya kutoa ushindani kwa *SME* zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna ajira nyingi ambazo zililengwa kutengenezwa, hivyo kuwakomboa Watanzania kuondokana na hali ngumu ya kiuchumi. Ni maombi yangu kwa Wizara kuliwekea msingi jambo hili kwani ni mojawapo ya njia kuu za kufikisha maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vyetu vya Nguo vimeachwa vimekufa kwa kuacha kuzalisha nguo zilizo bora na baadaye kununua nguo zisizo na ubora toka nje pia zenye bei kubwa. Naiomba Wizara husika pamoja na Serikali kwa jumla ili pamba yetu iongezeke bei ikiwa

viwanda vinashindana kwa kuzalisha nguo, lakini pia itawaongezea vijana wetu kupata ajira kwa wingi na kupungua kuzurura mijini na kupunguza kufanya maovu kwa ajili ya kisingizio cha kukosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kuna viwanda wanavyo wawekezaji na hawawezi kuvitumia kwa sababu mbalimbali, naomba Wizara iwanyang'anye na wapewe wawekezaji wa nchini ambao wanaweza kuvifufua na kuvirudisha katika hali ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kufufua viwanda, miundombinu ya kuzuia kusambaza *chemical* zenye madhara kwa binadamu pia kuzuia kumwaga maji machafu yenye madhara liangaliwe sana ili kuzuia uchafuzi wa mazingira na kupunguza mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri na timu yake kwa umakini mkubwa katika utekelezaji wa kazi za Wizara. Hata hivyo, tatizo la milolongo ya kodi na taasisi nyingi za kutoa vibali kabla ya kuanzisha biashara nchini bado ni kikwazo kikubwa kwa kupanuka kwa biashara nchini. Sekta ya kilimo na mifugo, tasnia ya maziwa na samaki, vyote vimekuwa na kodi nyingi mno kiasi kwamba wawekezaji wanashindwa kupanua uwekezaji. Hivi Serikali inapata kigugumizi gani kuwianisha kodi na vibali hivyo ili kurahisisha uanzishaji wa uwekezaji katika tasnia ya maziwa nchini. Kwa

upande wa viwanda vya samaki, viwanda vya Tanzania vinashindwa kushindana na vile vya Kenya na Uganda kwa sababu ya tofauti ya kodi zinazotozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kodi za viwanja vya ndege zinakatisha tamaa wasafirishaji bidhaa za samaki na maua ili ndege za mizigo ziweze kutua Mwanza na Kilimanjaro badala ya hali ya sasa ambapo mizigo hii hupakiliwa Nairobi na kumwongezea mwekezaji wa Tanzania gharama zaidi za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali hasa kwa utendaji kazi wa *BRELA*. Hata hivyo, *BRELA* bado ina upungufu makubwa wa wafanyakazi na vitendea kazi kama vile komputa ambapo unakuta watumishi kadhaa wanatumia kompyuta moja. Hii inachelewesha kasi ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Mwanza limekuwa mwenyeji wa Maonyesho ya Biashara ya nchi za Afrika Mashariki na Maziwa Makuu, lakini viwanja vya maonyesho yake vilivyoko Pasiansi havina miundombinu sahihi na vimechakaa. Mazingira ya jirani yako duni na vibanda duni kabisa. Hivi kwa nini maonyesho haya yasiwe na usimamizi thabiti kama yanayofanyika Dar es salaam (Sabasaba) hakuna mamlaka ya usimamizi? Naomba majibu. Kufanikiwa kwa maonyesho ya Mwanza kutaifungua Tanzania kwenye nchi za Maziwa Makuu na kuingiza fedha ya kigeni nchini. Hii pia inapaswa kuendana na upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ufanisi wa Tanzania katika biashara nchini na Kimataifa inategemea sana elimu ya ujasiriamali. Elimu bado haitolewi ya kutosha. *SIDO* wenye wajibu wa kuwafikia wananchi bado bajeti yao ni ndogo na bado wako kwenye Makao ya Mikoa tu. Hivi ni lini *SIDO* itawezeshwa kujitanua hadi ngazi za Wilaya? Mkoa wa Simiyu na Wilaya zake zote hawana kituo cha *SIDO* ni vipi wananchi wa Simiyu watafikiwa na *SIDO*? Nashauri *SIDO* wahamasishe Halmashauri za Wilaya ili kuanzisha vituo vya Viwanda vidogovidogo ambapo wananchi na vikundi vya ujasiriamali watapata mafunzo badala ya kulazimika kwenda Mikoani. Kunahitajika mpango wa *SIDO* kusambazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina bahati ya kupakana na nchi nyingi, lakini kwenye mipaka maeneo yetu hayajapimwa wala kuvutia uwekezaji ambapo kungefanyika biashara na hata kusafirisha bidhaa kwenye nchi jirani na hivyo kuingiza fedha za kigeni na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Serikali isaidie biashara ya zao la pamba. Hebu Waziri wekeza akili ili kuondoa kelele na hofu kwa biashara ya pamba ili wananchi wetu waweze kunuifaka na kuvutia viwanda na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi pekee duniani ambayo inaruhusu wafanyabiashara kuingiza nchini bidhaa za aina yoyote bila kujali ubora wake. Hili limesababisha nchi kuwa jalala la bidhaa duni, feki, mitumba iliyochoka na ni aibu kubwa. Serikali ieleze Bunge ni kwa nini hatuna viwango (*standards)* za bidhaa zinazoingizwa ndani ya nchi kutoka nje? Ni utaratibu gani umewekwa na Serikali kwenye mipaka yetu, kwenye bandari, kwenye viwanja vya ndege na maeneo mengine kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa ndani ya nchi ni za viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu gani na sheria ipi inatumiwa na Serikali kudhibiti wafanyabiashara wanaokwenda kutia *order* za bidhaa nje za nchi zilizo hafifu sana kwa bei ndogo sana kwa maelezo kwamba Watanzania hawana uwezo wa kununua bidhaa za viwango (*low purchasing power*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana, Tanzania tumekuwa soko la bidhaa za wenzetu kwa kila kitu hata kwa bidhaa ambazo tunaweza kuzitengeneza ndani ya nchi. Wakati tukiendeleza viwanda vya nchi za wenzetu vya kwetu tunazidi kuviua, vijana wetu wanazurura mitaani kwa kukosa kazi lakini vijana na nchi tunazonunua bidhaa tunaendelea kuwapatia ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze wananchi ni kwa nini tunaagiza na tunaruhusu uingizaji wa vitu kama *tooth pick, cotton buds,* kanga za Kichina, *pencil, pen* kutoka China, viberiti na kadhalika. Hivi kweli hata hizi hatuwezi kutengeneza na kuuza nje? Hii ni aibu kubwa, tuna misitu na mbao nyingi hata mtoto asiyejua kusoma anaweza kutengeneza *tooth pick*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mwaka 2009/2010, walitangaza ofisi zote za Serikali kusitisha kuagiza na kununua thamani za ofisini na maofisini kutoka nje na badala yake wangewezesha Magereza na JKT na viwanda vya ndani vya useremala ili kukuza soko la ndani na kupata bidhaa bora. Ni kwa nini mpaka sasa hivi maofisi yote yananunua samani kutoka China?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa feki hapa nchini bado ni tatizo kubwa sana. Kwenye maduka yote bidhaa zipo za aina mbili na wauzaji wanaeleza kabisa ukitaka halali, bei fulani, ukitaka feki, bei fulani, kwa uelewa wa watu wetu ni wangapi wenye uwezo wa kutambua tofauti hizo? Hizo bidhaa feki zimepitia wapi hadi kuuzwa madukani na Serikali inaona? Kuna sababu gani kuwepo na *TBS* kama mamlaka ya kudhibiti ubora wa bidhaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa dhaifu sana kukuza na kuinua viwanda vyetu hapa nchini. Kiwanda cha *General tyre* ni kiwanda pekee kilichokuwa kinatengeneza *tyre* za viwango vya hali ya juu. Tairi za kiwanda hiki zilikuwa imara sana na ziliweza kudumu kwa miaka mitatu hadi mitano bado nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kile kimekufa Serikali ipo na sasa tunaletewa *tyres* kutoka nje zinapasuka zikiwa mpya. Tumeongeza ajali za vyombo vya barabarani na tunateketeza maisha ya Watanzania. Kiwanda cha *machine tools* Moshi ni hazina kubwa kwa Taifa kutengeneza *boils* na vyuma vya ujenzi kinakufa, Serikali imetulia inasubiri wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku ni kukosa uzalendo wachache wananufaika na uagizwaji wa bidhaa nje ya nchi ambazo zingeweza kutengenezwa hapa nchini. Wakizileta hapa wanauza bei mbaya na watu wananunua hawana la kufanya. Naamini wapo viongozi wakubwa Serikalini wako kwenye biashara hizo ndiyo maana hakuna juhudi zozote za kufufua viwanda vyetu hata ule umuhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi yoyote inayoweza kupiga hatua haraka za maendeleo bila kukuza viwanda vyake na kuviendeleza. Habari ya Serikali kutulia wakisubiri wawekezaji waje kuendeleza viwanda vyetu imepitwa na wakati. Hata viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda na mboga mboga tunasubiri Wachina? Huu ni uvivu na kutowajibika. Taifa tuamke, tusaidie Watanzania, wengi ni maskini katika nchi iliyo tajiri wa rasilimali.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ugumu wa maisha na watu wa Rukwa niiombe Wizara yako wakati umeme wa

Mkongo utakapopita Mkoa wa Rukwa Serikali iwe tayari imejipanga kutuletea Kiwanda cha Kufua Vyuma na Rukwa tuko tayari kutoa nguvu kazi sisi wenyewe kuwa (*mascaveta)* kwani hatuna kazi nyingine mbali na kilimo na Mungu alichotujalia ni Milima mingi ya Mawe ya Vyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Rukwa kuna vikundi mbalimbali vya ujasiriamali ambavyo havina uwezo wa kujiendesha, hivyo tunaiomba Wizara yako ituwezeshe viwanda vidogo vidogo hata kama ni mashine za *SIDO* kama vile mashine za kupukuchua mahindi, karanga, kuvunia mazao na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya madini vimulikwe na vyombo vya Serikali, kwa mfano, wageni wetu wanadanganya kuwa wao wanavuna dhahabu na ile dhahabu inatoka kwenye mwamba wa kopa (*copper)* huenda wapi au tunalipwa kwa kifungu gani hali kadhalika na makaa ya mawe hutembea na dhahabu? Je, wanaochimba makaa ya mawe na dhahabu huwekwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Rukwa leseni hazijatolewa. Hivyo, naiomba Wizara yako itoe tamko la kuwapa ruhusa watumishi watoe leseni hizo ili waendelee kukusanya fedha za kuendesha Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mafuta mazito ya mitambo huwa ni takataka huko Ulaya, lakini yanapoletwa nchini bei yake inakaribia sawa na mafuta mengine masafi ni nini kinachojiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti vijana wanaoishi mijini kwa biashara ndogo ndogo kama zile zinazouzwa na maduka makubwa na kusababisha wafanyabiashara wakubwa kukosa mauzo ya kutosha. Ni lazima utaratibu na sheria ziwekwe kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo kama wanataka kuweka vibanda vyao mijini kama Miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na kadhalika walipe kodi ya mapato wala wasisamehewe, wasamehewe walioko pembeni mwa miji ili wafanyabiashara wetu wakubwa nao waone faida za maduka yao, wafanyabiashara wadogo watengewe maeneo ya biashara zao zenye uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakikisha Wizara hii inaimarisha mipaka kibiashara ili kuongeza pato la Taifa kama maeneo ya Kaseya, Rukwa kulikokuwa na Ofisi tayari za *Migration* na kadhalika; Kilando, Nkasi Kaskazini; Wampembe, Nkasi Kusini na Muze-Kwela kwani maeneo haya ya Mkoa wa Rukwa yamechangamka sana, hivyo katika Mkoa wa Rukwa tunaomba ushirikiano wa Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kusema naunga mkono hoja. Lakini pamoja na hayo yafuatayo naomba yazingatiwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi katika nchi yoyote kuendelea kwake kunategemea viwanda lakini

ajabu katika Tanzania yetu viwanda vingi vimekufa ni kwa nini? Naomba maelezo na pia Serikali ina mkakati gani katika kufufufa viwanda hivyo ambavyo faida zake ni ongezeko la uchumi, ongezeko la ajira kwa Watanzania hususani vijana na wanawake ambao ndio nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kule Mbeya viwanda vingi vimekufa na viko maeneo mazuri, majengo mazuri makubwa *with modern facilities* kama vile *Tanganyika Packers* (Mbalizi) Kiwira *Coal Mine, Hisoap* zana za kilimo na kadhalika. Nipatiwe maelezo juu ya viwanda tajwa hapo juu maana uchumi wa Mbeya unazidi kuzorota juu ya hili na ukizingatia ni mji mkubwa ambao ni *gate way* ya nchi za jirani Kusini na Kati (Afrika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni njia gani zinatumika katika kuboresha mazingira mazuri ya wawekezaji kwa sababu kazi ya wawekezaji viwandani (vya ndani na nje) imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara hususan kule Mbeya ushuru umekuwa mwingi *unconsistence while* mzunguko wa pesa ni mdogo tofauti na Jiji la Dar es Salaam hali inayopelekea kuumiza wafanyabiashara hawa na hivyo kushindwa kuhimili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje bidhaa za kutoka hapa Tanzania ziende Kenya na *packaging* ifanyike Kenya na kuonesha kuwa ni *product of Kenya.* Tanzania tuko wapi na tunafanya nini? Nini chanzo cha

haya na Wizara ina mkakati gani katika kulishughulikia hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha haya kwa leo.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono bajeti hii. Mkoa wa Tabora bado haujatenga maeneo ya uwekezaji *(EPZ)* jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya Mkoa kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Tabora umebarikiwa kuwa na matunda mengi kama vile maembe, lakini pia Tabora inazalisha asali kwa wingi, lakini bado uvunaji wa asali ni wa asili na hauendani na mahitaji makubwa ya asali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna Kiwanda cha Nyuzi *New TABOTEX* imedhihirika kuwa kiwanda hiki hakitumiki ipasavyo, tayari wakulima wamelima pamba jinsi ilivyoahidiwa na uongozi wa kiwanda hicho, lakini mpaka sasa haijanunuliwa na kiwanda hicho, jambo ambalo limeleta usumbufu mkubwa kwa wakulima wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hakijatoa ajira ya kutosha, nchi yetu inapoteza mapato na ajira kwa ajili ya kuuza mazao ghafi kwenda nje ya nchi. Kwa mfano, korosho kwa kuuza korosho ghafi nje ya nchi yetu inapoteza nafasi 30,000 za ajira na pia bei ya korosho ghafi inayolipwa haiwezi kumkomboa mkulima kwenye hali aliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora unakidhi kuwa na Kiwanda cha Tumbaku, naiomba Wizara iangalie namna ya kushawishi wanunuzi wa tumbaku wawekeze kwenye Kiwanda cha Tumbaku, Mkoani Tabora. Hii itaepusha hasara anazopata mkulima wa tumbaku kwani tumbaku inapokuwa kwenye ghala mpaka kufikishwa Morogoro kuna uzito unaopungua ambapo mkulima anakatwa tofauti ya uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri kwanza nakupongeza wewe na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu kwa kuweka kipaumbele katika ajira ya vijana na moja ya ajira ni vijana kufanya kazi za kujiajiri kwa kutumia pikipiki au boda boda na kujipatia riziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maonyesho ya Sabasaba mwaka huu makampuni mengi toka China yalishiriki katika maonyesho hayo na kuleta changamoto kubwa kwa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makampuni hayo toka China walikuwa wanauza pikipiki za aina tofauti. Nyingi ya pikipiki ambazo wanauza na kutangaza ndio ambazo zinazouzwa hapa nchini toka huko huko China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ambazo walikuwa wanauza hao Wachina katika maonyesho hayo ni sh. 790,000/= laki saba na elfu tisini wakati hapa kwetu wanauza pikipiki kama hizo kwa sh. 1,600,000/= hadi sh. 1,800,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua sababu ya tofauti hiyo kubwa ya bei kwa kweli jambo ambalo haliingi akilini kama kundi kodi kama wanatozwa pamoja na faida iweze kuwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tungependa kujua kodi ni asilimia ngapi Serikali hutoza kwa pikipiki hizo, naamini kodi hiyo haiwezi kufika bei hii kwa thamani hiyo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali yetu iweze kuwashawishi kampuni hizo za Kichina ziweze kuja kuwekeza hapa nchini katika nyanja tofauti ikiwemo hii kampuni ya kutengeneza pikipiki kwa kuweza kuja kuunganisha hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kama wataweza kuja kuwekeza hapa wataweza kutoa ajira na kuongeza kodi Serikali pamoja na hayo naamini bei yake itapungua na kuwawezesha vijana kuwa na uwezo wa kununua na kujipatia ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Serikali inafanya kazi nzuri na Wizara ya Viwanda na Biashara inajitahidi sana japo kuna changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia soko la bidhaa za vyakula zinazotoka nje ya nchi. Serikali idhibiti wafanyabiashara kwa sababu tukiulizia nchi za nje utakuta bidhaa hizi zina bei ndogo sana zinakotoka, lakini zinapofikia huku kama sukari inauzwa mpaka sh. 2000 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo gani linalopandisha bei hizi? Si hayo hata haya mafuta mazito ya mitambo hizi ni takataka zinauzwa kwa bei ndogo karibia ya bure huko Ghuba. Inakuwaje leo yanafikia kuwa kila lita 1,400 mpaka 1,600. Tatizo ni nini? Serikali iangalie kwa kina bei hizi nyingine ni za uzushi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara, naomba nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ili niweze kutoa mchango. Hata hivyo, nampongeza Mheshimiwa Daktari Abdallah Kigoda, Waziri wa Viwanda na Biashara; Naibu Waziri, Mheshimiwa Gregory Teu; Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuendeleza viwanda na kukuza biashara ili kuinua maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo kadhaa, ubora wa sementi ya tembo inayozalishwa na Kiwanda cha Sementi cha Mbeya uko chini ukilinganisha na sementi inayozalishwa Twiga ya Dar es Salaam na Simba ya Tanga. Je, ni kwa nini bei ya sementi ya tembo iko juu kuliko sementi ya twiga na simba hali ubora wake ukiwa hafifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa nini bei ya sementi ya tembo katika Mkoa wa Mbeya iko juu kuliko inavyouzwa Iringa na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nguo kimekuwa ni *godown* ya kuhifadhi tumbaku kinyume na makusudio yake vile vile, sehemu kubwa ya mashine za kutengenezea nguo zimeondolewa. Je, Serikali inawaambia nini wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imedhamiria kusambaza umeme kila Kata na Vijiji. Je, Serikali imejipanga vipi na ina mikakati gani ya kuwasaidia wananchi kuanzisha viwanda vidogo vidogo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Mbeya unapakana na nchi kadhaa Kusini mwa Afrika na kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Songwe karibu utakamilika mwishoni mwa mwaka huu. Je, kuna mkakati gani wa kibiashara ambao Serikali imeunda ili kuweka fursa ya kibiashara na Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa maandishi mazuri ya bajeti yao ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Naibu Waziri, Mwenyekiti wa Kamati na wanakamati wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushauri Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza katika maeneo yafuatayo:- Wingi wa wafanya biashara Jijini Dar es Salaam, uanzishwaji wa viwanda vipya, Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa *TANTRADE*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam limekuwa na wingi wa wafanyabiashara kwanza nipongeze Wizara kwa kuendelea vizuri na suala la usajili wa makampuni hakika kumekuwa na unafuu mkubwa kwa vijana wetu wanaokwenda kusajili makampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam una wingi wa wafanyabiashara hawapatiwi elimu ya uendeshaji wa biashara kifaida. Wafanyabiashara wengi wanashindwa kulipa mikopo na kufunga biashara zao kwa ukosefu wa elimu ya biashara. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuwa sasa watenge fungu la elimu ya biashara waanzie Manispaa mpaka

washuke katika kata zenye wafanyabiashara wengi. Mfano, maeneo ya Manzese, Mwenge, Mchikichini, Kariakoo, Tandika, Mbagala Rangi Tatu na Gongo la Mboto mwisho. Kata hizi zingepewa kipaumbele cha elimu ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Dar es Salaam kumeanzishwa viwanda vingi vipya. Je, Wizara inavitambua viwanda hivyo? Je, vimefuata taratibu zote lakini kubwa zaidi viwanda ni vizuri na tegemeo letu ni kuleta maendeleo kwa kupata bidhaa muhimu hapa nyumbani na kutuongezea ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikitiko yangu kuwa viwanda vile havikamiliki kuna matatizo gani? Mfano, Kiwanda cha Saruji cha Mbagala kina muda mrefu kimekwama wapi? Kiwanda cha kuli-*cycle* mafuta cha *ASPAM* kimeanza vizuri sana tukapata matumaini ya kupata bidhaa na ajira sasa kimesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri Serikali yangu kusimamia viwanda hivi hata kama ni binafsi visaidie wananchi wetu kwa kuwashauri maana mambo mengine yanayosimamisha maendeleo ya viwanda yanahitaji ushauri tu. Tukiwapa ushauri mzuri watapata ufumbuzi wa matatizo yao na viwanda vitaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uwanja wa Maonyesho wa *TANTRADE* Sabasaba nimekuwa nikiomba sana *TANTRADE* iongeze maendeleo na iwe ya kisasa zaidi. Sabasaba imechukua eneo kubwa sana katika Wilaya yetu ya Temeke. Tegemeo la

wananchi wa Temeke ni kupata maendeleo na kipato kutokana na viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yangu itafute fedha au mwekezaji kwa nchi marafiki kujengwe *Business MOO* kubwa ya Kimataifa yenye ghorofa hata kumi, hii itapandisha hadhi ya Mji wa Temeke, lakini pia itaingiza mapato Serikali yetu na itakuwa ni changamoto kwa wafanyabiashara na uwanja huu utalipa sana badala ya kupata gawio toka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *TANTRADE* wao kama taasisi kwa nini wanashindwa kufanya hata *import* ya vitu mbalimbali vya maendeleo au kuanzisha mambo yenye tija kama vile taasisi ya elimu Kibaha ina ufugaji, Chuo cha Maendeleo na kadhalika. *TANTRADE* ianze kutafuta eneo mbadala pembezoni mwa mji kufanya Maonyesho ya Kitamaduni na biashara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu uzingatiwe. Ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa nami kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza ni pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya, aidha, nawapongeza Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba nitoe mchango katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SMEs* kama mhimili wa sera ya kilimo kwanza. Serikali yetu imeamua kukuza kilimo kupitia kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, matarajio ya uamuzi huu ni kusambaza matokeo ya ukuaji wa uchumi kwa wananchi wengi zaidi kwa lengo sambamba la kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kamwe halitatimia iwapo uongezaji wa thamani hasa kwa kutumia viwanda vidogo vidogo halitapewa umuhimu unaofanana. Tatizo kubwa na la muda mrefu la kilimo ni masoko na kwa hiyo, kuongeza thamani kutasaidia sana kuongeza kipato na pia kupunguza *post harvest losses.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii isitulie mpaka itimize kutoa kipaumbele kwenye utekelezaji wa sera ya viwanda vidogo na kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa feki na viwanda vya ndani, utandawazi umeleta athari nyingi kwenye soko letu ikiwemo pia kuongeza umaskini kwa watu wetu kwa kununua bidhaa ambazo hazidumu, athari nyingine kubwa ni uharibifu wa mazingira na mara nyingine kwa bidhaa za elektroniki ambazo ni hatari kwa afya za watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa lingine ni maji ya viwanda vyetu vinavyozalishwa bidhaa zinazofanana au mbadala. Naishauri Wizara kupitia *TBS* kuzidisha jitihada za kudhibiti bidhaa zinazokosa viwango kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa ndani kama mbinu ya kupunguza umaskini na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANTRAD*E Zanzibar, kwa mujibu wa nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Tanzania Toleo la mwaka 1977 biashara za nje ni jambo la Muungano. Hata hivyo, katika kipindi kirefu uendeshaji wa jambo hili haukuzingatia matakwa hayo ya kikatiba kikamilifu. Naipongeza Wizara kwa kuanzisha Ofisi ya *TANTRADE* kuwepo na kuonekana kuwa ni taasisi ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo uliopo wa kufungua ofisi ya mtu mmoja ni kichekesho kwa kuwa ni sawa na kuwa hakuna kilichofanyika. Ninachojua ni kwamba, mfanyakazi wa *TANTRADE* ni mama na mara nyingi anakuwa yupo kwenye likizo za mzazi na kazi za ofisi kutofanyika. Hivi mnavyoandika najua kwamba mfanyakazi huyu yupo masomoni nje ya nchi na ofisi hiyo haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri waongezwe watumishi kwenye ofisi hii lakini pia ipatiwe vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri aliyowasilisha Bungeni pia nimpongeze Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu ya Tanzania kuna mifumo miwili ya ajira. Aidha, Serikalini ama katika sekta binafsi. Kulingana na takwimu zilizopo sasa zinaonesha kwamba sekta binafsi imechukua nafasi kubwa sana katika kutoa ajira kwa Watanzania. Kwa maana hii Wizara ya Viwanda na Biashara ni muhimu sana kuja na mikakati madhubuti ya namna ya kuboresha utendaji wa sekta hii. Mara nyingi utafiti umeonesha kwamba wananchi walio katika sekta binafsi hawana ujuzi wa kutosha. Ndiyo maana wanapoanzisha biashara katika kipindi cha mwaka mmoja biashara hizi hufa. Kwa maana hiyo ujuzi katika uendeshaji wa biashara hizi unahitajika sana. Nitoe wito kwa Wizara hii ibuni mkakati wa namna ya kufikisha mafunzo ya ujasiriamali kwa wafanyabiashara wadogo hasa walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuwawezesha wananchi kutambua namna ya kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali walizonazo wananchi wenyewe na hatimaye kuwawezesha wafanyabiashara kwa kuwaongezea mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni ombi katika Mkoa Mpya wa Geita na Kanda ya Ziwa, hatuna Kiwanda cha Saruji. Hii inapelekea bidhaa hii muhimu kuwa ghali sana kutokana na gharama za

usafirishaji na bidhaa hizi kutoka katika maeneo ya uzalishaji. Maendeleo ni pamoja na kuwa na nyumba na makazi bora. Niiombe Wizara ione uwezekano wa kujenga Kiwanda kikubwa cha Saruji, Geita ili kutoa huduma kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine linahusu kujengewa soko la Kimataifa la nafaka Katoro. Soko hili litahudumia masuala ya nafaka ndani katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na nchi jirani za Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la mwisho linahusu Viwanda vidogovidogo. Kwa kuwa katika Jimbo la Busanda na Geita kwa ujumla tunapata umeme wa uhakika, naomba Serikali initafutie wawekezaji watakaojenga viwanda vya *juice*, Viwanda vya Kusindika Samaki ukizingatia *raw material* zipo kwa wingi sana. Geita inalima matunda (mananasi) kwa wingi sana na pia wapo samaki kwa wingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba Serikali inisaidie katika haya. Naunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri na Naibu Waziri katika Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuchaguliwa kushika nafasi hizo. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia jambo moja tu. Nataka kujua ni lini masoko ya Kimataifa ya mpakani yaliyoainishwa na Wizara; ya

Mnanila, Kilelema na Kibande Wilaya ya Buhigwe mpya (zamani Kasulu-Kigoma) yataanza kujengwa. Naomba Waziri atueleze?

**MHE. SALEHE A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja. Nawapongeza kwa hotuba nzuri, inaonekana Wizara hii imeanza vizuri katika kufufua viwanda. Mchango wangu ni kwamba, sasa wakati umefika wa kuacha kuuza *raw materials* kama pamba, ngozi na kadhalika. Tuimarishe viwanda vya nguo na au kutengeneza nyuzi, kuimarisha viwanda vya ngozi badala ya kuunza ngozi ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha *EPZ/SEZ*, Wizara ime-*identify* maeneo mengi ya kuanzisha *EPZ/SEZ* na kutwaa maeneo mengi kwa ajili hiyo. Lakini bado *Authority* inayohusika haijalipa fidia kwa maeneo waliyotwaa kwa muda mrefu, suala hilo lipo Mkoa wa Tanga, Ruvuma na kwengineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la Kimataifa la Matunda na mbogamboga Segera. Wizara iliandaa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanzisha soko la Kimataifa pale Segera. Je, upembuzi huo umekamilika na mradi huu utaanza lini? Mpango huu ukikamilika utaimarisha uchumi wa Mkoa wa Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Sukari, nchi yetu inayo maeneo makubwa yanayofaa kwa uzalishaji wa sukari kama Bonde la Mto Pangani. Iwapo yataanzishwa mashamba makubwa, itapunguza hoja ya kuagiza sukari toka nje na hivyo

kuhifadhi fedha za kigeni. Je, kuna mpango wowote wa kuanzisha Kiwanda eneo la Pangani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya *ODOP*, je, programu hii imefikia wapi na inaanza lini? Je, ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya mradi huu? Je, Wilaya ya Pangani imetengewa kiasi gani kwa mradi huu?

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga Kiwanda cha Sukari Wilayani Serengeti. Kutokana na uwepo wa eneo la kutosha (hekta arobaini na mbili elfu) la kulima katika Bonde la Mto Mara ni vizuri Serikali kupitisha Wizara ya Viwanda kujenga Kiwanda cha Sukari kwa sababu bonde hili ni zuri pia eneo hilo hekta arobaini na mbili elfu linafaa na Serikali ilikuwa na mpango huo mwaka 1976 kwa kusaidiana na nchi ya Yugoslavia. Mpango huo mzuri umeishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga Kiwanda cha kutengeneza Mafuta ya Alizeti. Kwa vile Wilaya ya Serengeti inafaa sana kwa kilimo cha alizeti, wananchi wamehamasika sana juu ya kilimo hicho, ni kwa nini Serikali isishirikishe wadau wengine ili kuanzisha Kiwanda cha Mafuta ya Alizeti na hii itatoa ajira kwa wananchi wa Serengeti hususani vijana. Pia itasaidia kupunguza vitendo viovu kama wizi ujambazi na ujangili katika Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Mkakati mzuri wa SIDO nchini ni vizuri *SIDO* iimarishwe kwa sababu itawasaidia wananchi kwa ukaribu zaidi na pia kuwawezesha kuimarisha ujasiriamali. *SIDO* ipewe

mafungu ya kutosha na hii itapunguza sana ujangili katika hifadhi ya Taifa ya Serengeti. *SIDO* ndiyo itakomboa Watanzania kuibua vipaji na nchi zilizoendelea duniani walioanza hivyo na pia *SIDO* itatusaidia kuingia katika uchumi wa kati duniani. (*middle earning country*) shilingi bilioni nne hazitoshi waongezewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya utafiti wa vyanzo vya umeme. Wilaya ya Serengeti ina vyanzo vizuri vya asili, kama gesi na maporomoko ya maji, Mto Mara (Balagonja).

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimwa Spika, Serikali inahitajika kufufua Viwanda vya ndani. Hata hivyo, Serikali inaeleza kuwa Viwanda vilivyobinafsishwa vina utendaji mzuri, bado tunaona kuwa viwanda vingine vimefungwa na au kuuzwa kwa mali moja moja (*asset stripping*). Serikali itoe taarifa ya kina juu ya viwanda hivi na matatizo yanayokabili viwanda hivi. Wizara iweke mkakati imara wa kufufua na kuendeleza viwanda vya ndani. Kwa kuwa viwanda hivi vitaongeza ajira urahisi wa upatikanaji wa bidhaa ndani ya nchi kuliko kupokea bidhaa toka nje ya nchi ambavyo baadhi yake havina ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya viwanda vidogo. Walengwa wa mradi wa MUVI ni wakulima na wananchi walio vijijini ambao hupata mafunzo ya kilimo, masoko na teknolojia rahisi ili kuwaunganisha na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo yenye masharti nafuu lengo la programu hii ni nzuri. Lakini bado Serikali inahitajika kuongeza fedha zaidi katika

programu hii ili kuwafikia wakulima wengi zaidi katika Wilaya mbalimbali. Hata hivyo, Wizara ishirikiane na Halmashauri za Wilaya ili kuleta ufanisi katika programu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa sukari. Katika miezi iliyopita tumeona wananchi wakirudi kupanga foleni kama enzi za mkoloni kutafuta sukari, jambo ambalo linapelekea urasimu wa upatikanaji wa bidhaa hii. Serikali lazima ichukue hatua za haraka, nchi inakuwa na sukari ya kutosha kwa kuweka msisitizo wa uwajibikaji wa wafanyakazi wa viwanda, kuondoa urasimu wa bidhaa hii, lakini kubwa ni kuweka mkakati wa kuzuia uuzwaji wa sukari nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Nguo. Baada ya zoezi la ubinafsishaji wa viwanda taarifa zinaonesha viwanda vingi vimekufa na kubaki vitano tu vingine vipo mbioni kufungwa jambo ambalo linalenga kupunguza ajira na wakulima wa malighafi ya viwanda hivi kukosa soko la bidhaa zao. Mfano, wakulima wa pamba kwa sasa wanakabiliwa na tatizo kubwa sana la uuzaji wa pamba. Serikali iweke mkakati wa kunusuru Viwanda hivi vya Nguo ili wananchi wetu wasivae nguo zinazotoka nje ya nchi na wajivunie utamaduni wa kuthamini nguo za ndani ya nchi.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha Watanzania tunaposikitika kwamba vijana wetu wengi hawana ajira kwani pia hapana anayepinga kwamba Viwanda duniani kote ndio sekta ambayo inabeba vijana wengi katika ajira. Lakini kama haitoshi basi pia viwanda ndivyo

vinavyosaidia lile tatizo la bidhaa za kilimo (matunda) kuweza kuyahifadhi ili matunda hayo yaweze kuendelea kupatikana kwa kipindi chote cha mwaka tofauti na hali ya sasa kwamba msimu ukiisha na matunda nayo hayapatikani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Serikali kubinafsisha Viwanda kiholela bila taratibu za kisheria ndio zilizopelekea pia hata wale ambao wanapewa kama wabinafsishaji kuuza viwanda na mara nyingine kukongoa vifaa na kuhamisha kabisa na kwenda kutengeneza viwanda katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile dhana ya Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania; jambo hili nalo linanisikitisha na Serikali inakuwa kama mwigizaji kwani inasema lakini haisimamii inayosema. Mfano, mara kwa mara tunashuhudia baadhi ya majumba na hata Ofisi za Serikali zikiungua moto na kwamba chanzo ni nyaya za umeme pamoja na vifaa vingine vinavyotengenezwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, ni kwa nini Serikali inaruhusu bidhaa toka nje wakati hapa nchini bidhaa za namna hiyo hiyo zinatengenezwa? Kwa nini tusitilie mkazo na kuboresha kwa vile viwanda vyetu ambavyo vina uwezo wa kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kuondokana uagizaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipati tafsiri sahihi ya ubinafsishaji inapotokea kwamba viwanda vilivyo binafsishwa tarkibani vyote kabisa vimeonekana vimekufa, lakini ukiuliza au ukienda ndani zaidi utaona

kwamba viwanda hivyo vimeuzwa kwa bei poa kwa watu maarufu sana na pengine wanasiasa au wenye mahusiano makubwa na ya karibu na pengine na hata waliopata kuwa viongozi wakubwa hapa nchini na baada tu ya kumilikishwa kwao viwanda vinafanya kazi kama kawaida. Mfano, viwanda vya korosho vya Tanita I Mbagala, Tanita II Kongowe, Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba, ikiwa Serikali inakereketwa na vijana kukosa kazi na ukizingatia kwamba viwanda ndivyo vinavyoweza kubeba idadi kubwa ya vijana basi sasa iende iendako lakini ifufue viwanda ili vijana waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Daktari Abdallah Kigoda kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii muhimu kwa Maendeleo ya Watanzania hasa vijana. Viwanda ndio vinavyozalisha ajira na pia ndio vinavyotumia rasilimali ghafi (mfano mazao) toka kwa wananchi wengi hasa walio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara katika kuweka mazingira wezeshi na endelevu kwa ajili ya ukuaji wa viwanda biashara masoko na biashara ndogondogo. Hata hivyo, ningependa kupata ufafanuzi na maelezo ya Wizara katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Mbolea, Tanga. Kiwanda hiki kilibinafsishwa zaidi ya miaka kumi iliyopita, kinachosikitisha ni kuwa toka kibinafsishwe kiwanda hiki hakuna shughuli zozote za uzalishaji zinazofanyika. Mbaya zaidi kiwanda hiki kiko katika *prime area* ndani ya Jiji la Tanga. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini kisirudishwe Serikalini ili kuweza kufanya kazi na kutoa ajira kwa vijana wakazi wa Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha kutengeneza *Juice*- Tanga. Mkoa wa Tanga unajulikana kwa kuzalisha matunda mbalimbali hasa machungwa, maembe, mafenesi, mananasi na kadhalika. Wakulima hasa katika Wilaya ya Handeni, Muheza, Lushoto na Korogwe wanatumia matunda haya. Tatizo kubwa ni soko la kuuzia matunda. Je, ni kwa nini Serikali isijenge na kuwezesha kujengwa kiwanda cha *Juice* Segera au Handeni? Au ni kwa nini pia kusianzishwe soko la Kitaifa la matunda Segera? Nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ina mikakati gani ya kuwawezesha wanawake wajasiriamali wadogo wadogo, wanawake wengi wanajishughulisha na biashara ndogondogo. Lakini changamoto yao kubwa ni mitaji na elimu ya biashara na ujasiriamali. Je, Wizara inafanya nini kwa kundi hili?

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kupata fursa hii muhimu kuchangia

hoja ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili limerudi nyuma sana katika uzalishaji wa bidhaa za usindikaji hasa zinazotokana na mazao ya kilimo na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda ni miongoni, Wizara nyeti sana na ndio tegemeo la uchumi na ukuaji wa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti ya Wizara hii ni ndogo nina wasiwasi mkubwa kuwa haitaweza kukidhi mipango mahsusi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukweli huo ni vema sana tujiulize tunapata wapi rasilimali fedha ili kusaidia kutimiza ndoto na kilio cha Watanzania (vijana) kuhusiana na ajira? Ni vema basi nitoe ushauri ufuatao kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ichukue juhudi za makusudi za kuomba kutengewa maeneo ya viwanda kutoka kila Mkoa na hata Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yatumike kuweka viwanda maalum kwa mpango wa Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo au uwekezaji huu ulingane na uzalishaji wa malighafi zinazozalishwa katika maeneo husika. Hapa mifano michache ni kama utengaji wa eneo mahsusi la kuweka Kiwanda

cha Matunda na Mboga mboga pale Korogwe Mjini. Aidha, kwa maeneo ya madini, basi Wizara iainishe mahitaji ya wachimbaji wadogo na mwisho kwa maeneo ya uzalishaji pamba kuona ni jinsi gani tutaongeza thamani, kutoa ajira na hatimaye kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara na uwekezaji ni nguzo imara ya kukuza uchumi wetu kwa ukweli kuwa tumezungukwa na nchi nyingi jirani tukizalisha vizuri basi tutauza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkakati wa uanzishaji wa viwanda vipya vyenye kutumia malighafi na rasilimali za ndani ni suluhu ya mafanikio kwa jamii zetu. Niishauri Wizara kuimarisha masoko maalum ya bidhaa zinazoagizwa nje kwa mahitaji ya nchi jirani. Hili liende Sanjari na kuimarisha mahusiano na jirani zetu na kutangaza masoko haya kwenye nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wizara kuchagua maeneo ya msingi ya kuanzia hasa Mikoa ya pembezoni mfano Tanga, Mtwara, Mwanza, Arusha na Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa mujibu wa mgawanyo wa rasilimali. Si vyema kwa sasa kurudia kuzungumzia viwanda vilivyobinafsishwa kwani ni sawa na kurejea pale tunapotaka kuondoka. Sasa Wizara ijitathmini na ishiriki kampeni mahsusi wa Wizara za Kazi, Kilimo na Ardhi pamoja na Maendeleo ya Jamii ili kubainisha uwekezaji. Wizara itumie changamoto hizi kwa kushirikisha nchi marafiki na wadau wa maendeleo yetu ili kujua ni jinsi gani tutakomboa Taifa hili kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hotuba ya Wizara na kwamba maoni mbalimbali yatakayotolewa yazingatiwe. Tumpe Uhuru Waziri na kumhamasisha na kumpa ushirikiano ili kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile inaonekana nia nzuri ya Serikali ya kuhamisha maofisi yake Dar es salaam kwenda kuhamia Dodoma utekelezaji wake niwakusadikika zaidi badala ya kutekeleza hatuoni kwamba ipo haja ya kujenga ofisi ndogo kwenye Jiji la Dar es Salaam wakati tukisubiri kujenga Makao Makuu ya Wizara, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kusema hivyo ni matumizi makubwa yanayofanywa na Wizara hii kwa ajili ya ulipaji kodi. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2012/ 2013, jumla ya sh. 720,000,000/=, zimetega kwa ajili ya kulipa matumizi haya, ni mabaya ukilinganisha na uchumi wa nchi yetu. Ni matumizi mabaya ya rasilimali fedha za nchi kama yetu. Hivyo naomba Wizara itazame uwezekano wa kutafuta kiwanja na kujenga ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kutamka kuwa naunga mkono bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango *(TBS)*. Kazi ya shirika hili ni kudhibiti ubora wa vifaa vilivyokuwa havijafikia viwango ili kulinda afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bidhaa nyingi nchini zisizo na ubora, zinauzwa bila ya kificho katika maduka. Bidhaa hizi ni hatari sana kwa afya ya wananchi na lazima hatua za dharura zichukuliwe ili kuepusha maafa yanayoweza kutokea kutokana na kutumia bidhaa feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa ulinzi wa viwanda vya ndani, kuna umuhimu wa kulinda viwanda vya ndani kutokana na ushindani wa bidhaa kutoka nje. Bidhaa za nje zimekuwa zikiuzwa kwa bei ndogo ndani ya nchi yetu kwa makusudi kwa nia ya kuua viwanda vyetu. Bidhaa hizi mara nyingi huwa zenye ubora ulio finyu ukilinganisha na bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri bidhaa kama za nguo (khanga vitenge na kadhalika), bidhaa za mafuta, ngozi na bidhaa nyingine ambazo zinazalishwa ndani ya nchi zipunguziwe ushuru na zile zinazotoka nje zipandishwe ushuru ili viwanda vyetu vikue. Nchi za Mashariki ya mbali zina mikakati kama hii imewezesha kuendeleza viwanda vyao na hivi sasa wanaweza kuuza nje ya nchi.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dakatari Abdallah Omari Kigoda, Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu Waziri Mheshimiwa Gregory George

Teu, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Wakurugenzi wa Idara za Wizara na Watumishi wote, Wenyeviti na Watendaji wakuu walio chini ya Wizara hii kwa kazi wanayofanya ya kusimamia utekelezaji wa sera na Sheria za sekta za Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda. Nawapongeza sana viongozi na watumishi wa *EPZA* kwa jitihada kubwa wanazofanya kuandaa mazingira ya kuvutia wawekezaji kwenye viwanda vya bidhaa zitakazouzwa nje ya nchi. Mkoani Arusha wako wananchi ambao wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu kulipwa fidia ya ardhi yao iliyokaguliwa na kuzuiwa na *EPZA* kwa ajili ya uwekezaji, naomba Waziri awajulishe wananchi hao kupitia Bunge hili tarehe ambayo fidia hiyo italipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya magari. Shirika la Nyumbu lililo chini ya JWTZ lilibuni na kuanza utengenezaji wa magari hapa nchini kwa kuzingatia kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika kuagiza magari toka nje ya nchi, ni muhimu sana Serikali ikawekeza kwenye uendelezaji wa utafiti na utengenezaji wa magari kupitia Shirika la Nyumbu. Ili kufikia lengo hilo nashauri yafuatayo yafanyike.

Serikali iingie ubia na watengenezaji magari kama vile *Toyota Land Rover* na kadhalika ili kupata mtaji wa wataalam. Sera na Sheria ya Viwanda irekebishwe ili

kila gari litakaloagizwa toka litozwe ushuru wa 270 ambayo itapelekwa nyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vidogo. Naupongeza sana uongozi na watumishi wa *SIDO* kwa jitihada wanazofanya kuelimisha kuhamasisha na kuchangia uanzishaji wa viwanda vidogo nchini kwa bahati mbaya Wilaya na Jimbo langu haina hata kiwanda kimoja hadi sasa. Naomba Waziri ahimize uongozi wa *SIDO* wasaidie uanzishaji wa Kiwanda kidogo cha Kusindika miwa na kutengeneza sukari kwenye Kata ya Kimnyak/Olmotonyi ambako miwa hulimwa kwa wingi sana, lakini huishia kuuzwa kwa matumizi ya nyumbani mjini Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ushindani na viwango vya bidhaa. Tume ya Ushindani ilianza kazi miaka kadhaa iliyopita. Majukumu yake yalioainishwa kwenye Sheria ni mengi na makubwa. Hata hivyo, wananchi walio wengi hawana ufahamu wa kuwepo kwa Tume hii. Matokeo yake hawapati fursa ya kutumia huduma zake pale wanapokwazwa na watoa huduma na bidhaa mbalimbali. Nashauri kuwa Serikali kupitia Tume hii itoe elimu kwa Wabunge Madiwani na wananchi kwa ujumla ili waweze kuisaidia Tume kwa kutumia huduma zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuupongeza kwa dhati uongozi na watumishi wote wa *BRELA* kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya kazi zao kwa kujituma. Hata hivyo, kwa uzoefu nilionao kama mtumiaji wa huduma Wakala bado wanakabiliwa na uhaba wa nyenzo na vitendea kazi vya kisasa. Ili

kuboresha huduma za Wakala nashauri kuwa waongezewe fedha ili waweze kupata vifaa vya kisasa na kuboresha maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamka kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja ya Wizara hii nikijikita zaidi kuhusu Kiwanda cha Sukari Mtibwa na kushuka kwa uzalishaji wa sukari nchini. Kiwanda cha Mtibwa bado hakijazalisha sukari kwa kiasi kinachotakiwa. Hii ni kutokana na kuchakaa kwa mitambo, kupungua kwa kiasi cha miwa kutoka kwa wakulima wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji ni mdogo kutokana na mitambo kuchoka. Serikali itoe msukumo wa uwekezaji kukarabati mitambo. Aidha, miwa inayonunuliwa kutoka kwa wakulima wa nje ni kidogo kutokana na kwenda kutohimili miwa iliyopo. Pia bei ndogo ya miwa, kutovunwa miwa kwa wakati, kumepunguza kiasi cha miwa inayolimwa. Ombi langu kwa Serikali na Bodi ya Sukari ni kuomba mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa kipaumbele kununua miwa ya *outgrowers,* kuongeza bei ya miwa kwa wakulima wa nje, Mtibwa ifanane na ile ya Kiwanda cha Kilombero, Serikali ihamishe wawekezaji kuanzisha viwanda vidogo vya miwa, Tarafa ya Turiani ili kuleta ushindani wa bei na pia kuongeza uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atolee ufafanuzi ushauri huu nilioutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SLYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kuipongeza Serikali kwa mabadiliko mbalimbali ya kuboresha biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeendelea kuathirika kiuchumi na hasa kwa kuwa *balance of payment* za kigeni hafifu yaani kutumia fedha nyingi kununua vifaa toka nje na wakati nchi inapata fedha kidogo za kigeni kwa kuuza vichache vizalishwavyo au malighafi nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ya kuboresha na kuimarisha fedha yetu dhidi ya fedha ya kigeni ni kuongeza thamani ya bidhaa tunazozalisha kuanzia za kilimo, madini na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kiasi kikubwa cha mazao yetu ya biashara kinauzwa nje kikiwa malighafi. Maana yake tunatoa ajira na malighafi kwa nchi za wenzetu. Bidhaa hizo hizo ndizo aidha, zinarudishwa hapa nchini tunazinunua kwa gharama kubwa au zinauzwa nchi nyingine za ng’ambo kwa thamani kubwa na kwa faida ya nchi inayozizalisha viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Marekani waweza kula korosho ambazo zinatoka India kumbe ni hizo hizo za Mtwara, bei yake ni zaidi ya mara ishirini ya bei inayouzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara sasa ihimizwe na kwa makusudi kabisa isaidie mipango maalum ya kuchochea viwanda vya ndani. Kwa nini tusiangalie wenzetu hata wa Afrika Mashariki na Asia wanafanyaje? Hebu fikiria Tanzania inaongoza kwa ng'ombe na mbuzi Afrika Mashariki, lakini inanunua nyama nyingi na kwa gharama kubwa kutoka Kenya, shida ni kukosa ng'ombe walio na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara sasa ifanyie kazi jambo hili ambalo sasa linatufanya kuwa kichwa cha mwendawazimu kwenye viwanda liwe basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo kubwa katika ubinafishaji, nia ya Serikali ya kubinafsisha Mashirika na Makampuni yake kwa watu binafsi sio tu haikutekelezwa vyema bali hata waliouziwa au kupewa mashirika haya hawatekelezi masharti na kufanya makampuni na viwanda hivi kudorora au kufa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha zaidi ni kuwa viwanda vingine na mfano mzuri ni Kiwanda cha *TANITA* kilichopo Kibaha Mjini kilichokuwa cha kubangua korosho. Kwa zaidi ya miaka mitano kimekuwa gofu na haieleweki mwekezaji ana nia gani kulingana na matakwa ya masharti ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi yetu ina nafasi na fursa nyingi za uwekezaji, Watanzania wengi tayari wana uwezo mkubwa wa kielimu, kifedha na uzoefu

(*capacity)*. Cha msingi Serikali iweke utaratibu wa upendeleo kabisa katika kuwapa Watanzania kipaumbele katika miradi mbalimbali ya uwekezaji. Kuna tatizo gani mamlaka na taasisi husika kuja na mpango maalum utakaowaunganisha wafanyabiashara Watanzania kuwekeza katika sekta muhimu ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati uwekezaji wa moja kwa moja (*direct investment*) kutoka nje tunaukaribisha lakini na sisi sasa tusimamie Sheria na kanuni zetu za uwekezaji na kuona basi kwamba zile huduma zote muhimu katika uwekezaji zinatolewa na Watanzania na makampuni ya Kitanzania ili kupeleka manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wa Wizara hii kwa majukumu mbalimbali yanayowakabili hasa katika kuiongoza Wizara hii. Katika kuchangia hoja, binafsi nitajikita kuuliza maswali mbalimbali ambayo yakijibiwa yatakuwa ni msaada mkubwa katika kuleta ufanisi kwa jamii ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZA* lengo lake lilikuwa ni zuri, lakini hadi sasa inaonekana dhahiri kuwa lengo hilo halitatimia kwani mipango mingi haijatekelezwa. Swali Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kuhakikisha kuwa lengo la *EPZA* linakamilika ili kuweza kutoa ajira kwa Watanzania? Je, Serikali imekwishalipa fidia halali

kwa wananchi wote waliochukuliwa maeneo yao ya ardhi kwa ajili ya *EPZA*? Kama hawajalipwa Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha inawalipa fidia mara moja haraka iwezekanavyo wananchi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa hapa nchini hadi sasa ni muda mrefu havifanyi kazi vizuri au havifanyi kazi kabisa na mbaya zaidi vingine vimekwishabadilishwa matumizi bila hata kibali cha Serikali. Je, Wizara imechukua hatua gani dhidi ya wamiliki waliobinafsishiwa viwanda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba ni muhimu sana kwa utengenezaji wa nguo hapa nchini. Kuna magofu mengi ya majengo ya viwanda vya nguo vilivyoitwa *Mutex, Sunguratex, Kiltex, Mwatex*, Urafiki na kadhalika. Baadhi ya viwanda vimebinafsishwa kwa wawekezaji uchwara ambao wameanza kazi ya uzalishaji na baadhi ya wengine hawajaanza kazi ya uzalishaji. Je, Wizara ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha kuwa viwanda hivi vyote vinazalisha na vinatumia malighafi ya pamba inayozalishwa hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Tanzania hasa enzi za Mwalimu Nyerere kulikuwa na aina mbalimbali za viwanda vilivyokuwa vimeanzishwa kwa lengo la kuzalisha bidhaa zetu hapa nchini. Baadhi ya viwanda hivi hadi sasa vipo na vinaonekana kwa macho. Je, Serikali imebinafsisha viwanda vingapi hadi sasa? Je, Serikali ina miliki viwanda vingapi hadi sasa? Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vipya hadi

sasa hivi? Je, ni pato la Taifa kiasi gani linalopatikana kutokana na sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha uchapishaji na uchapaji wa vitabu cha *Afroplus Industry Limited*, kilichoko eneo la Mwenge jijini Dar es salaam kilibomolewa na Mtume Mwingira kwa kutumia mabavu na maguvu hali imesababisha ukosefu wa ajira kwa wafanyakazi waliokuwa wanafanyakazi kwenye kiwanda hiki. Serikali inalifahamu tatizo hili? Kama inalifahamu imechukua hatua zipi? Kubomoa kiwanda cha *Afroplus Industries Limited* kwa kutumia maguvu na mabavu kumerudisha nyuma maendeleo ya uchapaji wa vitabu hapa nchini hasa kwa wajasiriamali wadogo wadogo. Je, mtuhumiwa wa sakata hili amechukuliwa hatua gani hadi sasa? Kwa nini nchi yetu inashindwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo kama vile saruji, kusindika vyakula, mafuta, teknolojia rahisi na kadhalika. Kwa lengo la kutoa ajira kwa vijana wetu? Serikali ina mkakati gani wa haraka kati na muda mrefu kutekeleza azma hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wamiliki wa viwanda hapa nchini hasa wageni kuwanyanyasa, kuwaonea na kuwadhulumu wafanyakazi wazawa. Hali hii hupelekea wazawa kufanyishwa kazi ngumu kwa kupewa ujira mdogo, wengine wanafanya kazi bila mikataba. Je, Serikali kupitia Wizara hii inalifahamu hilo? Kama inalifahamu imechukua hatua zipi za makusudi ili kukomesha tabia hii? Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira inateteaje haki za wazawa wanaonyanyasika katika viwanda vya Wahindi na Waarabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tarime imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya uzalishaji mali kama vile mgodi wa dhahabu wa *North* Mara, mpaka wa Sirari, mazao ya biashara kama vile kahawa, chai na tumbaku. Lakini hakuna hata harufu ya kiwanda chochote Wilayani Tarime. Serikali inawashauri nini wananchi wa Tarime? Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kuanza kuwekeza katika viwanda vya kimkakati ili viweze kuleta mabadiliko ya kiuchumi Wilayani Tarime pamoja na sehemu nyingine za Tanzania zinazofanana na Tarime?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atafika lini Tarime ili aweze kushauri juu ya uanzishwaji wa viwanda vya kuongeza thamani mazao? Mkulima wa nchi yetu kuuza bidhaa au mazao yake yakiwa ghafi. Hali hii husababisha mazao haya kuuzwa kwa bei ya chini sana. Hali hii inatokana na tatizo la ukosefu wa viwanda. Serikali imelifumbia macho suala hili kwa muda mrefu. Swali kwa nini iwe hivyo kwa Serikali? Je, Serikali inawatendea haki wakulima wake? Je, Mheshimiwa Waziri una mkakati gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya maendeleo endelevu ya viwanda (*sustainable industrial development policy – STDP*) haijaleta faida yoyote hapa nchini zaidi ya porojo tu za kisiasa. Swali, Waziri anatueleza nini juu ya matatizo, mafanikio na changamoto tangu kuanzishwa kwa *STDP* hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* maeneo ya vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wajasiriamali hawana taarifa za kutosha kuhusu namna ya kupata masoko ya bidhaa zao hasa nje ya nchi. Pia baadhi yao wamekuwa wakijihusisha na biashara ndogondogo toka China, Dubai, Turkish, Hongkong, Thailand na kadhalika. Je, Serikali kupitia Wizara hii inafanikishaje upatikanaji wa taarifa za masoko kwa wajasirimali hao. Serikali ina mkakati gani wa kuwakopesha wafanyabiashara hao wadogo mitaji isiyo na riba? Kwa nini hakuna Tume ya Bei hapa nchini Tanzania? Ni lini nembo za mistari zitaanza rasmi kutumika hapa nchini? Serikali ina mpango gani wa kufanya ukanda wa Tarime na Sirari, Wilayani Tarime kuwa ukanda maalum wa biashara? Ni kwa nini biashara nyeti hapa nchini zimeshikwa na wageni? Je, Wizara imejipanga vipi kujenga masoko ya kisasa na yenye hadhi katika mipaka ya nchi hususani eneo la Sirari, Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zinazokaguliwa nje ya nchi kabla ya kusafirishwa kuja hapa nchini kuhusisha sana suala la rushwa kama ilivyokuwa *TBS*. Je, Serikali kupitia Wizara hii inalifahamu hilo? Imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vilivyobinafsishwa kwa

wawekezaji na sasa ama vimekufa au vimesimama. Serikali ichukue maamuzi magumu ya kuvirudisha Serikalini kwani hakuna nchi inayoendelea kwa bidhaa za kuagiza toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Korosho vilivyobinafsishwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara virudishwe Serikalini ili kutoa fursa na ajira kwa wakazi wanaozunguka viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Samaki. Kuna uhusiano baina ya kushuka kwa bei ya samaki, hivyo kufanya wafanyabiashara wa samaki kupeleka bidhaa hiyo kwenye viwanda vya Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo vidogo. Kuwa na viwanda vidogo vidogo vitawezesha wajasiriamali wadogo wadogo kupeleka mazao yao kama matunda kwenye viwanda vile ili kunaletea kipato wajasiriamali.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya utumishi wake kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri viwanda vyote vilivyobinafsishwa ambavyo havizalishi, Serikali wakae na wawekezaji ambao walinunua viwanda hivyo na ikiwezekana kupita meza ya mazungumzo waweze kupata suluhisho la kuendeleza viwanda hivyo kwa maslahi ya pamoja na ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo katika vikundi vidogo vidogo hasa vya kubangua mazao kama korosho ni muhimu sana kwa kuinua uchumi wa Taifa letu.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Daktari Abdallah Omari Kigoda na Mheshimiwa Gregory Teu kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii kubwa na pana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuiongezea bajeti *EPZA*. Naamini kwa dhati kuwa chini ya uongozi makini wa Daktari Meru, *EPZA* itaweka mazingira safi na viwanda vitajengwa kwa kasi tunayoitaka sote. Pili, naomba jitihada hizo hizo zifanywe kwa *SIDO*, kila mmoja wetu anafahamu kazi kubwa iliyofanywa na *SIDO* na *potential* kubwa ya *SIDO* katika kuendeleza sekta ya viwanda na biashara ndogo ya nchi hii. Tatu, naomba majukumu ya *FCC* na yale ya *TBS* yawekwe bayana sasa hivi kuna kuingiliana kwingi.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wao wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wanafaidika na Sekta ya Biashara na Viwanda kwani nchi bila Viwanda haiwezi kwenda na bila viwanda hakuna biashara iliyotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda ni muhimu sana kwa maendeleo ila inaonekana kwamba

viwanda vingi Tanzania hii vimekufa. Angalia Urafiki leo hii kuna gofu kuna ghala la chuma chakavu. Yule mwekezaji aling'oa mpaka ule mtambo, ameacha vyuma, mabati mabovu na kadhalika. Tanganyika *Packers* kimekufa na nyingine vingi tu ambavyo sina muda wa kuvitaja. Lakini Serikali inajua kila kitu, ni ufuatiliaji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali waipe kiupambele *SIDO* waweze kuendeleza viwanda vidogo vidogo. Tanzania kuna matunda mengi yanahitaji kusindikwa ili tunyanyue ajira kwa vijana, tunyanyue uchumi wetu kwa kukuza wigo wa biashara ili tuwakomboe wananchi kutoka katika hali ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukaguzi wa magari nje ya nchi bado ni utata, kwa nini Serikali isiweke sharti la kwamba gari inayotakiwa umri huo ikiingia nchini itozwe ushuru mara mbili kama vile Zanzibar wanavyofanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo hili la wafanyabiashara wa ngozi (WANGOT) na hawa *LAT*. Naiomba Serikali suala hili walishughulikie kwa haraka ili Watanzania wadau wa ngozi waweze kufanya biashara vizuri bila matatizo kwani inaonesha kwamba hawa wanunuzi wa ngozi wanasafirisha ngozi ghafi jambo ambalo ni kinyume na taratibu (wenye viwanda).

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Katika

mapitio ya Bajeti ya 2011/2012, zipo changamoto kadhaa katika ukuaji viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya pombe, vimekuwa kwa asilimia inayoridhisha kuliko viwanda vingine ni *blessing.* Lakini ni changamoto kwa sura yake kwamba Watanzania tunatumia mazao ya viwanda hivyo zaidi *implication* yake kwa maendeleo haiwezi kuwa mzuri kwa maendeleo ya mtu lakini pia kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiukwaji wa viwanda vingine, uliathiriwa na tatizo la umeme zaidi kama Taifa tunatakiwa tulione kama Taifa namna ya kuondoa kipingamizi hili la maendeleo ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *agro-processing* and *agri-business*, eneo hili lifanyiwe kazi kwani ni *potential.* Lakini bado hatujawekeza vya kutosha wakulima wanajitahidi sana kuzalisha lakini thamani ya mazao yao imebaki kuwa chini. Naomba yatengenezwe masharti ya wawekezaji katika sehemu ya kilimo Ziwa Tanganyika linatoa samaki wengi, lakini hakuna mchango wake kwa maana kwa sababu hakuna viwanda vya kuongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusindika samaki, mahindi, ulezi, maharage, mazao haya yanapatikana sana Rukwa. Lakini kuna viwanda vichache tu vya kusindika vya mahindi pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vidogo Rukwa. Rukwa kuna Shirika la Viwanda vidogo (*SIDO*) na lina mchango mkubwa Mkoani Rukwa.

Kinachokosekana ni mtaji mdogo wa kuwawezesha wajasiriamali waliomo Mkoani Rukwa. Naomba wapewe pesa za kutosha ili waendeleze kazi yao nzuri ya kuongeza ajira mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla uzalishaji katika viwanda vyetu lazima uweze kujali ubora ili kuleta ushindani katika masoko ya Kikanda *East Africa Corporation SADC* na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ukilinganisha sekta ya biashara baina ya Tanzania na majirani zake. Naona tuna fursa nzuri, lakini zaidi hasa katika bidhaa za viwanda na kwao zinaleta ushindani zaidi kwa maana hiyo tuboreshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matangazo katika bidhaa za Kitanzania bado hayajaboreshwa ukilinganisha na jirani zetu hasa Kenya. Sisi tunaishia kulalamika kwamba Wakenya wanatangaza bidhaa zetu au mali zetu badala ya kuleta mfumo utakaowaibisha bila malalamiko. Mfano, Mlima Kilimanjaro uko Kenya au Tanzania? Ni jambo la utaalam na ufundi wa matangazo ndio unaweza kujibu hilo 'tuwe wabunifu'.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kufanya zao la michikichi kuwa biashara. Naomba Wizara itazame uzoefu wa nchi ya Malaysia kuona namna zao hili linavyochangia *scheme* kubwa ya biashara nchini kwao na duniani. Malaysia ilikuja kujifunza zao hili Kigoma mwaka 1990. Naishauri kupitia *SIDO* Serikali ianze mchakato wa kuongeza thamani ya

mazao ya michikichi. Kwa mfano, makuti ya michikichi yanatumika Rwanda kutengeneza vikapu vya kifahari vinavyouzwa katika soko la *AGOA*. Maganda ya mise yanatumika kutengeneza vigae vinavyotumika kujenga nyumba za kifahari; *SIDO* wanaweza hapa kwetu.

Mafuta ya mise yanatengeneza sabuni, mabaki ya mafuta yanatengenezwa kuwa mafuta mazito ya kulainishia mitambo Malaysia. Haya yote tunaweza kuyafanyia kazi kuchochea soko la biashara la zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya maziwa. Ndani ya Wilaya mpya ya Uvinza tuna shamba lililokuwa *ranch* ijulikanayo kama Malagasi au Malahi. Hapa kuna ng'ombe zaidi ya laki moja. Maziwa yanayozalishwa hapa yanazikwa kwa kuwa hakuna mfumo wa kuyatunza au kusindika au kuyafanya yadumu kwa muda bila kuharibika. Naishauri *SIDO* itumike kuangalia fursa hii tuone namna ambayo tunaweza kuongeza thamani ya maziwa na maslahi ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya samaki. Ndani ya Mkoa wa Kigoma tunalo Ziwa na Mito kama Malagarasi. Hapa kuna uzalishaji mkubwa wa samaki. Lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kujenga hata viwanda vidogo vidogo vya kusindika samaki hawa na hakuna mkakati wowote wa kufanya eneo hilo lichochee biashara ya mazao ya Ziwa na Mito ili kujenga uchumi na biashara katika eneo hili. Kuna hoja ya umeme, lakini tangu mwaka 2010 Kigoma ina ziada ya 4MW ambazo haitumiki. Naomba sana jicho la

Mheshimiwa Waziri katika Viwanda na Biashara litazame Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubinafsishaji kiwanda cha chumvi. Naendelea kusisitiza kiwanda hiki kirejeshwe kwa Serikali kwa sababu mwekezaji huyu kauziwa kiwanda kwa milioni 900, lakini ameng'oa mitambo yote ya *plant* ya *PVD* na kuuza bilioni 4.5. Huu ni ujuha tu unaoweza kukubali hali hii. Ni mfano mbaya wa kifisadi usiomwogopa Mungu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, kaka yangu Mheshimiwa Abdallah Kigoda, kwa kuteuliwa kuwa Waziri mwenye dhamana. Uteuzi huu umenifariji sana, kwani natambua uwezo wake wa usimamizi na ufuatiliaji. Vile vile niendelee kuwapongeza Naibu Waziri - Mheshimiwa Gregory Teu, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii mahiri sana, yenye mwelekeo wa kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, kuna viwanda vingi nchini ambavyo uendeshaji wake hauna tija na husababisha hasara kubwa na vingine vimefungwa bila sababu zozote za msingi. Naishauri Serikali kukaa na kutafakari namna ya kufufua na kuboresha viwanda vyetu, ili viweze kuongeza uzalishaji pamoja na kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kuingia kwenye Soko la Kimataifa. Hii itasaidia bidhaa zetu kuuzwa nje ya nchi kwa lengo la kupata fedha za kigeni. Vilevile, wananchi wataacha

tabia ya kupenda kununua bidhaa za nje na kuzidharau za kwetu, jambo ambalo siyo zuri. Naomba mkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na utaratibu wa Serikali wa kubinafsisha viwanda. Mfano, Kiwanda cha Sigara, Kiwanda cha Bia, cha Dar es Salaam na Viwanda vya Simenti, kwani vina tija sana na kwa uendeshaji wake, naona kuna kiwango na nchi yetu inanufaika. Tatizo lipo kwenye viwanda vya kilimo. Mfano, Viwanda vya Korosho, Viwanda vya Pamba, Viwanda vya Katani na vinginevyo. Naiomba Serikali kuvifufua viwanda hivi kwa njia yoyote yenye tija hata kwa kuvipa Vyama vya Ushirika au wawekezaji wenye uhakika wa kufanya kazi vizuri. Nasubiri maelezo ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza sana juhudi za viwanda vidogo vidogo, hususan Mkurugenzi wa *SIDO* Singida, ambaye ni mwanamke shupavu na makini katika kazi zake. Amejitahidi sana kuelimisha jamii, hususan wanawake na vijana, ambao wako mstari wa mbele kuondokana na umaskini kwa kuendesha semina, warsha na kutoa mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijitahidi kupeleka fedha za kutosha *SIDO,* kwani wananchi masikini ndiko waliko na wananufaika sana. Huyu Mkurugenzi wa *SIDO* Singida, naomba atembelewe, atiwe moyo, aongezewe fedha na hata kufikiriwa kupandishwa cheo; italeta changamoto hata kwa

Watendaji wengine kutekeleza wajibu wao. Naiomba Serikali iseme neno wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana wafanyabiashara wa Viwanda vidogo vidogo vya binafsi kwa kazi kubwa wanayofanya, kuwasaidia wakulima wetu kupata maeneo ya karibu ya kupeleka mazao yao. Mfano, wakulima wa zao la Alizeti Singida, wanapata unafuu wa kutopeleka alizeti mbali kwenda kukamua mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu hapa kwa Serikali, ni kuwawezesha wafanyabiashara hao kwa kuwakopesha ili waweze kununua mashine kubwa zenye uwezo wa kusafisha mafuta mara mbili. Naomba maelezo ya Serikali, kama imetenga Mfuko wa Kukopesha Wafanyabiashara hawa wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Serikali kusimamia kwa karibu zoezi la kufufua Kiwanda cha Matairi cha Arusha, kwani matairi yake yalikuwa na kiwango na yalikuwa yanadumu. Tukifufua kiwanda cha matairi, itasaidia watumiaji wa matairi kupunguza kununua matari ya nje ambayo mengine hayana ubora, hupasuka mapema watumiaji wanapoyatumia. Hali hii huhatarisha maisha ya wasafiri wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea hoja yangu itachukuliwa, hivyo ninaunga mkono hoja nikijua kwamba, hata viwanda vya kusindika ngozi huko Singida na vya kusindika Maziwa, vitapelekewa Wataalam na kupewa fedha za kuviendesha ili viweze kuzalisha bidhaa zenye ubora.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli huu ni wakati muafaka kwa nchi yetu kuwa na viwanda vidogo vidogo. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba bidhaa nyingi zinazouzwa hapa Tanzania ni kutoka nje ya nchi. Ukiangalia mfumo huria wa kuagiza au kuruhusu bidhaa toka nje umepelekea kupokea bidhaa ambazo viwango vyake ni vidogo na havikidhi haja na ni hatarishi kwa afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni vyema nchi yetu ya Tanzania ikaweka mikakati ya kuwapa motisha maalum Watanzania wenye uwezo ili kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa hapa nchini na kupiga marufuku bidhaa feki toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanao uwezo wa kufanya yote hayo ila kinachohitajika ni Wizara kuandaa Mikutano maalum na wafanyabiashara wa ndani ili wawape miongozo ya namna gani Serikali itawapatia *incentives* na kuanza biashara ya viwanda badala ya kuagiza bidhaa toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayozalisha matunda wapewe mikopo ili wazalishe *juice* badala ya kuwaacha wakulima wa matunda kuona mazao yao yanawaozea mashambani. Maeneo ya ukanda wa Bahari wazalishe samaki, wasindike ili wauzwe ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala la *VAT* liondolewe kwa muda ili wamiliki wa viwanda waweze kuzalisha na iwapo biashara itaendelea vizuri, hivyo baadaye wataweza kurudishwa awamu kwa awamu katika ulipaji wa *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bidhaa ya maziwa ni muhimu ikapewa uzito kwa wingi na tunaweza kutumia wenyewe na nyingine kusafirisha badala ya sisi kuagiza. Hii ni aibu kwa vile sisi ni wazalishaji wakubwa wa bidhaa hiyo hasa ukizingatia kwamba tunao ng'ombe wengi. Hivyo kama mwamko wetu utakuwa wa kiviwanda, tatizo la ajira litapungua kwa kiasi. Yote haya yanahitaji ujasiri wa maamuzi na siyo wa maneno kama ilivyo kawaida yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu ni kuomba basi Wizara husika kutenga fedha maalum za kusaidia wale wote wenye dhamira ya kuanzisha viwanda vidogo kila bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuhakikishe kila mwaka tunafungua angalau viwanda kumi vipya ili soko la Afrika Mashariki liwe linahodhiwa zaidi na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini chini ya Mheshimiwa Dkt. Kigoda yanawezekana, kwani uwezo mkubwa alionao unaweza kutukomboa kiuchumi. Hongera Mheshimiwa Waziri, tekeleza ujenge vyema heshima yako na ya nchi na utukomboe na dimbwi la umaskini tulilonalo.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi kuu, kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupiga hatua katika maendeleo ya kiuchumi, ni muhimu nchi yetu kujenga viwanda vya kutosha na hivyo kuwapatia Watanzania ajira na hasa vijana ambao walio wengi, hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* inafanya kazi nzuri, lakini mashine zinazouzwa na *SIDO* Dar es Salaam ni ghali sana. Kwa mfano, mashine ya kutengeneza sabuni, mashine ya kukamua/kusafisha mafuta ya alizeti *SIDO* iangalie uwezekano wa kupunguza gharama za mashine hizi ili wajasiriamali wengi zaidi waweze kujikwamua kiuchumi kwa kununua mashine/mitambo hii hapa nchini na hivyo kujikwamua kimaisha. Pia wajasiriamali wasindikaji vyakula watafutiwe soko la nje ili wanufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie umuhimu wa kufufua viwanda vya nguo vilivyofungwa ambavyo vilikuwa vinatoa nafasi nyingi za ajira kwa wananchi. Kiwanda cha *Kiltex, Sungurates*, *Mwates, Mutex* na kadhalika. Aidha, kiwanda cha Urafiki ambacho uzalishaji wake umesimama na ambacho Serikali ina hisa 49% haijulikani nini kinachoendelea kiwandani hapo. Mwaka 2011, mabasi ya Kichina yalionekana yamepangwa katika uwanja wa kiwanda hicho. Jambo lililoashiria kwamba kiwanda hicho kimegeuzwa kama *show room* ya biashara ya magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wafanyakazi ambao waliosimamishwa, walilipwa kiinua mgongo

kidogo sana. Napendekeza Serikali kufuatilia ili kubaini ni kitu gani kinachoendelea katika kiwanda hicho na hatua stahili ziweze kuchukuliwa. Napendekeza kiwanda cha *General Tyre* pia kifufuliwe kwa haraka ili wananchi wanufaike kwa ajira na kuinua uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji kazi wa Shirika la Viwango *TBS* bado haurithishi. Lmekuwa ni jambo la kawaida katika maduka yetu kwa mfano, vifaa vya *spea* za magari, mnunuzi huulizwa au hata kuonyeshwa *spea* mbili na kuambiwa moja ni halisi *(original)* na nyingine ni (*fake)* bandia. Wauzaji hawa bila hofu yoyote wanajipatia faida kubwa kwa kuuza vifaa bandia. Ni aibu kwa Taifa letu kwamba hata madawa bandia yamejaa madukani. Kuna baadhi ya wagonjwa walifariki kwa kutumia madawa ambayo yalisadikiwa kuwa ya bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie utendaji kazi wa Maafisa wa *TBS* wanaothibitika kuwa na utendaji usiokidhi viwango katika uwajibikaji, basi wachukuliwe hatua pamoja na kufukuzwa kazi.

**MHE. MUSTAPHA BOAY AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naanza kwa kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa kukataza usafirishaji nje (*export)* wa ngozi na kuamua viwanda vya kutengeneza ngozi kufufuliwa. Nashauri hii ifanyike kwa haraka kwa madini ya *Tanzanite* na Dhahabu madini haya yanapouzwa bila ya kusafishwa kama *finished goods,* nchi yetu rasilimali yake inaibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya hivyo, *market intelligence* ifanywe ili kuzuia *transfer price* inayotumika na Makanpuni ya kigeni *(conglometes).* Iwapo Tanzania haitawekeza katika rasilimali watu *technicians* wa kuzalisha viwandani na kutekeleza Sera ya kuhakikisha nchi inasafirisha bidhaa ya viwanda *finished good for export,* nchi itabaki kuwa soko la nchi nyingine na watu wetu watakuwa machinga na wauza duka lenye bidhaa za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuzungumzia viwango *(standards).* Bidhaa nyingi zinazotengenezwa hapa nchini na nyingine za kutoka nje ni za viwango vya chini. Nashauri *TBS* ijengewe uwezo ili kuboresha vyanzo vya bidhaa zetu pamoja na *investment codes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, na hili naomba Mheshimiwa Waziri anitajie kwamba nimechangia uandikishaji wa majina ya biashara ufanyike Mkoani au Wilayani. Kufanyika uandishi Dar es Salaam ni ghali sana na usumbufu kwa wananchi. Nashukuru.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kwanza kuunga mkono Wizara yako ya Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda Tabora Mjini kuna kiwanda kimoja tu cha *TABOTEX* kiwanda hiki utawala wa pale unawadhalilisha sana wafanyakazi walioachishwa kazi zaidi ya miaka miwili sasa. Kwa

ufupi, wafanyakazi hawa walikatwa fedha zao za *PPF,* lakini mwajiri akashindwa kuwasilisha kunakohusika hata baada ya Mkuu wa Mkoa na mimi binafsi kulifuatilia suala hili kwa muda mrefu. Lakini wananchi hawa mpaka leo hawajalipwa haki zao za mafao ya *PPF*. Je, Mheshimiwa Waziri haoni iko haja ya sasa Serikali Kuu nayo iingilie kati ili wananchi hawa wasiendelee kuteseka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduka ya Tabora yamejaza vifaa feki vingi mno. Je, ni lini ufunguo wa *TBS* utafika katika Manispaa yangu? Kwani wananchi wanalalamika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono Wizara hii mia kwa mia.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii kwa maandishi. Awali ya yote, naunga mkono hoja na kumpongeza kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekosa viwanda vya zana za kilimo. Hii ni pamoja na majembe ya *plough,* ya mkono, matrekta na kadhalika ili kuinua uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Viwanda vilivyokuwepo na kubinafsishwa, vimeshindwa kuendelea na badala yake bidhaa hizi zimeagizwa toka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iweke mkazo katika viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yetu kama viwanda vya nyama, maziwa, ngozi,

mazao kama mahindi, alizeti, viazi, matunda, kahawa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la biashara linaonekana halijajipanga vizuri, kwani karibu kila mtu anataka kuwa mfanyabiashara kuanzia machinga mpaka wafanyabiashara. Ili Serikali iweze kupata kodi kwa wafanyabiashara, ni vizuri kila anayefanya biashara atoe ankara (risiti) na adhabu kali iwekwe, kwa yeyote atakayepokea fedha ya mauzo bila risiti atozwe faini kali na kifungo jela. Hii ndiyo itafanya Watanzania wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanaibiwa sana wanapouza au kununua mazao kwa kukosa mizani sahihi. Usimamizi kwenye eneo la *weights and measures* haviko, na hakuna adhabu kali zinatolewa kwa wanao-*temper* mizani kwa lengo la kujitajirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu baada ya miaka 50 tunahitaji kuwa na kiwanda cha kutengeneza baiskeli, pikipiki na hata magari.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, namshukuru sana mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia katika hoja hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri kuwa mimi ni mdau wa Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Kamati ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu ni kuona kwamba inawezekana Bunge lako Tukufu likashindwa

kuisimamia vizuri Serikali katika sekta hii kutokana na ukweli kwamba, kuna Wabunge ambao ndani ya Bunge hili ni wahusika wakuu wa kuendesha viwanda na biashara na wengine wako kwenye Bodi za Viwanda hivi na siyo hivyo tu, bali wengine ni wazalishaji, wahusika wakuu katika umiliki wa viwanda na pia waendesha biashara Wakuu wa vitu vya msingi, kama vile wengine ni Mawaziri halafu tena ni Wabunge, tena wengine wako kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara. Hapa naona kuna mgongano wa masilahi (*conflict of interest).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi ni kutaka Bunge lako lipewe orodha ya Wabunge walioko kwenye Bodi mbalimbali na sehemu wanayohusika kupatiwa nafasi zao katika mchakato mzima wa uboroshaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara mbalimbali tulizozifanya nchini, tumeona kuwepo kwa usiri wa mambo yanayofanya kuwa matatizo mengine yasiweze kupatiwa ufumbuzi. Mfano mzuri ni suala la vibali vya sukari. Usambazaji *(distribution)* wa sukari na uzalishaji pia unaelekea kushikwa na watu wale wale ambao wengi wao ni Waasia na pia wengine ni Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vipo Viwanda vya Nguo, Chuma na kadhalika. Masuala haya yanashindikana kutatuliwa huenda ni kutokana na utata wa mikataba iliyoingiwa na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingefaa tupate mkakati wa jinsi gani watashughulikia haya matatizo, kwa mfano mikataba ya viwanda vilivyokufa, sasa viko katika hali ya kubadilishwa matumizi yake, badala ya kuzalisha vinakuwa magodauni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi la kuzingatiwa ni kwamba ili kutatua masuala haya, kuna umuhimu wa kuwa na watu waadilifu, jasiri na makini, katika kuwasimamia Watendaji na kuchukua hatua chungu za kuwafilisi wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuwasilisha.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kusoma hotuba yako vizuri sana. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali fulani. Kwanza ni kuhusu *TBS.* Mwaka 2009 tulitunga Sheria Na. 2 ya Viwango *(TBS)* ambayo inawapa *TBS* mamlaka ya kukagua bidhaa huko huko zinakotoka *(reshipment verification of conformity to standards)* na vile vile kikao cha Afrika Mashariki mwaka 2010 tulikubaliana vile vile kuwa bidhaa zinazotoka nje zikaguliwe huko huko nje. Wenzetu wa Kenya wameanza mwaka 2005 na wameweza kudhibiti bidhaa za nje kwa 75%. Wenzetu wa Uganda walianza mwaka 2010.

Swali ni kwamba, mbona Tanzania bado hatujawa na vituo huko huko nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine ni kuhusu mipaka. Tanzania ina mipaka mingi na kila mpaka una vituo. Mpaka sasa kuna vituo zaidi 30, lakini vituo vilivyojengwa ni vitano tu, navyo ni Tanga Mjini – Tanga, Horohoro – Tanga, Holili – Kilimanjaro, Namanga – Arusha na Sirari - Mara.

Swali ni kwamba: Je, mbona Mikoa ya Kusini haijajengewa vituo wakati kuna maeneo ya mipaka na vituo vya kupenyeza bidhaa bandia? Vilevile vituo katika nchi nyingine za jirani ni bora kuliko vituo vya Tanzania, hivyo kukosa mvuto kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusini kama Mtwara, Lindi na Ruvuma kuna nchi za jirani kama Msumbiji, Malawi na Zimbabwe. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuwa na vituo maalumu katika mipaka hiyo ili kudhibiti bidhaa zinazoingia Tanzania kinyemela.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda na Waziri wa Viwanda na Biashara, pamoja na Mheshimiwa Gergory G. Teu kwa kuteuliwa kwao kuongoza Wizara hii nyeti na muhimu katika kuchangia uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda ni muhimu sana katika nchi yetu, ndio chanzo cha mapato, ajira na ndiko kwenye utatuzi mkubwa wa

tatizo la umeme kwa vyanzo vya makaa ya mawe (Ngaka, Kiwira na Mchuchuma) na umeme wa upepo, mfano Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na rasilimali tulizokuwa nazo, bado Serikali imekuwa inasita sana kuwekeza pesa ya kutosha kwenye Wizara hii. Sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuwekeza pesa ya kutosha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, namshukuru mwenyezi Mungu (S.W.) kwa neema na rehma zake nyingi anazonineemesha, sina budi kusema *Alhamdulilah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulimwengu wa sasa unategemea sana viwanda na biashara kwa ustawi wa nchi husika. Tanzania pia ni nchi inayohitaji sana haja ya kuwa na viwanda vya kisasa ili kukuza uchumi na pato la wananchi kwa ujumla. Viwanda ndiyo jiko la kupikia biashara nyingi. Hivyo Serikali ikaze buti katika kuweka Sera nzuri za kuvutia uwekezaji wa viwanda. Kwa kufanya hivyo, vijana wengi watapata ajira viwandani na kuinua hali zao za maisha. Pia wakulima watakuwa na masoko ya uhakika ya kuuza mazao yao ya kilimo, hivyo kukuza uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla. Viwanda vyenye tija ya uzalishaji wa bidhaa bora, pia vitafungua biashara zaidi za ndani na nje. Hiyo itasaidia sana pia kukuza pato la wananchi, kupunguza umasikini na kuboresha hali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu uliopo katika sekta ya viwanda, Serikali lazima iwe makini sana kwa wawekezaji hawa ili walipe kodi inayostahili kwa manufaa ya nchi. Wawekezaji wana mbinu za namna nyingi za kukwepa kodi, hivyo kuinyima Serikali mapato na dhana nzima ya kukaribisha wawekezaji kukosa maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi, *(PV.C),* Serikali iwe makini na isiwaonee aibu (isiwalee) Watendaji wake wasio waaminifu. Watendaji hawa wenye tamaa binafsi, badala ya maslahi ya nchi ndiyo tatizo na siyo namna ya ukaguaji wa bidhaa. Ni sawa tu bidhaa kukaguliwa ndani au nje ya nchi! Ushahidi wa hili ni utendaji wa *TBS* ambao wakikagua magari nje ya nchi, lakini kwa tamaa zao binafsi tumeona yaliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili pia linachangiwa na wafanyabiashara wakubwa wanaoagiza bidhaa nje. Wafanyabiashara hawa huagiza viwanda vya nje *(order)* viwatengenezee bidhaa zenye viwango duni kwa vile wanaleta bidhaa kwa wingi na kwa mkupuo hupewa *direct release* zifikapo Bandarini, hivyo inakuwa ni baada ya kushirikiana na Watendaji wasio waaminifu na wenye tamaa binafsi na *TRA* na *TBS*. Jambo hili ni hatari na ni lazima Serikali iweke macho na makucha yake wazi ili kulinusuru Taifa letu hili zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali, Serikali iwe makini sana katika kuangalia sekta ya

viwanda. Pia viwanda ambavyo Serikali ina ubia kujua uzalishaji halisi, ili Serikali isikose mapato yake na dhana hii kukosa mantiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukurani kwa kupata nafasi hii nami nitoe maoni yangu katika Wizara hii. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Hiyo ni imani kubwa ambayo Mheshimiwa Rais aliyonayo kwao. Nawaomba wasimwangushe, na ukweli Mheshimiwa Waziri tangu sijawa mwanasiasa ndani ya huu mjengo, nilikuwa nasikia sifa zake na uhodari wake wa kuchapa kazi na uadilifu wake. Mungu awasaidie ili waweze kusimamia vyema Ilani ya CCM na kuwaletea maendeleo Watanzania. Tafadhali wawe makini na makundi yafuatayo:-

Kwanza ni wapenda rushwa. Kuna watu ambao wao hawana lingine zaidi ya kutaka kutumia nafasi au mwanya wanaopata kwa maslahi yao binafsi.

Pili, watu wasioitakia mema Tanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri awe makini na baadhi ya watu wenye tabia ya kutotaka kutekeleza yapasayo ili mradi tu maendeleo yasionekane, ili tu kuleta hasira kwa walipa kodi. Watu kama hao hawastahili kupewa madaraka mfano ya kusimamia miradi, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya angalizo hilo, naomba niishukuru Serikali kwa maandalizi ya

marekebisho ya Sheria ya *COSOTA* ya mwaka 1999 na hatimaye wataileta hapa Bungeni kwa marekebisho. Pia makubaliano kati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo, ili *TRA* ianze kutoa stika za kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa kazi za muziki na filamu, lakini nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamasishaji wa masuala ya hakimiliki kupitia vyombo vya habari bado hautoshelezi, uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* kutoa elimu kwa wauzaji wa kanda na wanunuzi kuhusu *CD* na mikanda bandia kwa Maafisa Ugani na Maafisa Leseni kuhusu hatimiliki na hakishiriki, sina hakika kama imefanyika nchi nzima. Elimu hiyo itolewe tena na iwe nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* ina wanachana wengi ambao ni wasanii wa muziki, filamu, na kadhalika. Kwa nini isiwatumie hao kuhamasisha na kutoa elimu? Pia kuna shirikisho la wasanii, nashauri itoe maelekezo kuweza kupata msaada wa kutoa elimu zaidi, iwe kwa makongamano, ama nyimbo, muziki, maigizo (filamu) na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* imekuwa na tabia ya kuchelewesha kulipa mrahaba kwa wahusika. Suala hili limekuwa ni wimbo kwangu kila mwaka. Kwanini Wizara haiingilii kati suala la *COSOTA* kuchelewesha malipo kwa wasanii, na pia namna ya kutoa taarifa mara fedha zinapokuwa tayari? Hili tatizo ambalo niliwahi kushauri kwamba *COSOTA,* wanaposafiri wasanii, wachukue akaunti zao ili kwamba mgao wa mrahaba unapoiva, basi mtu

awekewe tu kwenye akaunti yake na atumiwe *pay slip* yake. Lakini *COSOTA* naona kama kuna kigugumizi. Sasa je, Mheshimiwa Waziri utachukua hatua gani? Maana ni wengi hawapati taarifa ya mgao wao na hivyo hawafiki. Mfano, aliyeko Kigoma hawezi kuja Dar es Salaam kwa kufuata mgao wa Sh. 100,000/= (laki moja) lakini akiwekewa kwenye akaunti siyo haba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* wana kisingizio cha kwamba *computer* ni mbovu, lakini hiyo siyo haki. Huko ni kutaka kuwapa imani potofu wasanii na kuona kama wanaibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *COSOTA* ifanye Mikutano ya mwaka kama ilivyo kuwa enzi za Mtetewanga, hivi ni chama gani ama taasisi gani inaendeshwa bila mkutano na wadau?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi iliyopo, na mimi ni Mjumbe, ni Bodi ambayo haikukidhi kanuni au taratibu, kwani iliteuliwa na Waziri tu, lakini hapakuwa na uchaguzi kwa wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* inapata lawama nyingi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake, lakini tatizo kubwa haipewi fedha inazoziomba kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* iwezeshwe Kisheria ili iweze kuendesha kesi au mashtaka kama ilivyo kwa Takukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Sheria iboreshwe kwenye maeneo ambayo bado yana kanuni za adhabu ndogo, pia na muda wa miliki baada ya kifo cha mtunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kwa kuwa Sheria ya Kuundwa Bodi ni kama ilikiukwa na *COSOTA* ilikaa kwa muda mrefu bila Bodi kuanzia mwaka 2007 hadi 2011: Je, hakukuwa na ufujaji? Naomba uchunguzi ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamishwe au kufafanuliwa kwani nadhani Serikali inajikanganya. Inawezekanaje kuweka *VAT* kwenye *capital good* na pia inawezekana vipi mwananchi amelipa *insurance* inayo-*cover* na moto halafu anakamatwa kwa kutokuwa na *fire extinguisher* kwenye gari? Naomba nieleweshwe kama hili lipo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida kuna viwanda vidogo vidogo vya kukamua mafuta ya alizeti, lakini kuna tetesi ya kupata mwekezaji toka nje. Kweli hilo ni jambo jema sana, kwani kitakuwa na uwezo wa *ku-double refine* mafuta ya alizeti. Ombi langu ni kwamba, kiwanda kile kisije kuwa chanzo cha kuua viwanda vidogo vidogo vilivyopo pale. Hivyo kuwe na mkataba au makubaliano ya mwekezaji. Kiwanda hicho kiwe kinanunua mafuta toka viwanda vidogovidogo na kuya-*double refine* tayari kwa ku-*export.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa nane wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kifungu cha 14 kinaelezea ukuaji wa uzalishaji wa viwanda vya vinywaji na sigara. Ukuaji huo ni dhahiri unaongeza pato la Serikali, lakini kwa sababu viwanda hivyo haviwagusi wananchi walio wengi katika nchi hii, ili uchumi wa mtu mmoja mmoja uonekane umekuwa, ni lazima pia ukuaji wa viwanda uwe kwenye bidhaa za kilimo, mfano matunda na kadhalika. Serikali ina mkakati gani kuwashawishi wawekezaji ili waanzishe viwanda vinavyohusiana na bidhaa za kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuwa na viwanda vinavyohusiana na bidhaa za kilimo na bidhaa hizo husafirishwa nje ya nchi itasababisha Serikali kupata fedha za kigeni kwa wingi na kupunguza kwa kuanguka mara kwa mara kwa thamani ya Shilingi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 25 wa hotuba ya Waziri kifungu cha 37 kinaelezea suala zima la uchimbaji wa magadi kwenye ziwa Natron. Katika kifungu hicho, nimeshindwa kuelewa: Je, uchimbaji huo utafanyika ndani ya Ziwa au Engaruka ambapo pia imeonekana uwepo wa mashapo ya magadi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kwamba Ziwa Natron ni mahali pekee katika Afrika ya Mashariki ambapo ndipo penye idadi kubwa ya uzalishaji wa ndege aina ya *heroe (flamingo).* Imewezekana hivyo kutokana na umbile la eneo hilo. Sasa kama uchimbaji wa magadi utafanyika ndani ya Ziwa, maumbile ya

Ziwa hilo utabadilika. Naomba Serikali inithibitishie uchimbaji huo utafanyika ndani ya Ziwa au eneo la Engaruka ambalo liko kilomita 50 kutoka kwenye Ziwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maonesho ya Saba Saba kila mwaka unapotembelea mabanda ya wajasiriamali huwa kuna malalamiko ya wafanyabiashara hao kukosa soko la bidhaa zao. Kwa mfano, wafanyabiashara hao ni wale wanaouza asali. Wizara ina mpango gani katika kuwatafutia soko la nje wafanyabiashara hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 132 kifungu 188 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza juu ya suala zima la uhifadhi wa mazingira kwenye miradi mipya itakayoanzishwa na Wizara. Je, Wizara inasemaje juu ya vile viwanda ambavyo vinazalisha mifuko ya plastiki yenye viwango kinyume cha Sheria? Je, ziko kesi ambazo zimepatikana kwa viwanda vinavyozalisha mifuko hiyo, kesi ambazo zimekamatwa na Wizara yako licha na zile ambazo *NEMC* wamezikamata kwa vile mazingira ni suala mtambuka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa ili nchi yoyote iendelee, inabidi ifanye jitihada za ziada katika kukuza biashara yake ya nje na ndani na pia kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa nyingi za kutosheleza matumizi ya ndani na kuwepo na ziada ya kuuza nje. Kila nchi inajitahidi kufanya hivyo, bali Tanzania haionekani kuwa na msukumo wa kutosha kwenye suala hili kiasi ambacho

hata viwanda vilivyoanzishwa miaka ya awali ya uhuru vimedorora kiasi cha nchi yetu kuletewa vitu vingi vya matumizi kutoka nje vikiwemo *tooth pick* na nguo chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini Serikali isipige marufuku uingizaji wa vifaa duni kama hizi zikiwemo nguo na viatu vya mitumba ili kuwapa moyo wananchi wenye taaluma ya kuvitengeneza wafanye hivyo wakijua soko lipo? Kwanini Serikali isitambue bidhaa kama hizo ili zitengenezwe hapa hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuboresha ufanisi kwenye taasisi zake, hasa Makampuni na Viwanda, Serikali ilichukua hatua zifuatazo: Kuwauzia watu binafsi chombo hicho ili kiwe ni chao kabisa kama ilivyofanyika kwa Benki ya Taifa ya Biashara, kufanyia *concession* chombo hicho na Serikali kuingia ubia kama ilivyofanyika kwa *TRL, ATCL* na *KADCO* na kukodisha chombo hicho kwa kampuni binafsi kama ilivyofanyika kwa karakana ya Ndege ya Kilimanjaro. Tegemeo ni kuwa, chombo hicho kitaendelezwa ili kifanye kwa ufanisi zaidi shughuli zile ambazo kimetengenezwa na kukusudiwa kufanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali huchukua hatua gani kama mkabidhiwa huyo anakitumia chombo hicho tofauti na lengo la Taifa? Inapodhihirika kuwa Taasisi ya Serikali au mwekezaji mwingine, inao uwezo wa kukitumia chombo hicho ipasavyo. Serikali hutumia hatua zipi kwa manufaa ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, kwanini Serikali isiangalie uwezekano wa kutafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kuitumia karakana ya Ndege ya Kilimanjaro kama ilivyonunuliwa kutumika, yaani kutengenezea Ndege hata zenye ukubwa wa B747 badala ya linavyotumika sasa chini ya Kampuni iliyopo hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kutoka maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Ubinafsishaji ni Sera nzuri na yenye matokeo mazuri pale tu inapotumika vizuri na hasa kwa manufaa ya wazawa. Pamoja na uzuri wake, Sera hii tangu ilipoanza miaka ya 1980 haijaonesha mafanikio mazuri kwa wananchi walio wengi wa Tanzania hasa wale wenye kipato kidogo. Sera ya Ubinafsishaji, hususan ya viwanda imepelekea Taifa letu kuwa tegemezi kwa kuagiza bidhaa zilizokwishazalishwa, na sisi kuendelea kusafirisha malighafi *(raw materials)* kwa nchi zenye viwanda na matokeo yake tunapunguza thamani ya bidhaa zetu na kununua bidhaa zinazotoka nje kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni msingi wa maendeleo kwa nchi yoyote ile. Bila viwanda, tusitegemee nchi yetu kuendelea na kutatua matatizo mbalimbali ikiwemo ajira kwa vijana. Mfano wa

viwanda vilivyobinafsishwa imeonekana kubadili matumizi yake na hata kingine kufungwa kabisa.

Mfano mzuri ni viwanda vya korosho (Likombe *Cashew Nut*, Newala I & II, Mtama na kadhalika). Viwanda hivi viliuzwa kwa bei za kutupwa, mfano Newala I & II viliuzwa kwa Shilingi milioni 75 tu. Tena cha kushangaza, kiwanda cha Newala I kiliuzwa kikiwa kipya kabisa. Lakini viwanda hivyo vimebadilisha matumizi yake ya kubangua korosho na badala yake vimegeuzwa kuwa maghala ya kutunzia korosho ghafi kwa stakabadhi ya mazao ghalani. Je, ni kwanini wawekezaji hawa, tena wazawa wamekiuka Mkataba wao wa kubangua korosho na kubadilisha matumizi ya viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwanini Serikali imekaa kimya mpaka sasa hivi wakati walionunua viwanda hivi wanajulikana na wengine walikuwa ni viongozi wakubwa wa Serikali? Ni kwanini Serikali haichukui hatua na kufanya maamuzi magumu ya kuvichukua viwanda hivyo na hao wamiliki kulipa fidia kwa kulipotezea Taifa mapato kwa muda wote waliokaa bila kufanya kazi? Naitaka Serikali itoe majibu sahihi kwa suala hilo la viwanda vya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida unaongoza kwa kuwa na ardhi inayoruhusu kilimo cha alizeti kwa kiwango cha hali ya juu. Tatizo lililopo ni ukosefu wa viwanda au kiwanda kikubwa cha alizeti ili kutengeneza mafuta ambayo yameonekana ni mafuta bora hasa katika kumfanya binadamu kutokupata maradhi kama ya moyo, kisukari, *obesity*

na *cancer*. Ni lini Serikali itajenga kiwanda kikubwa cha kisasa ambacho zaidi ya kuzalisha mafuta, Kiwanda hicho kitatoa ajira kwa vijana na akina mama wengi ambao wanashinda vijiweni bila ajira za maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asali ni zao lenye manufaa makubwa sana katika mwili wa binadamu, hasa kwa watoto wadogo na watu wazima ambao wamefikia umri wa kushambuliwa na maradhi ya uzeeni kama kisukari na moyo. Zao hili limekuwa likipewa kipaumbele na Serikali hasa kwa miaka ya hivi karibuni, lakini hakuna juhudi za makusudi za kuanzisha viwanda vikubwa na vya kisasa vya kuweza kusindika asali na kuifanya iendelee kuwa na ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi, hasa wa Mkoa wa Singida ambao ni wazalishaji wakubwa wa asali, hutumia njia za kizamani na zisizo salama *ku-process* asali baada ya kuivuna na wengine huichemsha na hivyo kuondoa ubora wa asali hii. Naishauri Serikali kutenga bajeti kwa makusudi ili kujenga viwanda vya asali, hususan kutoka Mikoa inayoongoza kwa uzalishaji kama Singida na Tabora ili kuwainua wananchi kiuchumi na vile vile kuendelea kuimarisha afya za wananchi wakiwepo watoto na wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hasa Mheshimiwa Kigoda kwa kuchukua maamuzi ya busara ya kumsimamisha kazi aliyekuwa Mkurugenzi wa *TBS* Ndugu Ekelege ili kuupisha uchunguzi wa kashfa

ya Makampuni ya kukagua magari yaliyotumika. Ni uamuzi wa busara, mgumu na wenye kupongezwa.

Sambamba na hilo, ni wajibu wa Wizara sasa kulitupia macho Shirika hilo, kwani bado linafanya kazi chini ya kiwango na kwa mazoea. Ni kwanini mpaka sasa tunaendelea kupokea bidhaa feki toka nje hususan China? *TBS* wana mkakati gani wa makusudi wa kuzuia bidhaa hizi zisiingie nchini na badala yake kulisababishia Taifa hasara kubwa kwa kupoteza mapato? *TBS* wana mipango gani endelevu ya kufanya nchi yetu haiendelei kuwa dampo la bidhaa feki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu pia, ni kwanini bidhaa zinazokamatwa kwa uwazi ili wananchi wawajue na wasusie bidhaa zao kama ambavyo wanafanya mamlaka ya chakula na lishe ambao mara nyingi tunashuhudia wakichoma dawa feki na kutangaza majina ya waagizaji wa madawa hayo na hivyo kuwafanya wananchi kuwa *aware* na maduka hayo na kuacha kununua dawa zao. Ni vyema *TBS* nao wawe na utaratibu huu mzuri wa kuwaweka wazi waagizaji wa bidhaa feki ambazo ni hatari kwa maisha na uhai wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwachukulie hatua kali wale wote walionunua viwanda vyetu na kisha wakavibadilishia matumizi, wakang‘oa mitambo na kuvitelekeza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ichukue mikopo mikubwa kwa kutumia dhamana ya akiba yetu ya gesi asilia, kisha ijenge Viwanda vya Pamba, kitu ambacho kitaongeza ajira na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vingapi nchini ambavyo vinamilikiwa na wazalendo na mauzo yake nje ni kiasi gani?

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuichangia hoja hii ya viwanda na biashara, nitachangia kuhusu viwanda vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi tajiri sana kulingana na Mikoa iliyopo na kila Mkoa una madini na mazao yake. Sasa, kwa nini Serikali kupitia Wizara hii isiandae utaratibu wa kujenga viwanda; kila Mkoa kiwanda kimoja cha usindikaji wa vyakula, mfano Mkoa unazalisha mazao ambayo Mkoa mwingine hauna? Kama Mkoa una madini, basi kijengwe Kiwanda cha Pamba na kama ngozi, kijengwe Kiwanda cha Ngozi. Faida yake, kwanza vijana watapata ajira na kulima mazao zaidi na kuacha kukimbilia Mijini. Serikali itakuwa na kazi ya kupeleka huduma za miundombinu ya barabara na umeme wa uhakika katika Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini Tanzania tumekuwa nyuma? Nakumbuka zamani tulikuwa na viwanda vingi *Mwatex, Cotex, SIDO* Bora, vyote hivi havipo au vimebinafsishwa, ila pia haviendelei.

Matokeo yake tumekuwa limbukeni wa kupapatikia bidhaa za nje ambazo hazina ubora kama bidhaa za China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kariakoo ya leo kuna sehemu Wachina wameeneza biashara zao, zetu zinakufa. Naiomba Serikali iandae mikakati ya makusudi ili kunusuru hali iliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaendelea kuwa dampo la kupokea bidhaa zilizo chini ya kiwango (feki) japokuwa tuna Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).* Kwa mfano, kuendelea kuingizwa kwa mbolea feki wakati tuna *TBS* na *TFDA* hii ni aibu kubwa kwa nchi yetu. Pia kuendelea kuingiza matairi mabovu na kusababisha ajali nyingi za barabarani ambazo zinagharimu maisha ya Watanzania, hii ni aibu kubwa. Je, Serikali kupitia Wizara hii inajipanga vipi kuhakikisha kuwa *TBS* wanafanya kazi kama inavyostahili na sio Watendaji wake kuendelea kujinufaisha binafsi na siyo kuangalia maslahi ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunasimuliwa hadithi ya kufufua viwango vya Ngozi. Je, ni kweli Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, ina dhamira ya dhati ya kufufua Viwanda vya Ngozi? Kwa sababu kama kweli tungewekeza kwenye Viwanda vya Ngozi, Watanzania leo hii tusingepata taabu ya

kuvaa viatu feki hasa kwa watoto wetu mashuleni. Hilo tayari ni soko tosha kwa ngozi yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine ni muunganisho wa ujasiriamali Vijijini (MUVI). Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 33 ametaja baadhi ya Mikoa ambayo imenufaika na programu hii ukiwepo Mkoa wa Pwani katika Wilaya ya Rufiji, Mkwanga na Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri: Je, ni kiasi gani Wilaya ya Rufiji imenufaika na programu hii ya MUVI na ni katika eneo gani? Namaanisha Kijiji gani hasa ambako programu hii imewanufaisha wananchi hawa wa Rufiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zimeendelea kwa uzalishaji bidhaa viwandani, kwa maana hiyo, basi nchi kama Tanzania ni lazima sasa kuangalia kwa makini mambo yafuatayao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufufuaji wa viwanda viko viwanda vingi ambavyo sasa havifanyi kazi kwa sababu ya ubovu na uchakavu wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kabisa ya kuona umuhimu wa kufufua viwanda na kuweza kuzalisha. Hata hivyo, uanzishaji wa viwanda uzingatie zaidi maeneo ya uzalishaji mkubwa wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya uvuvi hasa katika maeneo ya Bahari kama vile Tanga, Mtwara, Bagamoyo na sehemu nyingine ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itaimarisha viwanda katika Mkoa mbalimbali itaongeza ajira na kuongeza mapato ya Serikali. Ushauri wangu, Mipango iliyomo kwenye bajeti ya Wizara hii ni mikubwa sana na hivyo ni vigumu kuweza kuitekeleza kwa wakati, hivyo basi, Wizara hii ni lazima itoe vipaumbele kwa mujibu wa bajeti yake ili yale maeneo muhimu sana yaweze kutekelezeka katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imo katika *EAC* na kwa maana hiyo ina nafasi kubwa sana ya kibiashara dhidi ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama bidhaa hazina ubora katika uzalishaji, juhudi za Taifa zitadorora. Kwa maana hiyo, Wizara lazima izingatie kikamilifu ubora wa bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa biashara, bidhaa zinazozalishwa viwandani, lazima zidhibitiwe Kisheria ili kulinda jina la kiwanda husika katika uzalishaji ili kuimarika kwa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa bidhaa kutokutoka nje kabla ya mahitaji ya ndani ni muhimu sana. Hii itasaidia kwa wananchi kupata bidhaa muhimu kwa wakati na kwa bei nafuu. Bidhaa yenyewe ni kama vile sukari, mchele, na vifaa vya ujenzi. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuleta ufanisi na usimamizi wa ukusanyaji wa kweli kabla bidhaa haijatoka kwenda nje ya nchi. Biashara pia idhibitiwe kwa kulinda hali ya kiafya kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kutambua kwamba kama Taifa linalotaka kuwa na uchumi wa kitu ni lazima kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda vya kutosha, vile vidogo vidogo, vya kati na viwanda vikubwa. Wazo hili ni zuri sana. Hivyo tunayo kila sababu ya kuhakikishiwa fikra hizi tunaziishi kwa matendo ili kuondokana na hali ya kuuza malighafi mazao yetu bila ya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapouza mazao yetu kama malighafi, maana yake ni kwamba tunatoa ajira katika nchi za wenzetu ambao wao ndio wanakwenda kuongezea thamani na kurudishwa kuuzwa kwetu kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza mpango mzuri wa Wizara wa kuhakikisha tunaanzisha viwanda vidogo ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa sukari nchini, kwa kuanzisha kilimo cha miwa na viwanda vidogo vya kuzalisha sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwambao wa Ziwa Tanganyika hususan Wilaya za Nkonsi na Kalambo eneo kubwa ambalo Ziwa lipo, hakuna kiwanda chochote cha kusakata samaki na hivyo kulazimika kusafirisha samaki *unprocessed.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine ni *transaction cost* katika ufanyaji wa biashara. Sisi kama Taifa hatuko Kisiwani, hivyo ni vizuri tukahakikisha kwamba gharama za ufanyaji biashara unapungua ili kuvutia watu wengi kufanya biashara nchini, kwani tusipofanya sisi, wenzetu wa nchi jirani watafanya. Haiingii akilini mtu kuambiwa njoo kesho, mara mhusika hayupo, maneno haya hayafai hata kidogo kwa dunia ya leo. Mtu anahitaji kufika sehemu moja *(one center)* na kutimiziwa mahitaji yote badala ya kuzunguka ofisi chungu mzima kabla ya kupata leseni.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa namna ambavyo wameanza kazi, na katika muda mfupi tu tumeanza kuona mabadiliko kiasi cha kwamba tumeanza kupata matumaini ya mabadiliko ya dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mtikisiko mkubwa uliokuja kuikumba nchi yetu na kulazimika

kubinafsisha baadhi ya viwanda vyetu, tumeiomba Wizara kuandaa Sera na mkakati ambao utaanzisha upya ufufuaji wa viwanda ambavyo vinatumiwa moja kwa moja na wananchi wa kawaida, hasa vile ambavyo vinatumia mali ghafi kutoka ndani na yale ambayo yanatoka kwa wakulima wetu bila kusaka Viwanda vya Kusindika Nyama na Ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kutoa masikitiko yangu makubwa kuona namna ambavyo soko la biashara la Tanzania tumeliacha wazi, hasa kwa wageni na kujiwekea baadhi ya wawekezaji kuleta bidhaa feki na zilizomaliza muda wake au zilizo chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iwaonee huruma Watanzania na hususan afya zao, kwani wafanyabiashara wengi hasa wa Kiasia hawajali maisha ya Watanzania, bali wanajali zaidi faida yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iimarishe *TBS* na iibadilishe ili kitengo hiki kionekane machoni mwa Watanzania, kwani ndiyo kimbilio lao na siyo eneo la machinjio yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Sheria zinakwaza, basi ziletwe Bungeni ili ziweze kurekebishwa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Mary Nagu aliahidi wananchi

wa Kanda ya Ziwa kujenga Kiwanda cha *Cement* Mkoa wa Shinyanga kwa niaba ya Kanda ya Ziwa. Kiwanda kilitengwa na hata taratibu za fidia zilianza. Je taratibu hizo ziliishia wapi?

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Shinyanga Vijijini imeanza, na kwenye mpango wa mwaka huu tutajenga Soko la Mazao la Kimataifa katika Kata ya Didia. Naomba kujua, Wizara itakuwa na mpango gani wa kutusaidia kwa mwaka wa fedha ujao kutupa fedha ya kukamilisha soko hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna utaratibu ambao Halmashauri yetu itatakiwa kufanya, naomba kuelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Korosho ambavyo vimegeuka maghala katika Mikoa ya Kusini hususan Jimbo la Lindi Mjini vimekuwa vikielezewa kuwa vimebinafsishwa kwa wawekezaji wa ndani, lakini wananchi wa Jimbo langu hawajafahamishwa nani aliyebinafsishwa na kwa kipindi gani. Hivyo hoja iliyopo ni kumtaka Mheshimiwa Waziri aeleze viwanda hivyo kwa sasa ni mali ya nani na mwekezaji ameingia Mkataba lini na kwa kazi gani anazotakiwa kufanya? Inasemekana mwekezaji alikopa fedha kutoka Benki ya *CRDB* kwa ajili ya kuendeleza Kiwanda cha Lindi, lakini kiwanda hicho kipo kama kilivyo, wala hakuna mwendelezo. Serikali kupitia Wizara hii ina taarifa gani

kuhusiana na ukopaji wa fedha hizo? Ni hatua gani zimechukuliwa kuhakikisha kiwanda hicho kinafanya kazi na/au kinarudishwa mikononi mwa wamiliki wa awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara hii inatoa tamko gani kuhusiana na Kiwanda cha Saruji ambacho bado kipo katika kitendawili ambacho kilitakiwa kijengwe Mjini Lindi? Kwa kuwa katika hoja iliyowasilishwa Bungeni inaonyesha viwanda vitakavyojengwa ni vya Tanga, Mbagala, na Arusha. Ni lini ujenzi wa Kiwanda cha Saruji cha Lindi kitaanza ujenzi wake, na lini kinategemewa kwisha? Nani mmiliki na mwekezaji wa kiwanda hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lindi Mjini ni miongoni mwa wazalishaji wa korosho, lakini mpaka sasa korosho zimekuwa zikiyumba kutokana na bei na soko kutokuwa na uhakika. Lakini Serikali haijachukua hatua za makusudi kuhakikisha wajasiriamali wanaobangua korosho wanawezeshwa ili waweze kuingia katika ushindani wa soko. Hivi sasa ni Kampuni za watu binafsi ndizo zinazojihusisha na shughuli hiyo. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wajasiriamali nao wanajiunga pamoja na kuwezeshwa kupata vifaa vya kubangulia korosho pamoja na vifungashio ili kuinua ubora wa bidhaa zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Lindi umezungukwa na Bahari ya Hindi na wakazi wake hujishughulisha na uvuvi, lakini mpaka sasa wavuvi wake hutumia zana duni za kuvulia na kuvua samaki. Huu ni uvuvi usiokuwa wa kibiashara. Pamoja wa

kuanzishwa vikundi vya wajasiriamali waliopewa zana za uvuvi, lakini bado haziwasaidii kutokana na mitaji wanayopewa kuanzishia shughuli hizo ni midogo na haiwafikii kwa wakati; vyombo wanavyotumia kuvulia ni vidogo kiasi kwamba haviwezi kuhimili mikikimikiki ya kuvua bahari kuu; hawana vifaa vya ugunduzi wa maeneo yenye samaki kama *GPS* na kadhalika. Hivyo Serikali inawaambiaje wavuvi hawa kuwa miradi yao itaanzishwa kwa wakati na wapate mitaji ya kutosha na vyombo vya kisasa na vikubwa vyenye kuhimili misukosuko ya bahari? Vifaa vya ugunduzi vinapatikana, na ni lini watapatiwa viwanda ili kupanua wigo wa soko na kujiongezea kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine ni kuhusu biashara. Serikali kupitia *TSPF* imekuwa ikiwasaidia wajasiriamali kupata mitaji kupitia mashindano ya biashara kama *BDG*. Lakini utaratibu unaotumika kupata washindi kupitia mashindano hayo ya biashara unaonekana kufanywa ama kwa upendeleo au undugunaizesheni na/au misingi ya rushwa. Kwa kuwa imeruhusu baadhi ya watumishi wasio waaminifu kutoa washindi kwa njia ya upendeleo, Wizara ieleze kama inalitambua hilo na jitihada za kutatua tatizo hilo. *BDG* iwe na wasimamizi waaminifu na ikiwezekana majina yachujwe kwa kuonyesha maksi za washiriki na *TSPF* iandae wafanyakazi maalum watakaopita Mikoani kusimamia zoezi hilo badala ya utaratibu wa sasa wa kupitia *SIDO, TCCIA* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aelezee mamlaka iliyopewa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ya kuendelea kutoza ada ya Sh

20,000/= kwa pikipiki za magurudumu mawili na Sh. 30,000/= kwa Bajaji wakati katika bajeti ya Waziri Mkuu Serikali imefuta tozo zote zinazohusiana na pikipiki na bajaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahakikishaje kuhusu ubora wa madawa yatumikayo na binadamu Tanzania, yanayotengenezwa na Viwanda vya Tanzania kama dawa za *Panadol, SP*, na kadhalika ambazo hazionyeshi uwezo wa kupunguza maumivu au kuponya maradhi na pia kuuzwa kiholela Mitaani?

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya. Naishauri Serikali iimarishe viwanda vidogo vidogo vya ndani vya ubanguzi wa korosho, matunda, na mafuta ya alizeti ili kukuza ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwabane wenye viwanda vya *juice* ambazo badala ya kutumia matunda yanayozalishwa nchini, wao wanaagiza *concentrate* nje ya nchi na kuacha matunda yanayozalishwa nchini kukosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii baada ya kuleta ufafanuzi wa maeneo hayo mawili.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimwia Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa tukiimba kuwa Kilimo ni Uti wa Mgongo. Haiwezekani kilimo chetu kikaendelea bila kuyapa mazao yetu thamani. Kwa sababu hiyo, viwanda vya kati na vikubwa ni muhimu sana kwa uchumi wetu. Viwanda vya *juice*, matunda, Viwanda vya Nguo ambavyo vingi vimekufa kama *Mwatex*, Urafiki na vilevile Viwanda vya Nyama na Ngozi, Viwanda vya Kusindika Samaki na Viwanda vya Maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kujitoa katika biashara, ni muhimu Serikali ikaanzisha mikakati maalumu wa kuwawezesha wananchi au Taasisi kuanzisha viwanda ili kuendeleza kilimo kukuza uchumi wa kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuongezeka kwa bidhaa toka nje ya nchi katika soko letu. Zipo bidhaa ambazo tunaweza kutengeneza hapa nchini kama vile viatu vya plastiki, vijiti vya kusafisha meno, leso, mifagio na vitu vingine. Serikali itengeneze na itangaze orodha ya bidhaa ambazo zinaweza kuagizwa nje na bidhaa nyingine zinunuliwe hapa nchini. Kwa kufanya hivyo, tutaokoa fedha nyingi za kigeni na kulinda viwanda vyetu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Masoko mpakani, hasa soko la Mabamba – Kibondo, niliwahi

kuuliza swali Bungeni kuhusu ujenzi wa soko la Mpaka katika katika kijiji cha Mkalazi Kata ya Mabamba Wilaya ya Kibondo. Aliyekuwa Naibu Waziri - Mheshimiwa Nyarandu alinijibu kwamba Benki ya Rasilimali *(TIB)* imekubali kutoa fedha, kilichobaki ni michoro. Lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea na Mheshimiwa Waziri hajazungumzia soko hili kwenye hotuba yake. Napenda kutoa ushauri kwa Serikali, kwamba isimamie soko hili lijengwe, kwani ni muhimu kwa uchumi wa Wilaya ya Kibondo na Tanzania ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kutokana na ongezeko la ukosekanaji wa ajira *SIDO,* inapaswa kutoa elimu ya ujasiliamali kwa mapana. Mfano mzuri ni *SIDO* – Kigoma ambapo ni muda mrefu hawajatoa Elimu ya Ujasiliamali Wilaya ya Kibondo. Napenda kuiomba Wizara ikishirikiana na *SIDO* – Kigoma kutoa elimu Wilayani Kibondo, kwani wananchi wanaulizia, na wengi hawajui *SIDO* ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali, ifungue Ofisi za *SIDO* kila Wilaya ili huduma zao ziwafikie wananchi kwa urahisi. Mfano Mwananchi wa Kibondo kwenda Mkoani Kigoma zaidi ya kilometa 300 kufuata *SIDO* siyo kitu rahisi. Napenda kuiomba Serikali ifungue Ofisi za *SIDO* – Kibondo.

**MHE. JUMA OTHUMAN ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya ngozi hapa nchini kwetu, imekua mbaya sana wakati ngozi nyingi inapatikana. Naiomba Wizara iwezeshe wafanyabiashara wadogo wadogo kupitia *SIDO* ili

viwanda hivi viweze kukua na pia vijana wetu waweze kujiajiri wenyewe na kujitoa katika janga la umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mizani zinazotumika dukani kupimia chakula ziangaliwe mara kwa mara ili kutendewa haki kwa ununuzi. Serikali izidishe umakini kwa kuhakikisha *TBS* wanafanya kazi zao vizuri ili kulinda afya ya mlaji kwa kutoletewa vifaa visivyo na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika matatizo makubwa ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na baadhi ya wananchi na hata viongozi wa dini mbalimbali ni sehemu ya misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha zilizopo za *EPZs* na *SEZs* ambapo hata Viongozi wa Dini katika kitabu chao cha *The One Bilion Dolla Question,* walikilalamikia ni kama ifuatavyo: Msamaha wa kodi ya biashara kwa miaka 10 ya awali, msamaha wa kodi ya pango, gawiwo na riba kwa miaka 10 ya awali, msamaha wa kodi ya malighafi zinazoagizwa kutoka nje na uagizaji wa mitambo kwa ajili ya uzalishaji *(capital goods)* viwanda kwenye *EPZs*, msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani ya bidhaa kwenye huduma kama vile maji, umeme na huduma za bandarini *(wharfage)* na kupeleka faida kwao bila ya kikomo *(Unlimited repatriation of profit).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze uzoefu wa nchi nyingine katika misamaha ya kodi ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, uzoefu wa nchi mbalimbali zinazotekeleza mpango wa *EPZ* umeonyesha kuwa maeneo yaliyokuwa yametengwa hapo awali kwa ajili ya *EPZs* ni madogo sana. *EPZs* za sasa zina mfumo wa *Satelite Towns* ambazo pamoja na viwanda mbalimbali, pia kuna huduma zote muhimu kama makazi ya watu, mabenki, viwanja vya ndege, bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo, mwezi Novemba, 2006 Mheshimiwa Rais aliagiza yatafutwe maeneo yenye ukubwa siyo chini ya hekta 2000.

Mheshimwia Mwenyekiti, nataka kujua, mpaka sasa *EPZs* imetekeleza kwa kiwango gani agizo la Mheshimiwa Rais mpaka sasa? Serikali kupitia Waraka wa Mawaziri Na. 06/96 wa 1996, ilipatia *NDC* jukumu jipya la kuanzisha na kuendeleza miradi ya kiuchumi ya mchuchuma - Liganga, magadi ya Ziwa Natron na miradi mipya kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya maslahi ya Taifa na kujenga uchumi endelevu ni vyema Serikali ikahusika kufanya tafiti za rasilimali zake kubaini ubora wa wingi wa madini yaliyopo kabla ya majadiliano ya umiliki wa hisa na wawekezaji ili kuweza kuwa na nguvu wakati wa mjadala na kupata hisa hadi asilimia 49%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC* inahitaji kuongezewa uwezo kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ya uanzishaji viwanda mama kama ilivyoainishwa katika waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 06/96 1996 na maagizo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema mwenye kurehemu. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu wake kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya biashara katika nchi siyo nzuri na hii yote inasababishwa na urasimu na ugumu wa kupata leseni ya kuendesha biashara. Mara nyingi wawekezaji wanapokuja kutaka kufanya biashara, basi wanashindwa kwa sababu ya urasimu na badala yake wanakimbilia nchi jirani kama vile Kenya. Wanapofika Kenya wanapokelewa kwa urahisi, kwani hakuna urasimu, wanakaribishwa na kupewa leseni kwa haraka. Naishauri Serikali iondoe urasimu katika kutoa leseni za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zinazoingizwa nchini ambazo ziko chini ya viwango, zinaathiri sana biashara katika nchi yetu. Mimi nataka Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi, bidhaa zilizo chini ya kiwango zinazingia vipi wakati zinapitishwa katika Bandari zetu? Au viwanja vya ndege? Hawa watu wa *TBS* wanakuwa wapi? Au hawajui wajibu wao hata

wakaruhusu bidhaa hizi ziingizwe nchini kwetu? Hapa inaonyesha kuna tatizo la rushwa na maslahi binafsi kwa watendaji wetu wa *TBS* na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ichukue hatua madhubuti kwa Watendaji hawa ambao siyo waaminifu, ni wababaishaji na wala rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda ni muhimu sana. Naomba Serikali isimamie sekta hii ili viwanda vilivyokufa vifufuliwe na ianzishe viwanda vya kusindika mazao ili vijana wapate ajira, na pia wakulima wapate soko la kuuza mazao yao. Hapa umasikini utapungua kwa kiasi kikubwa na pia Serikali itapata mapato.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara, sijaona mpango mkakati wa Wizara kuanzisha au kufungua kiwanda chochote kipya katika mwaka huu wa fedha 2012/2013. Je, nini ni malengo ya Wizara katika hili? Nini matarajio ya Watanzania juu ya uanzishaji wa viwanda vipya ambavyo vingeweza kupunguza ajira kwa Watanzania walio wengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila mwaka wa fedha Wizara imekuwa ikisisitizwa kufungua Vyuo vingi vya Ufundi hususan *VETA*, lakini katika Wilaya ya Momba bado jambo hili limekuwa likikosekana. Je, vipi ni vigezo vya Halmashauri ya Wilaya ili zitimizwe, kwa Halmashauri ya Wilaya kupata sifa ya kujengewa *VETA*? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Naibu Waziri - Mheshimiwa Gregory Teu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vilivyobinafsishwa kwa wawekezaji, lakini mpaka sasa havifanyi kazi kama ilivyokusudiwa virudishwe Serikalini, viuzwe tena kwa wawekezaji wenye uwezo wa kuvifufua. Serikali itoe maelezo kuhusu hatima ya Kiwanda cha *General Tyre* kilichopo Mkoani Arusha ambacho hivi karibuni Mahakama iliamuru iuzwe kuwalipa mafao waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya *POAC* ilitembelea eneo la makaa ya mawe na chuma kule Ngara na baadaye kutoa ripoti yake Bungeni. Serikali ilikubali kutoa fedha kuiwezesha *NDC* na Kampuni ya Kichina iliyokuwa tayari kuchimba chuma Liganga. Nilitegemea hadi sasa kazi hiyo itakuwa imeanza japo kwa hatua za mwanzo za kutengeneza miundombinu inayohusiana na mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa mgodi wa makaa ya mawe waliiomba Serikali kutengeneza '*transmission line'* kutoka Makambako hadi Songea ili umeme utakaozalishwa uweze kusafirishwa. Serikali

inasema nini juu ya kuipa fedha *Tanesco* na kutengeneza '*transmission line'* kwa lengo hilo? Hatutaendelea kwa kusema kwenye makaratasi bila utekelezaji wa dhati na kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliyokuwa *Tanganyika Packers* iliuzwa kwa nani? Kwa kuwa mwekezaji huyo ameshindwa kuendeleza kiwanda, matokeo yake ameng'oa mashine zote na kubomoa kiwanda! Serikali inasema nini katika hili? Viwanda vya Korosho vilivyobinafsishwa haivibangui korosho tena, bali vimegeuzwa maghala. Nashauri viwanda hivyo virudishwe Serikalini ili wananchi Watanzania wapate ajira katika Viwanda hivyo vya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifugo mingi na Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi. Cha kushangaza, hatuna Viwanda vya Nyama wala Maziwa. Tuna Bahari ya Hindi na Maziwa makubwa kama vile Tanganyika, Victoria, Nyasa na kadhalika, lakini hatuna viwanda vya kutosha vya samaki. Tuna matunda mengi sana, lakini tunaagiza matunda kutokana na ukosefu wa viwanda vya kusindika matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutoa fedha za kutosha kwa *SIDO* na *VETA* ili waweze kutengeneza viwanda na mashine zinazoweza kununuliwa na *SACCOS* mbalimbali nchini kwa nia ya kuwa na viwanda vidogo vidogo vya matunda na hata maziwa na kadhalika.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo ya hekima ya kiwanda cha *general tyre*. Kuna taarifa za kupigwa mnada na kufunguliwa kesi Mahakamani. Nini hatima ya viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vimeshindwa kujiendesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kufufua viwanda vilivyokufa na kuanzisha viwanda vipya ili vipunguze tatizo la ajira kwa vijana? Wizara imejipangaje kimkakati ili kuwasaidia wafanyabiashara ndogo ndogo ambao wengi ni vijana na akina mama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini utekelezaji wa miradi wa *EPZ* inasusua na kuleta malalamiko karibu Mikoa yote ambayo mradi huo umepita?

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona jinsi Viwanda vyetu vya ndani vinapozidi kudumaa na kufifia na kutoa mwanya kwa bidhaa za nje kuingia kiholela. Haingii akilini mtu mpenda haki kuona eti tunaagiza vichokonoleo vya meno *(tooth pick)* kutoka nje (China). Hii ni aibu kwetu sote kama Taifa, na lazima kuketi kitako na kutafakari, kwanini hali hii tumeiruhusu? Kutokea kiashiria hiki kimoja tu, kinatosha kuelezea hali halisi iliyoko katika maeneo mengine kuhusiana na sekta hii. Zamani tulikuwa tunatengeneza baiskeli ya Swala, lakini sasa imeshatokomea. Kiwanda cha Matairi Arusha kiko hatarini kuuzwa, Serikali itueleze tunaelekea wapi kama Taifa kwa kutojali Viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wadau ukipita Mitaani wanaona sasa hivi ni bora *TFDA* kuliko *TBS*. Hisia

hizi za kudharau *TBS* na kuikubali *TFDA* zinatokana na ukweli kuwa *TBS* imepwaya sana katika kudhibiti vifaa feki kuingia nchini. Swali kubwa la kujiuliza: *TBS* inakuwa wapi wakati bidhaa hizi feki zinaingia nchini? Wizara na Serikali kwa ujumla ieleze umma uhalali wa kuwepo kwa *TBS* wakati bidhaa zenye madhara kama vile maziwa ya kopo, *blueband, TV* Radio na kadhalika zinazidi kuingia nchini kinyemela mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze umma wa Tanzania, kwa nini raia wa kichina wamegeuka kuwa Wamachinga? Hili suala ni la kuchekesha kidogo, lakini pia linakera. Kwani kuwashuhudia raia hawa wakifanya kazi ambazo ni za Watanzania, tena wa kipato cha chini siyo suala la kufurahisha hata kidogo. Ifahamike kuwa raia hawa wa kichina wanaonekana kwa urahisi sana kwa sababu ya rangi yao. Je, wale ambao hawaonekani kwa urahisi hali ikoje? Naisihi Wizara na Serikali yetu iwe sikivu na kushughulikia jambo hili kwa haraka na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nishati hasa ya umeme ni muhimu sana katika maendeleo na ufanisi ya Viwanda na Biashara. Ni ukweli usiopingika kuwa miaka ya hivi karibuni, nishati ya umeme imekuwa haitabiriki na kuleta usumbufu mkubwa kwa shughuli za biashara. Nishati siyo muhimu kwa wafanyabiashara wakubwa tu, bali pia wafanyabiashara wadogo. Mfano kutengeneza vinyuzi, *juice* na kadhalika. Ili tuwawezeshe watu wetu katika biashara, ni lazima tujikite katika kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa vijijini nao ili waweze kufaidikia na uwepo wa Wizara hii, wakiwemo wa Jimbo langu la Kibaha Vijijini, kuna umuhimu mkubwa wa kutengeneza uhusiano kati ya bidhaa za Kilimo na Viwanda. Mfano mzuri ni matunda ya kutengeneza *juice* kutoka kwa wakulima. Kinachohitajika ni kuhamasisha wale wenye viwanda kujenga utaratibu wa kununua bidhaa za wakulima kwa wingi ili wakulima wahamasike kulima zaidi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa wadhifa mpya walioupata kuongoza Wizara muhimu sana katika kuendeleza nchi yetu ifikie nchi yenye kiwango cha kati, jambo ambalo limewezekana kwa kupitia mkakati wa kuendeleza viwanda *(industrialization stategy).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa hoja hii, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la ushindani wa biashara za ndani. Kama kuwa na mtindo wa kupitia neno "wadau" vibaya. Sheria ya ushindani inataka wafanyabiashara katika eneo moja kufanya makubaliano namna ya kufanya hiyo biashara, ambayo ni pamoja na kupanga bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika biashara ya ujenzi wa barabara, ni kawaida kukuta wadau kwa mtindo wa Vyama kama Chama cha Wakandarasi wa Kichina. Katika zao la Pamba kuna Chama cha Wenye Viwanda vya Kuchambua Pamba *(ginner association).*

Chama hiki ni cha wanunuzi wa pamba na wanapanga bei. Naiomba Wizara imulike mtindo huu kwa kutumia neno “Wadau” kuhalalisha uvunjaji wa sheria na ushindani *(fair competition).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba ni zao muhimu katika viwanda vya kati. Pamba kama zao, ina mazao mawili, yaani mbegu ambayo ni asilimia 66, na nyuzi ambayo ni asilimia 34%. Pamekuwa na kutofahamu kwamba mkulima wa pamba ni mkulima wa mbegu ya mafuta kama vile alizeti, karanga na kadhalika. Mbegu ya pamba nayo iingie katika vitabu vya uchumi kama mbegu ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza hili ili mtazamo huu utumike katika kutoa kinga ya kikundi kama vile vinu vya mafuta ya alizeti, Aidha, Serikali isaidie usindikaji wa mbegu za pamba ili zao la mashudu litumike kama njia ya kusaidia mifugo kuondokana na kuhamahama. Kwani kwa kutumia mashudu, ng’ombe zitalishwa pale zilipo na kupata nyama bora. Mtazamo huu unaimarisha dhana ya *value chain.* Napendekeza utafiti ufanywe namna ya kuunganisha mbegu hizi za pamba na ufugaji bora, na viwanda vya vyama bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pamba ndiyo Viwanda vya Nguo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kuwa na nia ya kuvifufua viwanda hivi pamoja na viwanda vya mavazi *(again the courage of value of chain)* na ulinzi wa viwanda vyetu. Hakuna sababu mtu kuleta *grey cloth* kutengenezea kitenge au khanga. Viwanda tulivyonavyo vinatosheleza kutengeneza hizo nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PVOC* haifai na husaidia uharibu na zaidi wizi wa fedha za kigeni *(externalisation of foreign exchange)* ambazo ni adimu. Jambo hili lilishajaribiwa zamani, likaachwa kurejeshwa. Ni mradi wa Mafisadi. Majibu ya kuhakiki ubora ni rahisi sana. Bidhaa nyingine haiwezekani kwa *TBS, SSS* na kadhalika, kukagua *too diverse in quantity and quality.* Njia inayofaa *trade agreement quality* inayohitajiwa Tanzania na China isiruhusu *export* bidhaa chini ya viwango Tanzania inayohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ni-*cite* China, kwani bidhaa zinazoshukiwa kuwa siyo bora zinatoka China na zinaagizwa na wafanyabiashara wadogo wadogo. Mfano mzuri ni wafanyabiashara wa Kariakoo. Bidhaa hizi ni kama kucha, nywele na vyombo mbalimbali, haiwezekana kukagua kutoka nje. Kinachohitajika ni ushirikiano wa nchi tunayofanya nayo biashara kama China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata nchi za Magharibi zinafanya biashara na China, lakini *quality agreement* ni mojawapo ya masharti ya mkataba yanavyojaliwa na Serikali ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa, lakini vimeachwa na havifanyi kazi na kukosesha ajira Watanzania. Imekuaje viwanda vya ngozi havifanyi kazi kama zamani? Kiwanda cha Urafiki ni moja ya Viwanda vya Nguo muhimu sana nchini, vipi kinasuasua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tunaweza kujifunza Ethiopia jinsi ya kuendeleza bidhaa za ngozi? Kama siyo Ethiopia tunajifunze wapi Afrika?

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana kusikia Serikali imepanga kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini viwanda vinavyotengeneza thamani ya madini viwanda vikubwa vya saruji viwanda vya usindikaji. Ili kuweza kuboresha biashara ni lazima tufufue hivi viwanda vilivyokufa na viende sambamba na kujenga viwanda vingine vipya. Tutenge maeneo maalum ya uwekezaji mijini na vijijini na kukuza ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma, lakini Serikali naiomba kabla ya kufufua hivi viwanda wafanye utafiti kujua sababu ya kufa hivi viwanda na kwa ujenzi wa viwanda vipya pia Serikali ifanye utafiti sehemu zinazotakiwa kujengwa viwanda.

Pia naishauri Serikali, hizo sehemu zinazojengwa viwanda kabla ya kujenga tuhakikishe miundombinu inapatikana, yaani umeme na barabara na kama umeme na barabara havipo, siyo vizuri kujenga viwanda sehemu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa feki bado zinaingia nchini tena kwa wingi. Kwa mfano, matairi ambayo yamesababisha ajali nyingi katika nchi yetu. Lingine ni madawa ambayo wanatumia wanawake kwa kubadilisha ngozi zao, yanaleta madhara makubwa. Madawa haya kila siku yanauzwa madukani. Je, *TBS* wako wapi? Hawayaoni? Naishauri Serikali izidi kutilia mkazo jambo hili, kwani Sheria ya mwaka 2009 ya Udhibiti, inaonekana haitumiki vizuri. Je, Tume ya Ushindani ilikuja kwa kasi, mbona hivi sasa imelala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madai kuwa Shirika la *TBS* limeteua mashirika binafsi nchini Dubai kukagua magari yanayoingia nchini hapa Tanzania na kutakiwa kulipa Dola 150 kwa kila gari. Je, madai haya ni ya ukweli? Ikiwa ni ya ukweli, kwanini na hapa nchini magari yakiingia unatakiwa ulipe tena pesa kwa ajli ya gari chakavu? Kwa nini mwananchi alipie mara mbili? Serikali haioni kuwa inamkomoa huyu Mtanzania na ukiangalia *East Africa* kote hayatozwi Dubai. Je, hamtaki wananchi wanunue magari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine ni mfumuko wa bei. Bei za bidhaa ni kubwa sana hata zile bidhaa ambazo hazilipwi kodi kama vile *Computer,* zana za kilimo na nyingine pamoja na vyakula. Naishauri Serikali kupitia vitengo vyake, vipange bei na wawe wanapita madukani ili wajue zile bei walizopanga kama ndizo zinatumika.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara ni

miongoni mwa Wizara ambayo ni tegemeo la Taifa. Hata hivyo, bado Wizara hii haijashughulikia ipasavyo masuala ya Viwanda na Biashara katika nchi yetu. Kama kuna nchi ambayo ilikuwa na viwanda vingi vya uzalishaji, ni Tanzania. Leo hii viwanda vyote vimekufa kutokana na ukosefu wa miundombinu ya uzalishaji kama umeme pamoja na ukosefu wa vitendea kazi viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba suala zima la kufa kwa viwanda Tanzania limechangiwa kwa kiasi kikubwa na Serikali iliyo madarakani. Serikali haikuwa makini katika kushughulikia suala la viwanda jambo ambalo limerejesha nyuma maendeleo ya Taifa na kuchangia kwa kiasi kikubwa ukosekanaji wa ajira kwa vijana ambao wanamaliza masomo yao. Serikali ina wajibu wa kutoa kauli kwa Watanzania na sababu za msigni kabisa, ni kwanini miaka ya 50 hadi 70 viwanda nchini kote vilikuwa vinafanya kazi na umeme ulikuwa unapatikana, lakini leo baada ya miaka 50 umeme haupatikani? Ni kweli kwamba tunaendelea au tunarudi nyuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa biashara, Serikali imechangia kwa kiasi kikubwa uuaji wa biashara nchini kwa kukosa kuwaendeleza watu wa sekta binafsi, lakini pia kwa kukumbatia wawekezaji kutoka nje ambao wanaendeleza maendeleo ya biashara kwa nchi zao ndani ya nchi yetu, na kurejesha nyuma wawekezaji wa ndani ambao wangekuza maendeleo ya nchi yetu. Nchi hii imebarikiwa kuwa na zao la pamba ambalo likipatiwa viwanda, tuna uwezo

wa kuzalisha nguo, samaki, matunda, mabati, Viwanda na Kusindika Nyama na Viwanda vya Ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, biashara bila ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara wetu, hatutafika popote.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi vilivyobinafsishwa vya Korosho, Nguo, Ngozi na vingine havifanyi kazi na kusababisha ukosefu mkubwa wa ajira. Nashauri kwamba Serikali iwanyang'anye wote walionunua viwanda hivi na kuwapa wawekezaji watakaoweza kuviendesha. Kwa kufanya hivi, hata bei ya mazao itaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya nje ina sura ya unyonyaji kwa kiasi kikubwa, hususan kwa bidhaa za ndani zinazopelekwa nje na hasa kwa upande wa mazao ya kilimo. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba Serikali ifanye utafiti wa kina ili kujua bei halisi ya mazao yetu yanapouzwa nje kama korosho na pamba pamoja na maua, iangalie ni kwa nini bei zinashuka mara kwa mara kwa kisingizio kwamba bei katika Soko la Dunia limeshuka? Huu ni unyonyaji mkubwa na hasa kwa kuzingatia kwamba gharama za uzalishaji mashambani hupanda kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ichukue hatua ya kuwasiliana na Balozi zetu katika nchi mbalimbali ili watafute masoko mbadala kwa yale mazao ambayo masoko yake yanasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa jibu, ni kwanini maua yanayozalishwa Arusha yanasafirishwa nje kupitia Kenya na baadaye kutambulika kwamba yametoka Kenya? Je, Serikali inachukua hatua gani kwa lile sharti linalotolewa kwamba lazima maua yavunwe kwa mashine ndipo yapate soko Ulaya? Hatuoni kuwa tunawakosesha Watanzania ajira na pia kuzuia wananchi wenye uwezo mdogo wasiweze kufanya biashara ya maua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kidogo Sekta hii ya Viwanda na Biashara. Wizara hii inasikitisha sana kwa kuwatelekeza Watanzania na kuwabeba wageni toka nje hasa Wachina. Sababu ya kusema hivi ninayo. Mfano mzuri ni Jijini Dar es Salaam, maduka yaliyo mengi sasa hivi yanaendeshwa na Wachina kama maduka ya kuuza viatu, nguo, redio, simu, vifaa vya ujenzi, spea za magari, pikipiki na kadhalika. Je, Wachina hao wameingia nchini kama wachuuzi au wawekezaji? Mbona Watanzania wanaweza kuendesha shughuli hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie upya vibali vya biashara vya Wachina ili Watanzania

wasije kukosa kazi za kufanya na kujenga chuki kwa wageni na kuhatarisha usalama wa wageni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ushauri huu ufanyiwe uchunguzi wa kina sana, ili kuepusha madhara hapo baadaye.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mweyekiti, Taifa lolote lile ulimwenguni kama kweli linakusudia kuendelea na kupiga hatua, ni vyema kuwekeza katika Viwanda mama *(heavy industries)*. Sasa hoja yangu kwa Wizara ni kuomba Wizara kuwekeza katika uchimbaji wa madini ya chuma kwa kuliwezesha Shirika la Maendele la Taifa *NDC (National Development Corporation).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mchuchuma na Liganga ni wa kipekee katika shughuli za uchenjuaji wa madini ya chuma. Kuna mazao ya aina mbili yaani chuma chenyewe, na kitu kingine cha msingi ni uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu kwa sasa linakabiliwa na changamoto kubwa mbili na ambazo kwa hakika zisipopatiwa majibu ya uhakika na kwa haraka kuna hatari ya uchumi wa Taifa kuathirika vibaya sana. Moja, ni biashara haramu ya vyuma chakavu ambavyo vinachukuliwa kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo kuhujumiwa kwa miundombinu ya reli, barabara pamoja na miundombinu ya simu na

hata miundombinu ya Shirika la Umeme zikiwemo nyaya na mabomba ya maji pia hayakuachwa pembeni katika kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda na Biashara ni kiungo muhimu sana katika ukuaji wa uchumi. Sekta hizi zisiposimamiwa vizuri zinaweza kulemaza mustakabali wa nchi husika. Ni vyema sasa Wizara hii ya Viwanda na Biashara ichukue hatua stahiki kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na uzalishaji wa umeme wa uhakika, ili kutengeneza mazingira mazuri na wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa umeme wa uhakika na wa bei ya chini utasaidia katika kuzalisha bidhaa za bei nafuu na hivyo kuboresha hali ya maisha ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini, ni vyema Wizara ikaongeza juhudi zaidi katika kukabiliana na tatizo la uingizwaji wa bidhaa bandia kwa kuliwezesha Shirika la Viwango Nchini Tanzania *(TBS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwepo na chombo madhubuti cha kudhibiti ubora wa viwango wa bidhaa zinazoingizwa nchini, wakati mwingine afya za watumiaji huathirika na hatimaye athari pia huonekana katika ukuaji wa uchumi vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufufua upya Viwanda vya Nguo vilivyokufa na kuwekeza viwanda

vipya ni jambo ambalo litasaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha na kuinua bei ya zao la pamba, ambayo imekuwa haitabiriki kutokana na kuyumba kwake katika Soko la Dunia.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja tu ninalotaka kujua katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Mkoa wa Singida ni moja ya Mikoa ambayo haina viwanda wala mazao ya biashara na hivyo kuwa nyuma sana kimaendeleo, katika miaka ya hivi karibuni, zao la alizeti limeonekana kustawi vizuri katika Mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha Kusindika Mafuta ya Alizeti katika Mkoa wa Singida ili kuwahakikishia wakulima wa alizeti, kuongeza uzalishaji wa zao hili kupunguza uingizwaji wa mafuta ya kula toka nje ya nchi na hivyo kuinua uchumi wa Mkoa na Taifa kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri. Namshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa bajeti hii kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka bajeti ya Wizara hii haipandi kwa kiwango cha kutosha, hivyo kukwamisha juhudi za kuleta mapinduzi endelevu ya viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa viwanda vingi hapa nchini kunalighalimu Taifa hasa vijana kukosa ajira na nchi yetu kuwa soko la walaji wa bidhaa toka nje. Tena nyingi ya bidhaa hizo hazina ubora na hivyo kusababisha matatizo makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubora *(TBS)*, kwa huzuni sana naomba kutoa maoni yangu kwa Shirika hili ambalo kwa kweli linatia Serikali yetu aibu kubwa kwa kushindwa kufanya kazi yake kwa ufanisi. Watanzania tunaibiwa vitu vingi ambayo havina ubora kama TV, Deki, Radio, viwembe hata kucha vinashindwa kukata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji viwanda vidogo vidogo vijijini, naomba Mheshimiwa Waziri anijibu kuna mpango gani wa haraka juu ya kuanzishwa kwa viwanda vijijini ili vijana wengi wapate kazi? Wakipata kazi hata Mijini hawatakimbilia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Chokaa na Jipsam Iringa - Mvumi kimekufa. Wizara ina mpango gani wa kukifufua? Kiwanda hicho kiko katika Jimbo la Mtera na kilikuwa na wafanyakazi zaidi ya 400, sasa hawana kazi wote, na kijiji hicho hakina mapato tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Viwanda na

Biashara. Nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwateua Mheshimiwa Abdallah Kigoda kuwa Waziri, na Naibu Waziri wenye uzalendo na mwono wa mbali (*vision).* Pia uzoefu wao naamini utasaidia kuleta maendeleo katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi bila viwanda haina maendeleo. Viwanda ndiyo vinaongeza ajira, vinaongeza thamani ya malighafi mazao na maliasili yetu pia ni njia rahisi kwa Serikali kupata kodi kwa manufaa ya Taifa. Ningeshauri Serikali iunde Tume Maalum na pia iweke watafiti *(consultants)* wafanye utafiti wa namna ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini na kuanzisha na kuendesha viwanda kwa faida. Pia mazingira ya kufanyia biashara Kimkoa na Wilaya ili Serikali iweze kuongeza wigo wa kulipa kodi na mfumo wa ukaguzi unaofanana unaofanywa na vyombo vyetu vya udhibiti, yaani *regulatory authorities*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, madawa ya kilimo yanakaguliwa kwanza na *TBS,* baada ya hapo *TFDA* na mwisho *TPRI*, yote yanafanya kazi moja. Gharama za ukaguzi zinalipwa na mfanyabiashara, lakini mlaji wa mwisho ndiye anabeba mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, katika kiwanda, Wakaguzi mbalimbali wanakuja kila mmoja kwa wakati wao. Unakuwa mzigo wa gharama kwa mwenye kiwanda, lakini pia hasara kwa muda atakaotumia. Kuna Wakaguzi wako 15 au 16, maana yake ni kuwa atapoteza siku za kazi 15 au 16. *Time is money.* Unapoteza hela kuwahudumia hao Wakaguzi

ambao hawana muda maalum, wanakuja muda wanaotaka siku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingeweza kuandaa timu moja au mbili tu za ukaguzi wa viwanda hivi vyenye wataalamu mbalimbali ili kupunguza gharama na muda. Pia ingekuwa inapunguza gharama za Serikali kwa upande wa Wakaguzi. Ukaguzi wa dharura ufanyike wakati wowote tunapotilia mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha elimu kwa Maafisa Biashara wetu, wengi wao wamebaki wakikaa ofisini kukata na kukagua leseni tu. Hawana ubunifu wa kutoa elimu kwa wajasiriamali au wafanyabiashara, hawatoi elimu kwa Halmashauri zetu namna ya kuongeza mapato na kutafuta masoko, yaani kuboresha biashara katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Mheshimiwa Waziri angalie ada za leseni. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati wamependekeza kutoza leseni za kilimo kutoka Sh. 20,000/= hadi Shilingi milioni moja katika Bonde la Kiru na maeneo nje ya Bonde hilo kuwa Sh. 80,000/=. Je, ubaguzi huu ni sahihi? Hawa wote ni wakulima, kwa nini pawe na tofauti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna *fair play,* au usawa katika ushindani wa biashara? Pia viwanda vidogo na hati pamoja na ukubwa huwa bei ni moja. Katika bonde hilo na tofauti nje ya bonde hilo, huwezi

kushindana kama biashara yenu inafanana na mmoja analipishwa kodi na tozo na ada kubwa na mwingine analipa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali kwa kupita Wizara ya Viwanda na Biashara itutembelee Wilaya ya Babati ijionee fursa za uwekezaji uliopo katika Viwanda na Biashara mbali mbali Wilayani Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali itoe vipaumbele ili kukuza Sekta ya Viwanda nchini. Washirikiane na Wizara zote husika kuweka mazingira bora ya Biashara.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao wote kwa hotuba mahiri ambayo inatoa matumaini kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba pia kuipongeza Wizara kwa kusimamia Sekta ya Masoko ya Ndani ya Nchi na Nje ya Nchi, kwani Tanzania kwa kiasi kikubwa tunanunua kuliko kuuza. Huu umekuwa kama ni utamaduni kutokana na uduni wa kuwa na masoko ya ndani na nje. Watanzania ni wakulima wazuri na hata watengenezaji wa baadhi ya bidhaa ni bora. Tatizo letu lipo katika *packaging,* kwani vifaa tunavyouza pia huwa inatakiwa pia iwe na ubora ya kuvi-*pack* ili vivutie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo vidogo (*SIDO)* kwa kipindi kirefu vimedorora na havisikiki kwa wananchi. Hao Maafisa Ugani hawaonekani Mijini wala Vijijini. Wizara inahitajika kutoa wito kwa *SIDO* kujitangaza kuhusu utendaji kazi zao ili kurejesha matumizi kwa wananchi kama ilivyo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *SIDO* washirikiane na *VETA* kwa kutoa elimu ya wajasiriamali kwa jamii ya Kitanzania ili kuongeza nguvu ya utendaji kazi zake. Huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Abdallah Kigoda, Naibu Waziri -Mheshimiwa Gregory Teu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma una fursa ya kuweza kuwa na Viwanda vya Sukari na Mafuta yanayotokana na Mawese pamoja na alizeti sasa. Je, ni lini Serikali itahamasisha wawekezaji kuja kuwekeza katika Mkoa huo ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Kasulu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii kwa maandishi. Kwanza, namshukuru Mola kwa

kunipa afya nzuri na kuweza kuchangia hoja hii. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi hadi leo. Viwanda vingi vimekuwa havifanyi kazi na vingine kufa kabisa hasa vilivyobinafsishwa jambo ambalo uchumi wa Tanzania unaathirika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kwamba Wizara ivifuatilie viwanda hivyo na kuwa na mikakati ya makusudi ili viwanda hivyo vifufuliwe kwa sababu ndivyo vinavyoweza kuwapatia ajira vijana wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja cha maonyesho Saba Saba kinakabiliwa na changamoto ya baadhi ya wananchi kupora eneo hilo la kiwanja na kuweka *garage* ya magari. Tatizo hili ni la siku nyingi sana, halijapatiwa ufumbuzi na hivyo kuzorotesha baadhi ya mipango ya uendeshaji wa shughuli za mipango ya Saba Saba. Naomba Serikali isimamie haya ili sehemu iliyochukuliwa irudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC* ni shirika linaloweza kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo wengi sana, lakini Shirika haliwezeshwi vizuri kifedha na Serikali. Kwa hiyo, naomba Serikali kuliwezesha Shirika hili ili liweze kumudu shughuli zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hapa nchini bidhaa feki na bandia imekuwa jambo la kawaida kabisa, jambo ambalo linahatarisha afya ya wananchi na kuua baadhi ya bidhaa ambazo siyo feki. Kwa sababu bidhaa feki ni bei rahisi na wananchi wanakimbilia vitu ambavyo ni bei rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni lazima isimamie vizuri ili kudhibiti mambo hayo. Nazidi kukupongeza kwa kunipa fursa hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa nawaomba Waheshimiwa Mawaziri watoa hoja waanze kazi yao ya kuhitimisha hoja yao. Nitamwita sasa Mheshimiwa Naibu Waziri aanze na atafuatiwa na mtoa hoja Waziri mwenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Waziri wa Viwanda na Biashara kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Kwa sababu bajeti yenyewe inaongea na bajeti yenyewe inatekelezeka, kwa hiyo, ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kunijalia afya mpaka hivi leo na nipo mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kupitia kwake huyo Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema. Naomba nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani ambayo aliionyesha kwangu na kuniteua tena kwa awamu ya pili kama Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Namshukuru sana sana. Kwa sababu ni heshima pekee kwa kazi ambayo aliifanya na kama alivyoelekezwa na Mwenyezi Mungu, maana si yeye bali kupitia kwa Mwenyezi Mungu aliweza kufanya hayo aliyoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nimshukuru kipekee Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda kwa malezi na mwongozo ambao ananipa na ushirikiano ambao ananipa na nafasi ambayo ananipa katika kutekeleza majukumu yangu. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ungeniuliza je, unajisikiaje kufanya kazi na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, ningekujibu kwamba kusema kweli ninasikia raha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nitumie fursa hii kipekee kumshukuru Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na kwa ushirikiano ambao wananipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nichukue fursa hii niwashukuru sana wafanyakazi wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara pamoja na Taasisi zake zote ambazo zipo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano ambao wametuonyesha mimi na Waziri wangu tangu tumeingia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kwamba siku ya kwanza kabisa wakati tumeingia pale mimi na Waziri wangu, hawa wafanyakazi, Menejimenti ya Wizara walitupokea kwa shangwe kubwa sana na tulipoingia katika ofisi ile kwa mara ya kwanza tulipiga hodi mimi na mwenzangu tukawaambia wenzetu wafanyakazi wa Wizara hii hodi na wakajibu kwa matumaini makubwa wakisema karibu na wakaahidi kwamba watafanya kazi kwa kushirikiana pamoja na hivi ndivyo ilivyo mpaka sasa tunashirikiana nao vizuri sana wafanyakazi wote, menejimenti yote na Taasisi zote ambazo zipo chini ya Wizara hii na tupo pamoja katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, tunawashukuru sana kwa michango yote. Kama ilivyo ada, hapo baadaye Mheshimiwa Waziri wangu atawatambua mmoja mmoja wale waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia kwa kuongea. Lakini kwa ujumla tunasema ahsanteni sana kwa kuweza kujumuika nasi, ambacho tunaomba sasa ni kwamba mtuunge mkono ili muweze kupitisha bajeti hii siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana familia yangu na hasa hasa mke wangu, watoto wangu, wazazi wangu kwa uvumilivu mwingi ambao wananipa au wanakuwa nao wakati mimi natekeleza majukumu haya ambayo nimepewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kipekee naomba sana bila kuwasahau wapigakura wangu wa Jimbo la Mpwapwa, hawa ndiyo walionipa ridhaa ya kuingia hapa Bungeni na nasema hivi, mshikamano wetu uendelee daima. Maendeleo katika Jimbo letu ni daima, utengano unaleta udhaifu. Mambo mazuri hayataki haraka, tumethubutu, tumeweza na sasa lazima tusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali katika Jimbo langu la Mpwapwa kwa kazi ambayo imefanyika kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Nasema kwa sababu Jimboni la Mpwapwa sasa hivi tulikuwa na kiu ya kuweza kupata barabara ya lami ambayo inatoka maeneo ya Mbande inapita pale Kongwa *by pass* inaelekea Mpwapwa. Hiyo barabara hivi sasa imefikia katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu. Kwa hiyo, ndugu zangu wa Mpwapwa tutegemee kwamba katika miaka hii miwili au mitatu iliyobaki kazi hii itafanyika na msikie kutoka kwangu. Wapo watu wanapitapita hapo na kusema mambo ambayo si ya kweli. Msemakweli ni mimi Mbunge wenu. Tutapata umeme hivi sasa jambo ambalo lilikuwa lina matatizo, umeme uliokuwepo ulikuwa unapita milimani na

kuingia Mpwapwa, wakati wa matatizo nguzo zikianguka ilikuwa ni tabu sana kuweza kujua nguzo ambazo zimeanguka kwa sababu nguzo zilikuwa zinapita mlimani. Sasa hivi nguzo zote zitapita kwenye barabara na sasa umeme hata kama unakatika wanaweza waka-*trace* wakajua ni wapi ambapo umeme umeleta matatizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri sasa ungeanza kuingia kwenye hoja ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ilikuwa kwanza nipate muda kidogo wa kupiga siasa katika Jimbo langu, lakini ninakushukuru kwa kunishtua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mambo mengi tutayajibu kimaandishi na kuweza kuwatambua wale wote ambao wamechangia na kazi hiyo ataifanya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijikite moja kwa moja katika majibu ya hoja maalum ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, moja ni kuhusu matumizi ya shilingi bilioni 60 zilizotengwa maalum kwa *EPZ*. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge ambao wameuliza swali hili na Bunge lako Tukufu kwamba shilingi bilioni 60 zilizotengwa kwa *EPZ* zitatumika kwa ajili ya uthamini na ulipaji wa fidia kwa maeneo ya Kurasini ambapo Kituo cha *Tanzania China Logistic Centre* kitajengwa. Kituo

hicho kitaongeza ajira, soko la malighafi nchini pamoja na kuvutia wawekezaji kwa kuwa kituo cha kutangaza fursa za bidhaa za Tanzania kwenye soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine ambayo imeulizwa kwamba elimu ya vipimo kutolewa hasa kwa watumiaji wa ngazi za chini. Hoja hii inahusu Wakala wa Vipimo. Wizara kupitia Wakala wa Vipimo inaendelea kuelimisha umma juu ya vipimo sahihi kupitia televisheni, radio, magazeti, vipeperushi, kalenda pamoja na kushiriki maonyesho mbalimbali hapa nchini. Jumla ya vipindi 20 vya televisheni vimeandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, jumla ya vipindi 10 vya redio, taarifa 37 za magazeti ziliandaliwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, minong'ono imezidi, naomba wanaojadiliana wajadiliane kwa utaratibu ili tupate nafasi ya kusikiliza.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wakala ilishiriki jumla ya maonyesho manne (4) ya Kitaifa ambayo ni Sabasaba, Nanenane, Maonyesho ya *SIDO* na Maonyesho ya Wanawake Wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Ushindani kujitangaza kwa umma. Tume ya Ushindani imekuwa ikijitangaza kwa umma kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo uendeshaji wa semina katika Mikoa na hivyo kuelimisha umma juu ya kazi na majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Ushindani Na.8 ya

mwaka 2003. Tume itaendelea kujitangaza Mikoani kutegemeana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine maalum ni kwamba malipo kwa waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Karatasi Mgololo. Suala la wafanyakazi waliofukuzwa Mgololo limefanyiwa kazi na Kamati ya Maalum iliyohusisha wajumbe kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na *Consolidated Holding Corporation* (*CHC)* na kutoa mapendekezo ambayo kwa sasa yanashughulikiwa na *CHC* kwa kushirikisha mwekezaji ili kufikia muafaka kuhusu malipo ya wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kwamba kushawishi mazingira rafiki katika ulipaji kodi. Mamlaka ya Mapato Tanzania yaani *TRA* pamoja na majukumu yake ya kukusanya mapato ya Serikali pia hutoa elimu ya kodi kupitia semina za walipa kodi na makongamano na wadau kwa kutumia vipeperushi, vipindi vya redio na luninga, sanaa na matumizi ya Tovuti ya *TRA*. Kwa mwaka 2011/2012, *TRA* imeendesha jumla ya semina 307 ikilinganishwa na malengo ya semina 387 kwa walipa kodi wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *TRA* imeanzisha mkataba na mlipa kodi yaani *Tax Payers Charter* unaobainisha haki na wajibu wa mlipa kodi pamoja na viwango vya huduma bora. Pia *TRA* imeweka mfumo endelevu wa maboresho ya huduma zake kwa kutekeleza kanuni zinazozingatia viwango vya ubora za *ICO* 900 mpaka 8. Aidha, *TRA* imeanzisha mkutano wa

wadau yaani *Stakeholder Forum* ufanyikao mara nne kwa mwaka ambapo maoni ya walipa kodi hupokelewa na kutumika kuboresha mipango na shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa watumishi wanatoa huduma bora, *TRA* huendesha mafunzo ya huduma kwa wateja, yaani *customer care training* ambayo hufanyika mahali pa kazi na kwenye Chuo cha Kodi kilichopo Mikocheni Dar es Salaam. Vilevile *TRA* inashirikiana na wananchi katika kuwafichua watumishi wasiozingatia kanuni na maadili kwa kupokea taarifa kwa njia mbalimbali kama kupiga simu kwenye kituo cha huduma na mawasiliano (*call center)*, barua pepe, sanduku la maoni na kutoa maoni kwenye semina za *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni maboresho ya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es *Salaam (Dar es Salaam International Trade Fair).* Ushauri wa Waheshimiwa Wabunge umepokelewa na utazingatiwa katika maandalizi ya Maonyesho yajayo na tutahakikisha kwamba tunapata washiriki wengi zaidi hasa wajasiriamali wa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kujenga Ofisi Dar es Salaam. Wizara kwa muda mrefu imefanya jitihada za kupata jengo lake ili kuondokana na kodi kubwa ambayo ni ya pango ambayo inalipwa hivi sasa katika jengo la *Water Front* ambayo ni mali ya *NSSF*. Maeneo yaliyobainishwa kwa wakati huo ni pamoja na kiwanja cha *TIRDO* ambako Ofisi au Wizara inategemea kujenga jengo la Ofisi, ni jengo ambalo lipo katika

kiwanja cha *TIRDO*, kuna Kidongo Chekunde iliyokuwa *Etiens Club,* haya ni maeneo ambayo Wizara inategemea kujenga Ofisi yetu hapo, *Etiens, TIRDO* au Kidongo Chekundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ujenzi haukufanyika kutokana na sera ya maelekezi ambayo Serikali imeelekeza kwamba Ofisi za Wizara Dar es Salaam zisijengwe na badala yake zijengwe katika maeneo ya Chamwino katika Manispaa ya Dodoma. Kutokana na Dar es Salaam kuwa kitovu muhimu kwa shughuli za Viwanda na Biashara, Wizara inaangalia uwezekano wa kupata jengo la Serikali kwa sasa ambalo litatumika kwa ajili ya ofisi kwa kipindi hiki cha mpito ili kupunguza gharama kubwa za pango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kama nilivyoanza mwanzo kusema kwamba naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia na sasa nampa nafasi Mheshimiwa Waziri wangu aweze kufanya majumuisho mengine, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Kigoda ili aweze kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kujaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo wamezitoa kuhusiana na hotuba yetu ya Bajeti na Makadirio yetu ya fedha ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa namna ya kipekee kuishukuru sana Kamati ya Viwanda na Biashara chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa pamoja na Wajumbe wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kutusaidia Wizara yetu ya Viwanda na Biashara. Sisi Wizara yetu inaichukulia Kamati ile kama *think tank* ya kuona Wizara tunaendeleaje. Lakini vilevile nashukuru kwa michango mingi inayotoka hapa Bungeni, napenda kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wizara yangu inalichukulia Bunge letu Tukufu kama *think tank* ya kuendeleza shughuli zetu ambazo tunazifanya kwenye Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza, ningeomba sasa nichukue fursa hii ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia na kujadili hotuba hii. Tumepata Waheshimiwa Wabunge 115 ambao wamechangia kwa maandishi na Wabunge 10 ambao wamechangia hapa ndani ya Bunge. Sasa naomba kuwatambua wale waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Lucy Philemon Owenya, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani

Chibulunje na Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallac, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu na Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim,

Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Shaffin Sumar, Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Haroub M. Shamis, Mheshimiwa Lolecia J. Bukwimba, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar na Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** wengine ni Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Abdulsalaam Seleman Ameir, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa David Ernest Sillinde, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Dustan Kitandula, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Salvatory Machemli, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Rajab M. Mohammed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia ndani ya Bunge lako Tukufu ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Highness Kiwia, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga, Mheshimiwa Lolecia Jeremiah Masele Bukwimba, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Chiku Abwao na hatimaye Mheshimiwa Gregory George Teu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo vilevile waliochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Magale John Shibuda, samahani sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao ndio waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Wale niliowasahau, nawaomba radhi na tutawataja majina yatakapofika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kutoa majibu kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini ningeanza kwanza na mambo ya ujumla. Nimefurahi kwamba Wabunge wengi katika michango yao tumekubaliana kabisa kwamba sasa hivi ni lazima tuwe makini kwa maana ya *serious* kuangalia ni jinsi gani tunaendelea na mchakato wa ujenzi wa uchumi ambao unategemea viwanda na hili ni muhimu ili kubadili mfumo wa uchumi wetu uwe ni mfumo wa kutegemea viwanda badala ya kutegemea kilimo kwa sababu tukishaimarisha viwanda vyetu taratibu nyingine zote za kujenga

uchumi zitafuatia. Lazima tuhangaikie viwanda mama, viwanda unganishi, viwanda vya kati na viwanda vidogo. Kwa sababu vikishaimarika hivi biashara itafanyika vizuri, masoko yatafanya kazi vizuri, yatashamiri, wananchi watakuwa wanafanya kazi zao ili kujenga ajira na kuamsha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzoni sasa hivi natakiwa nimtambue Mheshimiwa Muhammad Sanya na utanisamehe Mheshimiwa, Mheshimiwa Mustapha Akunaay naye amechangia kwa maandishi, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Dustan Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanafikiri sekta ya viwanda kwa mfano hapa Tanzania inapochangia kwenye pato la Taifa kwa kiwango kikubwa tunasahau kwamba katika kutegemea uchumi wetu kuendeshwa na kilimo tunajikuta hatuwezi kupiga hatua kubwa sana katika kuendesha viwanda vyetu. Kwa hiyo, ni muhimu sasa hivi wote tukakubaliane kwamba mchakato tutakaokwenda nao ni mchakato wa kuboresha viwanda vyetu ili tuelekee kwenye uchumi wa nchi ya kati, lakini vilevile kwenye nchi ya kipato cha kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa kulisisitiza ni kwamba tukubaliane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba ile dhana ya kwamba Serikali itajenga viwanda, nadhani hii tuondokane nayo sasa. Tumeshakubaliana kabisa kwamba Serikali kazi yake kubwa ni kuweka mazingira wezeshi, kuweka mazingira mazuri ya kuvutia sekta

binafsi, sekta ambayo ndio itajitahidi katika uwekezaji wa viwanda, biashara na masoko. Sisi kama Serikali kazi yetu itakuwa ni kuweka mazingira mazuri. Hili linajionyesha wazi hapa nchini tayari tuna taasisi nyingi sana sasa hivi ambazo zinashughulikia masuala ya sekta binafsi. Tunayo *Tanzania Private Sector Foundation, TTCIA, CTI* tuna taasisi nyingi tu ambazo kazi zake kubwa ni kuona kwamba zinashirikiana na Serikali kuweka mazingira mazuri ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** suala la ubinafsishaji limezungumziwa kwa hisia nyingi tu, lakini napenda kulizungumzia suala hili kwa ufupi tu. Tunapozungumzia ubinafsishaji ni lazima tufahamu kwamba ni utekelezaji wa hatua kama tano hivi. Kwa sababu ubinafsishaji unahusisha uuzaji wa moja kwa moja wa viwanda au Shirika, lakini vilevile ubinafsishaji unahusisha uuzaji wa hisa, ubia, ukodishaji, lakini mwisho ubinafsishaji vilevile unahusisha utaratibu ambao wanapewa wafanyakazi wa kiwanda husika *Management by Out.* Sasa ni vizuri tunapozungumzia suala la ubinafsishaji, tufanye tathmini kutokana na aina hizo tano na tuone wapi tuna mafanikio na wapi tuna changamoto. Lazima nikubali kwamba sera yoyote inayoweza kuendeshwa haiwezi ikawa na mafanikio moja kwa moja lazima matatizo na changamoto zitajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuwahakikishieni kwamba hivi sasa Wizara yangu iko katika mtazamo makini kabisa wa kuona kwamba ni jinsi gani tutajaribu kuvifufua vile viwanda ambavyo aidha vimefungwa, havifanyi kazi, lakini vile viwanda ambavyo vinafanya kazi kwa kusuasua. Lakini vilevile

lazima tukubali kwamba hata viwanda vingine ambavyo tunaviita viwanda hivi sasa kwa uchakavu vilivyofikia na matatizo vilivyonavyo vitakuwa ni jina tu. Pale Korogwe tuna kiwanda tunakiita Kiwanda cha Matunda. Sasa pale pamebaki jina tu kwamba ni Kiwanda cha Matunda lakini ukifika pale kwa kweli utakuta hali ya pale ni kwamba hamna kiwanda. Kwa hiyo, hizo ni changamoto ambazo Wizara yangu inazifanyia kazi sasa hivi na kuona kwamba viwanda vile vilivyobinafsishwa vinafanyaje kazi kwa tija. Hivi sasa Serikali imeshaanda utaratibu wa kuandaa taarifa kwa Baraza la Mawaziri ambayo inaonyesha hali ya viwanda vyote nchini hasa vile vilivyobinafsishwa na baada ya majadiliano ya kina, tutajua kwamba Serikali inachukua hatua gani kwa maana ya viwanda vile ambavyo aidha vitamilikishwa kwa wawekezaji wengine au itabidi Serikali ivinyang'anye viwanda vile na kuangalia taratibu za kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezungumziwa hapa suala la ngozi na Waheshimiwa Wabunge wengi tu. Tunachosema, wakati mnapotaka kuendeleza zao letu la ngozi, simaanishi kwamba Serikali itakurupuka tu. Tayari tumekwishawaita wenye viwanda vya ngozi, tumekwishawaita wauza ngozi na nakubali kwamba Kamati yetu ya Viwanda na Biashara inafanya utaratibu wa kuvifuatilia, katika mchakato huo tutapata majibu sahihi ya kuonesha kwamba tunakwendaje na utaratibu wa kusitisha uuzaji wa ngozi ghafi nje. Mimi kama Waziri wa Viwanda na Biashara bado nina imani kwamba sasa hivi tumefikia wakati wa kuhahakikisha kwamba hatuuzi ngozi ghafi nje, ni lazima hili tulisitishe kwa sababu katika nchi zote za

Afrika Mashariki na Kati pamoja na Ethiopia nchi pekee inayouza ngozi ghafi nje ni Tanzania. Lazima tujiulize sisi tuna matatizo gani na tunakosa ujasiri gani. Kwa hiyo, kwa kweli hilo ni eneo ambalo nilitaka kuliweka sawa. Hatukurupuki, tutalifanyia kazi na ndiyo maana tukasema kwamba hata upandishaji wa ushuru kufikia asilimia 90 bado utaweza kutuletea matatizo ya uaminifu kwa maana ya *compliance* na Serikali imekuwa ikipoteza mapato kwa kiasi kikubwa sana kutokana na wafanyabiashara wa ngozi wasio waaminifu na hili ni suala ambalo ndiyo maana nasema lazima tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limegusiwa ni kuhusu ufufuaji na uendelezaji wa Kiwanda cha *General Tyre*. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi tayari *NDC* imeshaanza mchakato wa ufufuaji wa kiwanda kile na tayari wataalamu wetu wako *site* katika utaratibu mzima wa kukikarabati kiwanda kile. Kiwanda kile tulipokiangalia ni kwamba mashine zake zote kwa kweli ziko *intact,* kazi kubwa sasa ni kukifanyia ukarabati wa majengo na tunafikiria kwamba hadi ifikapo mwaka 2012/2013, kiwanda kile kitaweza kufufuliwa hivyo kutoa ajira kwa wakazi wa Tanzania na hususan wakazi wa eneo la Arusha. Bado yapo madeni ambayo Serikali inayashughulikia katika kiwanda kile. Tuna madeni ya shilingi bilioni 38.2, lakini Serikali inasaidiana na *NDC* kuona kwamba tunayaondoaje madeni hayo na tayari tumeshapata wawekezaji ambao wana *interest* ya kuwekeza katika kiwanda kile kutoka China, Malaysia na Afrika Kusini na wote hawa watapatikana kwa njia shindanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumetokea hoja ya jitihada za kuhuisha viwanda vya sekta ndogondogo ya nguo. Viwanda vya nguo na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo, ni eneo ambalo Wizara yangu imelipa kipaumbele kikubwa sana na ndiyo maana katika Hotuba yangu nimeelezea ushiriki wa *Tanzania Gatsby Trust* wakishirikiana na *Gatsby Charitable Foundation* ya Uingereza kuona ni jinsi gani wanaendeleza mkakati wa sekta ya nguo na mavazi ili tuweze kuinua viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tayari kuna makampuni mengi yamekuja na kuonyesha upenzi wa kuwekeza hasa katika sekta ya pamba. Nimetaja kampuni ya Nitori kutoka Japan, nimeshatembelea maeneo mengi Shinyanga na maeneo yale ya Kanda ya Ziwa na hawa wanataka kuingia kwenye suala la uongezaji wa thamani kwenye masuala ya *ginning* kwa maana ya uchambuaji wa pamba, usokotaji wa nyuzi pamoja na ufumaji wa nguo lakini vilevile wanataka kujiingiza katika ulimaji wa zao la pamba lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine imejitokeza sana katika michango ya Waheshimiwa Wabunge na hii ni hoja ya kutaka kukinusuru Kiwanda cha Urafiki. Mara baada ya kupata majukumu haya ya kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara na mimi pia nilifanya taratibu za kukitembelea Kiwanda hiki cha Urafiki. Nakubaliana kabisa na hoja za Waheshimiwa Wabunge hususan hoja za Kamati ya Viwanda na Biashara kwamba pana kazi kubwa sana inayohitajika

kufanyika katika kile Kiwanda cha Urafiki. Kiwanda kile nimeshakitembelea, taratibu za pale Serikali tunamiliki hisa asilimia 49 na mwekezaji wa China anamiliki asilimia 51 ya kiwanda kile. Tunachotaka kuangalia ni jinsi gani na tutatumia njia gani kuhakikisha kwamba kiwanda kile kinafanya kazi katika uwezo uliopo pale na kuendeleza ukarabati mkubwa ambao unahitajika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali na hata Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara wameelewa kwamba katika kiwanda kile kwa kweli pana deni kubwa sana la fedha. Sasa mwekezaji yeyote anatakayekuja pale ni lazima tuanze na deni lile litalipwa kwa utaratibu gani lakini si hivyo tu lazima tujue tunatumia njia gani, kama tunawapa asilimia wafanyakazi wa pale katika zile asilimia 49, je, wataendeshaje kiwanda baada ya hapo? Hayo ni maswali ya kujiuliza kama wakiwa na mwekezaji mahiri. Lakini hata kama tutazipeleka hisa hizi mathalani kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*, moja ya sharti ya *Dar es Salaam Stock Exchange* ni kiwanda kuwa na faida kwa miaka mitatu mfululizo, hilo nalo ni tatizo. Kwa hiyo kuna njia nyingi tunazifanyia kazi hivi sasa na ninawahakikishieni kwamba tutalipatia ufumbuzi wa haraka. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba uchungu wenu wa kuona viwanda hivi havifanyi kazi vilevile ni uchungu wangu mimi kama Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba ambazo zimekuwa hazitumiwi na wafanyakazi wa urafiki, nyumba hizi zilikodishwa kwa Polisi karibu *flats* 30 na

*flats* 20 zilikodishwa kwa watu binafsi. Lakini napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba wafanyakazi wa Urafiki wanalipwa mishahara yao kulingana na sheria za nchi. Wakati kima cha chini katika Sekta ya uzalishaji ni shilingi 80,000/- Urafiki wanalipwa shilingi 100,000/- kabla ya kuweka marupurupu mengine kama vile *bonus*, kulingana na utendaji wa mfanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lililogusiwa na Waheshimiwa Wabunge ni lile la Serikali kulinda viwanda vya ndani ili viweze kuhimili ushindani. Suala hili nimelizungumzia sana katika hotuba yangu. Nimesema iko haja kwa kweli sasa hivi uchumi wetu kulinda viwanda vyetu vya ndani hasa vile ambavyo vina mwelekeo wa kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza nje ya nchi. Sasa kitu kimoja ambacho lazima tuwe makini na Wizara yangu itakuwa makini katika hilo, katika taratibu hizi za kuwa na masoko ya pamoja kwa mfano Jumuiya ya Afrika Mashiriki inawezekana nchi nyingine zikatumia utaratibu wa kodi kama njia ya kupunguza ushindani kwa nchi nyingine kuongeza ushindani katika nchi zao. Hili tutaliangalia vizuri sana na ndiyo maana hata tunapotakiwa kuweka viwango vya kodi au ushuru ni vizuri tukafanya kwa umakini mkubwa viwango vile visije vikawa vinafaidisha maeneo mengine na kutuachia matatizo hasa ya kuendeleza viwanda vyetu katika nchi yetu. Tunazungumzia masuala ya ngozi, masuala ya sukari, masuala ya mafuta na yote hayo tumesema kwamba Wizara yangu itajitahidi kuona kwamba tunafanya nini ili kuboresha mawanda ya kodi na ushuru ili kuvifanya viwanda vyetu viwe na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lililozungumziwa ni eneo la *TBS*. Kama mnavyokubali Waheshimiwa Wabunge tumeanza kulifanyia kazi, muda ni mfupi lakini nawahakikishieni matatizo ya pale tutayaweka sawasawa, nimeshaitisha kikosi kazi na kimeshanipa mapendekezo. Mapendekezo yale kama nilivyowaambia asubuhi ni pamoja na kuangalia uwezekano wa *PVOC* kufanyika ndani au nje ya nchi au yote kwa pamoja. Lakini kwa sababu suala lile liko kisheria itabidi tuje tulitolee maamuzi hapa ndani ya Bunge baada ya kupata maamuzi ya Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna hoja ambayo imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara ya kuelezea kwamba kuna haja ya ku-*overhaul* muundo wa Shirika zima hususan Idara ya Udhibiti na Ubora ili ifanye kazi yake vizuri. Nawahakikishieni hilo tutalifuatilia kwa karibu na majibu yake mtayapata hivi karibuni, nadhani hata kabla ya Bunge lijalo tutakuwa tumeshaweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka ni kupunguza athari za kupata bidhaa *fake*, bidhaa za bandia na bidhaa dhaifu katika uchumi wetu. Bidhaa dhaifu katika uchumi wetu kwanza zinamaliza ushindani katika viwanda vyetu. Bidhaa nyingi zikiingia nchini dhaifu tayari zimeshatuingizia ushindani usio wa haki kwa viwanda vyetu. Hilo tunataka tulifanyie kazi. Lakini vilevile bidhaa hafifu hizi vilevile ni hatari kwa usalama wetu. Kuna wakati tumesikia kuna maziwa ambayo si mazuri yanaingia ndani, tunaambiwa wengine wanachakachua maji lakini yale ni kwa matumizi ya binadamu kwa hiyo hilo ni eneo ambalo

kwa kweli tutalifanyia kazi. Sasa hivi tunataka kuweka utaratibu wa ushirikiano wa karibu zaidi kati ya *TBS* na Idara nyingine ambazo zinashughulikia masuala ya bidhaa bandia au bidhaa ambazo ni dhaifu. Kwa mfano *TFDA, FCC* wote wafanye kazi kwa pamoja ili tuweze kushirikiana vizuri pamoja na kulihusisha Jeshi letu la Polisi kwa maana ya kufanya uvamizi wa ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda Bunge hili wakati tunapojadili mambo ya viwanda, ni kweli kuna changamoto, lakini tusijadili kama vile nchi yetu haina viwanda kabisa. Vipo viwanda vingine vinafanya kazi vizuri lakini kazi kubwa ni kupambana na changamoto na kuona kwamba vile visivyofanya kazi vizuri tunaviamusha namna gani. Kwa mfano hivi sasa mpaka Desemba 2101 tutakuwa na viwanda zaidi ya 11 au 12 vya ngozi ambavyo vitakuwa vinafanya kazi nchini kama nilivyoelezea kwenye hotuba yangu. Lakini haya kwenye *EPZA,* uwekezaji unaofanyika pale kwa kweli ni uwekezaji mkubwa sana na *we can live on the past.* Hatuwezi kusema vile viwanda vya zamani chenye teknolojia ya mwaka 1964 ukalinganisha na teknolojia mpya. Teknolojia imebadilika, taratibu zimebadilika, haya ndiyo masuala ambayo Wizara yangu inajaribu kuyafanyia kazi na ndiyo maana tunasema kwamba tunahakika Waheshimiwa Wabunge mtatusaidia katika kuendeleza eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto kubwa sana ya kuongeza masoko yetu. Hivi sasa wawekezaji wengi na nchi nyingi zina ari kubwa ya kufanya biashara na Tanzania. Maana sasa uwanda wa kufanya biashara umepanuka, tunataka kuingia

kwenye maeneo ya *SADC, COMESA* na *EAC* kama eneo huru la biashara. Lakini vilevile kwa taratibu tulizonazo kwa mfano masoko yale ya nje ya nchi *AGOA*, yale masoko ambayo tunayapata kutokana na *European Union*, masoko yale kabla ya kufanya kazi na sisi yanaangalia utaratibu wetu wa kuwekeza na mazingira ya kuboresha masoko yetu. Ndiyo maana sasa hivi tunajitahidi sana kushughulikia suala la *One Boarder Post* katika mipaka yetu na hii tutaiweka katika mipaka yote na kuhakikisha kwamba ukishachekiwa mzigo wako Kenya basi ukiingia Tanzania ule mzigo umeshachekiwa, sio unachekiwa pale Hororo, unakuja kuchekiwa tena huku ndani, yote ni kupoteza muda tu. Zile ndizo tunazoziita *non tariff barriers*, vikwazo ambavyo si vya kiushuru. Ukishachekiwa Namanga pale ukienda Kenya unaingia tu. Haya ndiyo mambo tunataka kuyafanya sasa hivi ili kuboresha biashara katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tunataka kufungua masoko katika maeneo mbalimbali tuliyoyasema. Sasa hivi tunataka kufungua masoko kwa mfano katika Mikoa ya Kusini, tumesema pale Mtambaswala, maeneo ya Kilelema tunataka kufungua masoko haya ili kuhakikisha kwamba wananchi wanauza bidhaa zao, wanapata mapato yao na kunakuwa na mwingiliano mzuri kati ya nchi mbalimbali na nchi jirani ambazo tunashirikiana katika biashara. Kitu kikubwa kinachotukwaza ni jinsi gani tutaondoa *supply constraints* kwa upande wa uzalishaji ili tuzalishe zaidi tukidhi masoko yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna atakayekataa umuhimu wa kuendeleza viwanda vidogo. Viwanda vidogo ndiyo ukombozi katika nchi hii. Viwanda vidogovidogo ndiyo ukombozi kwa sababu ndiyo sekta inayowaajiri waliosoma na wasiosoma. Wote kwa pamoja ndiyo sekta ambao inatengeneza ajira na kutengeneza mapato ya Watanzania hasa wale wa kipato cha chini na kipato cha kati. Kazi yetu kubwa kwa kweli ni kuweka mazingira wezeshi, kuondoa urasimu, haya ni lazima tuyapunguze. Mimi nimefurahi juzi hapa *BRELA* sasa hivi wanashirikiana na *TCCIA* katika kutoa leseni zao kutoka maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, sasa hivi mwekezaji kutoka Ngara, kutoka Katavi hana haja ya kuja Dar es Salaam atakuwa anafanyia kazi kulekule aliko ili kupunguza gharama za kufanya biashara yake. Kwa hiyo, eneo hili tunalifanyia kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi sana kuongeza fedha katika *SIDO*, tunajua hazitatosha lakini tukilinganisha na mwaka jana kipindi hiki tunapata fedha nyingi zaidi kuliko miaka yote iliyopita. Kwa hiyo, tunahakika kwamba jinsi tunavyoendelea *SIDO* tutaifanyia kazi kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Kiwia alizungumzia suala la mazingira magumu ya biashara. Nakubaliana naye, suala la kuboresha mazingira magumu ya biashara ni *cross cutting,* linajumuisha Idara mbalimali za Serikali na ndiyo maana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameagiza kuundwa kikosi kazi cha kuboresha mazingira ya biashara nchini kikiongozwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na

kujumuisha Makatibu Wakuu wote na Wakuu wa Idara mbalimbali za Serikali. Kazi ya kikosi kazi hiki ni kuainisha na kuweka mikakati katika maeneo mbalimbali yanayoonekana kukwamisha mazingira ya biashara ambayo ni ya kisera, kisheria na kimuundo. Kikosi kazi hiki kiliandaa kitu ambacho tunakiita *Government Road Map*, mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Wizara ya Viwanda na Biashara inasimamia kipengele cha kuanzisha na kufunga biashara na mambo yafuatayo yamefanyiwa kazi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kupunguza siku za kusajili kampuni na majina ya biashara kutoka siku tano mpaka siku tatu kwa makampuni na kutoka siku tatu hadi siku moja kwa majina ya biashara. Pili, kuweka kumbukumbu za makampuni majina ya biashara, alama za biashara na hataza katika mifumo ya *electronic*. Nne, kuweka *Memorandum of Articles of Association* kwenye tovuti ya *BRELA* ili kuwezesha uaandaji wa nyaraka za kufungua makampuni kwa urahisi. Tumeweka fomu mbalimbali za usajili kwenye tovuti ya *BRELA, BRELA* na *TRA* sasa wanashirikiana kwa karibu, wanaandaa utaratibu wa kutoa *TIN* wakati wa usajili unapofanyika ili kumwondolea adha mfanyabiashara wa kufuata *TIN TRA* katika ofisi mbalimbali lakini vilevile kuna Sheria tutazifanyia mapitio. Kwa mfano Sheria ya Makampuni, Sheria ya Majina ya Biashara, Sheria za Alama za Biashara na Sheria ya *TANTRADE* ili kuweka mazingira rafiki katika biashara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilijitokeza katika michango ya Waheshimiwa Wabunge ni suala la safari za Mheshimiwa Rais nje ya nchi kwamba hazina faida. Mimi nafikiri hili si sahihi kwamba safari za Rais nje hazina faida. Takwimu halisi kutoka Kituo cha Uwekezaji kwa maana ya *TIC* na *EPZA* zinaonyesha kwamba ziara hizo zimeleta mchango mkubwa sana katika sekta yetu ya viwanda na sekta mbalimbali na hususan sekta ya kilimo. Kwa mujibu wa takwimu za *TIC* na *EPZA,* hizi taasisi zilivutia jumla ya miradi 656 mwaka 2009, ilipofika mwaka 2010/2011 tulipata miradi 843 na iliingiza mtaji wa karibu dola bilioni moja za kimarekani. Lakini vilevile tunavyoangalia kwenye *EPZA* kama hotuba yangu ilivyosema tayari tumeshaingiza mitaji ya karibu dola za Kimarekani milioni 700, ajira karibu 15 zimeshatengenezwa na wawekezaji wengi wanakuja na hivi karibuni Mheshimiwa Rais alikwenda Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali imepata karibu dola za kimarekani 689 milioni kwa ajili ya kuendeleza mpango wetu wa *SAGCOT* kule Kusini mwa nchi yetu. Fedha hizo ninahakika zikitumika vizuri na zinalenga zaidi vijijini, kuboresha miundombinu ya vijijini ambayo ndiyo hoja kubwa tunayoizungumzia Waheshimiwa Wabunge kwa maana ya barabara, upatikanaji wa umeme na upatikanaji wa maji. Tukifanya hivyo nadhani shughili zingine zitakuwa zinafanyika kwa utaratibu mzuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo wawekezaji watajitokeza kwa wingi na hapa juzijuzi tumeona, tumepata ujumbe mkubwa sana wa

wawekezaji kutoka nchi mbalimbali lakini vilevile tumepata wawekezaji kutoka nchi ya China, sasa hivi tunaendelea na uboreshaji wa viwanda vyetu mama kupitia *NDC* katika kuzalisha Makaa ya Mawe na vilevile katika kuzalisha mradi wa chuma ambao nafikiri utakuwa ni *spring board* kubwa sana ya kutupeleka kwenye mchakato wa ujenzi wa viwanda ambao tunauhitaji hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema hoja za Wabunge ni nyingi sana na hatuwezi kuzimaliza, lakini zote tumezichukua. Kazi yetu kubwa sasa ni kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tutazijibu hoja hizi vizuri, tutazileta na mtaziona na itakuwa ni sehemu ya mchango ambao mmetupa Wizara yetu kutoka kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la mwisho nataka kumalizia, ile safari ya *TBS* ya kwenda China iliandaliwa na Bodi ya *TBS*, Mheshimiwa George Simbachawene alikwenda kule siyo kama Mbunge alikwenda kama Mjumbe wa Bodi ya *TBS*. Kwa hiyo, alikwenda kufanya kazi za bodi ya *TBS*. Nataka kuliweka hili sawa kwa sababu niliona liliuliziwa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kwamba kwa hatua ambazo tutazichukua, tutajitahidi kuhakikisha kwamba sekta yetu ya viwanda na biashara inafanya kazi vizuri na nitashukuru sana Wabunge mkituunga mkono kwa kuangalia dhana ya kwamba sasa tunakwenda kwenye mchakato wa ujenzi wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa maana ya

*Industrialization* badala ya kuangalia kiwanda kimoja kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mheshimiwa Assumpter Mshama alichangia kwa maandishi, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum alichangia vilevile kwa maandishi na Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo na Mheshimiwa Sabreena Sungura walichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 44 - WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Kif.1001 *Administration and HR Management*…….................Tshs.8,562,553,100/=

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu mpango wa Serikali kuifanya Taasisi ya *SIDO* iweze kuyafikia maeneo mengi. Taasisi ya *SIDO* ndiyo inayotoa elimu ambayo inawagusa wananchi

hata wa kawaida, akina mama, vijana katika masuala ya uwekezaji lakini hadi sasa taasisi hii bado iko kwenye Makao Makuu ya Mikoa ambapo inakuwa vigumu sana na ni gharama kuweza kuwafikia wananchi kwa urahisi. Nilitaka kufahamu Serikali ina mpango gani kufanya taasisi hii ifike hata ngazi za Wilaya ikiwemo Wilaya ya Busega? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *SIDO* ipo katika Makao Makuu ya Mikoa lakini vilevile tunapoangalia takwimu tutaona kwamba *SIDO* imejitahidi sana kuwafikia wajasiriamali wengi katika maeneo mbalimbali lakini tatizo moja kubwa linaloikwaza *SIDO* ni ukosefu wa rasilimali za kutosha za kuanzisha ofisi katika maeneo mengi hata kufikia ngazi za Wilaya. Lakini Wizara inafanya utaratibu wa kuona ni jinsi gani tunaweza kupata fedha kutoka mashirika ya nje kuhakikisha kwamba *SIDO* inapanuka zaidi kutoka ngazi za Mikoani na kufikia ngazi za Wilayani.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu Viwanda vya Korosho ambavyo vipo Mkoa wa Mtwara na Lindi, vimebinafsishwa kwa muda mrefu na mpaka sasa hivi vimeshindwa kufanya kazi na hivyo kupoteza ajira za wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi. Je, Waziri anazungumzia nini kuhusu viwanda hivi?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita niliwaita wamiliki wote wa Viwanda vya Korosho vilivyobinafsishwa hapa Dodoma

na kwa bahati nzuri nashukuru Mheshimiwa Mitambo alikuwepo kwenye kikao kile, wamiliki wale walitueleezea changamoto zao, ukosefu wa mitaji, matatizo ya urasimu hasa katika uendeshaji wa kesi Mahakamani, lakini vilevile tatizo la bei za ubanguaji wa korosho wanazozipata lakini kubwa zaidi ni tatizo la mitaji. Imeonekana kabisa kwamba vyombo vya fedha bado havijahamasika sana katika kupeleka fedha za mitaji kwenye viwanda hivi, tumeshaanza taratibu ambazo nilizielezea za kuongea na *TIB* kuona kwamba ni jinsi gani wanaweza kusaidia mitaji ili *at least* viwanda hivi, hatuwezi kuvimaliza vyote kwa kipindi hiki lakini kama viwili, vitatu au vinne vikiweza kufanya kazi, tuna hakika kwamba hali ya kule itabadilika.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilimweleza Waziri jinsi Mkurugenzi wa *SIDO* Singida, ambaye ni mwanamama anavyofanya kazi nzuri ya kuelimisha jamii. Nikataka Waziri amtambue huyu mama, pamoja na kumtambua atunzwe na kuongezewa pesa za kuendesha shughuli zake kwa sababu shughuli zake kwa kweli zinaleta matumaini katika Mkoa wa Singida. Ninaomba sana Waziri alipokee ombi langu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea ombi, nitamtunza, nitamwangalia, nitamwongezea pesa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anifahamishe kwa mujibu wa Sheria ya

*COSOTA* ya mwaka 1999 inapaswa Watangazaji wote waanze kulipa *royalties* kwa wasanii. Naomba kufahamishwa ni lini Watangazaji wataanza kutekeleza Sheria hii ya *COSOTA*?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima nikiri kwamba sina tarehe *definitely* kwamba ni lini wasanii watalipwa na wale *Broadcasters* lakini kitu ambacho kinaendelea, jibu alilolitoa jana Naibu Waziri wa Mawasiliano na kuonesha uhusiano wa Wizara ya Mawasiliano, Viwanda na Biashara, Habari, Vijana na Utamaduni, ile ni njia nzuri ya kuonesha kwamba tunalifuatilia kwa karibu na tunahakikisha kwamba wasanii hawa wanapata haki zao kama wanavyopaswa kuliko wanavyoumizwa hivi sasa.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu kwa Waziri kwamba Viwanda vya Korosho vya Mikoa ya Lindi na Mtwara ambavyo vilibinafsishwa wakati Mheshimiwa Waziri wa sasa akiwa Waziri, waliochukua viwanda vile wana uwezo, baadhi yao walikuwa ni Mawaziri wastaafu. Wakati Waziri akijibu swali hapa amesema wengine hawana mtaji, lakini inaonekana baadhi yao wana mitaji na alisema kwamba katika mazungumzo ambayo atayafanya wale ambao atagundua kwamba hawataviendeleza viwanda vile atawapa watu wengine. Kwa msingi huo, sasa napenda kupata maelezo juu ya nafasi aliyonayo na mkakati wake wa ziada na muda gani atawaambia Watanzania na hasa wananchi wa Lindi na Mtwara kwamba mkakati huo

utazaa matunda maana haya mengine ni makubwa zaidi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la ubinafsishaji ukiliangalia kwa makini sana ni la uwezeshaji hasa kwa viwanda vya korosho. Kwa sababu viwanda vile vyote kimsingi vilipewa wazawa kwa maana ya Watanzania pale mwanzoni lakini kama nilivyosema kwamba bado tulikuwa tunahitaji kufanya kazi ya ziada ya kuweka mazingira bora ya uwekezaji kuwawezesha kwa maana ya kuendeleza viwanda vile, kuweka utaratibu wa ufuatiliaji. Utaona kwamba hivi sasa Wizara yetu na mimi kama Waziri ambaye nilihusika na masuala ya ubinafsishaji, nimeshaanza kuwa makini sana. Tayari nimekwishawaita wamekuja hapa Dodoma na nina hakika kwa kero zao walizozisema tukishirikiana Serikali na wao kama wadau wakubwa, hatuwezi kuvifufua vyote lakini tukivifufua vitatu hali kule itabadilika kidogo na tutakuwa tunaendelea na mchakato huo. Tukumbuke toka viwanda vile vilipobinafsishwa teknolojia imebadilika na kwa sababu mimi ndiye niliyevibinafsisha na sasa nimerudi, nakuhakikishia vitafanya kazi. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumwuuliza Waziri na kwa kuwa amekiri mwenyewe kwamba ndiye aliyehusika na ubinafsishaji wakati wa Awamu ya Tatu ya Rais Mkapa, kuna Kiwanda cha Chumvi Uvinza, kilibinafsishwa kwa milioni mia tisa, mwekezaji yule Ndugu Manek ambaye ni Mhindi, ameuza mitambo ya *Plant* ambayo ilikuwa inazalisha chumvi kwa kutumia umeme kwa shilingi

bilioni 4.5. Waziri amesema kwamba moja ya lengo la ubinafsishaji ilikuwa ni kuongeza teknolojia lakini kilichotokea pale ni kwamba wale Wahindi wanazalisha chumvi kwa kutumia jua, wanaanika kama bustani. Naomba kujua *position* ya Serikali kwamba ni lini itachukua kiwanda kile ilihali mwekezaji yule amefanya utapeli na unyama wa hali ya juu?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na anayoyasema lakini katika maelezo yangu nimesema tayari sasa hivi Serikali imeshafanya uchambuzi wa viwanda vyote vilivyobinafsishwa na kujua *status* yake ikoje na tayari sasa hivi tunatayarisha utaratibu wa Hati ya Baraza la Mawaziri kuvizungumzia viwanda hivyo kimoja baada ya kingine na kuona uharibifu uliofanyika pale au nini kinahitajika kufanyika. Tukishajiridhisha hapo, Serikali itatoa maamuzi yake. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Kafulila kwamba viwanda vilivyopata matatizo kama hivyo si cha chumvi peke yake, vipo vingine pia vimekuwa *vandalized* na ndiyo tunataka kuvitolea maamuzi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka Wizara itueleze ni jinsi gani ambavyo wataweza kuvilinda viwanda vya ndani hasa kwa mazao ambayo yanazalishwa na kukidhi mahitaji kama viwanda vya chumvi lakini vilevile viwanda vya sabuni na malighafi za sabuni? Katika ufungaji hapo Waziri hajatoa maelezo yoyote na wala hatujasikia lolote kuhusiana na hili.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, ulinzi wa viwanda vyetu ni suala muhimu sana katika kujenga uchumi wetu, lakini ulinzi huu vilevile usiwe ni njia ya kupunguza ushindani katika viwanda vyetu, ndiyo maana nimesema hata katika masuala ya kodi ni lazima tuwe makini sana jinsi tunavyoweka ushuru wetu kulingana na sisi wenyewe na viwanda vyetu, lakini vile vile kulingana na mahusiano yetu tuliyonayo, kwa mfano Jumuiya ya Afrika Mashariki au Jumuiya ya *SADC*. Kwa sababu vigezo hivyo ndiyo vinaweza vikatumika vikadidimiza viwanda vyetu na viwanda vya wenzetu vikaendelea lakini ulinzi mzuri kwanza ni lazima uendane na mazingira bora ya uwekezaji, ni lazima uendane na mazingira bora ya kupunguza gharama za kufanyia kazi kwa mfano kupunguza gharama za umeme, lakini jambo la mwisho la msingi ni upangaji wa mawanda yetu ya kodi na tozo mbalimbali tunazotoza, pamoja na mawanda ya kifedha na kikodi kwa maana ya *fiscal earned tax regime* tunazoziweka.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliuliza kwamba wawekezaji walionunua viwanda vya magunia nchini wanaweza kutengeneza magunia milioni tano na laki tano kwa mwaka, lakini mahitaji ya magunia nchini ni milioni sitini na mbili. Katika magunia haya, yapo mazao ambayo yanaweza kutumia magunia ya *jute* na *sulphate* lakini mazao kama kahawa, mahindi, korosho na maharagwe yanaweza kutumia magunia ya katani. Je, ni lini Serikali itawapa *guarantee* wawekezaji hawa ili wafungue viwanda,

watengeneze magunia ya katani, vijana wapate ajira na Serikali ipate pato la Taifa na zao la katani liweze kuwa *promoted*?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Betty Machangu kwamba wawekezaji hawa mara tu watakapotokea na kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, tutawa-*support*, tutawahamasisha ili kupunguza tatizo hilo.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna chumvi nyingi sana inayozalishwa kule Bukundi katika Mkoa wa Simiyu, Wilaya ya Meatu lakini chumvi hii haitumiki na badala yake inatumika kwa mifugo tu kutokana na kutokuwa na madini joto. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuwekeza kiwanda katika eneo hili ili chumvi iweze kuzalishwa kwa ubora iweze kuuzwa na kuleta kipato na kuiingizia Serikali fedha za kigeni?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Mbunge tunaupokea.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimwelezea Mheshimiwa Waziri athari zinazopatikana kutokana na usafirishaji wa chuma chakavu. Hivi sasa katika Mji wa Dar es Salaam kutembea na gari katika baadhi ya mitaa lazima uwe na macho zaidi ili uweze kujinusuru na janga linalotokana na mashimo yaliyomo katika Jiji la Dar es Salaam. Wizara ilizuia leseni za usafirishaji wa

chuma chakavu lakini wakati huohuo wakatoa ruhusu kwa wasafirishaji wa *cast iron*, hapo ndipo walipata mwanya wa kuutumia kusafirisha chuma chakavu. Je, kuna mpango gani sasa wa kuzuia kabisa leseni za usafirishaji chuma chakavu ili kuepuka athari hizi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaandika *paper* ambayo tumependekeza kwamba Sheria hii iundwe kwanza, ya kuzuia haya mambo na bado utekelezaji wake upo katika mkakati mzuri sasa hivi.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nampongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya kule Kilimanjaro. Naomba niulize lile Soko la Kitaifa la Njiapanda la ndizi na mboga na lile soko la Kimataifa la Lokorova la nafaka, ningeomba kujua kama Wizara ina mpango gani wa kuhamasisha wananchi wa Tanzania, wawekezaji wa ndani na nje ili wawekeze kwenye masoko hayo na pia ningeomba kujua huo mpango wa *EPZ* utaanza kutekelezwa lini kwenye masoko haya? Ahsante sana.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu Mstaafu Mzee Mrema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi nampongeza sana Mheshimiwa Mrema kwa dhati kabisa kwa sababu kwanza amekuwa jasiri na eneo lao wamekuwa wabunifu. Yako maeneo mengi nchini

Tanzania sasa hivi watu wanaingia mpaka kutoka nchi za nje wanachukua bidhaa zetu wanaondoka, wanachukua mahindi, wanachukua mpunga, wanaondoka, maeneo hayo ndio yana uwezo mkubwa, *potential* kubwa ya kuanzisha masoko ya kitaifa. Mimi napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mrema kwamba mara tutakapotoa kibali cha *EPZ* na kwa bahati nzuri kwa sheria zilizowekwa za kinchi anayetoa mamlaka ile ni mimi kama Waziri wa Viwanda vya Biashara na ninamhakikishia tutakitoa kibali hicho moja kwa moja, masharti yale ya EPZ ya kuzalisha asilimia 80 kuuza nje, asilimia 20 kuuza ndani na *value chain* itakayoanzishwa, tutapata wawekezaji haraka sana. Hilo tunamhakikishia na tutalifanyia kazi haraka. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu liko kwa Wakala wa Vipimo. Hadi jana katika vituo 242 vilivyokaguliwa kuhusu mizani, mizani 119 zilizokaguliwa kati ya hizo mizani 75 ni mbovu na humwibia mkulima kilo 10 mpaka 30. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mizani tulikwishalitabiri tokea mwanzo. Mizani hizi zilitakiwa ziwe za *digital* na waliotakiwa kununua mizani hizi si Serikali lakini ni *Tanzania Cotton Growers Association*. Ilihitajika mizani 8000 lakini mpaka msimu wa kuuza pamba ulipoanza kulikuwa na mezani kama 2600, kwa hiyo wadau wote tukaitana hapa, tukakubaliana kwamba ni vizuri tukatumia mizani zote kwa maana ile ya *digital* na ile ya *ruler* wakati hii *digital* ikiondoka sokoni. Lakini kwa

vile ilikuwepo sokoni tulikwishatuma Wakala wa Vipimo wahakikishe kwamba wanasambaa katika maeneo yote kuangalia na kuhakikisha kwamba wenye mizani zile hawawadhulumu wakulima hasa wa pamba. Sasa Mheshimiwa Mbunge anapoelezea kwamba kuna mizani zimekamatwa inatupa *encouragement* kwamba Wakala wa Vipimo wanafanya kazi zao lakini namhakikishia kwamba tuko katika mchakato wa kuwahamasisha *Tanzania Cotton Growers Association* walete upesi zile mizani za *digital* tuondokane na matatizo hayo.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi ingawaje Mheshimiwa Waziri hajanitaja pamoja na kumwekea vi-*note* viwili bado kaendelea kuniweka kapuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rachel Mashishanga, endelea kwenye swali, muda wetu ni mfupi sana.

**MHE. RACHAEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kuwa Shinyanga tumepata Kiwanda cha Ngozi na mwekezaji amepatikana. Nataka nijue hicho kiwanda kitaanza kufanya kazi lini na kama ndio kitaanza kujengwa, kitatumia muda gani ili wananchi wa Mkoa wa Shinyanga wakae mkao wa kula? Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge Rachael Mashishanga, mtani wangu, aniwie radhi kwa kutokumtambua, ilikuwa si kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kile tayari kibali tumeshatoa kwamba sasa wawekezaji waanza kujenga, kitagharimu dola milioni 7.2 za Kimarekani. Kitakuwa maeneo ya Ibadakuli kule Shinyanga kwa sababu tumeshatoa *go ahead*, kazi ni kwa mwekezaji aanze kufanya kazi.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 12 mwezi huu, niliomba mwongozo hapa kuhusiana na kuwepo taarifa kwenye gazeti kuuzwa kwa Kiwanda cha *General Tyre* Arusha. Serikali ikatoa majibu kwamba tayari wameomba Mahakamani wamepata *court injunction* na kwamba sasa kiwanda hicho kitakuwa hakiuzwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuweka *injunction* kiwanda kutouzwa ni kuonyesha kwamba kiwanda hicho kina mgogoro lakini Mheshimiwa Waziri hapa wakati anajumuisha amesema kwamba tayari *NDC* wameanza kufufua kiwanda hicho na kwamba kuna mchakato wa kupata wabia kwa ushindanishi ambao utakuwa ni halali. Sasa mimi nashindwa kuelewa katika mazingira ambayo kiwanda kina mgogoro inakuwaje tena Serikali inasema kwamba *NDC* wanafufua? Naomba maelezo ni uchawi gani unatumika katika kufufua kiwanda ambacho kina mgogoro wa Kimahakama?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo pale kimsingi si mafao ya wafanyakazi, lakini ni yale malipo yanayoitwa *golden handshake,* yale malipo ambayo ni ya mkataba,

malipo ya hiari ya kimkataba baada ya shughuli zile kuisha. Fedha zenyewe zinazodaiwa pale ni shilingi milioni 83, tayari Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kwa maana *CHC* na *Treasurer Registrar,* tunakaa chini kuona utaratibu wa kulipa fedha zile za shilingi milioni 83 lakini hapohapo kwa sababu suala hili liko Mahakamani na Mawakili wanashughulikia, tuna hakika kwamba halitafikia kiasi cha kwamba lengo linalotakiwa la kukiuza kwa mnada kiwanda kile kikubwa linafanyika.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilishauri kwamba ni vizuri maeneo ambayo ni *potential* kuinua uchumi katika nchi yaangaliwe kwa macho yote mawili. Wilaya ya Serengeti ni *potential* katika kuinua uchumi ukitilia maanani kwamba asilimia 17 ya uchumi unachangiwa na utalii, Serengeti ikiwemo. Nilishauri kwamba ni kwa nini kusiwe na Kiwanda cha Alizeti ambako kuna *window* ya mahitaji asilimia 60, mafuta haya ya chakula tunayapata kutoka nje, asilimia 40 tu tunapata nchini. Ni kwa nini tusiwe na kiwanda kikubwa cha alizeti pale Serengeti kwa sababu hali ya hewa ni nzuri, zao linastawi vizuri, ndio swali langu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kebwe ameeleza hoja nzuri. Ameeleza vizuri kwa sababu hiyo *potential* ambayo iko Serengeti inaangukia mara mbili kama tulivyosema kwenye hotuba yetu leo. Katika ule Mpango wetu Mkakati Unganishi *(Integrated Industrial Development)* tunaangalia sekta ya utalii na sekta ya

viwanda hasa vya kusindika chakula. Kitu ninachomshauri na ninachomhamasisha na tunaweza kushirikiana, mwekezaji wa kuwekeza katika kiwanda cha alizeti itakuwa vizuri yeye amhamasishe kwa sababu itakuwa ni sekta binafsi na mimi kwenye Wizara yangu nitakuwa tayari ku-*support* uhamasishaji huo ili tupate mwekezaji pale kwa kumwekea mazingira wezeshi aweze kujenga kiwanda hicho, kwa sababu Serikali haiwezi kujenga viwanda, imeshajitoa katika ujenzi wa viwanda.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilieleza kwamba Mkoa wa Singida hauna viwanda wala mazao ya biashara lakini kwa miaka ya karibuni zao la alizeti limeonekana kustawi vizuri. Wizara ina mpango gani kwa kushirikiana na wadau binafsi kujenga kiwanda cha kusindika alizeti katika Mkoa wa Singida?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wajenzi wa viwanda hivyo ni *private sector* na kwa sababu Mheshimiwa Christina tulikuwa wote katika Kamati ya Fedha na Uchumi, tukutane tupeane mikakati ni jinsi gani tutavutia wawekezaji hao kuja kuwekeza Singida.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia kuhusu huduma mbalimbali ambazo zinatolewa, huduma hizi ambazo ni za viwanda kwa mfano huduma hizi zimesambazwa karibu nchi nzima kwa kugawa kikanda. Sasa mimi ninaulizia kwa maana

ya viwanda vya saruji, je, kwa Kanda ya Ziwa ambapo kiwanja kilishapatikana Shinyanga, Mheshimiwa Waziri Mary Nagu anajua, je, kwa sasa hivi mnafikiriaje na sisi Kanda ya Ziwa kutuletea kiwanda cha saruji? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Hewa, swali lake linafanana kabisa na la Mheshimiwa Lolensia Bukwimba ambalo aliomba Geita nako kuwe na kiwanda cha saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu nimesema kwamba Wizara yangu imefanya tathmini na kuona kwamba tunapofuata taratibu za uwekezaji tusiende na zile *investment code* za *all size fixed all* maana yake nini, koti hilohilo kila mtu litamuenea. Kuna maeneo mengine kwa kweli yana fursa tofauti na maeneo mengine ndio maana nikasema lazima tuangalie taratibu za kujua wapi tunawekeza ili kuibua hizo *potentials* katika maeneo hayo. Tutalifuatilia kwa karibu tuone ni jinsi gani na ni utaratibu gani tunaweza kuhamasisha uwekezaji wa kiwanda cha saruji maeneo ya Mwanza au Geita tofauti na taratibu ambazo tunaweza kuziweka Dar es Salaam au Lindi au Mtwara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu Kanuni 104(2) kwa madaraka yangu naomba sasa tupitishe bajeti hii kwa mafungu ya ujumla.

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* ...................Tshs. 8,562,553,100/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts*....Tshs. 451,212,400/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning* …….Tshs. 4,159,767,500/=
Kif.1004–*Government Communication Unit* ……………..........................Tshs.160,190,600/=
Kif.1005–*Internal Audit Unit* ………….TShs.197,760,200/=
Kif. 1006 – *Legal Services Unit* ………Tshs.81,890,200/=
Kif.1007–*Management Information System* ……………...........................Tshs.196,353,200/=
Kif.1008–*Procurement Management Unit* ……………...........................Tshs.237,337,900/=
Kif.2001–*Industry* …………………….  TShs.5,270,093,400/=
Kif. 2002–*Small and Medium Enterprises Division* … ................................Tshs. 5,645,671,800/=
Kif.2003–*Commerce*………………… Tshs.1,907,035,000/=
Kif.4002–*Commodity Market Development* ….......................Tshs.11,949,189,700/=

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kif.1003 – *Policy and Planning* ......Tshs.121,553,139,000/=
Kif.2001–*Industry*…………………  …TShs.75,000,000/=
Kif.2002–*Small and Medium Enterprises Division* ……............Tshs.4,003,408,479/=
Kif.3001–*Commerce* …………………Tshs.1,045,277,941/=
Kif.4002–*Commodity Market Development* ……….................Tshs.1,703,961,580/=

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Matumizi ya Viwanda

na Biashara na Taasisi zake zote mafungu kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Kwa hiyo, naomba Bunge lako tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hotuba hii na Bajeti ya Wizara hii imepitishwa rasmi na Bunge.

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda na Naibu Waziri sisi tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu hayo mazito, Watanzania wana imani na ninyi. Kwa kweli suala la viwanda, ni suala la msingi sana katika maendeleo ya nchi yetu, tunawatakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja halafu nitatoa maelekezo ya mwongozo baada ya Kamati ya Uongozi kuketi leo saa saba na robo mchana.

Mheshimiwa Mohammed Hamis Missanga, kwa niaba ya Wabunge Waislam wote hapa Bungeni, anaomba kuwaalika Wabunge wote waliofunga na wasiofunga na wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge waliofunga katika futari maalum ya pamoja, siyo leo, kesho Ijumaa saa 12.30 katika Ukumbi wa Bunge wa *Basement*. Kwa hiyo, siyo leo ni kesho saa 12.30 jioni. Mwongozo wa leo sijapata labda kama kuna anayeweza kujitolea.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa mnisikilize kwa makini haya sasa ni maelezo ya Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe. Nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Spika aliendesha Kikao cha Kamati ya Uongozi leo saa saba na robo mchana na yaliyokubaliwa katika Kamati hiyo ya Uongozi ni haya yafuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Uongozi ya Bunge, imekutana mara baada ya kupitisha shughuli za Bunge mchana wa leo kama nilivyokuwa nimeelekeza asubuhi ili kujadili na kumshauri Mheshimiwa Spika namna bora ya kushughulikia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo asubuhi ya leo. Baada ya kujadiliana kwa kina ndani ya Kamati ya Uongozi ilidhihirika kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 48 ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Jafo haikukidhi matakwa ya kanuni hiyo, hivyo haikuwa hoja ya dharura bali Kamati ya Uongozi iliona kabisa hoja hiyo ilikuwa ni hoja ya msingi sana. Hata hivyo, baada ya Kamati ya Uongozi kuridhika kwamba hoja hiyo ilikuwa ni hoja ya msingi

imemshauri Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo kwamba aandae hoja yake sawasawa na kuiwakilisha kwa Mheshimiwa Spika ili iweze kupelekwa katika Kamati husika ya Bunge kwa lengo la kufanyiwa kazi kwa upana zaidi ikiwa ni pamoja na kuita wadau mbalimbali wanaohusika na jambo hilo na hatimaye kutoa ushauri kwa Bunge letu namna ya kulishughulikia jambo hilo kwa umoja wake.

Hayo ndio maelekezo ambayo ninayasoma yamejadiliwa kwa kina na ni maamuzi sasa yaliyotokea katika Kamati ya Uongozi baada ya kuipitia hoja hiyo kwa upana wake.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa shughuli hii ya leo. Bila kupoteza muda, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho, saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa, Tarehe 27 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*